JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI
TUME YA TAIFA YA MIPANGO

MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2027/28

Oktoba 2026

ORODHA YA VIFUPISHO

ADC	Aquaculture Development Centres
ADEM	Agency for the Development of Educational Management
AFCON	Africa Cup of Nations
AFDP	Agriculture and Fisheries Development Programme
AHSP	Annual Health Sector Performance Report
AMIS	Airport Management Information
ASDP II	Agricultural Sector Development Programme II
ATCL	Air Tanzania Company Limited
ATE	Association of Tanzania Employers
AU	African Union
BAKITA	Baraza la Kiswahili Tanzania
BBT	Building Better Tomorrow
BEVAC	Beekeeping Value Chain
CAMARTEC	Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology
CBE	College of Business Education
CBR	Central Bank Rate
CNG	Compressed Natural Gas
COSTECH	Commission for Science and Technology
DAWASA	Dar es Salaam Water and Sewerage Authority
DIT	Dar es Salaam Institute of Technology
DMDPII	Dar es Salaam Metropolitan Development Project II
DMGP	Dar es Salaam Maritime Gateway Program
DMI	Dar es Salaam Maritime Institute
DRC	Democratic Republic of the Congo
EAC	East African Community
EACOP	East African Crude Oil Pipeline
EASTRIP	East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project
EIA	Environmental Impact Assessment
EOCC	Emergency Operations and Communication Centre
EP4R	Education Programme for Results
EPZA	Export Processing Zones Authority
MW	Megawatt
NACTE	National Council for Technical Education
NCAA	Ngorongoro Conservation Area Authority

NCT	National College of Tourism
NDC	National Development Corporation
NEMC	National Environment Management Council
NHC	National Housing Corporation
NHIF	National Health Insurance Fund
NIDA	National Identification Authority
NIT	National Institute of Transport
NMT	National Museum of Tanzania
NPS	National Prosecution Service
NRW	Non-Revenue Water
PAMOJA	Project for Advancing Gender Equality in Tanzania
PCP	Programme for Country Partnership
PFMRP	Public Finance Management Reform Programme
PIM-OM	Public Investment Management Operational Manual
PPP	Public-Private Partnership
PPPC	Public-Private Partnership Centre
PSRP	Public Service Reform Programme
PSRS	Public Service Recruitment Secretariat
PSSN	Productive Social Safetynet
SADC	Southern African Development Community
SDGs	Sustainable Development Goals
SDL	Skills Development Levy
SEZ	Special Economic Zones
SGR	Standard Gauge Railway
SIDO	Small Industries Development Organization
SMMRP	Sustainable Management of Mineral Resources Project
SPV	Special Purpose Vehicle
SRWSSP	Sustainable Rural Water Supply and Sanitation Programme
TaESA	Tanzania Employment Services Agency
TAFICO	Tanzania Fishing Corporation
TAISP	Tanzania Agricultural Input Support Project
TAKUKURU	Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa
TANAPA	Tanzania National Parks
TANIPAC	Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxin Contamination
TANROADS	Tanzania National Road Agency
TANTRADE	Tanzania Trade Development Authority

TANZIS	Tanzania Innovation Systems
TASAF	Tanzania Social Action Fund
TaSUBa	Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo
TATC	Tanzania Automotive Technology Centre
TAWA	Tanzania Wildlife Management Authority
TAWIRI	Tanzania Wildlife Research Institute
TAZAMA	Tanzania Zambia Mafuta
TAZARA	Tanzania - Zambia Railway Authority
TBC	Tanzania Broadcasting Cooperation
TBS	Tanzania Bureau of Standards
TDHS-MIS	Tanzania Demographic and Health Survey and Malaria Indicator Survey
TEA	Tanzania Education Authority
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TEMDO	Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization
TFSRP	Tanzania Food Systems Resilience Program
TGC	Tanzania Gemological Centre
TIC	Tanzania Investment Centre
TIRDO	Tanzania Industrial Research and Development Organization.
TIRP II	Tanzania Intermodal Railway Project II
TMCHIP	Tanzania Maternal and Child Health Program
TPSF	Tanzania Private Sector Foundation
TUCTA	Trade Union Congress of Tanzania
U&T	Ufuatiliaji na Tathmini
UDSM	University of Dar es Salaam
UNFPA	United Nations Population Fund
UNICEF	United Nations Children's Fund
USD	United States Dollar
UVIKO – 19	Ugonjwa wa Virusi vya Korona – 2019
VHF	Very High Frequency
VVU	Virusi Vya Ukimwi
WMA	Weight and Measurement Agency
WRRB	Warehouse Receipt Regulatory Board
WSDP	Water Sector Development Programme

YALIYOMO

ORODHA YA VIFUPISHO i

SURA YA KWANZA 1
UTANGULIZI 1
1.1 Usuli 1
1.2 Malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 1
1.3 Mfumo wa Kusimamia Utekelezaji wa Matokeo 2
1.4 Mawanda ya Mpango 3
1.5 Mbinu za Uandaaji wa Mpango wa Mwaka 2027/28 3
1.6 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2027/28 3
1.7 Mpangilio wa Kitabu 4

SURA YA PILI 5
HALI YA UCHUMI 5
2.1 Utangulizi 5
2.2 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda 5
2.2.1 Uchumi wa Dunia 5
2.2.2 Uchumi wa Kikanda 6
2.2.3 Mfumuko wa Bei wa Dunia 8
2.2.4 Mfumuko wa Bei wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara 8
2.2.5 Mfumuko wa Bei katika Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki 9
2.3 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa 11
2.3.1 Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Taifa 11
2.3.2 Mfumuko wa Bei Nchini 13
2.3.3 Sekta ya Nje 14
2.3.4 Akiba ya Fedha za Kigeni 16
2.3.5 Sekta ya Fedha 16
2.3.6 Deni la Serikali 19
2.3.7 Demografia na Maendeleo ya Watu 20
2.3.7.1 Demografia 20
2.3.7.2 Hali ya Umaskini Nchini 20
2.3.7.3 Ajira 21
2.3.7.4 Maendeleo ya Watu 21
2.4 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2027/28 22
2.4.1 Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi Jumla 22
2.4.2 Misingi ya Mpango kwa Mwaka 2027/28 23

SURA YA TATU 25
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO 25
3.1 Utangulizi 25

SEHEMU A: UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA 2025/26 25
Miradi ya Kielelezo 25
3.2 Mageuzi katika Sekta za Kimkakati 26
3.2.1 Sekta ya Kilimo 26
3.2.2 Sekta ya Mifugo 26
3.2.3 Sekta ya Uvuvi 27
3.2.4 Sekta ya Viwanda 27
3.2.5 Sekta ya Ujenzi 28
3.2.6 Sekta ya Madini na Uchimbaji 29
3.2.7 Sekta ya Utalii 31
3.2.8 Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo 31
3.2.9 Biashara na Uwekezaji 32
3.3 Kujenga Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii 40
3.3.1 Elimu 40
3.3.2 Nguvu Kazi, Vijana na Ajira 41
3.3.3 Ustawi na Maendeleo ya Jamii 41
3.3.4 Afya 41
3.3.5 Maji na Usafi wa Mazingira 42
3.3.5.1 Mazingira 43
3.3.6 Ardhi na Maendeleo ya Makazi 43
3.4 Vichocheo vya Maendeleo 44
3.4.1 Nishati 44
3.4.2 Mifumo ya Usafirishaji na Uchukuzi Fungamanishi 45
3.4.3 Sayansi, Teknolojia na Ubunifu 46
3.4.4 Utafiti na Takwimu 47
3.4.5 Mapinduzi ya Kidijitali, TEHAMA na Mawasiliano 47
3.5 Misingi ya Uendelevu wa Taifa 48
3.5.1 Utawala Bora, Demokrasia, Usalama na Utulivu 48
3.5.2 Serikali za Mitaa 49
3.5.3 Utawala wa Kidijitali 49
3.5.4 Uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi 49

SEHEMU B: MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2026/27 KWA ROBO YA KWANZA 50

SURA YA NNE 54
VIPAUMBELE VYA MPANGO KWA MWAKA 2027/28 54
4.1 Utangulizi 54
4.2 Maeneo ya Kipaumbele ya Mpango 54
4.2.1 Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani 54
4.2.1.1 Utulivu na Utabirifu wa Uchumi Jumla 54
4.2.1.2 Kuimarisha Uwezo wa Kifedha wa Serikali 54
4.2.1.3 Uhimilivu na Usetushaji wa Sekta ya Nje 55

4.2.2 Mageuzi katika Sekta za Kimkakati 55
4.2.2.1 Sekta ya Kilimo.....55
4.2.2.2 Sekta ya Viwanda 55
4.2.2.3 Sekta ya Ujenzi.....56
4.2.2.4 Sekta ya Madini na Uchimbaji.....56
4.2.2.5 Sekta ya Mafuta na Gesi 56
4.2.2.6 Sekta ya Utalii 56
4.2.2.7 Sekta ya Fedha.....57
4.2.2.8 Sekta ya Michezo, Sanaa na Ubunifu 57
4.2.2.9 Maendeleo ya Makazi na Biashara ya Ardhi na Majengo.....57
4.2.2.10 Mageuzi ya Biashara na Shughuli za Kibiashara.....58
4.2.2.11 Kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi.....58
4.2.2.12Mikakati ya Ushirikiano kati ya Nchi, Kikanda na Kimataifa katika Dunia Inayobadilika 58
4.2.2.13 Urasimishaji wa Uchumi na Usimamizi Wake 59
4.2.3 Kujenga Uwezo wa Rasilimali Watu na Maendeleo ya Jamii 59
4.2.3.1 Jamii Iliyoelimika, Yenye Ujuzi na Inayojifunza 59
4.2.3.2 Nguvukazi Yenye Uwezo na Ari.....59
4.2.3.3 Demografia na Idadi ya Watu.....59
4.2.3.4 Soko na Taratibu za Ajira 60
4.2.3.5 Jamii Yenye Hifadhi na Muundo Jumuishi.....60
4.2.3.6 Huduma Bora za Afya kwa Wote.....60
4.2.3.7 Usalama wa Chakula na Lishe Ulioimarishwa.....61
4.2.3.8 Upatikanaji na Uunganishaji wa Maji na Usafi wa Mazingira ...61
4.2.3.9 Jamii yenye Mshikamano, Inayowajibika na Kushirikiana.....61
4.2.3.10 Maendeleo Jumuishi Vijijini.....62
4.2.3.11 Mageuzi ya Vyama vya Ushirika 62
4.2.3.12 Kupanua Tabaka la Kipato Cha Kati 62
4.2.4 Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi ..62
4.2.4.1 Uhifadhi wa Mazingira 62
4.2.4.2 Ukuaji Endelevu wa Miji Iliyopangika na Kusimamiwa Vizuri ...63
4.2.4.3 Mageuzi kwa Usimamizi Endelevu wa Ardhi.....63
4.2.4.4 Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi 63
4.2.4.5 Uwezo wa Taasisi na Mifumo ya Utoaji wa Tahadhari.....63
4.2.4.6 Kuimarisha ushiriki katika Biashara ya Kaboni.....63
4.2.4.7 Kuchagiza Manufaa ya Uchumi wa Buluu 64
4.2.5 Kutumia Kikamilifu Vichocheo vya Maendeleo 64
4.2.5.1 Nishati.....64
4.2.5.2 Mifumo ya usafirishaji na Uchukuzi Fungamanishi 64
4.2.5.3 Sayansi, Teknolojia na Ubunifu 64
4.2.5.4 Utafiti na Maendeleo 64
4.2.5.5 Matumizi ya Takwimu 65
4.2.5.6 Mapinduzi ya Kidijitali 65

4.2.5.7 Miundombinu na Huduma za TEHAMA.....65
4.2.5.8 Huduma za Mawasiliano na Posta 65
4.2.5.9 Mazingira Wezeshi ya Biashara na Uwekezaji.....65
4.2.6 Kuimarisha Misingi ya Uendelevu wa Taifa.....66
4.2.6.1 Utawala Bora, Demokrasia, Usalama na Utulivu.....66
4.2.6.2 Serikali za Mitaa Thabiti na Zenye Ufanisi 66
4.2.6.3 Matumizi Sahihi ya Takwimu.....66
4.2.6.4 Mabadiliko ya Mitazamo na Fikra 66
4.3 Programu za Kielelezo 66

SURA YA TANO 68
SEKTA BINAFSI 68
5.1 Utangulizi.....68
5.2 Mwenendo wa Mchango wa Sekta Binafsi 68
5.2.1 Mchango katika Uwekezaji 69
5.2.2 Mchango katika Uzalishaji 69
5.2.3 Mchango katika Ajira 70
5.2.4 Mchango katika Mauzo ya Nje.....70
5.3 Maeneo ya Kipaumbele ya Uwekezaji 70
5.4 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) 71
5.5 Mkakati wa Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Utekelezaji wa Mpango 72
5.6 Mfumo wa Ufuatiliaji wa Uwekezaji 72

SURA YA SITA 74
UGHARAMIAJI WA MPANGO..... 74
6.1 Utangulizi.....74
6.2 Mahitaji ya Rasilimali Fedha kwa Mwaka 2027/28 74
6.2.1 Vyanzo vya Mapato ya Serikali kwa Mwaka 2027/28 74
6.2.2 Uwekezaji wa Mashirika ya Umma.....74
6.2.3 Uwekezaji wa Sekta Binafsi 75
6.3 Vyanzo Bunifu na Mbadala 75

SURA YA SABA 77
USIMAMIZI WA UTELEKEZAJI NA UFUATILIAJI WA MATOKEO YA MPANGO 77
7.1 Utangulizi.....77
7.2 Ufuatiliaji, Tathmini na Matumizi ya Mfumo wa e-Delivery.....77
7.3 Utoaji na Matumizi ya Taarifa 77
7.4 Mgawanyo wa Majukumu ya Ufuatiliaji na Uwasilishaji wa Taarifa.....78

SURA YA NANE 79
VIHATARISHI VYA MPANGO KWA MWAKA 2027/28 NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO 79
8.1 Utangulizi 79
8.2 Maeneo ya Vihatarishi na Mikakati ya Kukabiliana navyo 79
8.2.1 Ufungamanishaji wa Vihatarishi na Mfumo wa e-Delivery 81
8.3 Ufuatiliaji na Udhibiti wa Vihatarishi 81
8.3.1 Viwango vya Uwezekano na Athari 82
8.3.2 Mzunguko wa Ufuatiliaji, Utoaji Taarifa na Kuwasilisha Maamuzi 82

KIAMBATISHO NA. I: AFUA ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2027/28 83

KIAMBATISHO NA. II: MAELEZO YA KINA KUHUSU PROGRAMU ZA KIELELEZO, MIRADI SHIKIZI, NA MAENEO YA MINYORORO YA THAMANI 261

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Dira 2050) imeweka mwelekeo wa muda mrefu wa kuifanya Tanzania kuwa Taifa Jumuishi Lenye Ustawi, Haki na Linalojitegemea. Katika kipindi cha miaka 25 ijayo, Dira 2050 inalenga kujenga uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu, ulio mseto, himilivu, jumuishi na shindani; kuboresha maisha na ustawi wa wananchi; kuhakikisha matumizi endelevu na yenye tija ya rasilimali za taifa; pamoja na kujenga jamii yenye ujuzi, ubunifu na uwezo wa kutumia teknolojia za kisasa katika kuongeza ushindani wa Taifa.

Ili kufikia malengo hayo, utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 wenye dhima ya "Mageuzi kwa ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji Ajira" unalenga kuweka mazingira na kutekeleza hatua zitakazowezesha Tanzania kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi, tija na ushindani, kuongeza uwekezaji, fursa za ajira na kipato kwa wananchi pamoja na kukuza uzalishaji.

Kwa kipindi cha mwaka 2027/28, Mpango wa Maendeleo wa Taifa ambao ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27-2030/31 utaweka mkazo katika kuongeza tija na thamani ya uzalishaji, kuimarisha ushindani wa bidhaa na huduma, kuchochea uwekezaji wa ndani na nje, kuongeza ushiriki wa sekta binafsi na kuboresha huduma za kijamii na ustawi wa wananchi. Aidha, maandalizi ya Mpango huu yamezingatia mafunzo muhimu yaliyotokana na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2026/27. Aidha, yamezingatia hali, mwenendo, na mazingira ya ndani, kikanda na kimataifa yanayoweza kuathiri ukuaji wa uchumi, biashara, uwekezaji, ajira, ustawi wa wananchi na uwezo wa kutekeleza vipaumbele vya maendeleo.

Hivyo, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 utaweka mkazo katika kuongeza tija na thamani ya uzalishaji, kuimarisha ushindani wa bidhaa na huduma, kuchochea uwekezaji wa ndani na nje na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi. Vilevile, Mpango unalenga kuendeleza miundombinu wezeshi, kukuza biashara na masoko, kuongeza fursa za ajira na kipato pamoja na kuboresha huduma za kijamii na ustawi wa wananchi.

1.2 Malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28

Mapendekezo haya yanatoa msingi wa maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28. Lengo kuu la Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 ni

kuendelea kutekeleza afua za kimkakati ili kuleta mageuzi kwa ajili ya ukuaji jumuishi wa uchumi na uzalishaji wa ajira.

Malengo mahsusi ya Mpango ni: kuimarisha ukuaji wa uchumi, mazingira ya biashara na uwekezaji; kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi; na kuongeza fursa za ajira na kipato. Kadhalika, kuchochea maendeleo ya watu na ustawi wa jamii; kuboresha miundombinu na kuendeleza vichocheo vya mageuzi; kuimarisha ustahimilivu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi; pamoja na kuimarisha utawala, uratibu na utekelezaji wa Mpango.

1.3 Mfumo wa Kusimamia Utekelezaji wa Matokeo

Utekelezaji wa Mpango 2027/28 utategemea mfumo wa uratibu wa kitaifa unaofungamanisha upangaji, uidhinishaji, ugharamiaji, utekelezaji, ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa kama ilivyoanishwa katika Mwongozo wa Kitaifa wa Uandaaji wa Mipango, Mwongozo wa Kitaifa wa Uidhinishaji wa Miradi, Mwongozo wa Kitaifa wa Upimaji wa Matokeo na Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo pamoja na Mfumo wa Usimamizi wa Miradi (e-Delivery).

Pamoja na miongozo iliyobainishwa, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 utatumia Mbinu ya Maabara (Lab Delivery Approach). Mbinu hii inalenga kufanya mageuzi katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kuleta matokeo makubwa na yanayopimika. FYDP IV imejengwa juu ya programu saba za kielelezo zinazotekelezwa kupitia miradi shikizi (anchor projects) inayohitaji rasilimali nyingi na uratibu wa karibu wa wadau wengi. Kwa kutumia mbinu ya maabara, kila eneo la kipaumbele litachambuliwa kwa kina, kubainisha mahitaji halisi ya rasilimali, muda, wahusika, na viashiria vinavyopimika vyenye kuleta matokeo tarajiwa na kuongeza uwajibikaji ili kufikia malengo makubwa yaliyowekwa katika Dira 2050 na Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP IV).

Ili kuimarisha uratibu na ufanisi, mfumo wa kitaasisi wa utekelezaji wa mpango umeainisha majukumu mahsusi ya taasisi za umma na wadau mbalimbali katika hatua za upangaji na utekelezaji. Mgawanyo huu unalenga kuondoa mwingiliano wa majukumu na kuimarisha uwajibikaji. Majukumu hayo ni kama ifuatavyo:

(i) Tume ya Taifa ya Mipango itaratibu maandalizi, uidhinishaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa lengo la kuhakikisha ufungamanishaji wa Dira 2050, Mpango wa IV, Mpango wa mwaka na mipango ya kisekta na kitaasisi.

(ii) Wizara ya Fedha itaratibu utafutaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele vya mpango pamoja na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

(iii) Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI itaratibu utekelezaji katika ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha vipaumbele vya kitaifa vinatafsiriwa katika mipango na bajeti za ngazi hizo.

(iv) Ofisi ya Msajili wa Hazina itakuwa na jukumu la kusimamia utendaji na usimamizi wa mashirika ya umma, hususan katika kuongeza ufanisi wa mashirika ya umma katika utekelezaji wa vipaumbele vya kitaifa.

(v) Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa: zitawajibika kutekeleza programu na miradi kwa mujibu wa majukumu yao, bajeti zilizoidhinishwa, viashiria vya utendaji na matokeo yaliyokusudiwa.

(vi) Sekta binafsi na washirika wa maendeleo watawajibika kutafasiri uwekezaji na ugharamiaji wa mipango yao kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa.

(vii) Mashirika ya kiraia (CSOs)—ikiwemo mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), mashirika ya kidini, na mashirika ya kijamii wataendelea kushirikiana na jamii kwa lengo la kufuatilia shughuli za Serikali zinazolenga kuchochea maendeleo ya watu na ustawi wa jamii.

1.4 Mawanda ya Mpango

Mawanda ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 yatazingatia maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV), kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa vipaumbele vya Taifa na kufikia matokeo tarajiwa ya kiuchumi na kijamii. Mpango utajikita katika vipaumbele vya uzalishaji, huduma za jamii na miundombinu katika ngazi ya Taifa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Utekelezaji utaelekezwa kwenye Programu za Kielelezo saba (7) za FYDP IV, kwa kuhakikisha miradi shikizi iliyobainishwa inaandaliwa na kutekelezwa kwa wakati kwa kuzingatia utayari wa miradi. Kwa msingi huo, Mpango huu utazingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika sekta za uzalishaji, kijamii na miundombinu katika ngazi zote za kitaifa, mikoa na halmashauri.

1.5 Mbinu za Uandaaji wa Mpango wa Mwaka 2027/28

Maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2027/28 yatatumia mbinu shirikishi, zinazotegemea ushahidi (evidence-based) na zinayozingatia matokeo. Mbinu hizo zitawezesha kubainisha vipaumbele vya Mpango 2027/28 vitafikiwa kikamilifu kama vilivyoainishwa katika Mpngo wa IV na Dira 2050. Kwa msingi huo, maandalizi ya Mpango yatahuisha majadiliano ya wadau mbalimbali kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta binafsi, Mashirika ya Umma na Washirika wa Maendeleo. Aidha, maandalizi ya mpango huu yatazingatia uchambuzi wa takwimu na ushahidi wa kiuchumi, kijamii na kimazingira pamoja na mapitio ya mipango ya maendeleo ya kitaifa, ajenda za kikanda na kimataifa ikiwemo Dira ya Jumuia ya Afrika Mashariki, Dira ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Ajenda 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na Ajenda 2063 ya Umoja wa Mataifa.

1.6 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2027/28

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2027/28 utahitaji mfumo wa uwekezaji na ugharamiaji wa sekta ya umma na sekta binafsi kwa kuzingatia uwiano wa 30:70 ulioanishwa katika Mpango wa IV. Serikali itazingatia uwezo halisi wa rasilimali zilizopo, uhimilivu wa deni la Serikali, thamani ya fedha na umuhimu wa kuelekeza

rasilimali katika maeneo yenye matokeo makubwa ya kiuchumi na kijamii. Kwa kuzingatia azma ya kuongeza nafasi ya sekta binafsi katika utekelezaji wa Dira 2050, Serikali itaendelea kuimarisha mifumo itakayowezesha sekta binafsi kushiriki katika uwekezaji na kugharamia utekelezaji wa miradi na programu za kimkakati.

Vyanzo vya mapato vitakavyotumika katika utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2027/28 ni kama ifuatavyo: mapato ya ndani ya kodi na yasiyo ya kodi, uwekezaji unaotokana na faida za mashirika ya umma; mikopo nafuu ya biashara na misaada; mitaji ya sekta binafsi kupitia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi pamoja na uwekezaji wa moja kwa moja wa ndani na kutoka nje Vilevile, vyanzo bunifu vya ufadhili ikiwemo hati fungani za kijani na za miundombinu vitatumika katika Mpango huu. Aidha, Benki ya Uwekezaji, Benki ya Kilimo, mifuko ya hifadhi ya jamii, kampuni za bima, benki za biashara, taasisi za fedha za maendeleo na masoko ya mitaji zitakuwa sehemu muhimu ya mfumo wa kukusanya rasilimali fedha kwa ajili ya kuwekeza katika sekta na miradi yenye umuhimu wa kimkakati.

1.7 Mpangilio wa Kitabu

Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 kimegawanyika katika sura nane (8). Sura ya kwanza ni utangulizi unaojumuisha usuli, malengo na mfumo wa utekelezaji na matokeo. Sura ya pili inawasilisha mapitio ya viashiria muhimu vya kiuchumi na kijamii na mwelekeo kwa mwaka 2027/28. Sura ya tatu inaelezea kwa muhtasari utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango ya Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Vile Vile, sura hii inaelezea uchambuzi na mapitio ya utekelezaji wa vipaumbele na programu zilizotekelezwa katika mwaka 2026/27. Sura ya nne inaainisha maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2027/28. Sura ya tano inaelekeza ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango 2027/28. Sura ya sita inabainisha mahitaji ya fedha, vyanzo vya fedha, mgawanyo wa rasilimali na mikakati ya kuongeza ufanisi na uendelevu wa ugharamiaji wa Mpango. Sura ya saba inafafanua mfumo wa kufuatilia utekelezaji, viashiria vya matokeo, majukumu ya taasisi, mifumo ya taarifa na taratibu za tathmini. Sura ya nane inajadili vihatarishi vya kiuchumi, kifedha, kimazingira, kiteknolojia na kiutendaji vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa Mpango, pamoja na hatua za kukabiliana navyo.

SURA YA PILI

HALI YA UCHUMI

2.1 Utangulizi

Sura hii inatoa tathmini ya mwenendo wa viashiria vya kiuchumi na kijamii katika ngazi ya dunia, kikanda, na kitaifa kwa mwaka 2025 na 2026, pamoja na matarajio kwa mwaka 2027. Uchambuzi wa viashiria vya hali ya uchumi ni muhimu katika kupanga maendeleo ya Taifa kwa kuwa unawezesha kutathmini ufanisi wa sera, mipango na mikakati ya maendeleo; kulinganisha mwenendo wa uchumi wa ndani na mazingira ya kikanda na kimataifa; kubaini maeneo yanayohitaji hatua za kisera; na kuweka msingi wa maamuzi ya kimkakati. Viashiria vilivyochambuliwa katika sura hii ni pamoja na Pato la Taifa, mfumuko wa bei, mwenendo wa sekta ya nje, sekta ya fedha, deni la Taifa, demografia na maendeleo ya watu.

2.2 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda

2.2.1 Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia umeendelea kukua licha ya changamoto mbalimbali, ikiwemo migogoro ya kikanda na kutotabirika kwa sera za biashara. Kwa mujibu wa taarifa ya *World Economic Outlook (WEO) Update* ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Oktoba 2026, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia ilikuwa asilimia 3.5 mwaka 2025. Hata hivyo, kasi ya ukuaji inatarajiwa kupungua hadi asilimia 3.1 mwaka 2026 kunatokana na athari za migogoro inayoendelea Mashariki ya Kati, ambayo imeongeza shinikizo katika bei za nishati, kuathiri minyororo ya ugavi na kudhoofisha mazingira ya biashara na uwekezaji duniani. Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajiwa kuongezeka na kufikia asilimia 3.4 mwaka 2027 kutokana na kuongezeka kwa mahitaji yanayochochewa na maendeleo na matumizi ya teknolojia, hususan ongezeko la uwekezaji unaohusishwa na maendeleo na matumizi ya teknolojia ya akili unde (Artificial Intelligence - AI).


Kwa upande wa Tanzania, kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia kunaweza kupunguza mtiririko wa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje, kudhoofisha mahitaji na bei za baadhi ya bidhaa zinazouzwa katika soko la dunia, kuongeza gharama za nishati na usafirishaji, pamoja na kupunguza upatikanaji wa misaada na mikopo yenye masharti nafuu. Ili kupunguza athari hizo na kutumia fursa zinazotokana na mabadiliko ya teknolojia duniani, Serikali itaendelea kuimarisha vyanzo vya ndani vya ukuaji wa uchumi, kupanua na kutofautisha masoko ya bidhaa na huduma, kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini, kuimarisha usalama wa nishati na minyororo ya ugavi, pamoja na kukuza uwekezaji wa ndani na matumizi ya teknolojia mpya kupitia ushiriki mpana wa sekta binafsi.

2.2.2 Uchumi wa Kikanda

Ukuaji wa uchumi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ulifikia asilimia 4.5 mwaka 2025. Hata hivyo, kasi ya ukuaji inatarajiwa kuimarika na kufikia asilimia 4.5 kwa mwaka 2026 na 2027. Pamoja na mwelekeo huo wa jumla, matarajio ya ukuaji yanatofautiana kati ya nchi na nchi kutokana na tofauti katika nafasi ya utekelezaji wa sera, kasi na ufanisi wa utekelezaji wa mageuzi ya kimuundo, pamoja na kiwango cha kuathiriwa na mishtuko kutoka nje. Nchi zinazoagiza mafuta na zile ambazo uchumi wake hautegemei kwa kiasi kikubwa rasilimali asilia zinatarajiwa kuathirika zaidi kutokana na ongezeko la bei za nishati na chakula, kupungua kwa misaada rasmi ya maendeleo (Official Development Assistance - ODA), pamoja na ushiriki mdogo katika fursa za ukuaji wa teknolojia duniani zinazochochewa na maendeleo na matumizi ya akili unde (Artificial Intelligence - AI). Hali hii inaonesha umuhimu wa nchi hizo kuimarisha uthabiti wa uchumi, kuongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali za ndani, kuharakisha mageuzi ya kimuundo na kupanua matumizi ya teknolojia ili kupunguza athari za mishtuko ya nje na kuendeleza ukuaji jumuishi.

Ukuaji wa uchumi wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ulikua kwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2025 na unatarajiwa kukua kwa kiwango hicho kwa mwaka 2026 na 2027. Kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 11.1 mwaka 2025 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.2 mwaka 2026 na asilimia 6.0 mwaka 2027. Aidha, kuimarika kwa uchumi kwa mwaka 2027 kunatarajiwa kuchangiwa na ukuaji imara nchini Uganda, Rwanda na Tanzania.


Kielelezo Na. 2.1: Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) Mwaka 2025 na Maoteo kwa mwaka 2026 na 2026



Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF)

*Takwimu za maoteo

Kielelezo Na. 2.2: Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Mwaka 2025 na Maoteo kwa Mwaka 2026 na 2027



Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa

*Takwimu za maoteo

***Katika kutoa taswira ya hali ya uchumi wa kikanda, mapitio na maoteo ya takwimu za Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) hutumika ili kufanya ulinganifu sahihi baina ya nchi za

kanda husika. Hivyo, katika eneo hili takwimu maoteo ya uchumi ya Tanzania yamezingatia maoteo ya IMF.

Aidha, utofauti wa takwimu za IMF na za ndani ya nchi unasababishwa na utofauti wa moduli zinazotumika katika kuandaa takwimu husika; viashiria vinavyotumika; na misingi (assumptions) iliyotumika katika maandalizi ya takwimu husika.

2.2.3 Mfumuko wa Bei wa Dunia

Kwa mujibu wa taarifa ya IMF ya Oktoba 2026, mfumuko wa bei wa dunia unategemea kuongezeka kutoka wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2025 hadi asilimia 4.7 mwaka 2026, kabla ya kupungua hadi asilimia 4.1 mwaka 2027. Ongezeko linalotarajiwa mwaka 2026 linatokana na kupanda kwa bei za nishati na chakula kufuatia athari za mgogoro wa Mashariki ya Kati. Aidha, mwenendo wa mfumuko wa bei unatofautiana kutokana na tofauti katika athari za mabadiliko ya kiwango cha ubadilishaji wa fedha kwenye bei za ndani, kuendelea kwa shinikizo la bei katika sekta ya huduma, hali ya masoko ya ajira na mazingira mahususi ya kila nchi.

2.2.4 Mfumuko wa Bei wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara

Kwa mujibu wa taarifa ya IMF ya Oktoba 2026, nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 12.6 mwaka 2025. Hali hiyo ya mfumuko wa bei ilitokana na sababu mbalimbali ikiwemo athari za kushuka kwa thamani ya fedha pamoja na uzalishaji usioridhisha katika shughuli za kilimo. Nchi zilizokuwa na mfumuko wa bei wa juu ni pamoja na Sudan Kusini (asilimia 97.6), Zimbabwe (asilimia 81.4), Burundi (asilimia 34), Malawi (asilimia 28.4), Nigeria (asilimia 23.0) na Angola (asilimia 20.2). Mfumuko wa bei katika ukanda huo unakadiriwa kupungua zaidi hadi asilimia 8.6 mwaka 2026 na 2027.

Aidha, wastani wa mfumuko wa bei katika nchi za SADC ulipungua hadi asilimia 10.5 mwaka 2025 kutoka asilimia 22.4 mwaka 2024. Mfumuko wa bei katika ukanda huo unakadiriwa kupungua zaidi hadi asilimia 6.1 mwaka 2026 na kuongezeka hadi asilimia 6.2 mwaka 2027 (**Jedwali Na. 2.1**)

Jedwali Na. 2.1 : Mwenendo wa Mfumuko wa Bei katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Nchi/ Miaka	2024	2025	2026 (Maoteo)	2027 (Maoteo)
Angola	28.2	20.2	10.6	10.2
Botswana	2.8	2.8	7.2	7.4
Comoros	5	3.2	4.0	3.2
DRC*	17.7	7.4	4.3	7.4

Nchi/ Miaka	2024	2025	2026 (Maoteo)	2027 (Maoteo)
Eswatini	4	3.1	2.9	3.2
Lesotho	5.2	4.4	4.6	3.9
Madagascar	7.6	8	8.4	8
Malawi	32.2	28.4	21.9	25
Mauritius	3.6	3.7	4.7	5.5
Namibia	4.2	3.5	4.1	4.2
Mozambique	3.2	4.4	5.6	6.8
Seychelles	0.3	0.3	0.9	2.3
Afrika ya Kusini	4.4	3.2	4.4	3.9
Tanzania	3.1	3.3	4.0	4.2
Zambia	15	13.9	8.0	7.5
Zimbabwe	736.1	81.4	4.0	5

*Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

Chanzo: Shirika la Fedha Duniani - IMF.

2.2.5 Mfumuko wa Bei katika Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki

Mfumuko wa bei katika nchi za EAC uliendelea kutofautiana mwaka 2025. Sudani Kusini ilirekodi kiwango cha juu zaidi cha wastani wa mfumuko wa bei cha asilimia 97.6, ikilinganishwa na asilimia 99.8 mwaka 2024. Nchi hiyo ilifuatiwa na Burundi ambapo mfumuko wa bei uliongezeka kutoka asilimia 20.2 mwaka 2024 hadi asilimia 34 mwaka 2025. Katika nchi nyingine wanachama, mfumuko wa bei ulikuwa DRC (asilimia 7.4), Rwanda (asilimia 7.0), Kenya (asilimia 4.1), na Uganda (asilimia 3.6). Tanzania imeendelea kudumisha utulivu wa bei, ambapo mwaka 2025 mfumuko wa bei umefikia wastani wa asilimia 3.3. Utulivu huu ulichangiwa na utekelezaji wa sera thabiti za fedha, utulivu wa soko la chakula na kupungua kwa bei za bidhaa katika masoko ya kimataifa. Hali hii inaonesha tofauti ya hali ya kiuchumi ndani ya ukanda wa EAC. Hata hivyo, baadhi ya nchi zinakabiliwa na shinikizo kubwa la bei na nyingine zimeendelea kudumisha uthabiti wa bei.

Jedwali Na. 2.2: Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Mwaka 2022 - 2025 na Maoteo kwa mwaka 2026

Nchi/ Miaka	2024	2025	2026 (Maoteo)	2027 (Maoteo)
Burundi	20.2	34	10.5	12.2
DRC*	17.7	7.4	4.3	7.4
Kenya	4.5	4.1	6.0	5.0
Rwanda	4.8	7	12.3	7.9
Sudani Kusini	99.8	97.6	27.6	28.3
Tanzania	3.1	3.3	4.0	4.2

Nchi/ Miaka	2024	2025	2026 (Maoteo)	2027 (Maoteo)
Uganda	3.3	3.6	4.2	5.3
Wastani	**19.9**	**20.2**	**7.2**	**10.043**

**Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo*

Chanzo: Shirika la Fedha Duniani – IMF

Katika kipindi cha kufikia Juni 2026, mfumuko wa bei katika nchi wanachama wa EAC kwa ujumla uliendelea kuwa ndani ya kiwango cha mtangamano kilichowekwa isipokuwa Rwanda. Aidha, nchi zote wanachama zilishuhudia ongezeko la mfumuko wa bei hali iliyochangiwa kwa kiasi kikubwa na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia kufuatia mgogoro wa Mashariki ya Kati.

Kielelezo 2.3: Mfumuko wa Bei katika Nchi Teule za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kipindi cha kufikia Juni 2026




2.3 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa

2.3.1 Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Taifa

Uchumi umeendelea kuonesha ukuaji mzuri, ambapo Pato la Taifa halisi lilikua kwa asilimia 5.9 mwaka 2025, ikilinganishwa na asilimia 5.6 mwaka 2024 (**Kielelezo Na. 2.3**). Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi; kuboreshwa kwa miundombinu ya usafirishaji; kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo na madini; kuongezeka kwa shughuli za ujenzi; pamoja na kuendelea kwa utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya Serikali na uwekezaji wa sekta binafsi, hususan katika sekta za nishati, usafirishaji na huduma za jamii.


Kielelezo 2.3: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Taifa, Mwaka 2021 - 2025



Chanzo: *Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)*

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2025, shughuli za kiuchumi zilizoongoza kwa ukuaji ni fedha na bima asilimia 15.7, uzalishaji umeme (asilimia 11.8) pamoja na uchimbaji madini na mawe (asilimia 9.4). Shughuli za kilimo ziliongoza kwa kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa kwa kuchangia asilimia 24.3, ikifuatiwa na ujenzi (asilimia 11.9), madini (asilimia 10.3), biashara na matengenezo (asilimia 8.6), na usafirishaji na uhifadhi mizigo (asilimia 8.3) (Kielelezo Na. 2.4).


Kielelezo 2.4: Mchango wa Baadhi ya Shughuli za Kiuchumi Katika Pato la Taifa, Mwaka 2021-2025



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Katika robo ya kwanza ya mwaka 2026, Pato la Taifa halisi lilikua kwa asilimia 6.0, ikilinganishwa na asilimia 4.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2025 (Kielelezo Na. 2.5). Muundo wa uchumi uliendelea kuwa kwa kiasi kikubwa bila mabadiliko, ambapo shughuli za kilimo na ujenzi kwa pamoja zilichangia takriban theluthi moja ya Pato la Taifa. Ukuaji wa uchumi katika kipindi hicho ulichangiwa zaidi na shughuli za kilimo na huduma za fedha na bima, ambazo zilichangia ukuaji kwa asilimia 16.8 na asilimia 16.7 mtawalia. Huduma za fedha na bima ziliongoza kwa kuwa na kiwango cha juu zaidi cha ukuaji cha asilimia 20.5 kutokana na kuendelea kuongezeka kwa matumizi ya bidhaa na huduma za kifedha, zikifuatiwa na huduma za afya na ustawi wa jamii zilizokua kwa asilimia 13.1 na elimu kwa asilimia 11.3. Tathmini ya mwenendo wa Pato la Taifa katika robo ya kwanza na mwenendo wa viashiria vingine vya uchumi katika nusu ya kwanza ya mwaka 2026 inaonesha kuwa uchumi unaendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha. Hivyo, uchumi unatarajiwa kukua kwa makadirio ya asilimia 6.3 mwaka 2026 na asilimia 6.6 mwaka 2027 kulingana na mwelekeo uliowekwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27-2030/31).

Kielelezo Na. 2.5: Mwenendo wa Uchumi wa Taifa kwa Robo ya Kwanza ya Mwaka 2026




Chanzo: *Wizara ya Fedha*

2.3.2 Mfumuko wa Bei Nchini

Mfumuko wa bei nchini uliendelea kubaki katika kiwango cha chini na himilivu katika mwaka 2025/26, ambapo ulifikia wastani wa asilimia 3.6 ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2024/25 (Kielelezo Na. 2.6). Mwenendo huo ulichangiwa na utekelezaji wa sera thabiti za kibajeti na fedha, pamoja na kupungua kwa kasi ya ongezeko la bei za bidhaa zisizo za chakula. Hata hivyo, katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2026, mfumuko wa bei ulivuka asilimia 4.0 kwa mara ya kwanza tangu Mei 2023, kutokana zaidi na kuongezeka kwa bei za nishati katika soko la dunia kufuatia kuongezeka kwa migogoro Mashariki ya Kati. Mabadiliko ya bei za nishati duniani yaliathiri bei za mafuta katika soko la ndani na kuongeza bei za bidhaa na huduma nyingine, hususan kupitia ongezeko la gharama za usafirishaji. Aidha, mwezi Agosti, 2026 mfumuko wa bei ulifikia asilimia 4.3.

Pamoja na ongezeko hilo, mfumuko wa bei uliendelea kuwa ndani ya lengo la kitaifa la muda wa kati la asilimia 3.0 hadi 5.0, wigo wa mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki usiozidi asilimia 8.0, na kigezo cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika cha asilimia 3.0 hadi 7.0.

Kielelezo Na. 2.6: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Nchini, Mwaka 2023 hadi 2026.



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)

2.3.3 Sekta ya Nje

Sekta ya nje iliendelea kuwa himilivu mwaka 2025/26 licha ya changamoto katika mazingira ya uchumi wa dunia. Kuendelea kwa mgogoro wa Mashariki ya Kati kuliongeza shinikizo katika bei za nishati na gharama za usafirishaji wa mizigo. Pamoja na changamoto hizo, mauzo ya bidhaa na huduma nje yaliendelea kukua kwa kasi, yakichangiwa na bei nzuri ya dhahabu katika soko la dunia, kuendelea kuimarika kwa sekta ya utalii na kuongezeka kwa biashara ya kikanda. Hata hivyo, uagizaji wa bidhaa na huduma uliongezeka kwa kasi kuliko mauzo ya nje kutokana na mahitaji makubwa ya malighafi za viwandani, bidhaa za petroli na bidhaa za mitaji, pamoja na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji. Kutokana na mwenendo huo, nakisi ya urari wa malipo ya kawaida iliongezeka kwa asilimia 8.8, kutoka dola za Marekani milioni 2,178.9 mwaka 2024/25 hadi dola za Marekani milioni 2,370.4 mwaka 2025/26.

Mwaka 2026/27, nakisi ya urari wa malipo ya kawaida inatarajiwa kupungua hadi asilimia 2.4 ya Pato la Taifa kutoka asilimia 2.5 mwaka 2025/26, na kufikia wastani wa asilimia 2.3 katika kipindi cha muda wa kati. Matarajio hayo yanatokana na uagizaji wa bidhaa na huduma kutarajiwa kukua kwa kasi ndogo ikilinganishwa na mauzo ya bidhaa na huduma nje. Mauzo ya nje yanatarajiwa kuendelea kuimarika kutokana na bei nzuri ya dhahabu, kuongezeka kwa mapato ya utalii na kupanuka kwa biashara ya kikanda. Mwenendo huo

unatarajiwa kupunguza shinikizo katika urari wa malipo ya kawaida na kuimarisha ustahimilivu wa sekta ya nje katika kipindi cha muda wa kati.

(a) Mwenendo wa Mauzo ya Bidhaa Nje na Mapato ya Huduma

Mwaka 2025/26, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 15.5 na kufikia dola za Marekani milioni 19,625.0, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 16,987.0 mwaka 2024/25. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuimarika kwa mauzo ya dhahabu, mapato ya huduma za utalii, bidhaa za viwandani na bidhaa asilia, hususan tumbaku, korosho na kahawa.

Katika kipindi hicho, mauzo ya dhahabu nje ya nchi yalifikia dola za Marekani milioni 5,578.9, sawa na ongezeko la asilimia 37.8 ikilinganishwa na mwaka 2024/25. Dhahabu iliendelea kuwa chanzo kikuu cha mapato ya mauzo ya bidhaa na huduma nje kwa kuchangia asilimia 28 ya mapato yote ya mauzo ya nje. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na bei nzuri ya dhahabu katika soko la dunia na kuimarika kwa mauzo ya bidhaa za viwandani na bidhaa asilia hususan tumbaku, korosho na kahawa.

Mapato yatokanayo na huduma zinazotolewa nje yaliongezeka kwa asilimia 12.0 na kufikia dola za Marekani milioni 7,971.5 mwaka 2025/26, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 7,115.4 mwaka 2024/25. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kuimarika kwa mapato ya huduma za utalii, ambayo yaliongezeka kwa asilimia 5. Mwenendo huo uliendana na ongezeko la asilimia 4.5 la idadi ya watalii walioingia nchini na kufikia watalii 2,291,479 mwaka 2025/26.

Mwaka 2026/27, uwiano wa mauzo ya bidhaa na huduma nje kwa Pato la Taifa unatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 21.1 kutoka asilimia 20.3 mwaka 2025/26. Ongezeko hilo linatarajiwa kuchangiwa na kuendelea kuimarika kwa sekta ya utalii na mauzo ya dhahabu, pamoja na kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji viwandani kufuatia kukamilika kwa Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) na kuongezeka kwa upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa shughuli za uzalishaji. Aidha, uwiano wa mauzo ya bidhaa na huduma nje kwa Pato la Taifa unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 20.4 katika kipindi cha muda wa kati.

(b) Mwenendo wa Uagizaji wa Bidhaa na Huduma

Thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka kwa asilimia 15.1 mwaka 2025/26 na kufikia dola za Marekani milioni 20,285.7, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 17,629.8 mwaka 2024/25. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa uagizaji wa vifaa vya usafirishaji kwa ajili ya shughuli za viwandani, mitambo na vifaa vya kimakanika, malighafi za viwandani na bidhaa za petroli. Katika kipindi hicho, thamani ya bidhaa pekee zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka kwa asilimia 16.5 na kufikia dola za Marekani milioni 16,858.1, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 14,465.9 mwaka 2024/25.

Malipo ya huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 8.3 na kufikia dola za Marekani milioni 3,427.5 mwaka 2025/26, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,163.9 mwaka 2024/25. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kupanda kwa malipo ya usafirishaji wa mizigo, sambamba na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje.

Mwaka 2026/27, uwiano wa uagizaji wa bidhaa na huduma kwa Pato la Taifa unatarajiwa kubaki katika asilimia 21.0, sawa na kiwango cha mwaka 2025/26. Katika kipindi cha muda wa kati, uwiano huo unatarajiwa kupungua hadi wastani wa asilimia 19.9 kutokana na uagizaji wa bidhaa na huduma kutarajiwa kukua kwa kasi ndogo baada ya kukamilika kwa baadhi ya miradi mikubwa ya kimkakati.

2.3.4 Akiba ya Fedha za Kigeni

Hadi Agosti 2026, akiba rasmi ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,888.2. Kiasi hicho kilitosheleza kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi 4.2, kiwango ambacho kilikuwa juu ya lengo la nchi la kuwa na akiba inayotosheleza uagizaji kwa angalau miezi minne. Utoshelevu wa akiba hiyo ulichangiwa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi pamoja na kuendelea kutekelezwa kwa programu ya Benki Kuu ya ununuzi wa dhahabu katika soko la ndani.

2.3.5 Sekta ya Fedha


Katika mwaka 2026/27, Benki Kuu inatarajia kutekeleza sera ya fedha inayolenga kupunguza ukwasi ili kudhibiti athari za awamu ya pili za kupanda kwa bei za bidhaa duniani, sambamba na kuendeleza mageuzi ya kuelekea uchumi unaopunguza matumizi ya fedha taslimu (cash-lite economy) na kuongeza ujumuishaji wa kifedha. Sanjari na hili, mnamo mwezi Julai 2026, Kamati ya Sera ya Fedha iliamua kuongeza Kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) kutoka asilimia 5.75 ya mwezi Juni 2026 hadi asilimia 6.25 kwa robo mwaka inayoishia Septemba 2026 kabla ya kuamua kutokubadili riba hiyo katika kikao kilichofanyika mwezi Oktoba 2026. Uamuzi huu unalenga kudhibiti athari zinazoweza kutokana na ongezeko la bei za mafuta, mbolea na gharama za usafirishaji kutokana na mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati. Kwa muktadha huo, utekelezaji wa sera ya fedha umeendelea kuhakikisha riba ya mikopo ya siku saba baina ya mabenki (7-day IBCM rate) inabaki ndani ya wigo wa asilimia 4.75 hadi asilimia 7.75, sawa na asilimia 1.5 juu au chini ya Riba ya Benki Kuu.

Hadi kufikia mwezi Septemba 2026, utekelezaji wa sera ya fedha ulikuwa wa kuridhisha, huku ukihakikisha uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi katika sekta ya kibenki. Hali hii iliakisiwa na mwenendo wa riba ya mikopo ya siku saba baina ya mabenki ambayo ilikuwa tulivu ikiwa, na ndani ya wigo unaokubalika. Aidha, Benki Kuu imeendelea kusimamia ukwasi katika mfumo wa kibenki kwa kutumia mikopo ya muda mfupi "reverse repo" na mauzo ya dhamana za serikali za muda mfupi.

(a) Viwango vya Riba

Katika mwaka 2025/26, riba za mikopo na amana zilibaki bila mabadiliko makubwa ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Wastani wa riba za mikopo ulipungua hadi asilimia 15.19 kutoka asilimia 15.42 mwaka 2024/25. Mwenendo huo uliakisi utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kuongeza ukwasi katika mzunguko wa fedha. Aidha, wastani wa riba za amana uliongezeka hadi asilimia 8.49 kutoka asilimia 8.22 mwaka 2024/25. Kutokana na mwenendo huo, tofauti kati ya wastani wa riba za mikopo na amana ilipungua hadi nukta za asilimia 6.70 mwaka 2025/26 kutoka nukta za asilimia 7.20 mwaka 2024/25, hali inayoashiria kupungua kwa kiasi kwa gharama za mikopo ikilinganishwa na mapato yatokanayo na amana (**Kielelezo 2.7**).

Kielelezo Na. 2.7: Wastani wa Viwango vya Riba za Mikopo na Amana



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania


(b) Mikopo kwa Sekta Binafsi

Katika mwaka ulioishia Juni 2026, mikopo iliyotolewa na benki za biashara kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 21.1, ikilinganishwa na asilimia 15.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Hadi kufikia mwezi Agosti 2026, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 33, ikilinganishwa na asilimia 28.1 ya mwezi Juni, 2026. Ongezeko hilo liliakisi utekelezaji wa sera za fedha na bajeti zinazochochea shughuli za kiuchumi, pamoja na kuendelea kuimarika kwa shughuli za uzalishaji na biashara nchini.

Katika mwaka 2025/26, mikopo iliyoelekezwa katika shughuli za uchimbaji wa madini na mawe iliongoza kwa kukua kwa asilimia 45.2, hali iliyochangiwa zaidi na utekelezaji wa jitihada za Serikali za kuboresha upatikanaji wa fedha kwa wachimbaji wadogo na wa kati. Mikopo kwa shughuli za biashara, uchukuzi na mawasiliano, pamoja na kilimo, pia ilikua kwa zaidi ya asilimia 30 kwa kila shughuli. Aidha, mikopo kwa watu binafsi, ambayo kwa sehemu kubwa hutumika kugharamia shughuli za uzalishaji za biashara ndogo na za kati,


iliendelea kuchukua sehemu kubwa zaidi ya mikopo kwa sekta binafsi kwa kuchangia asilimia 35.5, ikifuatiwa na biashara kwa asilimia 14.5 na kilimo kwa asilimia 13.7. **Kielelezo Na. 2.9** kimeainisha mchanganuo wa mikopo kwa sekta binafsi.

Kielelezo Na. 2.9a: Mchanganuo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi



Chanzo: Benki kuu ya Tanzania

Kielelezo Na. 2.9b: Mchanganuo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi



Chanzo: Benki kuu ya Tanzania

(c) Ukwasi na Faida za Biashara katika Benki

Hali ya ukwasi katika sekta ya benki iliendelea kuwa ya kuridhisha na juu ya kiwango cha chini kinachohitajika kisheria. Uwiano wa ukwasi (Liquidity Coverage Ratio - LCR) ulikuwa asilimia 232.86 Juni 2026, ikilinganishwa na asilimia 255.24 Juni 2025, na hivyo kuendelea kuwa juu ya kiwango cha chini cha kisheria cha asilimia 100. Aidha, uwiano wa mtaji wa msingi kwa rasilimali zilizopimwa kwa vihatarishi pamoja na shughuli zilizo nje ya mizania ulikuwa asilimia 18.57 Juni 2026, ikilinganishwa na asilimia 18.69 Juni 2025, na kuendelea kuwa juu ya kiwango cha chini cha kisheria cha asilimia 10. Hali hii inaonesha kuwa benki zilikuwa na ukwasi na mtaji wa kutosha kugharamia shughuli zake za kila siku, ikiwemo kutoa mikopo.

Mapato ya benki yatokanayo na rasilimali (Return on Assets - ROA) yalikuwa asilimia 4.88 Juni 2026, ikilinganishwa na asilimia 5.36 Juni 2025. Vilevile, mapato yatokanayo na mtaji (Return on Equity - ROE) yalikuwa asilimia 23.29 Juni 2026, ikilinganishwa na asilimia 24.96 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Pamoja na kupungua kwa kiasi kwa viashiria hivyo vya faida, sekta ya benki iliendelea kuwa himilivu na yenye uwezo wa kutengeneza faida.

2.3.6 Deni la Serikali

Hadi kufikia Juni 2026, deni la Serikali Kuu lilifikia shilingi bilioni 117,384.01 kutoka shilingi bilioni 109,441.30 mwezi Juni 2025, sawa na ongezeko la asilimia 7.2. Kati ya kiasi hicho, deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 78,058.16, sawa na asilimia 66.5 ya deni lote, na deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 39,325.85. Ongezeko la deni lilitokana na mikopo mipya kuzidi marejesho ya mikopo iliyoiva, pamoja na kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani.

Uhimilivu wa Deni

Tathmini ya uhimilivu wa deni ya Novemba 2025 ilionesha kuwa deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda wa kati na mrefu. Katika mwaka 2025/26, thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ilikuwa asilimia 24.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ilikuwa asilimia 123.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180; malipo ya deni la nje kwa mapato yatokanayo na mauzo ya nje yalikuwa asilimia 12.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 15; na malipo ya deni la nje kwa mapato ya ndani yalikuwa asilimia 15.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 18. Aidha, thamani ya sasa ya jumla ya deni la ndani na nje kwa Pato la Taifa ilikuwa asilimia 39.6 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55.

Uwezo wa Nchi Kukopa na Kulipa Madeni katika Masoko ya Kimataifa

Mwezi Februari 2026, Moody's Ratings iliendelea kuipa Tanzania daraja la B1 lenye mtazamo thabiti (Stable Outlook), kutokana na ukuaji imara wa uchumi, uthabiti wa mfumuko wa bei, maboresho katika usimamizi wa sera za uchumi na deni la Serikali

linaloendelea kuwa himilivu. Aidha, mwezi Agosti 2026, Fitch Ratings iliithibitisha Tanzania katika daraja la B+ na kuboresha mtazamo wa nchi kutoka thabiti (Stable) kwenda chanya (Positive), kutokana na kuimarika kwa uhimilivu wa deni la umma na sekta ya nje, pamoja na kuboreka kwa mtazamo na uaminifu wa sera za uchumi. Matokeo hayo yanaweza kuimarisha imani ya wawekezaji na wakopeshaji kuhusu uthabiti wa uchumi na uwezo wa Serikali kuhudumia deni, na hivyo kuboresha upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

2.3.7 Demografia na Maendeleo ya Watu

2.3.7.1 Demografia

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) idadi ya watu inakadiriwa kufikia milioni 67.9 mwaka 2026 na milioni 69.7 mwaka 2027 kwa Tanzania Bara. Kasi ya ongezeko la idadi ya watu inatoa fursa chanya zikiwemo uwepo wa nguvu kazi ya kutosha pamoja na misingi ya kuchochea mageuzi ya kidigitali katika shughuli mbalimbali za uzalishaji kutokana na uwepo wa kundi kubwa la vijana wenye umri wa miaka 15-35 ambao ni asilimia 33.7 ya watu wote Tanzania Bara kwa mwaka 2027. Aidha, ongezeko hili linaashiria uhitaji wa kuwekeza zaidi katika huduma za kijamii pamoja na mageuzi katika mifumo mbalimbali ya elimu na utendaji pamoja na kutekeleza mikakati mahsusi ya kuwawezesha vijana kuzalisha kwa tija. Utekelezaji wa mikakati hii utawezesha rasilimali watu ya nchi kuwa shindani kimataifa hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi.

2.3.7.2 Hali ya Umaskini Nchini

Serikali imeendelea kutekeleza hatua mbalimbali zinazolenga kuimarisha ustawi wa jamii, kupunguza umaskini na kuongeza fursa za kiuchumi kwa wananchi. Hatua hizo zinajumuisha kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za msingi, hususan maji, elimu na afya; kuendeleza miundombinu ya nishati, usafiri na barabara; pamoja na kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji na kupata fursa za kiuchumi ili kufikia shabaha za FYDP IV za kupunguza kiwango cha umaskini hadi chini ya asilimia 15 ifikapo mwaka 2030/31.

Taarifa ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi Tanzania wa mwaka 2025 inabainisha kuwa asilimia 24.9 ya watu nchini wanaishi katika umaskini wa mahitaji ya msingi. Kiwango hicho ni asilimia 25.1 kwa Tanzania Bara na asilimia 19.9 kwa Tanzania Zanzibar. Kwa Tanzania Bara, kiwango cha umaskini kimepungua kutoka asilimia 34.4 mwaka 2007 hadi asilimia 28.2 (mwaka 2012), asilimia 26.4 (mwaka 2017/18) na asilimia 25.1 (mwaka 2025). Aidha, kiwango cha umaskini ni kikubwa zaidi vijijini ambapo asilimia 30.7 ya watu wa Tanzania Bara wanaishi katika umaskini wa mahitaji ya msingi, ikilinganishwa na asilimia 14.8 mijini. Kwa upande wa kina cha umaskini, pengo la umaskini (poverty gap) nchini ni asilimia 6.2 na ukali wa umaskini (poverty severity) ni asilimia 2.2. Vile vile, utafiti unaonesha kuwa utofauti wa kipato na matumizi bado ni mkubwa, ambapo kipimo cha gini ni 0.42 nchini, ambapo Tanzania Bara (0.41) na Tanzania Zanzibar (0.44). Matokeo haya yanaonesha umuhimu wa kuchochea ukuaji wa uchumi jumuishi, kuongeza ajira zenye tija na kipato, pamoja na kuongeza tija katika

kilimo na shughuli nyingine za uchumi vijijini. Afua hizi ni muhimu ili kuwezesha Tanzania kufikia lengo lililowekwa katika DIRA 2050 la kuondoa umaskini uliokithiri na kupunguza umaskini wa mahitaji ya msingi kuwa chini ya asilimia 5.

2.3.7.3 Ajira

Matokeo ya Utafiti wa Watu wenye Uwezo wa Kufanya Kazi – ILFS wa mwaka 2025 yanabainisha kuwa, kiwango cha Ushiriki wa Nguvu kazi (Labour Force Participation Rate) kimefikia asilimia 75.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 73.2 mwaka 2024. Idadi kubwa ya nguvu kazi ikiwa imeajiriwa kwa masharti ya muda (dependent contractors) kwa asilimia 51.5 na asilimia 13.2 zikiwa ni ajira zenye ujira wa kulipwa mishahara. Sekta ya Kilimo imeendelea kuwa uti wa mgongo kwa kuajiri takriban asilimia 54.4 ya nguvu kazi mwaka 2025 ikifuatiwa na sekta ya huduma (asilimia 35.5), na kiwango cha nguvu kazi kilichoajiriwa katika sekta ya viwanda ni asilimia 10.1 mwaka 2025.

Kwa upande wa kiwango cha ukosefu wa ajira kimepungua na kufikia asilimia 5.9 mwaka 2025, ukilinganisha na asilimia 6.2 mwaka 2024. Aidha, kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana (miaka 15 – 35) kimepungua hadi asilimia 7.5 mwaka 2025 kutoka asilimia 8.1.

2.3.7.4 Maendeleo ya Watu

Serikali imeendelea na jitihada za kuboresha maendeleo ya watu kwa lengo la kuimarisha maisha ya watu ili kufikia matamanio yaliyoainishwa katika Dira 2050. Juhudi hizo ni pamoja na: kuendelea kutoa elimu bila ada; kuendelea kuboresha upatikanaji wa maji mijini na vijijini; kuendelea kuboresha ushiriki wa sekta binafsi katika kutoa huduma za afya hususan maeneo ya vijijini; kuendelea na ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali; na kuendelea na ujenzi wa barabara za kufungua fursa za kiuchumi katika maeneo ya mijini na vijijini. Kutokana na utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo, kumekua na matokeo chanya katika viashiria vya maendeleo ya watu [1] ikiwemo:

(i) Kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 68.0 mwaka 2024 hadi miaka 68.3 mwaka 2025. Aidha, wastani wa umri wa kuishi kwa kuzingatia jinsia, umefikia miaka 70.7 kwa wanawake na miaka 65.9 kwa wanaume mwaka 2025; Hii ni kwa mujibu wa makadirio yaliyotakana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022;

(ii) Kupungua kwa vifo vya watoto wa umri chini ya miaka mitano na kufikia vifo 43 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2022 kutoka vifo 81 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2019/20;

(iii) Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2019/20 hadi vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022;

(iv) Kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya sekondari kutoka asilimia 47.4 mwaka 2021 hadi asilimia 53.1 mwaka 2025;

[1] Kutofautiana kwa vipindi vya ulinganifu na kutobadilika kwa takwimu kunatokana na baadhi ya viashiria kutumia tafiti kuzalisha takwimu husika.

(v) Kuongezeka kwa idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba kama chanzo kikuu kutoka asilimia 72.3 mwaka 2020/21 hadi asilimia 83 mwaka 2024/25;
(vi) Kuunganishwa na huduma ya umeme kwa vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara mwaka 2026/27 na kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa kuunganisha vitongoji vyote nchini;
(vii) Fahirisi ya maendeleo ya watu imefikia 0.556 mwaka 2024 kutoka 0.529 mwaka 2019, fahirisi hii inaashiria kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za jamii za muhimu kama vile afya, elimu na maji pamoja na kuimarika kwa kiwango cha maisha. Hii ni kwa mujibu wa taarifa za UNDP.

2.4 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2027/28

Uchumi wa Tanzania unatarajiwa kuendelea kukua kwa wastani wa asilimia 6.3 mwaka 2026 na asilimia 6.6 kwa mwaka 2027. Ukuaji huu utachangiwa na uwekezaji katika sekta za mageuzi na maeneo yanayochochea mageuzi ya kiuchumi ili kufikia malengo ya Dira 2050. Hili kufikia matarajio ya ukuaji wa uchumi Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2027/28 yanajielekeza katika maeneo sita (6) mahsusi:

(i) Kujenga Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani;
(ii) Mageuzi katika sekta za Kimkakati
(iii) Kujenga uwezo wa Rasimali Watu na Maendeleo ya Jamii;
(iv) Kuhifadhi mazingira na kujenga ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi;
(v) Kutumia kikamilifu vichocheo vya maendeleo; na
(vi) Kuimarisha Misingi ya Uendelevu wa Taifa.

2.4.1 Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi Jumla

Malengo na shabaha za msingi za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 6.3 na 6.6 kwa mwaka 2026 na 2027 mtawalia, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.9 kwa mwaka 2025;
(ii) Kudhibiti mfumuko wa bei kubaki katika wigo wa asilimia 3.0 – 5.0 katika kipindi cha muda wa kati, ili kulinda uwezo wa wananchi kumudu mahitaji muhimu;
(iii) Kuongeza mapato ya ndani kufikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa mwaka 2027/28, kutoka asilimia 17.0 mwaka 2026/27;
(iv) Kuongeza mapato ya kodi kufikia asilimia 13.9 ya Pato la Taifa mwaka 2027/28, kutoka asilimia 13.8 mwaka 2026/27;
(v) Kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa mwaka 2027;
(vi) Kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na
(vii) Kuongeza uzalishaji wa wastani wa ajira 1,700,000 kwa mwaka 2027.

Maoteo ya ajira zinazotarajiwa kuzalishwa mwaka 2027/28 yanaonesha kuwa kati ya lengo la ajira mpya milioni 1.7, sekta ya kilimo, misitu, na uvuvi inatarajiwa kuongoza kwa kuzalisha ajira 935,000 sawa na asilimia 55 ya ajira zote; ikifuatiwa na biashara jumla, rejareja pamoja na matengenezo ya magari na pikipiki (261,800); Utengenezaji (91,800);

Huduma za malazi na chakula (78,200); Usafirishaji na uhifadhi (74,800). Kwa ujumla, maoteo haya yanaakisi mabadiliko ya kimuundo yanayolenga kukuza ajira kupitia sekta za kimageuzi na huduma zenye athari pana katika uchumi.

Jedwali Na. 2.3: Mchanganuo wa Maoteo ya Fursa za Ajira Zitakazozalishwa katika Mwaka 2027/28

Shughuli za Kiuchumi	Idadi	Asilimia
Kilimo, misitu na uvuvi	935,000	55.00
Uchimbaji wa madini na michanga	20,400	1.20
Utengenezaji	91,800	5.40
Umeme, gesi, mvuke na viyoyozi	3,400	0.20
Usambazaji wa maji, majitaka, na usimamizi wa taka	1,700	0.10
Ujenzi	51,000	3.00
Biashara jumla, rejareja pamoja na matengenezo ya magari na pikipiki	261,800	15.40
Usafirishaji na uhifadhi	74,800	4.40
Huduma za malazi na chakula	78,200	4.60
Habari na mawasiliano	4,250	0.25
Shughuli za kifedha na bima	8,840	0.52
Shughuli za mali isiyohamishika	1,700	0.10
Shughuli za kitaalamu, kisayansi na uhandisi	3,230	0.19
Shughuli za utoaji wa huduma mbalimbali	52,700	3.10
Utawala wa umma na ulinzi na shughuli za hifadhi ya jamii	8,500	0.50
Elimu	30,600	1.80
Afya ya binadamu na shughuli za kijamii	12,070	0.71
Sanaa burudani na starehe	5,100	0.30
Shughuli nyingine za utoaji wa huduma	12,410	0.73
Shughuli za kaya kama muajiri	42,500	2.50
Jumla	**1,700,000**	**100.00**

2.4.2 Misingi ya Mpango kwa Mwaka 2027/28

Ufanisi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2027/28 utajengwa katika misingi ifuatayo:

(i) Kuendelea kuwepo kwa demokrasia, amani, usalama na utulivu wa ndani na katika nchi jirani, inayowezesha shughuli za kiuchumi, kijamii na uwekezaji kustawi;

(ii) Kudumisha misingi ya utawala bora na utawala wa sheria, ikiwa ni pamoja na uwajibikaji, uadilifu, uwazi na ufanisi katika matumizi bora na endelevu ya rasilimali za umma;

(iii) Kuendeleza miundombinu wezeshi hususan nishati, bandari, barabara na reli kwa ili kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara, viwanda na usafirishaji katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na Kusini;

(iv) Kuimarika kwa ubunifu na matumizi ya teknolojia za kidijitali katika huduma za kijamii na uzalishaji;

(v) Utekelezaji wa mageuzi ya kitaasisi na kiutawala ili kuongeza ufanisi, uwazi, uwajibikaji na tija katika utekelezaji wa majukumu;

(vi) Kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji na biashara kupitia ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na fursa zinazotokana na ushirikiano wa kikanda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika;

(vii) Kuendelea kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, majanga ya asili na yasiyo ya asili, ikiwemo ukame, mafuriko, milipuko ya magonjwa, migogoro ya kikanda na misukosuko ya kiuchumi duniani;

(viii) Kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa;

(ix) Kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini; na

(x) Kuwepo kwa mifumo thabiti ya uratibu, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha kuwa programu, miradi na afua zilizopangwa zinatekelezwa kwa wakati na kuleta matokeo yanayotarajiwa.

SURA YA TATU

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO

3.1 Utangulizi

Sura hii inaainisha mapitio ya utekelezaji wa Mpango ambayo yanalenga kupima hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa afua, programu na miradi iliyopangwa, kwa lengo la kubaini mafanikio na maeneo yanayohitaji hatua za ziada, pamoja na kuweka msingi wa vipaumbele vya Mpango wa mwaka 2027/28. Mapitio ya utekelezaji wa Mpango yamegawanyika katika sehemu kuu mbili (02) ambazo ni sehemu A na sehemu B. Sehemu A inahusu mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2025/26 ambao ni Mpango wa Tano na wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III). Vilevile, Mpango wa Mwaka 2025/26 ni Mpango wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Aidha, Sehemu B inahusu mapitio ya robo ya kwanza (Julai – Septemba 2026) ya Mpango wa Mwaka 2026/27 ambao ni Mpango wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV) na ni Mpango wa Kwanza wa mwaka katika utekelezaji wa Dira 2050.

SEHEMU A: UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA 2025/26

Sehemu hii inaeleza mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26. Mapitio hayo yamejikita katika miradi ya kielelezo na miradi ya kimkakati. Vilevile, sehemu hii inaonesha matokeo ya utekelezaji wa afua na miradi pamoja na viashiria vya mpango kwa kulinganisha hatua iliyofikiwa mwaka 2025/26 na hatua ya utekelezaji kwa mwaka 2024/25.

Miradi ya Kielelezo

Hadi Juni 2026, Serikali ilifanikiwa kukamilisha ufungaji wa mitambo yote tisa (9) ya Bwawa la Julius Nyerere (MW 2,115) na kuunganisha umeme wake katika Gridi ya Taifa; kukamilisha madaraja ya JPM (Kigongo – Busisi) na Tanzanite pamoja na barabara za juu za Uhasibu na Chang'ombe; kukamilisha ujenzi reli ya SGR kwa vipande vya SGR vya Dar es Salaam – Morogoro (km 300) na Morogoro – Makutupora (km 422); na kukamilika kwa Kiwanda cha Sukari Mkulazi. Miradi ya umeme wa maji ya Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222), kiwanda cha LNG, Mchuchuma na Liganga imeendelea na hatua mbalimbali za maandalizi ya utekelezaji, ambapo hadi kufikia Juni 2026 majadiliano na mwekezaji kuhusu miradi ya Mchuchuma na Liganga yalikuwa yamekamilika, huku mradi wa Magadi Soda Engaruka ukiendelea na mchakato wa kutafuta mwekezaji wa kushirikiana naye katika ujenzi na uendeshaji wa kiwanda unaendelea.

Vilevile, mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la EACOP (km 1,443) utekelezaji wake ulifikia asilimia 86; ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko ulifikia asilimia 97; utafutaji

wa mafuta na gesi katika vitalu vya Eyasi – Wembere na Mnazi Bay ulifikia asilimia 40;, miradi iliyosajiliwa katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi iliongezeka kutoka 29 mwaka 2024/25 hadi 35 mwaka 2025/26; na thamani ya uwekezaji katika miradi hiyo ilikuwa Dola za Marekani milioni 430.586 hadi Juni 2026, ikilinganishwa na milioni 430.62 mwaka 2024/25, huku ajira 15,076 zikizalishwa mwaka 2025/26.

3.2 Mageuzi katika Sekta za Kimkakati

3.2.1 Sekta ya Kilimo

Utekelezaji wa Mpango uliwezesha: ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji; upanuzi wa miundombinu ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), ambapo uwezo wa kuhifadhi uliongezeka hadi tani 776,000 mwaka 2025/26, kutoka tani 251,000 mwaka 2024/25; kuimarisha upatikanaji wa pembejeo, huduma za ugani na masoko ya mazao; na kuimarisha vyama vya ushirika, ambapo viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika viliongezeka kutoka 329 mwaka 2024 hadi 336 mwaka 2025, na wanachama wa vyama vya ushirika walipungua hadi kufikia milioni 2.1 mwaka 2025, kutoka milioni 2.8 mwaka 2024. Kupungua kwa wanachama wa ushirika kulitokana na jitihada zilizochukuliwa na Serikali za kutumia mfumo wa kidijitali wa usimamizi wa vyama vya ushirika (MUVU) unaoratibiwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II); Programu ya Mifumo Himilivu ya Chakula Tanzania (TFSRP); Mradi wa Upatikanaji wa Pembejeo (TAISP); Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT); na Programu ya Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi (AFDP).

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: eneo la kilimo cha umwagiliaji liliongezeka kutoka hekta 727,280.6 mwaka 2024 hadi hekta 983,466.1 mwaka 2025; mchango wa sekta katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 24.3 mwaka 2025, kutoka asilimia 24.9 mwaka 2024; sekta ilikua kwa asilimia 5.5 mwaka 2025, kutoka asilimia 5.1 mwaka 2024; utoshelevu wa chakula ulifikia asilimia 130 mwaka 2025/26, kutoka asilimia 128 mwaka 2024; uzalishaji wa mazao ya chakula ulifikia tani 23,783,128 mwaka 2024/25, mazao ya bustani tani 9,781,236.74 na mazao asili ya biashara tani 1,596,311.18, kutoka tani 17,148,290, 7,304,723 na 973,436, mtawalia, mwaka 2023/24; thamani ya mauzo ya nje ya mazao ya kilimo ilifikia Dola za Marekani bilioni 3.73 mwaka 2025, kutoka bilioni 3.54 mwaka 2024; na upotevu wa mazao baada ya kuvuna ulipungua hadi asilimia 30 mwaka 2025/26, kutoka asilimia 35 mwaka 2024.

3.2.2 Sekta ya Mifugo

Utekelezaji wa Mpango uliwezesha upatikanaji na matumizi ya chanjo za mifugo; ujenzi na ukarabati wa majosho na kuongeza mwitikio wa uogeshaji wa mifugo; upatikanaji wa mbari bora za mifugo ikiwemo madume na mitamba; na kuongeza uzalishaji na uongezaji thamani wa mazao ya mifugo. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Mradi wa Mageuzi ya Tasnia ya Maziwa kwa Kuzingatia Mabadiliko ya Tabianchi (C-SDTP);

Mageuzi ya Mifumo ya Chakula Usangu; na Jenga Kesho Iliyo Bora – Vijana na Kilimo Biashara.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: matukio ya vifo vya mifugo yalipungua kwa asilimia 11.5, kutoka 34,029 mwaka 2024/25 hadi 30,109 mwaka 2026; kiwango cha magonjwa ya mifugo kilipungua kutoka asilimia 2.5 Desemba 2024 hadi asilimia 1.8 Desemba 2025; kiwango cha uogeshaji wa mifugo kiliongezeka kutoka asilimia 82 hadi 85, na utoaji wa chanjo uliongezeka na kufikia 70 kutoka asilimia 42 katika kipindi hicho; uzalishaji wa maziwa uliongezeka kutoka lita bilioni 4.1 Desemba 2024 hadi lita bilioni 4.2 Juni 2026; na mauzo ya nyama nje ya nchi yalifikia tani 12,763.77 Juni 2026, ikilinganishwa na tani 13,112.44 mwaka 2024/25.

3.2.3 Sekta ya Uvuvi

Utekelezaji wa Mpango uliwezesha ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko ambao utekelezaji umefikia asilimia 97; upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya uvuvi ikiwemo boti na vizimba; na kuongeza uzalishaji wa vifaranga vya samaki, ambao uliongezeka hadi kufikia 202,657,335 Juni 2026 kutoka vifaranga 140,018,196 mwaka 2024/25. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko; mradi wa TASFAM; Bandari ya Uvuvi Bagamoyo; uhuishwaji wa TAFICO; na Mradi wa Uchumi wa Buluu.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: sekta ilikua kwa asilimia 6.3 mwaka 2025 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.0 mwaka 2024, na mchango wake katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.0 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 2.3 mwaka 2024; uzalishaji wa mazao ya uvuvi uliongezeka na kufikia tani 659,242.69 Juni 2026 kutoka tani 575,000 mwaka 2024/25; hadi Juni 2026 mauzo ya mazao ya uvuvi nje yalifikia tani 37,988.30 zenye thamani ya shilingi bilioni 493.16 ikilinganishwa na tani 52,565.56 kwa mwaka mzima wa 2024/25; na viwanda vikubwa vya kuchakata samaki viliongezeka hadi 64 mwaka 2025 kutoka 25 mwaka 2024, na vidogo 38 kutoka 32.


3.2.4 Sekta ya Viwanda

Utekelezaji wa Mpango uliwezesha kuongeza uzalishaji wa viwandani ikiwemo Kiwanda cha Sukari Mkulazi ambacho kiliongeza uzalishaji hadi tani 26,470 za sukari msimu wa 2025/26, kutoka tani 19,124 msimu wa 2024/25; kulipwa kwa asilimia 98.7 ya fidia kwa mradi wa Magadi Soda Engaruka; na kuongezeka kwa miradi iliyosajiliwa katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi hadi 35 mwaka 2025/26 kutoka 29 mwaka 2024/25, yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 430.6. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Engaruka Soda Ash/Lake Natron; Integrated Industrial Development Programme; Tanzania Mini Tiger Plan; Export Processing Zone Development; Liganga Vanadium Titanium; na Mchuchuma.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: sekta ilikua kwa asilimia 5.2 mwaka 2025, kutoka asilimia 4.9 mwaka 2024; mchango wa sekta katika Pato la Taifa

ulipungua hadi asilimia 5.9 mwaka 2025, kutoka asilimia 6.8 mwaka 2024; watu walioajiriwa viwandani waliongezeka hadi 397,953 mwaka 2025 kutoka 391,275 mwaka 2024; na mauzo ya bidhaa za viwandani yalifikia Dola za Marekani milioni 1,264.6 katika soko la EAC na milioni 3,545 katika soko la SADC mwaka 2025, kutoka milioni 1,160.5 na milioni 2,968.3, mtawalia, mwaka 2024. Kielelezo Na: 3.1

Kielelezo Na.3.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Sekta ya Viwanda na Mchango wake katika Pato la Taifa, 2019 – 2025



Chanzo: Wizara ya Fedha


3.2.5 Sekta ya Ujenzi

Mpango uliwezesha kukamilika kwa madaraja makubwa ya JPM (Kigongo – Busisi) na Tanzanite pamoja na barabara za juu za Uhasibu na Chang'ombe; kuendelea na ujenzi wa Daraja la Jangwani ambao umefikia asilimia 42; kukamilika kwa madaraja 81 ya dharura yaliyoathiriwa na mvua za El-Nino na Kimbunga Hidaya; na kukamilika kwa ujenzi wa km 243.13 za barabara za lami na km 94.36 za changarawe mwaka 2025/26. Aidha, utekelezaji wa miradi takriban 103 ya barabara uliendelea katika hatua mbalimbali, ikiwemo: barabara ya Tanga – Pangani (km 50) iliyofikia asilimia 77; Tungamaa – Mkange (km 95.2) asilimia 63; daraja la Pangani asilimia 68.85; upanuzi wa Uyole – Ifisi (km 29) asilimia 46; kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mkiu – Mavanga – Madaba (km 112); na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Kigamboni – Chanika – Kibaha – Mbweni (km 77.5). Vilevile, ukarabati na matengenezo yaliendelea katika barabara za Arusha – Moshi – Holili ipo katika hatua ya manunuzi, Mtwara – Mingoyo – Masasi, Lot I asilimia 27.13 na Lot II asilimia 5.3 Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi, Sehemu ya Vikonge – Luhafwe (km 25) asilimia 60.24 na Sehemu ya Luhafwe – Mishamo/Bulamata Jct Section (km 37.35) asimilia 22.6 , Geita – Bulyanhulu – Kahama,

asilimia 87, BRT awamu ya (I – V), BRT I Awamu ya kwanza asilimia 83.13, BRT II imekamilika, BRT III awamu ya kwanza imekamilika, awamu ya pili imefikia asilimia 19.12, BRT IV Lot I asilimia 64.24, Lot II asilimia 51.16, Lot III asilimia 35.0 DMDP II, na Uendelezaji wa Bonde la Msimbazi.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: mtandao wa barabara kuu na za mikoa zinazopitika wakati wote uliongezeka hadi km 37,734.41 Juni 2025 kutoka km 37,435 mwaka 2024; sekta ilikua kwa asilimia 4.0 mwaka 2025, kutoka asilimia 3.0 mwaka 2024; mchango wa sekta katika Pato la Taifa ulipungua hadi asilimia 11.9 mwaka 2025, kutoka asilimia 12.5 mwaka 2024; mchango wa kampuni za ndani katika soko la ujenzi uliongezeka hadi asilimia 60 ya thamani ya miradi mwaka 2025/26 kutoka asilimia 40 mwaka 2023; na ajira katika miradi ya ujenzi zilifikia 18,988 hadi Desemba 2025, ikilinganishwa na ajira 21,527 kwa mwaka 2024. Kielelezo Na: 3.2

Kielelezo Na. 3.2: Mwenendo wa Ukuaji wa Sekta ya Ujenzi na Mchango wake katika Pato la Taifa, 2019 – 2025



Chanzo: Wizara ya Fedha

3.2.6 Sekta ya Madini na Uchimbaji


Mpango uliwezesha kuimarishwa kwa masoko na vituo vya ununuzi wa madini; kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kusafisha na kuchenjua madini nchini; kuwezesha wachimbaji wadogo na wa kati; na kutekeleza tafiti za kina za jiolojia, ambapo asilimia 16 ya eneo la nchi imefanyiwa tafiti hizo mwaka 2025/26 huku Serikali ikipanga kuongeza kiwango hicho hadi kufikia asilimia 34 kupitia utafiti wa kina katika maeneo ya mikoa 10 ambayo hayajafanyiwa utafiti wa kina ya Kigoma, Kagera, Rukwa, Katavi, Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Ruvuma na Tabora. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni

pamoja na: Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP); Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC); na TEITI.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: ukuaji wa sekta uliongezeka hadi asilimia 9.4 mwaka 2025, kutoka asilimia 8.1 mwaka 2024; mchango wa sekta katika Pato la Taifa uliongezeka hadi asilimia 10.3 mwaka 2025 kutoka asilimia 7.8 mwaka 2024; na thamani ya mauzo ya madini nje ilifikia Dola za Marekani milioni 5,401.9 mwaka 2025, kutoka milioni 3,116.4 mwaka 2021. Aidha, asilimia ya madini kati ya bidhaa sisizo asilia zilizouzwa nje iliongezeka kufikia asilimia 63.8 mwaka 2025 kutoka asilimia 54.1 mwaka 2021

Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na makusanyo ya maduhuli kufikia shilingi trilioni 1.39 mwaka 2025/26 ikilinganishwa na shilingi bilioni 624.61 mwaka 2021/22; kuwezesha ununuzi wa dhahabu tani 27.79 kufikia Juni 2025; kati ya mwaka 2021 na mwaka 2025 watoa huduma na wakandarasi wa ndani walichangia manunuzi yenye thamani ya dola bilioni 5.07, sawa na asilimia 87 kupitia *local content*; kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa nane (08) kwa ajili ya shughuli za uongezaji thamani madini katika kituo cha TGC jijini Arusha; kusainiwa kwa mkataba wa kuendeleza mradi wa uchimbaji madini ya niobium wa Panda Hill, wenye thamani ya dola za Marekani milioni 442; uwepo wa viwanda vya ungezaji thamani madini mbalimbali ikiwemo dhahabu kama *Mwanza Precious Metal*, *Geita Gold Refinery* na ununuzi wa mitambo 15 ya uchorongaji kwa ajili ya kutoa huduma kwa wachimbaji wadogo wa madini. **Kielelezo Na 3.3**

Kielelezo Na. 3.3: Mwenendo wa Ukuaji wa Sekta ya Madini na Mchango wake katika Pato la Taifa, 2019 – 2025




Chanzo: Wizara ya Fedha

3.2.7 Sekta ya Utalii

Mpango umewezesha kutangaza utalii ndani na nje ya nchi; kuibua na kuendeleza mazao mapya ya utalii ya kimkakati; kuboresha miundombinu ya utalii na uhifadhi; na kuimarisha vyuo vya utalii na ukarimu. Tanzania ilishika nafasi ya 11 duniani mwaka 2025 kwa ongezeko la wageni wa kimataifa. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: miradi ya TANAPA; Kuendeleza Utalii Kusini mwa Tanzania; Mradi wa TAWA; Kujenga Uwezo wa NCT; Capacity Building in Game Reserves; na Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio (MICE) pamoja na programu ya Royal Tour.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: idadi ya watalii iliongezeka hadi 5,935,561 sawa na ongezeko la asilimia 10.7 Desemba 2025, kutoka watalii 5,360,247 mwaka 2024; watalii wa kimataifa waliongezeka kwa asilimia 7.1, kutoka 2,141,895 hadi 2,294,495; watalii wa ndani waliongezeka kwa asilimia 13.1, kutoka 3,218,352 hadi 3,641,066; na mapato yatokanayo na watalii wa kimataifa yaliongezeka kwa asilimia 12.8, kutoka Dola za Marekani bilioni 3.9 mwaka 2024 hadi bilioni 4.4 mwaka 2025. Kielelezo Na. 3.4.

Kielelezo Na. 3.4: Idadi ya Watalii wa Kimataifa, 2019 – 2025



Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

3.2.8 Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

Mpango ulilenga kuwezesha ujenzi wa miundombinu saba (7) mipya ya michezo, na hivyo kufikisha jumla ya miundombinu 37 mwaka 2025/26, kutoka 30 mwaka 2024/25; kuimarisha mifumo ya usajili na ulinzi wa kazi za sanaa; na kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili kikanda na kimataifa. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: ujenzi wa Maeneo Changamani ya Michezo Arusha na Dodoma; National Sports Complex; Mfuko wa Maendeleo ya Michezo; Akademia ya Michezo Malya; upanuzi wa usikivu wa TBC; na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: filamu (TFB) na muziki (BASATA) zilizoidhinishwa zilifikia 14,581 mwaka 2025/26, kutoka 4,342 mwaka 2024/25; wasanii waliosajiliwa katika tasnia ya ubunifu walifikia 15,667, kutoka 7,310; wataalamu wa tasnia ya ubunifu waliopata mafunzo walifikia 4,656, ikilinganishwa na wataa 11,500; wanariadha walioshiriki mashindano nje ya nchi walifikia 132, kutoka 62; michezo na mashindano ya kimataifa yaliyoandaliwa au kushirikiwa na Tanzania yalifikia 337, kutoka 110; na wataalamu wa Kiswahili wanaofanya kazi nje ya nchi walifikia 678, kutoka 384mwaka 2024/25.

3.2.9 Biashara na Uwekezaji

Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, ambapo sheria na kanuni 28 ziliboreshwa mwaka 2025/26 dhidi ya lengo la 12; kuimarisha Kituo cha Huduma za Mahali Pamoja kwa wawekezaji, ambacho kimefikia taasisi 15 kati ya 18 zilizolengwa; kuendeleza Maeneo Maalum ya Kiuchumi, yakiwemo Benjamin William Mkapa SEZ, Bagamoyo SEZ na Mtwara SEZ ambapo miradi iliyosajiliwa imeongezeka kutoka 29 hadi 35; kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za viwandani katika masoko ya EAC na SADC; kusajiliwa kwa miradi ya kimkakati ukiwemo mradi wa kuhifadhi gesi ya LPG wa Chongoleani, Tanga (Dola za Marekani milioni 125); na kusajiliwa kwa miradi ya ubia (PPP) yenye thamani ya shilingi trilioni 6.9 hadi Februari 2026, ambapo miradi ya PPP iliyofikia hatua ya utekelezaji iliongezeka kutoka mitano (5) mwaka 2024/25 hadi saba (7) mwaka 2025/26. Miradi saba (7) ya PPP iliyo katika utekelezaji ni pamoja na Kariakoo One Stop Commercial Complex (shilingi bilioni 37), DART Awamu I na II, Bandari ya Dar es Salaam – DPW, Bandari ya Dar es Salaam – ADANI na TAZARA, huku majadiliano ya mkataba yakiendelea kwa miradi 3, miradi 4 ikiwa katika ununuzi wa wabia, 22 katika upembuzi yakinifu na 33 katika upembuzi wa awali.

Hadi Juni 2026, jumla ya miradi 114 iliibuliwa ambapo miradi tisa (9) imefikia hatua ya utekelezaji kwa utaratibu wa PPP katika sekta mbalimbali yenye thamani ya shilingi trilioni 8.5. Miradi hiyo ni Ujenzi wa Kituo cha Biashara (Business Complex) cha DDC Kariakoo; Uboreshaji wa Miundombinu na Uendeshaji wa Bandari (TPA na DP World); Uboreshaji wa Miundombinu na Uendeshaji wa Bandari (TPA na ADANI); Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza (DART na TRANSDAR); Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili (DART na MOFAT); Mradi wa Njia Mlishi za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili (DART na Metro Link City Company Ldt); Mradi wa Njia Mlishi za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili (DART na Y.K City Link Ltd); Mradi wa Vituo vya Ukaguzi wa Vyombo vya Moto (Shirika la Uzalishaji Mali la Polisi na Kampuni ya MVI –TANZANIA Ltd); na Mradi wa Ukarabati na Uendeshaji wa Reli ya TAZARA. Aidha, miradi mingine 105 ipo katika hatua za maandalizi, ununuzi na majadiliano ya mkataba kwenye Mamlaka mbalimbali za Serikali. (miradi 3 ipo hatua ya majadiliano ya mkataba, miradi 3 ikiwa katika ununuzi wa wabia, 21 katika upembuzi yakinifu na 36 upembuzi awali na dhana ya maandiko (concept note ni miradi 42).

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa na TISEZA ilifikia 934 mwaka 2025/26, kutoka 940 mwaka 2024/25; thamani ya miradi ya uwekezaji iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 11,267.29 mwaka 2024/25 hadi milioni 12,500 mwaka 2025/26; ajira zinazotarajiwa kutoka miradi hiyo ziliongezeka kutoka 151,284 hadi 307,743; jumla limbikizi ya tozo, ada na ushuru uliofutwa au kupunguzwa iliongezeka kutoka 452 hadi 697; na ardhi iliyotengwa kwa uwekezaji iliongezeka kutoka ekari 391,030.94 hadi ekari 420,516.29.

3.2.9.1 Mwenendo wa Uwekezaji na Utekelezaji wa Miradi kwa Ushirikiano na Sekta Binafsi

Katika mwaka 2025/26, jumla ya miradi 934 ya uwekezaji yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 12.5 ilisajiliwa, ikitarajiwa kuzalisha ajira 307,743. Aidha, katika kipindi cha Julai hadi tarehe 15 Oktoba 2026, miradi 243 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 3.44 ilisajiliwa, ikitarajiwa kuzalisha ajira 55,836. Sekta ya viwanda iliendelea kuongoza kwa idadi na thamani ya miradi iliyosajiliwa. Vilevile, katika robo ya kwanza ya mwaka 2026/27, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), kwa kushirikiana na sekta binafsi, liliendelea na hatua za utekelezaji wa miradi minne (4) ya mafuta na gesi asilia yenye gharama zinazokadiriwa kufikia dola za Marekani bilioni 20.03 na shilingi bilioni 20.41. Miradi hiyo inahusisha uchakataji wa gesi asilia, ujenzi wa mtambo wa kusafisha mafuta, ukarabati wa miundombinu ya kuhifadhi mafuta na uendelezaji wa Kitalu cha Ruvuma.

Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa kwa Kisekta katika Kipindi cha Julai 2025 hadi Juni 2026

Sekta	Idadi ya Miradi	Fursa za Ajira	Mtaji (Dola za Marekani, Milioni)
Kilimo	96	57,299	3,341.63
Biashara	100	33,318	1,116.71
Teknolojia ya Kompyuta	2	82	5.15
Miundombinu ya Kiuchumi	25	21,761	811.63
Nishati	11	680	137.60
Huduma za Fedha	1	7	1.92
Rasilimali Watu	5	407	11.62
Viwanda	457	65,374	4,288.23
Madini na Petroli	18	106,266	335.32
Huduma	21	1,066	175.72
Mawasiliano ya Simu	3	177	125.26
Utalii	90	6,741	1,389.47
Uchukuzi	105	14,565	759.74
Jumla	**934**	**307,743**	**12,500.00**

Chanzo: TISEZA

Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa kwa Kisekta katika Kipindi cha Julai hadi tarehe 15 Oktoba 2026

Sekta	Idadi ya Miradi	Fursa za Ajira	Mtaji (Dola za Marekani, Milioni)
Kilimo	13	16,405	56.58


Biashara	39	3,473	927.14
Miundombinu ya Kiuchumi	14	3,680	672.24
Nishati	4	449	184.82
Viwanda	139	28,697	1,455.05
Madini na Petroli	2	78	12.25
Huduma	2	295	2.00
Utalii	21	1,662	74.23
Uchukuzi	9	1,097	55.05
Jumla	**243**	**55,836**	**3,439.36**

Miradi Inayotekelezwa Na TPDC Kwa Kushirikiana Na Sekta Binafsi Kwa Robo Ya Kwanza Ya Mwaka Wa Fedha 2026/27 (Julai – Septemba, 2026)

NA	JINA LA MRADI	ENEO LA MRADI	JINA LA SEKTA BINAFSI	HATUA ILIYOFIKIWA	GHARAMA ZA MRADI
1.	Miradi Midogo ya Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (Mini - LNG).	Mkoa wa Pwani – (Mkuranga)	Rosetta Energy Solutions.	• Mkataba wa Mauziano ya Gesi Asilia (Gas Sales Agreement – GSA) ulisainiwa tarehe 05 Agosti, 2026. • Kwa sasa mkandarasi anaendelea na kazi ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) katika eneo la mradi.	Dola marekani milioni 11.5.
2.	Mradi wa Ujenzi wa Mtambo wa Kusafisha Mafuta (Refinery) chini ya mpango wa Tanga Reginal Energy Hub	Tanga	Vitol Bahrain Energy Company	• Mkataba wa Makubaliano (MoU) ulisainiwa kati ya UNOC, TPDC na Vitol B. E. Company tarehe 06 Agosti, 2026. • Kazi inayoendelea sasa ni maandalizi ya Upembuzi Yakinifu	Dola za Marekani Bilioni 20.
3.	Mradi wa Ukarabati Tenki Na. 8	Dar es Salaam (Kigamboni)	BSL Infrastructure Ltd	• Mkandarasi na TPDC walisaini mkataba ya ujenzi tarehe 10 Agosti, 2026. • Mkandarasi anaendelea na kazi ya mobilization ya vifaa vya ujenzi huku akiendelea na kazi nyingine za awali za ukarabati.	Gharama za mradi ni TZS 20.41 bilioni
4.	Mradi wa uendelezaji wa kitalu cha Ruvuma (eneo la Ntorya. – Uchimbaji kisima cha Ntorya 3.	Mtwara (Mtwara vijijini)	ARA Petroleum	*Award letter* imetolewa tarehe 18 Septemba, 2026 kwa ajili ya kazi za uchimbaji wa kisima cha Ntorya 3 kwa Mkandarasi CPTDC.	Gharama za mradi USD 20 million.

Chanzo: TPDC

Uchambuzi wa mwenendo wa uwekezaji unaonesha kuendelea kuimarika kwa nafasi ya sekta binafsi katika kuchochea shughuli za uzalishaji na maendeleo ya uchumi, hususan katika sekta za viwanda, biashara, miundombinu na nishati. Sekta ya viwanda imeendelea kuwa kinara katika kuvutia uwekezaji, ambapo mchango wake katika idadi ya miradi yote iliyosajiliwa uliongezeka kutoka asilimia 48.9 katika mwaka 2025/26 hadi asilimia 57.2 katika kipindi cha Julai hadi tarehe 15 Oktoba 2026. Aidha, mchango wa sekta hiyo katika thamani ya mtaji wa miradi iliyosajiliwa uliongezeka kutoka asilimia 34.3 hadi asilimia 42.3 katika vipindi hivyo, hali inayoashiria kuendelea kuelekezwa kwa uwekezaji katika shughuli za uzalishaji viwandani. Kwa upande wa ajira, sekta ya viwanda ilichangia asilimia 51.4 ya fursa zote za ajira zilizotarajiwa kutokana na miradi iliyosajiliwa katika kipindi cha Julai hadi tarehe 15 Oktoba 2026. Vilevile, ushirikiano kati ya TPDC na sekta binafsi katika miradi ya mafuta na gesi asilia unaonesha fursa za kuongeza uwezo wa ndani wa kuchakata na kuhifadhi bidhaa za nishati, kuimarisha usalama wa upatikanaji wa nishati, kuongeza thamani ya rasilimali za ndani na kupanua fursa za ajira na uwekezaji.



Aidha, katika kipindi cha mwaka 2025/26, Serikali iliendelea kuimarisha ushirikiano na Sekta Binafsi katika sekta mbalimbali. Katika sekta ya afya, Sekta Binafsi ilikuwa na vituo 5,460, sawa na asilimia 40 ya vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini, na ilifungua vituo vipya 241. Aidha, Serikali ilishirikiana na Hospitali za Mashirika ya Kidini katika kugharamia mishahara ya watumishi na vifaa tiba, huku hospitali za Bugando na KCMC zikichangia utoaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi. Vilevile, Taasisi ya Mifupa

(MOI) na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road ziliendelea na hatua za upembuzi yakinifu kwa ajili ya kupata wabia wa kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini.

Katika sekta ya madini, Kampuni ya Panda Hill Tanzania Limited ilisaini mkataba wa kuendeleza mradi wa uchimbaji madini ya Niobium wa Panda Hill, wenye thamani ya dola za Marekani milioni 442, na mitambo 15 ya uchorongaji ilinunuliwa kwa ajili ya kuboresha huduma kwa wachimbaji wadogo. Aidha, uzalishaji uliendelea katika migodi ya Geita Gold Mine, Shanta Gold Mine, North Mara na Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira – Songwe. Kwa upande wa shughuli za uongezaji thamani madini ziliendelea katika viwanda mbalimbali, ikiwemo Mwanza Precious Metals, Geita Gold Refinery na Eyes of Africa. Vilevile, uendelezaji wa migodi ya dhahabu ya Nyanzaga – Sengerema, urani ya Mkuju River – Namtumbo na Nikeli ya Kabanga uliendelea. Hatua hizi zilichangia kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi, kupanua uwekezaji, kuongeza thamani ya rasilimali za madini nchini na kuweka mazingira ya kukuza ajira na shughuli za kiuchumi.

Miradi ya Ushirikiano na Uwekezaji na Sekta Binafsi katika Sekta ya Madini

Na.	Jina la Mradi	Kampuni ya Ubia	Eneo	Jina la Sekta Binafsi	Umiliki wa Hisa (%)	Thamani ya Uwekezaji
1.	Mradi wa Uchimbaji madini ya dhahabu katika mgodi wa madini ya dhahabu, Northmara (Northmara Gold Mine)	Twiga Minerals Corporation	Nyamongo, Tarime	Barrick Gold Corporation (Barrick)	Barrick 84% Serikali 16%	USD 827,125,000
2.	Mradi wa Uchimbaji madini ya dhahabu katika mgodi wa madini ya dhahabu, Bulyanhulu	Twiga Minerals Corporation	Kahama, Shinyanga	Barrick Gold Corporation (Barrick)	Barrick 84% Serikali 16%	USD 856,740,000
3.	Mradi wa Uchimbaji madini ya	Twiga Minerals Corporation	Kahama, Shinyanga	Barrick Gold Corporation (Barrick)	Barrick 84% Serikali 16%	USD (103,564,000)

	dhahabu katika mgodi wa madini ya dhahabu, Buzwagi kupitia kampuni ya Pangea Minerals					
4.	Mradi wa Uchimbaji madini ya almasi katika mgodi wa almasi wa Mwadui.	Williamson Diamond Limited (WDL)	Mwadui, Shinyanga	Pink Diamond (Subsidiary of Taifa Mining Group)	Pink 63% Serikali 37% Ambapo kwa upande wa Serikali 21% ni hisa za daraja A na 16% ni hisa za daraja B zisizohafifishwa.	USD (312,339,757)
5.	Mradi wa Kabanga Nickel	Tembo Nickel Corporation Ltd	Ngara, Kagera	Lifezone Metals Ltd (Lifezone)	Lifezone 84% Serikali 16%	USD (6,423,074)
6.	Mradi wa Uchimbaji madini mchanga katika mgodi wa madini mchanga Fungoni	Nyati Mineral Sands Ltd	Kigamboni, Dar es Salaam	Shenghe Resources Ltd (Shenghe)	Shenghe 84% Serikali 16%	TZS (14,822,321,000)
7.	Mradi wa Uchimbaji madini mchanga katika mgodi wa	Nyati Mineral Sands Ltd	Panganii, Tanga	Shenghe Resources Ltd (Shenghe)	Shenghe 84% Serikali 16%	

	madini mchanga Tajiri					
8.	Mradi wa Uchimbaji madini Kinywe katika mgodi wa madini kinywe Mahenge	Faru Graphite Ltd	Mahenge, Morogoro	Black Rock Mining Ltd (Black Rock)	Black Rock 84% Serikali 16%	USD (5,011,450)
9.	Mradi wa Uchimbaji madini ya dhahabu katika mgodi wa madini ya dhahabu Nyanzaga	Sotta Mining Co. Ltd	Sengerema, Mwanza	Perseus Mining Ltd (Perseus)	Perseus 84% Serikali 16%	USD (3,134,228)
10.	Mradi wa uchimbaji wa madini muhimu Ngualla (Ngualla Rare Earth Project)	Mamba Minerals Corporation Ltd	Songwe, Songwe	Shenghe Resources Ltd (Shenghe)	Shenghe 84% Serikali 16%	TZS 22,005,540,000
11.	Mradi wa Uchimbaji madini Kinywe Epanko (Epanko Graphite Project)	Duma TanzGraphite Ltd	Mahenge, Morogoro	EcoGraf Ltd	EcoGraf Ltd 84% Serikali 16%	TZS (1,581,842)
12.	Mradi wa	Kudu	Nachingwea,	Evolution	Evolution	USD

	Uchimbaji madini Kinywe Chilalo (Chilalo Graphite Project)	Graphite Ltd	Lindi	Energy Minerals	Energy Minerals 84% Serikali 16%	3,757,496
13.	Mradi wa Uchimbaji madini ya niobium Panda Hill (Panda Hill Niobium Project)	Chui Niobium Mining	Mbeya Rural District, Mbeya.	Tremond Investment & Cradle Resources Ltd	Tremond Investment & Cradle Resources Ltd 84% Serikali 16%	New Company
14.	Mradi wa Uchimbaji madini ya Helium kusini mwa Rukwa (Southern Rukwa Helium Project)	Songwe Helium Ltd	Momba and Sumbawanga, Rukwa.	HeliumOne Global	HeliumOne Global 83% Serikali 17%	New Company
15.	Mradi wa Uchimbaji madini kinywe Lindi Jumbo (Lindi Jumbo Graphite Mine)	Ndovu Graphite Ltd	Ruangwa, Lindi.	Walkabout Resources Ltd (Under Germcorp Administration)	Walkabout Resources Ltd 84% Serikali 16%	New Company
16.	Mradi wa uchimbaji wa madini kinywe	Graphica Graphite Corporation	Ruangwa, Lindi.	Graphica Resources Limited	Graphica Resources Limited 83%	New Company

	Graphica	Ltd			Serikali 17%	
17.	Mradi wa uchimbaji wa madini kinywe Eminent	Swala Graphite Corporation	Ruangwa, Lindi.	Eminent Minerals Limited	Eminent Minerals Limited 83% Serikali 17%	New Company
18.	Mradi wa uchimbaji wa madini kinywe Yudi	Yudi Mining	Morogoro, Morogoro.	Yudi Mining	Yudi Mining 83% Serikali 17%	New Company

Chanzo: OTR

3.3 Kujenga Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii

3.3.1 Elimu

Mpango uliwezesha kuongezeka kwa: ujenzi wa vyumba vya madarasa hadi 254,393 mwaka 2025/26 kutoka 191,708 mwaka 2024/25, shule za msingi hadi 17,986 kutoka 16,406, shule za sekondari hadi 4,894 kutoka 3,863 maktaba hadi 2,665 kutoka 1,537, maabara hadi 8,710 kutoka 8,072, mabweni hadi 3,245 kutoka 2,245, mabwalo hadi 1,004 kutoka 871, nyumba za walimu hadi 60,429 kutoka 58,637, na matundu ya vyoo hadi 286,243 kutoka 206,670 katika shule za msingi na hadi 131,152 kutoka 92,724 katika shule za sekondari; kuajiri walimu 68,279, wakiwemo walimu 7,000 wa sayansi na hisabati; kutoa ruzuku ya Elimu Bila Ada ya shilingi bilioni 510.97, kutoka shilingi bilioni 484.3 mwaka 2024/25; na kuongeza bajeti ya mikopo ya elimu ya juu hadi shilingi bilioni 916.7, kutoka shilingi bilioni 878.0 mwaka 2024/25. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Mikopo ya Elimu ya Juu; HEET; ESPJ II; EP4R; Support to VET and Teacher Education; SEQUIP; na Mfuko wa Elimu Tanzania (TEA).

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: uwiano wa wanafunzi kwa darasa katika elimu ya msingi uliboreka kutoka 1:75 mwaka 2020 hadi 1:62 mwaka 2025, na uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu mwenye sifa uliboreka kutoka1:51 mwaka 2024 hadi 1:50; uandikishaji jumla katika sekondari ya chini uliongezeka kutoka asilimia 51.7 mwaka 2024 hadi 53.1 mwaka 2025, na katika sekondari ya juu kutoka asilimia 9.1 hadi 9.8; uandikishaji jumla katika vyuo vya elimu ya ufundi ulifikia asilimia 10.4, kutoka asilimia 5.8 mwaka 2023/24; wahitimu wa elimu ya ufundi waliongezeka kutoka 89,967 hadi 129,766; wanafunzi waliopata mikopo ya elimu ya juu waliongezeka kutoka 229,652 mwaka 2024 hadi 248,331 mwaka 2024/25; wahitimu wa vyuo vikuu waliongezeka kutoka 56,520 hadi 62,570; ufaulu wa kidato cha nne ulikuwa asilimia 92.37 mwaka 2024, na ufaulu wa darasa la saba na kidato cha sita ulifikia asilimia 81.8 na 99.62 mwaka 2025, mtawalia, kutoka asilimia 80.9 na 99.9 mwaka 2024.

3.3.2 Nguvu Kazi, Vijana na Ajira

Mpango ulilenga kuwezesha utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi, ambapo vijana 5,746 walipata mafunzo ya uanagenzi, 2,500 mafunzo ya utarajali, mafunzo ya kuongeza ujuzi kwa wafanyakazi 1,365, na vijana 7,826 mafunzo ya kushindania fursa za ajira. Vile vile, kutoa mikopo ya shilingi bilioni 52.2 kwa vikundi 5,199 vya vijana; kuwezesha vikundi 299 vya vijana (vijana 2,226) kupata zabuni za umma zenye thamani ya shilingi bilioni 13.2 kupitia mfumo wa NeST; na kuanzisha mfuko wa ruzuku kwa vyama vya watu wenye ulemavu. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Programu ya Ukuzaji Ujuzi; Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; na Uimarishaji wa Mifumo ya Kitaifa kwa Maendeleo ya Vijana.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: ajira 981,000 zilizalishwa mwaka 2025/26, kutoka 876,916 mwaka 2024/25; wigo wa kinga ya jamii ulifikia asilimia 28 mwaka 2025/26, kutoka asilimia 27.4 mwaka 2024/25; na watu waliopata mafunzo ya ujuzi walifikia 168,667 mwaka 2025/26, kutoka 157,867 mwaka 2024/25.

3.3.3 Ustawi na Maendeleo ya Jamii

Mpango uliwezesha utekelezaji wa programu za uwezeshaji wanawake kiuchumi na kurasimisha wafanyabiashara wadogo, ambapo wafanyabiashara 6,735 walipata mikopo; kusajili vituo vya kulelea watoto wadogo mchana; na kuwapatia wazee 229 wanaohudumiwa katika makazi 13 ya Serikali bima ya afya. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: PAMOJA; TASAF; Mfuko wa Machinga; na Jinsia na Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: vituo vya kulelea watoto mchana vilivyosajiliwa viliongezeka hadi 4,916 mwaka 2025/26 kutoka 4,178 mwaka 2024/25; na wafanyabiashara wadogo waliotambuliwa na kusajiliwa waliongezeka hadi 138,438 kutoka 84,318, ambapo asilimia 60 ni wanawake.

3.3.4 Afya

Mpango uliwezesha kuongeza vituo vya kutolea huduma za afya kufikia 10,540 mwaka 2025/26 (zahanati 8,706, vituo vya afya 1,359 na hospitali 475), kutoka 10,044 mwaka 2024/25; kuongeza watumishi wa sekta ya afya kufikia 177,711, kutoka 126,925 mwaka 2024; na kuongeza viwanda vya dawa nchini kutoka 11 hadi 12. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Dawa na Bidhaa za Afya; Uimarishaji wa Huduma za Chanjo; Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa; Programu ya Afya ya Mama na Mtoto; Hospitali ya Taifa Muhimbili; Hospitali Maalum ya Mama na Mtoto Dodoma; na Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: chanjo ya Penta iliwafikia watoto 2,361,592 sawa na asilimia 95 mwaka 2025, kutoka asilimia 96.5 mwaka 2024; wastani wa umri wa kuishi uliongezeka kutoka miaka 66.8 mwaka 2022 hadi miaka 68.3 mwaka 2025; vifo vya watoto chini ya miaka mitano vilipungua kutoka 67 kwa kila vizazi

hai 1,000 mwaka 2015/16 hadi 43 mwaka 2022; na vifo vitokanavyo na uzazi vilipungua kutoka 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2015/16 hadi 104 mwaka 2022.

Kwa upande wa bima ya afya, jumla ya kaya 198,709 kati ya kaya 276,004 zimehakikiwa na kupatiwa kadi, sawa na asilimia 72 ya lengo. Vilevile, idadi ya wanufaika 542,829 wamepatiwa kadi kati ya wanufaika 1,206,319 waliolengwa sawa na asilimia 45. Aidha, jumla ya wazee 196 wamepatiwa kadi za bima ya afya kati ya wazee 205 waliopo kwenye makazi ya Serikali sawa na asilimia 83 ya lengo. Vilevile, watoto 205 kati ya 255 waliopo kwenye makao ya Serikali wamepatiwa kadi za bima ya afya sawa na asilimia 80 ya lengo. Vilevile, kaya 6,591 sawa na asilimia 35 zimehakikiwa na kupatiwa kadi kati ya kaya 18,844 zilizolengwa sawa na wanufaika 6,545 kati ya 51,871 waliolengwa sawa na asilimia 13 ya lengo. Kwa upande wa wazee na watoto wanaokaa kwenye Makazi na makao maalumu, jumla ya wazee 196 wamepewa kadi kati ya wazee 235 waliolengwa. Hadi Juni 2026, wanachama wa Bima ya afya nchini ikijumuisha wanachama wa bima ya afya kwa wote na bima zingine imefikia asilimia 11.3 ya Watanzania wote ikilinganishwa na lengo la asilimia 25 ya Watanzania wote mwezi Juni 2027.

3.3.5 Maji na Usafi wa Mazingira

Katika kipindi cha mwaka 2025/26, Wizara ya Maji iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma endelevu ya majisafi na usafi wa mazingira kwa wananchi wote, mijini na vijijini. Ili kufikia lengo hilo, Wizara ilitekeleza kazi zifuatazo:

(a) Usimamizi na uendelezaji wa Rasilimali za Maji

Serikali iliendelea kusimamia rasilimali za maji nchini kupitia Bodi tisa (9) za Maji za Mabonde zilizoanzishwa ili kuhakikisha usimamizi na uendelezaji endelevu wa rasilimali hizo. Katika kipindi husika, mtandao wa vituo 1,186 vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji umeanzishwa, na zaidi ya miti milioni 6 rafiki kwa maji imepandwa ili kuimarisha uhifadhi wa vyanzo vya maji. Aidha, vyanzo 106 vya maji vimetangazwa katika Gazeti la Serikali kwa ajili ya ulinzi na uhifadhi, vibali 247 vya utupaji wa maji taka vimetolewa ili kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji, na vibali 14,536 vya matumizi ya maji vimetolewa ili kudhibiti matumizi ya maji. Vilevile, ili kuimarisha ushirikishwaji wa jamii katika kutunza na kuhifadhi vyanzo vya maji, Kamati 34 za Vidaka Maji na Jumuiya 272 za Watumia Maji zimeanzishwa.

(b) Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini

Huduma ya maji vijijini inatekelezwa na kusimamiwa na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA). Ili kuimarisha upatikanaji wa huduma hii, katika mwaka 2025/26 Serikali ilipanga kutekeleza jumla ya miradi 1,318 kwenye maeneo ya vijijini. Utekelezaji huo ulihusisha kukamilisha miradi iliyokuwa inaendelea, kujenga miradi mipya, pamoja na kupanua na kukarabati miundombinu ya maji.

Kwa upande wa usambazaji wa maji vijijini, RUWASA iliendelea kutekeleza miradi ya maji na usafi wa mazingira, ambapo jumla ya miradi 54 yenye vituo 946 vya kuchotea maji

imekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi wapatao 493,932 wanaoishi katika vijiji 151. Aidha, utekelezaji wa miradi 992 yenye vituo 29,865 unaendelea, ikiwa katika hatua mbalimbali; miradi hiyo itakapokamilika itahudumia wananchi wapatao 38,611,800 wanaoishi katika vijiji 7,030.

(c) Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo iliendelea kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira mijini kupitia ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya maji. Katika mwaka 2025/26, jumla ya miradi 226 ilipangwa kutekelezwa ambapo jumla ya miradi 12 imekamilika na inahudumia wananchi wapatao 880,633. Jumla ya miradi 190 inaendelea na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na miradi 16 imefikia zaidi ya asilimia 95 na imeanza kutoa huduma kwa wananchi. Aidha, miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Ukarabati na Upanuzi wa Maji Mijini; Ziwa Victoria – Kahama – Shinyanga; WSDP; Uboreshaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini; LVWATSAN Awamu ya II; na Tanga Water Supply and Sanitation.

Vilevile, utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: upatikanaji wa maji ya bomba vijijini uliongezeka kutoka asilimia 83.1 mwaka 2024/25 hadi asilimia 85.2 mwaka 2025/26; katika makao makuu ya mikoa uliongezeka kutoka asilimia 90.6 hadi 92.5; na kaya za vijijini zenye miundombinu bora ya usafi wa mazingira ziliongezeka kutoka asilimia 72.0 hadi 78.5 katika kipindi hicho.

3.3.5.1 Mazingira

Mpango ulilenga kupandwa kwa miti milioni 276 ambapo kwa mwaka 2025/26 miti milioni 241 ilipandwa, kati ya hiyo, miti milioni 184.1 imestawi sawa na asilimia 76; vibali 212 vya usimamizi wa taka hatarishi vilitolewa kwa wadau; kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki ambapo jumla ya tani 60 zilikamatwa na kuteketezwa; kukusanywa kwa tani 150,000 za taka za chupa za plastiki, ambapo tani 75,000 zilirejelezwa. Katika uhifadhi wa mazingira, miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Kuimarisha Usimamizi wa Mashamba ya Miti ya Serikali; Programu ya Kujenga Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi Kigoma katika halmashauri za Kasulu, Kibondo na Kakonko; Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mifumo Ikolojia, Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai Tanzania katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Katavi na Rukwa; Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Katika Jamii zinazozunguka Misitu ya Miombo Tanzania Bara na Zanzibar; Mradi wa "Scaling Up Locally Led Climate Action - SLR"; na FOLUR.

3.3.6 Ardhi na Maendeleo ya Makazi

Mpango uliwezesha kuimarisha miundombinu ya TEHAMA katika ofisi za ardhi za mikoa na halmashauri zote nchini, kusambaza Mfumo wa e-Ardhi, kutoa elimu na kuwajengea uwezo watumiaji katika upimaji na umilikishaji wa ardhi. Aidha miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Uboreshaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani (LDI) wenye thamani ya shilingi bilioni 56.32. Mradi wa Uboreshaji wa Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP); na Mradi

wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK), huku Shirika la Nyumba la Taifa likijenga nyumba za gharama nafuu.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: Viwanja na mashamba yaliyopimwa yalifikia 3,079,886 mwaka 2025/26, kutoka 2,857,349 mwaka 2024/25; hati zilizotolewa zilifikia 2,675,848 mwaka 2025/26, kutoka 2,573,849 mwaka 2024/25; na vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi vilifikia 4,953 asilimia 40.47, kutoka vijiji 4,672 asilimia 37.76 mwaka 2024/25.

3.4 Vichocheo vya Maendeleo


3.4.1 Nishati

Mpango uliwezesha kukamilika kwa ufungaji wa mitambo yote tisa (9) ya Bwawa la Julius Nyerere (MW 2,115); kuunganishwa kwa Mkoa wa Katavi na Gridi ya Taifa na kufikisha mikoa 24 kati ya 26, hatua iliyookoa takriban shilingi bilioni 68.4 za gharama za kuzalisha umeme kwa mafuta; kuunganishwa na umeme kwa vijiji vyote 12,318 na vitongoji 39,003 kati ya 64,359; kuendelea na ujenzi wa EACOP uliofikia asilimia 86 Juni 2026; na kuendelea na utafutaji wa mafuta na gesi kwa mradi wa Eyasi-Wembere na mradi wa Lindi-Mtwara. Miradi ya Ruhudji, Rumakali, Kakono (MW 87) na LNG imebaki katika hatua za maandalizi, utekelezaji wa mradi wa Malagarasi (MW 49.5) umefikia asilimia 29.25 na ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa nishati ya jua cha Kishapu, Shinyanga (MW 50, Awamu ya Kwanza) umekamilika. Aidha, Awamu ya Pili ya mradi wa Shinyanga/Kishapu Solar (MW 100) imeanza kutekelezwa.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme uliongezeka kutoka MW 4,437.53 Juni 2025 hadi MW 4,606.14 Juni 2026; urefu wa Gridi ya Taifa ya umeme uliongezeka kutoka km 7,809.67 hadi km 8,500.38, na mtandao wa usambazaji umeme kutoka km 200,266.25 hadi km 233,133; wateja waliounganishwa na umeme waliongezeka kwa asilimia 12.97 kutoka 5,336,415 mwaka 2024/25 hadi 6,131,695 mwaka 2025/26; kaya zilizounganishiwa huduma ya umeme ziliongezeka kutoka asilimia 39.9 mwaka 2019/20, na kufikia asilimia 52.1 mwaka 2024/25. Aidha, wananchi waliofikiwa na huduma ya umeme waliongezeka kutoka asilimia 78.4 mwaka 2019/20 hadi asilimia 85.5 mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 7.12; matumizi ya umeme kwa mtu yaliongezeka kutoka kWh 170 mwaka 2024/25 hadi kWh 243 mwaka 2025/26; na vituo vya kujazia gesi asilia kwenye vyombo vya moto viliongezeka kutoka vituo 9 mwaka 2025 hadi 19 mwaka 2026. Kielelezo Na. 3.5

[2] *National Bureau of Statistics (NBS), Energy Access and Use Situation Survey III (2024/25)*

Kielelezo Na. 3.5: Mwenendo wa Uwezo wa Mitambo ya Kuzalisha Umeme (MW), 2019/20 – Juni 2026 na Shabaha za FYDP IV



3.4.2 Mifumo ya Usafirishaji na Uchukuzi Fungamanishi

Mpango ulilenga kuimarisha mifumo ya usafirishaji na uchukuzi kwa kupanua na kuboresha miundombinu ya reli, bandari, usafiri wa anga na miundombinu shikizi. Katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali iliendelea kutoa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya reli ya SGR katika vipande vya kutoka Dar es Salaam –Morogoro na Morogoro – Makutupora ambavyo ujenzi wake ulikamilika. Aidha, ujenzi katika kipande cha kutoka Makutupora - Tabora, Tabora – Isaka, Isaka – Mwanza na Tabora – Kigoma na Uvinza – Musongati uliendelea na kwa ujumla urefu ulikamilishwa ujenzi wake ulifikia kilomita 722 hadi kufikia mwezi Juni, 2026.

Katika ujenzi na ukarabati wa meli, Serikali ilikamilisha Ujenzi wa Meli ya Abiria na Mizigo ya MV. Mwanza pamoja na kukamilisha MV. Liemba katika Ziwa Tanganyika. Ukarabati wa MT. Ukerewe katika Ziwa Victoria ulifikia asilimia 95. Katika eneo la bandari, Serikali iliendelea na ujenzi na ukarabati wa bandari kavu saba (7). Kati ya hizo, bandari kavu za Kwala, Ex-NASACO na Mwambani zilianza kutoa huduma za kibandari na bandari nyingine ziliendelea na ukarabati na ujenzi. Aidha, mifumo ya usimamizi wa taarifa za viwanja vya ndege ilifungwa katika viwanja 10 kati ya 14; jumla ya mitambo 103 kati ya 71 ya ulinzi (X-ray machines) kwenye viwanja vya ndege ilinunuliwa na jumla ya viwanja vya ndege 26 kati ya 27 vilizungushiwa uzio wa usalama na rada tano (5) kati ya saba (7) za hali ya hewa zilikuwa zimefungwa. Hatua hizi za kuboresha miundombinu zinatarajiwa kuongeza ufanisi wa huduma za uchukuzi na kurahisisha mnyororo wa usafirishaji wa mizigo nchini.


Utekelezaji wa viashiria unaonesha kuwa sekta ya uchukuzi ilikua kwa asilimia 8.0 mwaka 2025, kutoka asilimia 4.2 mwaka 2024, na mchango wake katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 7.5 hadi 8.3. Mapato ya fedha za kigeni kutokana na huduma za uchukuzi

yaliongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 2.35 mwaka 2024 hadi bilioni 2.79 mwaka 2025.

Utendaji wa Sekta ya Uchukuzi uliimarishwa ambapo huduma za usafiri wa anga kupitia ATCL zilitolewa katika vituo 33 kwa mwaka 2025/26 ikilinganishwa na 27 kwa mwaka 2024/25 kwa kutumia ndege 16 zilizonunuliwa na Serikali. Hivyo, abiria 1,427,439 walisafirishwa kwa mwaka 2025/26, ikilinganishwa na abiria 1,178,025 katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia, sawa na ongezeko la asilimia 21.2. Kwa upande wa shehena iliyohudumiwa nchini iliongezeka kutoka tani milioni 32.753 zilizohudumiwa mwaka 2024/25 hadi kufikia tani milioni 39.899 mwaka 2025/26 sawa na ongezeko la asilimia 21.8. Wastani wa makasha yaliyohudumiwa kwa mwezi ulifikia TEUs 102,000, kutoka TEUs 61,000 sawa na ongezeko la asilimia 40, wakati muda wa kuhudumia meli za makasha gatini ulipungua hadi wastani wa siku 3 na muda wa meli kusubiri nangani ulipungua hadi siku 7 katika kipindi hicho.

Usafirishaji wa abiria na mizigo kwa reli ya SGR ilisafirisha abiria 3,552,650, ikilinganishwa na abiria 2,862,088 mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 24.12. Aidha, Shirika la Reli Tanzania (TRC) ilisafirisha jumla ya tani 501,155 ikilinganishwa na shehena ya tani 246,824 iliyosafirishwa mwaka 2024/25. Mamlaka ya reli ya Tanzania na Zambia – TAZARA kupitia reli ya TAZARA ilisafirisha jumla ya tani 214,848 ikilinganishwa na tani 207,928 zilizosafirishwa mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 3.3.

Kielelezo Na. 3.6: Shehena Iliyosafirishwa kwa Reli, 2024/25 na 2025/26 (Tani)



Chanzo: Wizara ya Uchukuzi

3.4.3 Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

Mpango uliwezesha kuimarika kwa Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Sayansi na Teknolojia (MTUSATE) ambao umekusanya zaidi ya shilingi bilioni 129, zikiwemo zaidi ya shilingi

bilioni 85 kutoka Serikalini; kuzinduliwa kwa programu ya Grand Challenges Tanzania Juni 2026; na kuimarisha ulinzi wa ubunifu wa ndani kupitia haki miliki.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: hataza zilizotolewa na BRELA ziliongezeka hadi 61 mwaka 2025/26 kutoka 30 mwaka 2024/25; alama za biashara na huduma zilizosajiliwa ziliongezeka hadi 3,455 kutoka 3,148; na nafasi ya Tanzania katika Fahirisi ya Ubunifu Duniani ilikuwa ya 121 kati ya nchi 139 mwaka 2025, kutoka nafasi ya 120 kati ya nchi 133 mwaka 2024.

3.4.4 Utafiti na Takwimu

Mpango uliwezesha utekelezaji wa Vipaumbele vya Taifa vya Utafiti vya 2021/22–2025/26 na Mpango Kabambe wa Pili wa Takwimu (TSMP II), pamoja na kuimarisha matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 katika upangaji, ufuatiliaji na tathmini ya maendeleo.


Utekelezaji wa viashiria katika eneo hili unaonesha kuwa alama ya Tanzania katika Kiashiria cha Utendaji wa Kitakwimu cha Benki ya Dunia (Statistical Performance Indicators – SPI) ilikuwa 68.2 mwaka 2024. Kiashiria hiki hutathmini uwezo na utendaji wa mfumo wa kitaifa wa takwimu katika uzalishaji, upatikanaji na matumizi ya takwimu kwa ajili ya maamuzi na upangaji wa maendeleo.

3.4.5 Mapinduzi ya Kidijitali, TEHAMA na Mawasiliano

Mpango uliwezesha kukamilisha ujenzi wa minara 758 ya mawasiliano katika kata 688 inayohudumia takriban watu milioni 8.5, na kupandisha hadhi minara 304 kutoka 2G kwenda 3G/4G; kukamilika kwa minara 495 kati ya 636 ya awamu inayofuata; kupanua Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano hadi km 15,167 kati ya km 16,280 zilizopangwa; Kuunganisha Wilaya 10 Nchini na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kufanya jumla ya wilaya 122 kati ya 139 na nchi jirani saba (7) kati ya nane (8) kuunganishwa; kutoa huduma ya Wi-Fi kwa umma katika maeneo 50; na kusajili anwani 12,857,892 katika Mfumo wa Anwani za Makazi (NaPA). Aidha, ukarabati wa vituo 32 vya kutolea huduma za Serikali katika eneo na dirisha moja uliendelea, pamoja na utekelezaji wa miradi ya ICT Parks na Tanzania ya Kidijitali.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: uwiano wa watumiaji wa intaneti uliongezeka hadi asilimia 85 mwaka 2025 kutoka asilimia 74 mwaka 2024; ueneaji wa intaneti uliongezeka hadi asilimia 89.7 Juni 2026 kutoka asilimia 79.3 mwaka 2025; wananchi waliofikiwa na mitandao ya simu waliongezeka hadi asilimia 98.65 kutoka asilimia 98.4; upatikanaji wa mtandao wa 4G uliongezeka hadi asilimia 94.39 Juni 2026 kutoka asilimia 90 mwaka 2024, na wa 5G hadi asilimia 34.18 kutoka asilimia 26; majengo yenye anwani za makazi yaliongezeka hadi 18,558,268 mwaka 2025/26 kutoka 18,186,000 mwaka 2024/25; na makosa ya kimtandao yaliyoripotiwa Polisi yaliongezeka hadi 1,323 kutoka 748 kati ya Julai – Aprili ya mwaka 2024/25 na 2025/26; na upenyo wa simu janja uliongezeka hadi asilimia 44.74 Juni 2026 kutoka asilimia 37 mwaka 2025.

Kielelezo Na. 3.7: Mwenendo wa Upatikanaji wa Mitandao ya 3G, 4G na 5G (Asilimia ya Watu), 2020/21 – 2025/26



Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

3.5 Misingi ya Uendelevu wa Taifa

3.5.1 Utawala Bora, Demokrasia, Usalama na Utulivu

Mpango uliwezesha kukamilika kwa Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki (IJC) tisa (9) vipya; kukamilika kwa majengo 72 ya Mahakama za Mwanzo; kutafsiriwa kwa sheria kuu 433 kwa lugha ya Kiswahili; kuanzishwa kwa madawati ya msaada wa kisheria katika Mamlaka 184 za Serikali za Mitaa; kufikia Ofisi za Mashtaka za Wilaya 118; na kuendelea na ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba uliofikia asilimia 94, ambapo wizara 15 kati ya 25 zimehamia. Kituo cha Menejimenti ya Maafa Nzuguni kimefikia asilimia 70. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Vitambulisho vya Taifa (NIDA); Upatikanaji wa Haki kwa Maendeleo Endelevu; PSRP III; e-Justice; na Strengthening Anti-Human Trafficking.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki vinavyotoa huduma viliongezeka hadi 18 Juni 2026 kutoka 9 mwaka 2024/25; wananchi wanaoishi katika mikoa yenye Mahakama Kuu inayofanya kazi waliongezeka hadi asilimia 97 mwaka 2025/26 kutoka asilimi 69 mwaka 2024/25, baada ya huduma kupanuka kutoka mikoa 14 hadi 25; majengo ya Mahakama za Mwanzo yaliongezeka hadi majengo 746 kutoka 674; wastani wa muda wa kutoa hukumu katika Mahakama Kuu ulipungua hadi siku 202 kutoka siku 730; watumishi waliopata mafunzo ya maadili ya utendaji katika utumishi wa umma waliongezeka hadi watumishi 30,966 mwaka 2025/26 kutoka watumishi 6,000 mwaka 2024/25; taasisi zinazotumia e - Mrejesho ziliongezeka hadi taasisi 207 mwaka 2024/25 kutoka 40 mwaka 2024/25; Tanzania ilishika nafasi ya 14 kati ya nchi 35 katika Fahirisi ya World Justice Project ya 2025, kutoka nafasi ya 15 kati ya 37;

na makosa makubwa ya jinai yaliyoripotiwa yalipungua hadi 39,027 kutoka 40,022 kati ya Julai – Aprili ya mwaka 2024/25 na 2025/26, huku ajali za barabarani zikipungua kwa asilimia 6.7 na vifo vitokanavyo na ajali kwa asilimia 16.4; na kiwango cha uhalifu nchini kilipungua hadi asilimia 3.2 mwaka 2024/25, kutoka asilimia 5.2 katika mwaka wa kizio.

3.5.2 Serikali za Mitaa

Mpango uliwezesha kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, matumizi ya mifumo ya kidijitali katika usimamizi wa mapato na utendaji, pamoja na kuimarisha uwezo wa rasilimali watu katika Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri. Utekelezaji wa viashiria unaonesha kuwa bajeti ya mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2025/26 ilikuwa shilingi trilioni 1.68. Hadi Desemba 2025, makusanyo halisi yalifikia shilingi bilioni 774.0, sawa na asilimia 94.4 ya makadirio ya shilingi bilioni 820.1 kwa kipindi cha Julai–Desemba 2025. Kwa mwaka mzima wa 2024/25, mapato ya ndani ya Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 1,437.3.

3.5.3 Utawala wa Kidijitali

Mpango uliwezesha kuunganisha mifumo 252 ya taasisi 200 kupitia GovESB, ikiwemo mifumo mipya 28; kuzindua Orodha ya Huduma za Serikali (Government Services Directory) tarehe 24 Juni 2026 ikiwa na huduma 9,777 za taasisi 554; kuzindua Mfumo wa Ngao wa usalama wa mtandao unaotumiwa na taasisi zaidi ya 700; kuunganisha taasisi 147 na mfumo wa NIDA; na kuanza kutumika kwa mfumo wa e-Utendaji katika taasisi zote 571 za umma.

Utekelezaji wa viashiria katika sekta hii unaonesha kuwa: watu waliosajiliwa na NIDA waliongezeka kutoka 879,213 mwaka 2024/25 hadi kufikia watu 1,772,985 mwaka 2025/26, na kufikisha jumla ya watu 27,374,283 hadi kufikia Juni 2026; taasisi zinazotumia mfumo wa e-Office zilifikia 425 kati ya 571 na zinazotumia saini za kidijitali 528 kati ya 780 Juni 2026.

3.5.4 Uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi

Mpango uliwezesha uboreshaji wa taswira ya Tanzania katika medani ya kimataifa kwa kuimarisha diplomasia ya siasa na uchumi kupitia ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa; kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika jumuiya na mashirika ya kikanda na kimataifa kwa maslahi ya Taifa; na kuchangia juhudi za kukuza amani, ulinzi na usalama kwa maendeleo jumuishi.

Utekelezaji wa Mpango umechangia: kuongezeka kwa uwakilishi wa Tanzania nje kupitia balozi 45 na konseli kuu tano; kuimarika kwa ushiriki wa Tanzania katika mikutano mbalimbali na kufanikisha Tanzania kushiriki mikutano 110 ya kikanda na kimataifa; Kufanyika kwa ziara 90 za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nje ya nchi na ziara 33 za viongozi wa nchi, Serikali na Mashirika mbalimbali nchini Tanzania. Aidha, ziara na mikutano hiyo imewezesha kusainiwa kwa mikataba na hati za makubaliano 81, kuanzishwa kwa safari za ndege za moja kwa moja katika baadhi ya vituo vya kimkakati, kuongezeka kwa

mchango wa Diaspora katika maendeleo ya Taifa, pamoja na Tanzania kupata nafasi za kimkakati katika jumuiya za kikanda na kimataifa.

Vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha matumizi na uenezaji wa Kiswahili katika ngazi ya kikanda na kimataifa. Juhudi hizo zimechangia kuongezeka kwa idadi ya nchi na watu wanaojifunza na kutumia Kiswahili, pamoja na kuimarisha nafasi ya lugha hiyo katika majukwaa ya kimataifa.

SEHEMU B: MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2026/27 KWA ROBO YA KWANZA

Serikali imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 kwa kuzingatia FYDP IV ili kufikia malengo ya Dira 2050. Katika kipindi cha mwaka 2026/27, Serikali ililenga kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani, kujenga uwezo wa watu na maendeleo ya jamii, uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, kutumia kikamilifu vichocheo vya maendeleo, mageuzi katika sekta za kimkakati, na kuimarisha misingi ya uendelevu wa taifa.

Katika kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani: Serikali imeendelea kudhibiti mfumuko wa bei, kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kuhakikisha kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje, kuimarisha ukuaji wa uchumi, kusimamia matumizi ya Serikali pamoja na sera za fedha na bajeti.

Kujenga uwezo wa watu na maendeleo ya jamii: Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo, 2014 toleo la 2023 kwa kuandaa na kutekeleza mitaala mipya, ili kujenga rasilimaliwatu yenye ujuzi unaohitajika kufikia malengo ya Dira 2050. Aidha, Serikali imeendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na ruzuku ya elimu bila ada kwa shule za msingi na sekondari, pamoja na kutekeleza miradi ya HEET, ESPJ II, EP4R, Support to VET, SEQUIP, GPE-TSP na Mfuko wa Elimu Tanzania. Vilevile, Serikali inaendelea kutoa ufadhili kupitia Samia Scholarship kwa wanafunzi kusoma Sayansi ya Data na Akili Unde nje ya nchi. Serikali imeendelea kuongeza fursa za ajira kupitia miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa na utekelezaji wa miradi mbalimbali. Aidha, Serikali inaendelea kuwajengea uwezo makandarasi wazawa na kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Urasimishaji wa Wafanyabiashara Ndogondogo ili kuwawezesha kiuchumi.

Serikali imeendelea kuwawezesha vijana kiuchumi kupitia upatikanaji wa mitaji, ujuzi na fursa za uzalishaji, ambapo mikopo 1,473 imetolewa kwa vikundi vya vijana vyenye wanufaika 40,263, huku vijana 30,137 wakipatiwa elimu ya fedha, ujasiriamali, usimamizi wa biashara na fursa za kiuchumi. Aidha, vituo viwili vya ubunifu vimetathminiwa kwa ajili ya ukarabati na kuimarisha ufanisi, na vikundi saba (07) vya vijana vyenye wanachama 80 vimeunganishwa na kuunda Vijana AMCOS, vikapatiwa mkopo wa pembejeo na zana za kilimo wenye thamani ya shilingi milioni 361.63 pamoja na kutengewa ekari 300 kwa ajili ya uzalishaji wa mahindi.

Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi: Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa mazingira kupitia utekelezaji wa shughuli mbalimbali, ikiwemo utoaji wa vibali kwa miradi mikubwa inayohitaji Tathmini za Athari kwa Mazingira na Kaguzi za Mazingira, ambapo vyeti 189 vya mazingira vilitolewa. Aidha, vibali 66 vya usimamizi wa taka hatarishi vilitolewa kwa wadau, hatua iliyowezesha usimamizi salama na urejelezaji wa taka hizo. Serikali pia imeendelea kuratibu hatua za kukabiliana na athari za mvua za El Niño katika maeneo ya mijini na vijijini, kuhamasisha matumizi ya nishati safi katika taasisi za umma, pamoja na kuratibu biashara ya kaboni, ambapo mapato yatokanayo na mauzo ya nje ya viwango vya kaboni yameongezeka kufikia Dola milioni 2. Aidha, mapato ya utalii yalifikia shilingi bilioni yalifikia bilioni 1.07.

Kutumia kikamilifu vichocheo vya maendeleo: Serikali imeendelea na ujenzi wa Reli ya Kati ya SGR ambapo hadi Agosti 2026 utekelezaji wa vipande vya Dar es Salaam – Morogoro (km 300) umekamilika na Morogoro – Makutupora (km 422) asilimia 98.79, Makutupora – Tabora (km 368) asilimia 15.54, Tabora – Isaka (km 165) asilimia 9.12; Isaka – Mwanza (km 341) asilimia 69.31, Tabora – Kigoma (km 506) asilimia 11.35 na Uvinza – Musongati (km 282) asilimia 0.62. Aidha, ujenzi wa viwanja vya ndege katika mikoa mbalimbali unaendelea na imefikia hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo, viwanja vya ndege vya Sumbawanga, Tabora na Geita ujenzi wake umekamilika. Ujenzi wa kiwanja cha Ndege cha Kigoma umefikia asilimia 75.5, Shinyanga (asilimia 97.5), Musoma (asilimia 70), Iringa (Awamu ya II) (asilimia 47), Tanga (asilimia 11.18), Moshi (asilimia 69), na Lake Manyara (asilimia 12.2). Aidha usimikaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege katika kiwanja cha ndege cha Arusha umekamilika. Vilevile, huduma ya Mkongo wa Taifa inaendelea kusambazwa katika wilaya mbalimbali nchini, na ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam unaendelea kuimarika kupitia ushiriki wa sekta binafsi.

Katika utekelezaji wa Mradi wa Reli ya TAZARA kwa upande wa Tanzania: upembuzi yakinifu na usanifu wa reli umefikia asilimia 95; maandalizi ya michoro na usanifu wa jengo la kuongozea treni, kituo cha mafunzo, Stesheni ya Kurasini na ukarabati wa Stesheni ya Dar es Salaam vimekamilika; ujenzi wa karakana ya Kongolo umefikia asilimia 85; ununuzi wa tani 5,250 za reli umekamilika; na mikataba ya ununuzi wa mabehewa 760 na utengenezaji wa vichwa vitatu vya treni vilisainiwa, ambapo uzalishaji wa mabehewa 300 na vichwa hivyo ulianza nchini China. Aidha, mradi umeajiri Watanzania takribani 296.

Serikali imepiga hatua katika kuongeza mtandao wa usambazaji wa gesi asilia na uwezo wa kuzalisha umeme hivyo kuweka msingi imara wa upatikanaji wa nishati ya uhakika kwa shughuli za uzalishaji na matumizi ya nyumbani. Aidha, uzalishaji wa gesi asilia ulikuwa futi za ujazo milioni 16,778, uwezo wa mitambo ya uzalishaji wa umeme ulifika MW 4,606.14, urefu wa Gridi ya Taifa ya umeme uliongezeka hadi km 8,845.38, kuunganishwa na umeme kwa vijiji vyote 12,318 na vitongoji 41,038 kati ya 64,359 sawa na asilimia 64, kuongezeka kwa vituo vya kujazia gesi asilia kwenye vyombo vya moto

kufikia 22, na ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania (EACOP) umefikia asilimia 92.7. Vilevile, huduma ya Mkongo wa Taifa inaendelea kusambazwa katika wilaya mbalimbali nchini, na ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam unaendelea kuimarika kupitia ushiriki wa sekta binafsi.

Mageuzi katika sekta za kimkakati: Serikali imeendelea kuimarisha usalama wa chakula, kupunguza upotevu wa mazao na kuongeza mauzo ya nje ya mazao ya kilimo. Vilevile, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya biashara, hatua iliyowezesha kuongezeka kwa uwekezaji wa moja kwa moja na kupungua kwa muda wa kuanzisha biashara. Hadi Septemba 2026, uwekezaji wa miradi ya Ubia wa sekta ya umma na sekta binafsi umeongezeka na kufikia miradi kumi (10). Miradi hiyo inajumuisha: ujenzi wa kituo cha biashara Kariakoo; ujenzi wa kituo cha usaifirishaji; uendeshaji na ukarabati wa bandari ya Dar es Salaam; ukarabati, uendeshaji, na usimamizi wa reli ya Tanzania - Zambia (TAZARA); ujenzi wa vituo vya ukaguzi wa magari; na uendeshaji wa mabasi yaendayo haraka Awamu ya Kwanza na ya Pili Dar es Salaam.

Katika maeneo mengine, Serikali inaendelea na umilikishaji wa viwanja na mashamba, ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama, na uendelezaji wa michezo, sanaa na ubunifu. Serikali imeendelea kuongeza upatikanaji wa taarifa za msingi za rasilimali madini kupitia utafiti wa kina wa jiofizikia, jiokemia na jiolojia. Hadi Septemba 2026, Sekta ya Madini imefanikiwa kubaini maeneo yatakayofanyiwa utafiti kupitia Mfuko wa Utafiti wa Madini; kuzindua programu ya kuendeleza wanawake vijana na makundi maalumu (Mining for Brighter Tomorrow - MBT) ambao utekelezaji wake umeanza kwa kutoa leseni 273 kwa vikundi 2,550 vya wachimbaji katika Mikoa ya Mara, Kagera, Shinyanga, Morogoro, Dodoma na Njombe; kuzindua programu ya kuendeleza wachimbaji wadogo; kuendelea kusimamia makusanyo ya maduhuli ya takribani shilingi bilioni 411.7; na kuendelea kushirikiana na wawekezaji kusimamia ujenzi wa miradi mikubwa ya madini ikiwemo ya Sengerema, Mantra na Mradi wa Niobium wa Panda Hili.

Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi na matumizi bora ya ardhi kupitia upimaji, urasimishaji, upangaji na usajili wa milki. Asilimia ya ardhi iliyopimwa imefikia asilimia 28, huku viwanja na mashamba mashamba na viwanja vilivyopimwa ikifikia 59,795. Aidha, mali 48,713 katika makazi yasiyopangwa zimerasimishwa na leseni 3,239 za makazi zimetolewa kwa wamiliki wa mali. Vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha mipango ya matumizi bora ya ardhi vijijini, huku ramani 88 za msingi zikiwa zimehuishwa, na Hatimiliki za Milki (CROs) 41,843 zimesajiliwa katika kipindi hicho. Vilevile, jumla ya hekta 265,804.51 zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji na ekari 875,360 zimetengwa na kulindwa kwa matumizi ya umma.

Serikali imewezesha kusainiwa kwa Mikataba na Hati za Makubaliano 16 katika sekta za kilimo, madini, ajira, usafirishaji na utalii. Aidha, ushirikishwaji wa Diaspora umeimarishwa kupitia *Diaspora Mapping* na uzinduzi wa *Zanzibar Diaspora Registration Portal*, huku juhudi za kukuza Kiswahili zikiendelea katika nchi mbalimbali. Vilevile, Serikali imeendelea

kuimarisha taswira ya Tanzania nje ya nchi kupitia ujenzi na ukarabati wa majengo ya uwakilishi, ikiwemo Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu Arusha (asilimia 59), Ubalozi Tanzania Uingereza (asilimia 38) na Ubalozi Tanzania Marekani (asilimia 35).

Sekta za michezo na ubunifu imeendelea kuimarika ambapo Tanzania imepiga hatua katika viwango vya kimataifa vya michezo, hususan kwa wanawake, huku nafasi katika viwango vya CAF ikifikia nafasi ya 18 kwa wanawake. Aidha, wachezaji 1,075 wameendelea kushiriki michezo ya kitaalamu, wakiwemo wanaume 825 na wanawake 250, huku wasanii watatu (03) wa muziki na wadau sita (06) wa filamu wakipokea tuzo za kimataifa. Vilevile, miradi 48 ya filamu imepatiwa mikopo, hatua inayochochea uwekezaji, ajira na ukuaji wa sekta za ubunifu na maudhui ya kidijitali.

Kuimarisha misingi ya uendelevu wa taifa: Serikali imeendelea kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika utumishi wa umma kupitia utoaji wa mafunzo ya maadili ya utendaji kwa watumishi 1,474 na kuwezesha taasisi za umma 22 kutumia Mfumo wa e-Mrejesho, hatua inayolenga kuongeza uwajibikaji, uwazi na mapambano dhidi ya rushwa katika utumishi wa umma.

SURA YA NNE

VIPAUMBELE VYA MPANGO KWA MWAKA 2027/28

4.1 Utangulizi

Vipaumbele vya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 vimeandaliwa kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele, malengo, shabaha na afua za kimkakati zilizoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 (FYDP IV). Vipaumbele hivi vinachangia katika utekelezaji wa malengo, shabaha na matarajio ili kufikia lengo kuu la Dira 2050 inayolenga kuifanya Tanzania kuwa taifa jumuishi lenye ustawi, haki na linalojitegemea.

4.2 Maeneo ya Kipaumbele ya Mpango

Mapendekezo ya Mpango kwa mwaka 2027/28 yamejikita katika maeneo sita (6) ya kimkakati yaliyoainishwa katika FYDP IV ambayo ni: (i) Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani; (ii) Kujenga Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii; (iii) Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi; (iv) vichocheo vya maendeleo; (v) Mageuzi katika Sekta za Kimkakati; na (vi) Kuimarisha Misingi ya Uendelevu wa Taifa

4.2.1 Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani

Kipaumbele hiki kinalenga kuweka mazingira thabiti ya usimamizi wa uchumi, kuongeza imani ya wawekezaji na kuwezesha utabirifu wa mwenendo wa uchumi. Maeneo yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na:

4.2.1.1 Utulivu na Utabirifu wa Uchumi Jumla

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kufikia ukuaji wa uchumi wa asilimia 6.6 mwaka 2027. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuhakikisha uthabiti wa sera za bajeti;
(ii) Kuimarisha ushirikiano wa kimataifa;
(iii) Kuongeza uwezo wa ufuatiliaji na kujenga uwezo wa kukabiliana na athari za mitikisiko ya nje;
(iv) Kutekeleza mageuzi ya kimfumo yatakayolenga kuboresha na kupanua minyororo ya ugavi wa ndani;
(v) Kudhibiti mfumuko wa bei za chakula; na
(vi) Kuongeza matumizi ya mifumo ya kidijitali katika malipo.

4.2.1.2 Kuimarisha Uwezo wa Kifedha wa Serikali

Katika mwaka 2027/28, Mapendekezo ya Mpango yanalenga kudumisha nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3 ya Pato la Taifa. Ili kufikia malengo hayo, vipaumbele vitakua katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha usimamizi wa vihatarishi vya kifedha;
(ii) Kuongeza uhimilivu wa kiuchumi;

(iii) Kufungua vyanzo vipya vya mapato yasiyo ya kodi; na
(iv) Kuboresha matumizi ya rasilimali za umma.

4.2.1.3 Uhimilivu na Usetushaji wa Sekta ya Nje

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kudumisha nakisi ya urari wa malipo ya kawaida usiozidi asilimia 2.5 ya Pato la Taifa. Ili kufikia shabaha hizo utekelezaji katika afua zifuatazo:

(i) Kupunguza utegemezi wa bidhaa ghafi;
(ii) Kujenga uchumi mseto wa uzalishaji na mauzo ya nje yaliyoongezwa thamani;
(iii) Kuongeza uzalishaji viwandani na uchakataji wa bidhaa za kilimo;
(iv) Kuwekeza katika mifumo ya uwezeshaji wa biashara na miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi; na
(v) Kuimarisha mtangamano katika biashara ya kikanda

4.2.2 Mageuzi katika Sekta za Kimkakati

4.2.2.1 Sekta ya Kilimo

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kufikia ukuaji wa sekta ya kilimo wa asilimia 6.46 mwaka 2027/28 na mapato ya mauzo ya nje ya sekta ya kilimo kufikia dola za Marekani bilioni 4.12. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuongeza thamani ya bidhaa za kilimo;
(ii) Kuzalisha bidhaa bora na ajira zenye staha;
(iii) Kujenga kongani za viwanda na kuendeleza ujuzi;
(iv) Kuongeza wigo wa upatikanaji wa mitaji kwa wakulima na wawekezaji wadogo na kati;
(v) Kuimarisha mifumo ya udhibiti;
(vi) Kuasili matumizi ya teknolojia za kidijitali ili kuimarisha ufuatiliaji wa vyanzo wa mazao na huduma za ugani;
(vii) Kuimarisha miundombinu wezeshi kwa ajili ya kuongeza mauzo ya nje ya mboga mboga; kukuza ufugaji wa samaki katika maziwa na maeneo ya nchi kavu; na
(viii) Kuhimiza matumizi ya mbinu bora za kilimo.

4.2.2.2 Sekta ya Viwanda

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza mchango wa sekta ya uzalishaji viwandani kufikia asilimia 7.58 ya Pato la Taifa mwaka 2027/28 na mchango wake katika mapato ya mauzo ya nje kufikia asilimia 12. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuendeleza kongani za viwanda na maeneo maalumu ya uchumi;
(ii) Kuendeleza viwanda vya kimkakati;
(iii) Kukuza ubunifu kupitia maeneo mahsusi ya ukuzaji wa teknolojia;
(iv) Kujenga ikolojia ya mfumo imara wa viwanda unaojiendesha kwa ufanisi;
(v) Kuziunganisha biashara ndogo, za kati na kubwa, katika minyororo ya biashara ya ugavi ya kimataifa;
(vi) Kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula;

(vii) Kukuza viwanda vya nguo na mavazi;
(viii) Kuongeza thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi; na
(ix) Kuzingatia viwango vya kimataifa vya ubora wa bidhaa na mazingira.

4.2.2.3 Sekta ya Ujenzi

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza mchango wa sekta ya ujenzi kufikia asilimia 13.88 ya Pato la Taifa mwaka 2027/28. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuwezesha wakandarasi na makampuni ya ndani ya ujenzi kushindana na kuongeza ushiriki katika miradi mikubwa ya ujenzi;
(ii) Kuwezesha matumizi ya mifumo ya kuasili na uhawilishaji wa teknolojia za kisasa za ujenzi, sambamba na hatua za kuendeleza ujuzi wa wahandisi wa ndani; na
(iii) Kuongeza tija, ubora na kuinua ufanisi katika sekta ya ujenzi.

4.2.2.4 Sekta ya Madini na Uchimbaji

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza mchango wa sekta ya madini kufikia asilimia 11.06 ya Pato la Taifa mwaka 2027/28 na mchango wake katika mapato ya mauzo ya nje kufikia asilimia 49.6. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuvutia uwekezaji mkubwa katika uchenjuaji, usafishaji, uchakataji na utumiaji wa madini kwa ajili ya kutengeneza bidhaa za viwandani zenye thamani kubwa;
(ii) Kukamilisha utafiti wa kijiolojia;
(iii) Kuimarisha usimamizi wa uendeshaji wa sekta ya madini;
(iv) Kuimarisha nafasi ya Tanzania katika soko la kimataifa la madini; na
(v) Kurasimisha na kusaidia wachimbaji wadogo kwa kuwawezesha wanawake na vijana.

4.2.2.5 Sekta ya Mafuta na Gesi

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza mtandao wa usambazaji wa gesi asilia kufika kilometa 289.57. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kukuza matumizi ya gesi asilia, ukichagizwa na mikakati ya kujenga uchumi wa viwanda vya ndani; na
(ii) Kuanzisha kituo cha umahiri cha kuendeleza ujuzi unaohitajika katika sekta.

4.2.2.6 Sekta ya Utalii

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza mchango wa sekta ya utalii katika mapato ya mauzo ya nje kufikia asilimia 30.2. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuendeleza utalii wa kimataifa wa fukwe, utamaduni, matukio na mikutano; na
(ii) Kuongeza msukumo katika uwekaji wa mifumo ya kidijitali kupitia majukwaa ya utalii mamboleo.

4.2.2.7 Sekta ya Fedha

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza ujumuishaji, upanuzi, na uimara wa huduma za fedha. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha usimamizi wa vihatarishi, na kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha kwa biashara ndogo na za kati, sekta ya kilimo na wakazi wa vijijini;
(ii) Kuimarisha taasisi za fedha za maendeleo na kukuza ikolojia ya upatikanaji wa mitaji ya ubia;
(iii) Kuimarisha masoko ya mitaji; na
(iv) Kupanua wigo wa huduma za bima, sanjari na kuendesha programu za elimu ya fedha kitaifa.

4.2.2.8 Sekta ya Michezo, Sanaa na Ubunifu

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza ukuaji halisi wa sekta ya michezo, sanaa na ubunifu kufikia asilimia kufikia asilimia 10. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kukuza biashara, weledi na upatikanaji wa mapato kutokana na kazi za ubunifu;
(ii) Kujenga minyororo jumuishi ya thamani kupitia uwekezaji katika miundombinu, maendeleo ya vipaji, mifumo ya fedha na biashara ya kazi za ubunifu;
(iii) Kujenga vyuo vya kikanda vya vijana vya kukuza vipaji na kituo cha kitaifa cha michezo ya ubora wa juu na ubunifu;
(iv) Kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya viwanja kwa ajili ya AFCON; na
(v) Kuboresha mfumo wa usajili wa waandaaji wa maudhui ya kidijitali, ulinzi wa hakimiliki, na ukuzaji wa ushirikiano na majukwaa ya kimataifa ya kidijitali.

4.2.2.9 Maendeleo ya Makazi na Biashara ya Ardhi na Majengo

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza ardhi iliyopimwa kufikia asilimia 42.92. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha usimamizi wa ardhi, kupanua upatikanaji wa fedha za ujenzi wa nyumba, na kuharakisha maendeleo ya miji iliyopangwa.;
(ii) Kulinda haki miliki za ardhi, kuboresha mifumo ya umiliki, kuongeza matumizi ya mifumo ya kidijitali katika umilikishaji wa ardhi na miamala, pamoja na kuongeza upatikanaji wa ardhi iliyopimwa iliyohudumiwa na iliyopangwa vizuri;
(iii) Kuimarisha taasisi za fedha za nyumba, kupunguza gharama za mikopo ya nyumba kuongeza matumizi ya masoko ya mitaji kupitia dhamana za uwekezaji katika majengo; na
(iv) Kuboresha maendeleo ya miji ya kisasa yatakayoimarisha upatikanaji wa usafiri wa umma, maeneo ya biashara na vituo vya ugavi.

4.2.2.10 Mageuzi ya Biashara na Shughuli za Kibiashara

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza thamani ya mauzo ya nje kwa Pato la Taifa kufikia asilimia 21.1 na kuongeza mchango wa Tanzania kwenye biashara baina ya nchi wanachama kikanda kufikia asilimia 17.8. Ili kufikia malengo hayo, vipaumbele vitakuwa katika afua zifuatazo:

(i) Kuondoa utegemezi wa mauzo ya bidhaa ghafi na kuelekea katika mfumo shindani unaotumia teknolojia ya kidijitali na kushiriki kikamilifu katika minyororo ya thamani ya kikanda na kimataifa;

(ii) Kutumia kikamilifu fursa za usindikaji wa mazao ya kilimo, matumizi ya madini yanayohitajika katika uzalishaji wa bidhaa muhimu za viwandani, pamoja na uwekezaji adilifu katika utafiti na maendeleo;

(iii) Kujenga majukwaa ya kisasa ya biashara mtandao na mifumo ya malipo ya kidijitali katika biashara za kikanda na kimataifa;

(iv) Kuimarisha biashara ya ndani na miundombinu ya masoko na maghala; na

(v) Kuwezesha ushiriki wa wafanyabiashara ndogo na za kati, wanawake na Vijana katika minyororo ya thamani ya kikanda na kimataifa.

4.2.2.11 Kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza mchango wa uwekezaji wa sekta binafsi kwenye rasilimali za kudumu kufikia asilimia 77. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kufanya mapitio ya kina ya mfumo wa taasisi, udhibiti na urekebu, kupunguza gharama za kutimiza masharti, kurahisisha taratibu za kisheria, kutoa motisha kwa wafanyabiashara, na kujenga mazingira ya biashara yanayokidhi viwango vya kimataifa;

(ii) Uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu na teknolojia za kidijitali, katika biashara ndogo na za kati, kuziwezesha kujiunga na minyororo ya thamani ya Kimataifa; na

(iii) Kuwekeza katika viwanda vinavyotumia nguvukazi kwa wingi, hususan katika mikoa yenye kiwango cha chini cha maendeleo ya kiuchumi pamoja na kuimarisha ushiriki wa Watanzania katika uwekezaji wa kigeni kupitia mifumo ya kisheria na kiutendaji.

4.2.2.12 Mikakati ya Ushirikiano kati ya Nchi, Kikanda na Kimataifa katika Dunia Inayobadilika

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza hisa za uwekezaji wa nje kufikia dola za Marekani milioni 386.18. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi;

(ii) Kutumia kikamilifu shughuli za kidiplomasia katika kutangaza biashara na uwekezaji;

(iii) Kubaini na kutumia fursa za ushirikiano na washirika wa kimkakati kwa kuzingatia mabadiliko ya uchumi wa dunia, maslahi ya Taifa na fursa za uwekezaji, biashara, teknolojia na maendeleo ya viwanda na

(iv) Kusasisha miundombinu ya biashara, usafirishaji na uchukuzi kwa kuwekeza katika bandari za kisasa, matumizi ya akili unde, mifumo ya kidijitali ya biashara na usimamizi wa kanzidata, pamoja na nyenzo za kisasa za kidiplomasia.

4.2.2.13 Urasimishaji wa Uchumi na Usimamizi Wake

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kupunguza mchango wa sekta isiyo rasmi katika Pato la Taifa kufikia asilimia 44.6. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kupunguza vikwazo vya kiutawala na kifedha vinavyokwamisha biashara, kwa kuunganisha biashara mbalimbali katika mkondo wa uchumi rasmi;

(ii) Kuanzisha mifumo ya kidijitali ya usajili kupitia taasisi moja, kutoa motisha zinazolenga biashara mahsusi, pamoja na utekelezaji wa programu za kuinua ujuzi; na

(iii) Kutoa fursa kwa biashara zisizo rasmi kuingia katika minyororo rasmi ya ugavi, kupata mikopo na ulinzi wa kisheria.

4.2.3 Kujenga Uwezo wa Rasilimali Watu na Maendeleo ya Jamii

Eneo hili linalenga kuimarisha uwekezaji katika elimu, afya, huduma za maji safi na salama ili kujenga nguvukazi yenye afya, maarifa na ujuzi unaokidhi mahitaji ya soko la ajira. Maeneo muhimu yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na:

4.2.3.1 Jamii Iliyoelimika, Yenye Ujuzi na Inayojifunza

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha IV kwenda V kufikia asilimia 26.24. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za malezi na makuzi ya watoto na elimu bora ya awali kwa wote ili kuimarisha maandalizi yao ya kielimu na maisha;

(ii) Kuwekeza kimkakati katika maendeleo ya walimu, hususan katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati;

(iii) Kuendelea na maandalizi ya kundi rika mbili (Double cohort) na

(iv) Kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia kwa kutumia zana za kidijitali na miundombinu ya kisasa.

4.2.3.2 Nguvukazi Yenye Uwezo na Ari

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza nguvukazi yenye uwezo wa juu kufikia asilimia 6.6, na yenye uwezo wa kati asilimia 21. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuwianisha mifumo ya elimu na mafunzo ili kuendana na mahitaji ya sasa ya uchumi wa viwanda; na

(ii) Kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za elimu na sekta ya uzalishaji kwa kuweka msisitizo wa mafunzo kwa vitendo kwa ubia kati ya sekta za umma na binafsi.

4.2.3.3 Demografia na Idadi ya Watu

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kupunguza kiwango cha utegemezi wa umri kufikia asilimia 84.2. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuwianisha kwa makusudi, mifumo ya elimu na mafunzo ya ufundi na stadi za kazi na mahitaji halisi ya ujuzi kwa uchumi wa kisasa;
(ii) Kujenga utamaduni wa ujasiriamali kwa vijana na kuwaunganisha na fursa za uchumi wa kidijitali na ajira mtandao;
(iii) Kuimarisha usawa wa kijinsia kwa kuwawezesha wanawake na vijana;
(iv) Kukuza ushiriki wenye tija wa watanzania waishio ughaibuni; na
(v) Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya ya uzazi na mifumo imara ya kinga ya jamii kwa wazee.

4.2.3.4 Soko na Taratibu za Ajira

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza kiwango cha ushiriki wa nguvukazi kufikia asilimia 73.76. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kupunguza utegemezi wa ajira katika shughuli zisizo rasmi na zenye tija ndogo na kujielekeza kwenye ajira zenye staha na tija kubwa kwa kuweka mazingira wezeshi ya kukuza biashara changa, ndogo na za kati zinazotumia teknolojia za kisasa;
(ii) Kuweka mazingira ya kuvutia uwekezaji mkubwa unaotoa ajira nyingi kwa wakati mmoja;
(iii) Kuwianisha moja kwa moja uendelezaji wa ujuzi na mahitaji halisi ya sekta zenye kasi kubwa ya ukuaji; na
(iv) Kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji wa ubia kati ya sekta za umma na binafsi.

4.2.3.5 Jamii Yenye Hifadhi na Muundo Jumuishi

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza kiwango cha waliojiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii kufikia asilimia 13.31. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuunganisha sekta isiyo rasmi katika mifumo ya kinga ya jamii;
(ii) Kubadili mifumo ya kinga ya jamii kwa kushirikisha sekta binafsi na kuongeza kipato na shughuli za kujikimu;
(iii) Kuimarisha usalama wa watumishi katika maeneo ya kazi; na
(iv) Kujumuisha huduma muhimu, ikiwemo afya ya akili katika mifumo ya elimu na maisha.

4.2.3.6 Huduma Bora za Afya kwa Wote

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kupunguza kiwango cha vifo vya watoto wachanga kufikia 30.6 kwa kila vizazi hai 1000, na kuongeza kiwango cha wazazi wanaohudumiwa na wataalamu wa afya kufikia asilimia 86.12. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha kinga dhidi ya magonjwa kama malaria;

(ii) Kuwekeza katika mifumo ya afya ya kinga, ubunifu wa kidijitali na uzalishaji wa bidhaa za afya nchini; na
(iii) Kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya;
(iv) Kuwekeza katika wataalamu wa afya;
(v) Kuimarisha uwekezaji wa viwanda vya uzalishaji dawa na vifaa tiba nchini;
(vi) Kuendelea na ujenzi wa hospitali bingwa na bobezi kwa ajili ya tiba utalii; na
(vii) Kuongeza huduma za bima ya afya kwa wote.

4.2.3.7 Usalama wa Chakula na Lishe Ulioimarishwa

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kupunguza kiwango cha utapia mlo mkali wa dharura wa watoto wenye umri wa miezi 0 – 59 kufikia asilimia 2.46 na kupunguza kiwango cha udumavu kwa watoto wenye umri wa miezi 0 – 59 kufikia asilimia 23.9. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuongeza upatikanaji wa vyakula vyenye virutubisho muhimu;
(ii) Kuhakikisha usalama wa chakula;
(iii) Kuwekeza katika kilimo kinachostahimili athari za mabadiliko ya tabianchi;
(iv) Kupunguza upotevu baada ya mavuno; na
(v) Kuimarisha minyororo ya thamani.

4.2.3.8 Upatikanaji na Uunganishaji wa Maji na Usafi wa Mazingira

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza upatikanaji wa maji katika maeneo ya mjini na vijijini kufikia asilimia 93.4 na 85.76 mtawalia. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kubadili mwelekeo kutoka kuongeza huduma za usambazaji pekee na kuwekeza katika usimamizi jumuishi, wenye ufanisi na unaostahimili athari za mabadiliko ya tabianchi;
(ii) Kuendeleza matumizi ya nishati jadidifu hususan katika mifumo ya maji inayotumia umeme wa jua;
(iii) Kuimarisha usimamizi, uhifadhi, na uendelezaji wa rasilimali za maji; na
(iv) Kuhakikisha huduma bora za usafi wa mazingira kwa wote.

4.2.3.9 Jamii yenye Mshikamano, Inayowajibika na Kushirikiana

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kupunguza kiwango cha ukatili wa kijinsia kufikia asilimia 31.34. na kupunguza alama ya wastani ya farihisi ya uhalifu kufikia 51.04. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kukuza usawa wa kijinsia kupitia mageuzi ya kisheria na programu za kimkakati za uongozi kwa wanawake katika sekta zote;
(ii) Kuweka mkazo katika maadili kupitia mfumo wa elimu;
(iii) Kuimarisha malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto;
(iv) Kuimarisha familia katika malezi na makuzi; na
(v) Kuhamasisha majadiliano ya kijamii kupitia sanaa na utamaduni.

4.2.3.10 Maendeleo Jumuishi Vijijini

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza farihisi ya maendeleo vijijini kufikia 0.38. Ili kufikia malengo hayo, vipaumbele vitakua katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha usalama wa umiliki wa ardhi,
(ii) Kuwekeza katika miundombinu ya kilimo inayostahamili mabadiliko ya tabianchi;
(iii) Kuboresha barabara vijijini; na
(iv) Kuongeza upatikanaji wa huduma na elimu za kifedha kwa wanawake na vijana.

4.2.3.11 Mageuzi ya Vyama vya Ushirika

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika kufikia 13,231,000. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuboresha miundo na mifumo ya utawala wa vyama vya ushirika ili kuongeza uwajibikaji , uwazi na ushindani; na
(ii) Kuongeza upatikanaji wa mitaji kwa gharama nafuu.

4.2.3.12 Kupanua Tabaka la Kipato Cha Kati

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza idadi ya watu walioko katika tabaka la kipato cha kati kufikia asilimia 14.4. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuinua kipato cha jamii kwa kutumia njia mseto na jumuishi;
(ii) Kuwawezesha wananchi kumiliki ardhi na mali zisizohamishika; na
(iii) Kuendeleza sekta za uchumi wa kijani na buluu.

4.2.4 Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi

Eneo hili linalenga kujenga uchumi endelevu, unaostahimili mabadiliko ya tabianchi na unaotumia maliasili kwa ufanisi, huku ukilinda mazingira, kuongeza fursa za kiuchumi na kuboresha ustawi wa wananchi. Maeneo mahsusi ya kipaumbele ni:

4.2.4.1 Uhifadhi wa Mazingira

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza nafasi ya Tanzania katika nchi za Afrika kwenye farihisi katika kukabiliana na athari za mazingira kufikia 16.8 na farihisi ya utendaji katika uhifadhi wa mazingira kufikia 17.4. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa mazingira;
(ii) Kukabiliana na athari za El-Nino;
(iii) Kuzingatia vigezo vya mazingira, utawala bora katika uwekezaji na ugharamiaji wa miradi; na
(iv) Kuiwezesha jamii kulinda rasilimali katika maeneo yao na kuchochea ukuaji wa uchumi unaotokana na uhifadhi wa mazingira.

4.2.4.2 Ukuaji Endelevu wa Miji Iliyopangika na Kusimamiwa Vizuri

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kupunguza kiwango cha ardhi yenye makazi yasiyo rasmi kufikia asilimia 45.4 na kuongeza mikoa yenye mipango kabambe na mipango miji kufikia asilimia 88.6. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuchukua hatua zinazozingatia mbinu za kisasa za usimamizi wa ujenzi wa miji;
(ii) Kuimarisha afya na ustawi wa wananchi kwa kutumia mifumo ya kisasa, mathalan mifumo ya usafiri wa umma ya kisasa; na
(iii) Kutumia mfumo wa ubia kati ya serikali na sekta binafsi katika kupunguza nakisi ya nyumba za makazi.

4.2.4.3 Mageuzi kwa Usimamizi Endelevu wa Ardhi

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza kiwango cha ardhi iliyosajiliwa na kupatiwa hatimiliki kufikia asilimia 40. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kujumuisha masuala ya tabianchi katika mipango ya maendeleo;
(ii) Kuhamasisha mbinu bunifu za fedha, kama hatifungani za kijani, ili kugharamia afua za maendeleo;
(iii) Kufanya maboresho ya kina ya sheria yatakayowezesha upatikanaji wa ardhi kwa usawa;
(iv) Kuanzisha mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa ardhi;
(v) Kuanzisha benki ya kitaifa ya ardhi ; na
(vi) Kuandaa mipango maalumu ya matumizi ya ardhi kwa maendeleo ya viwanda.

4.2.4.4 Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kupunguza kiwango cha uharibifu wa ardhi kufikia asilimia 15.2. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kufungamanisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika mipango ya kitaifa;
(ii) Kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu na teknolojia zinazozingatia athari za mabadiliko ya tabianchi katika kilimo, uchukuzi na viwanda;
(iii) Kuweka mifumo imara ya taifa ya kukabiliana na athari za mazingira; na
(iv) Kuongeza bima dhidi ya vihatarishi vya kimazingira.

4.2.4.5 Uwezo wa Taasisi na Mifumo ya Utoaji wa Tahadhari

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza idadi ya watu wanaopata taarifa tahadhali ya mapema kwa wakati sahihi kufikia asilimia 13.2.

4.2.4.6 Kuimarisha ushiriki katika Biashara ya Kaboni

(i) Kujenga mfumo wa kidijitali wa kiwango cha kimataifa wa ufuatiliaji, upimaji, utoaji taarifa na uthibitishaji;
(ii) Kuanzisha mfumo wazi wa uhifadhi wa kumbukumbu za kitaifa unaothibitisha uadilifu na kuvutia mitaji ya kimataifa ya programu na biashara za kaboni;

(iii) Kutengeneza kanzidata ya miradi inayokidhi masharti ya biashara ya kaboni katika sekta za misitu, uchumi wa buluu na mbinu endelevu za uendeshaji wa kilimo; na
(iv) Kuweka mifumo ya uwazi inayowezesha ushiriki wa jamii, vyama vya ushirika vya maeneo husika, pamoja na mgawanyo wa manufaa kutasaidia kuhakikisha kuwa biashara hii inakuwa jumuishi.

4.2.4.7 Kuchagiza Manufaa ya Uchumi wa Buluu

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza mchango wa uvuvi na ufugaji wa viumbe wa majini katika Pato la Taifa kufikia asilimia 2.42. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuboresha miundombinu ya bahari, maziwa na mito ili iwe katika kiwango cha kimataifa;
(ii) Kuimarisha usafirishaji wa majini kwa kutumia teknolojia za kisasa za bandari; na
(iii) Kuongeza udhibiti wa maeneo ili kulinda ikolojia.

4.2.5 Kutumia Kikamilifu Vichocheo vya Maendeleo

4.2.5.1 Nishati

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza uwezo wa mitambo wa uzalishaji wa umeme kufikia MW 4,804 na kuongeza kiwango cha matumizi ya umeme kwa kila mtu kufikia kWh 342. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuboresha miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme;
(ii) Kufanya mabadiliko ya kimkakati kuelekea matumizi mseto ya vyanzo vya uzalishaji, hususan nishati jadidifu.

4.2.5.2 Mifumo ya usafirishaji na Uchukuzi Fungamanishi

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza mchango wa sekta ya uchukuzi katika Pato la Taifa kufikia asilimia 8.8 na kuongeza ukuaji halisi wa sekta ya uchukuzi kufikia asilimia 5.96. Ili kufikia malengo hayo, vipaumbele vitakua katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikiwemo bandari, reli, barabara na viwanja vya ndege; na
(ii) Kushirikisha sekta binafsi katika uendelezaji na uendeshaji wa huduma za uchukuzi.

4.2.5.3 Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza kiwango cha matumizi ghafi ya utafiti na maendeleo katika Pato la Taifa kufikia asilimia 0.67. Ili kufikia malengo hayo, vipaumbele vitakua katika afua zifuatazo:

(i) Kuanzisha mifumo maalum ya ugharamiaji wa shughuli za ubunifu; na
(ii) Kuimarisha ulinzi wa miliki za ubunifu.
(iii) Kuimarisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

4.2.5.4 Utafiti na Maendeleo

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza matumizi ya kitaifa katika utafiti na maendeleo kama asilimia ya Pato la Taifa kufikia asilimia 0.67. Ili kufikia malengo hayo, vipaumbele vitakua katika afua zifuatazo:

(i) Kuanzisha mfumo wa kitaifa unaounganisha moja kwa moja uvumbuzi wa kisayansi na matumizi ya kibiashara; na
(ii) Kuanzisha ushirikiano madhubuti kati ya sekta za umma na binafsi.

4.2.5.5 Matumizi ya Takwimu

(i) Kuimarisha ushirikiano wa kimkakati kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; na
(ii) Kujenga uwezo wa rasilimali watu katika maeneo mahususi.

4.2.5.6 Mapinduzi ya Kidijitali

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza idadi ya watu wanaotumia intaneti ya kasi kufikia asilimia 52 na kuongeza mchango wa TEHAMA katika Pato la Taifa kufikia asilimia 12.58. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuongeza upatikanaji wa huduma za intaneti ya kasi nchi nzima; na
(ii) Kukuza sekta ya ndani ya ubunifu.

4.2.5.7 Miundombinu na Huduma za TEHAMA

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza upenyo wa intaneti kufikia asilimia 86.78. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuongeza upatikanaji wa miundombinu na vifaa vya kidijitali vilivyo salama, vyenye kasi, na gharama nafuu;
(ii) Kuimarisha mawasiliano katika kila pembe ya nchi;
(iii) Kujenga nguvukazi yenye ujuzi na uelewa wa kidijitali kupitia taasisi maalum za mafunzo, mitaala ya kisasa, na programu endelevu za kuwajengea uwezo wataalamu; na
(iv) Kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

4.2.5.8 Huduma za Mawasiliano na Posta

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza idadi ya watu wanaoweza kupata huduma za posta ndani ya kilometa tano (5) kufikia asilimia 83 na kuongeza idadi ya watu wanaofikiwa na intaneti ya kasi ya mkononi (5G) kufikia asilimia 43.6. Ili kufikia malengo hayo, vipaumbele vitakua katika afua zifuatazo:

(i) Kuunda mtiririko jumuishi na wenye ufanisi wa bidhaa, habari, na huduma; na
(ii) Kuunganisha mifumo ya posta usafirishaji wa vifurushi na biashara mtandaoni.

4.2.5.9 Mazingira Wezeshi ya Biashara na Uwekezaji

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza farihisi ya ubora na udhibiti kufikia 0.33. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kupitia mpango wa kuboresha mazingira na biashara;
(ii) Kuendeleza maeneo maalumu ya kiuchumi;

(iii) Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi kupitia utaratibu wa ubia; na
(iv) Kufanya urasimishaji wa shughuli za uchumi.

4.2.6 Kuimarisha Misingi ya Uendelevu wa Taifa

Kipaumbele hiki kinalenga: Kuimarisha uwazi, uwajibikaji, maadili, na tunu za kidemokrasia, pamoja na amani na utulivu; kuimarisha utumishi wa umma unaoendana na mahitaji ya wananchi, unaowajibika na unaozingatia maadili; na kuimarisha uadilifu na kuaminika kwa taasisi zinazosimamia mahusiano ya wananchi. Maeneo yatakayopewa kipaumbele katika eneo hili ni:

4.2.6.1 Utawala Bora, Demokrasia, Usalama na Utulivu

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza farihisi ya utulivu wa kisiasa, kutokuwepo kwa ghasia na ugaidi kufikia 0.01 na kuongeza farihisi ya ufanisi wa Serikali kufikia -0.4. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuweka mfumo imara wa kudhibiti uhalifu wa mtandaoni;
(ii) Kuimarisha mifumo ya utawala bora;
(iii) Kuboresha sheria ili kuendana na utekelezaji wa Dira 2050; na
(iv) Kuimarisha uwajibikaji.

4.2.6.2 Serikali za Mitaa Thabiti na Zenye Ufanisi

Katika kipindi cha mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza idadi ya huduma zilizowekwa kidigitali katika ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kufikia asilimia 47. na kupunguza alama ya wastani ya farihisi ya uhalifu kufikia 51.04. Ili kufikia malengo hayo, vipaumbele vitakua katika afua zifuatazo:

(i) Kuziwezesha Serikali za Mitaa na jamii kuwa wadau wakuu na injini za maendeleo;
(ii) Kujenga mifumo madhubuti ya wananchi kutoa mrejesho wa maoni; na
(iii) Kujenga uwezo wa serikali za mitaa.

4.2.6.3 Matumizi Sahihi ya Takwimu

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza idadi ya watu wenye vitambulisho vya kidigitali vilivyounganishwa na huduma za baruapepe za umma kufikia asilimia 60. Ili kufikia shabaha hizo, utekelezaji utajikita katika afua zifuatazo:

(i) Kuimarisha utawala wa kidijitali unaotumia mifumo inayowasiliana na takwimu sahihi; na
(ii) Kuunganisha majukwaa ya TEHAMA yaliyogawanyika hadi ngazi ya chini.

4.2.6.4 Mabadiliko ya Mitazamo na Fikra

Katika mwaka 2027/28, Mpango unapendekeza kuongeza alama ya Tanzania katika farihisi ya maendeleo ya jamii kufikia 60.64.

4.3 Programu za Kielelezo

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 utaendelea kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa Programu za Kielelezo ikijumisha miradi shikizi na maeneo ya minyororo ya thamani kama zilivyoainishwa katika FYDP IV. Programu hizo ni:

(i) Mji wa Ikolojia ya Bahari Bagamoyo na Usafirishaji Fungamanishi;
(ii) Kitovu Changamani cha Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga;
(iii) Programu ya Kitaifa ya Umwagiliaji na Mageuzi ya Viwanda vya Uchakataji wa Mazao;
(iv) Kitovu cha Teknolojia na Uchakataji wa Madini Adimu Dodoma;
(v) Kiwanda cha Kuchakata Gesi asilia ya Kimiminika Lindi;
(vi) Kitovu cha Kisasa cha Viwanda na Uchumi wa Buluu katika Ukanda wa Ziwa Makuu; na
(vii) Programu Shirikishi ya Uendelezaji wa Miji Nchini.

Afua mahususi za utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele katika mwaka 2027/28 zimeainishwa katika **kiambatisho Na. I**. Vile vile maelezo ya kina yanayohusu programu za kielelezo yameainishwa katika **kiambatisho Na.II.**

SURA YA TANO

SEKTA BINAFSI

5.1 Utangulizi

Sekta binafsi ni mhimili muhimu wa utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV) katika kufikia malengo ya Dira 2050. Sekta hii ni kichocheo cha uwekezaji, uongezaji wa thamani katika bidhaa na huduma, matumizi ya teknolojia na ubunifu, uzalishaji wa ajira, pamoja na kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika minyororo ya thamani ya kikanda na kimataifa. Serikali inalenga kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika maendeleo na utekelezaji wa FYDP IV kupitia uwekezaji, biashara, ubunifu, ugharamiaji na utekelezaji wa miradi ya kimkakati.

Aidha, sura hii imeainisha mchango wa sekta binafsi katika uchumi, mazingira ya biashara na uwekezaji, na maeneo ya kipaumbele kwa uwekezaji. Aidha, inafafanua ushiriki wa sekta binafsi katika programu za kielelezo na miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP); hatua za kuwezesha biashara za ndani; viashiria na mfumo wa kufuatilia uwekezaji halisi; pamoja na mikakati ya ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28.

5.2 Mwenendo wa Mchango wa Sekta Binafsi

Shughuli za sekta binafsi zimeendelea kukua ambapo jumla ya shughuli 257,405 zilisajiliwa mwaka 2024 ikilinganishwa na shughuli 219,371 mwaka 2023. Ongezeko hili liliongozwa na sekta ya viwanda kutoka asilimia 8.3 mwaka 2023 kufikia asilimia 14.3 mwaka 2024; sekta ya kilimo kutoka asilimia 0.2 mwaka 2023 kufikia asilimia 0.5 mwaka 2024; na sekta ya huduma kutoka asilimia 91.5 mwaka 2023 kufikia asilimia 85.1 mwaka 2024. Aidha, katika mwaka 2025, mikopo iliyotolewa na benki za biashara kwa sekta binafsi iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 44,603.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 36,097.4 mwaka 2024. Hali hii inaakisi kuongezeka kwa uwekezaji wa sekta binafsi katika shughuli za uchumi. Vilevile, kiwango cha ajira katika sekta isiyo rasmi kimeongezeka kutoka asilimia 27.3 mwaka 2024 hadi asilimia 28.2 mwaka 2025.

Aidha, kiwango cha ukuzaji wa rasilimali kilichofanywa na sekta binafsi kiliongezeka kutoka shilingi milioni 50,244,050 mwaka 2024 kufikia milioni 52,547,201 mwaka 2025; mikopo kwa sekta binafsi ilikua kutoka asilimia 12.4 mwaka 2024 kufikia asilimia 23.6 mwaka 2025; na kiwango cha amana katika benki za biashara kimeongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 40.05 mwaka 2024 kufikia dola za Marekani bilioni 53.03 mwaka 2025.

Sekta za uzalishaji na utoaji wa huduma zimeendelea kunufaika na mchango wa sekta binafsi kupitia uwekezaji na shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Miongoni mwa matokeo yaliyopatikana ni uzalishaji wa tani 50.88 za mbegu; kuongezeka kwa vituo vya huduma za afya vinavyomilikiwa na sekta binafsi kutoka vituo 4,123 mwaka 2024 hadi


vituo 4,368 mwaka 2025, ambapo ongezeko kubwa lilijitokeza katika polyclinic, zahanati na hospitali; pamoja na kuongezeka kwa idadi ya shule zinazomilikiwa na sekta binafsi kutoka shule 314,668 mwaka 2024 hadi shule 335,131 mwaka 2025.

5.2.1 Mchango katika Uwekezaji

Uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje uliongezeka kwa asilimia 12.1 na kufikia dola za Marekani milioni 24,754.1 mwaka 2024 kutoka dola za Marekani milioni 22,074.4 mwaka 2023. Kati ya kiasi hicho, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ulifikia dola za Marekani milioni 21,698.9, sawa na asilimia 87.7, uwekezaji wa hisa ulifikia dola za Marekani milioni 272.7 (asilimia 1.1) na uwekezaji wa mwingine ulifikia dola za Marekani milioni 2,782.5 (asilimia 11.2). Uwekezaji huo ulielekezwa zaidi katika uchimbaji wa madini, huduma za fedha na bima, uchakataji wa bidhaa, na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Mwaka 2025, jumla ya miradi 956 yenye thamani ya dola za Marekani milioni 11,429.8 ilisajiliwa ikilinganishwa na miradi 901 yenye thamani ya dola za Marekani milioni 9,312.7 iliyosajiliwa mwaka 2024. Kati ya hiyo, miradi 297 ilikuwa ya wawekezaji wa ndani, miradi 473 ya uwekezaji wa nje na miradi 185 ya ubia kati ya wawekezaji wa ndani na wageni. Kielelezo Na. 1 kinatoa takwimu kwa asilimia ya miradi iliyowekezwa kwa mwaka 2025/2026.

Kielelezo Na. 1: Miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa kwa mwaka 2025/26



.

5.2.2 Mchango katika Uzalishaji

Kwa mujibu wa Sensa ya Uzalishaji Viwandani ya Mwaka 2023, sekta binafsi inamiliki asilimia 92.6 ya shughuli za uzalishaji viwandani na asilimia 99 ya shughuli ndogo za uzalishaji viwandani. Hali inaakisi mchango mkubwa wa sekta binafsi katika umiliki na uendeshaji wa shughuli za uzalishaji viwandani. Aidha, sehemu kubwa ya uzalishaji wa sekta binafsi umeelekezwa katika uchimbaji wa madini na uzalishaji viwandani, huku


shughuli zinazofanywa kwa ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ni asilimia 0.4. Takwimu hizi zinaonesha ushirikiano hafifu katika uwekezaji wa ubia wa sekta ya umma na sekta binfasi.

5.2.3 Mchango katika Ajira

Kwa mujibu wa NBS, takribani asilimia 90 ya nguvu kazi ilijishughulisha na shughuli za sekta binafsi. Aidha, kwa mujibu wa *Tanzania Informal Sector Employment and Earning Survey* 2024/25, sekta binafsi imeajiri watu 3,185,947, sawa na asilimia 71 ya walioajiriwa katika sekta rasmi, ambapo asilimia 89 walikuwa katika taasisi zinazolenga kupata faida, asilimia 10 katika taasisi za utoaji huduma, na asilimia 1 katika vyama vya ushirika.

5.2.4 Mchango katika Mauzo ya Nje

Mchango wa sekta binafsi katika mauzo ya nje ulifikia takribani dola za Marekani bilioni 17.6 mwaka 2025/26 kutoka dola za Marekani bilioni 16.0 mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 10.2. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani, tumbaku na kahawa, pamoja na mapato yatokanayo na huduma za usafiri na utalii.



5.3 Maeneo ya Kipaumbele ya Uwekezaji

Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano umebainisha na kufungamanisha minyororo ya thamani katika programu za kielelezo ili kuhakikisha zinakuwa na manufaa kwa biashara, uzalishaji, kukuza ushindani, kupanua wigo wa mapato, mauzo nje na kuongeza ajira. Kwa msingi huo, katika mwaka 2027/28, Sekta binafsi ina fursa ya kuwekeza na kushiriki katika hatua mbalimbali za minyororo ya thamani inayolenga kuharakisha maendeleo na ukuaji wa uchumi. Maeneo yatakayohusika katika kila mnyororo wa thamani ni kama ifuatavyo:

(a) **Kilimo cha maua na mazao ya bustani**: Eneo hili linahusisha matunda, mbogamboga, maua na viungo. Fursa za uwekezaji zinapatikana katika hatua zote

za mnyororo wa thamani, kuanzia utafiti na upatikanaji wa pembejeo, uzalishaji, uhifadhi na uchakataji, hadi usambazaji, usafirishaji na uuzaji katika masoko ya nje.

(b) **Ufugaji wa viumbe maji**: vipaumbele vya uwekezaji katika eneo hili vinahusisha uzalishaji wa mbegu na chakula cha viumbe maji; utengenezaji na usambazaji wa vifaa vya ufugaji; huduma za ugani; pamoja na ufugaji katika mabwawa na vizimba. Aidha, eneo hili linajumuisha uchakataji wa mazao, ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ya uhifadhi na usafirishaji wa bidhaa katika hali ya ubaridi, ubunifu katika matumizi ya mifumo ya kidijitali katika usimamizi wa shughuli za ufugaji, na uendelezaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi.

(c) **Uchimbaji na uongezaji thamani wa madini**: Fursa za uwekezaji katika eneo hili zinahusisha matumizi ya teknolojia na ubunifu katika uchimbaji, uendelezaji wa migodi, uchakataji na uthibitishaji wa ubora wa madini. Kipaumbele pia kitawekwa katika utengenezaji wa bidhaa zitokanazo na madini, usafirishaji, na upanuzi wa masoko ya nje, ili kuongeza thamani inayobaki nchini.

(d) **Uzalishaji wa mafuta ya kula**: Katika eneo hili fursa zipo katika utafiti, uzalishaji wa mbegu bora, kilimo cha kibiashara na uendelezaji wa viwanda vya uchakataji.


(e) **Uzalishaji wa Nguo na Mavazi**: Katika eneo hili fursa zipo katika kuendeleza viwanda vinavyounganisha uzalishaji wa pamba na hatua zinazofuata za uchakataji, utengenezaji wa nguo na mavazi, hadi mauzo ya nje. Mnyororo huu wa kimkakati unaunganisha shughuli za kilimo na viwanda.

Aidha, Serikali itakuwa na jukumu la kuweka mazingira wezeshi ya kufungua fursa katika minyororo ya thamani kimkakati.

5.4 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)

Sekta binafsi itashirikishwa katika mchakato wa upangaji, utekelezaji, uendeshaji na utoaji wa bidhaa na huduma katika programu na miradi ya maendeleo. Aidha, kwa mwaka 2027/28, ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi utajielekeza katika ukamilishaji wa maandalizi ili kufikia hatua ya utekelezaji wa miradi 121 iliyopo katika hatua mbalimbali za maandalizi kama ilivyoainishwa katika Kielelezo Na. 2.

Kielelezo Na.2: Miradi na Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi



5.5 Mkakati wa Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Utekelezaji wa Mpango

Kwa kuzingatia nafasi ya sekta binafsi, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV) umeainisha umuhimu wa kuimarisha makubaliano na ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika maeneo mbalimbali. Haya yanajumuisha ushiriki wa sekta binafsi katika programu za kielelezo ili kuwezesha upatikanaji wa matokeo endelevu, pamoja na kutumia njia mbadala za ugharamiaji wa uwekezaji.

Katika mwaka wa fedha 2027/28, Serikali itaimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango kwa kuelekeza juhudi katika kubadili fursa zilizoainishwa kwenye minyororo ya thamani kuwa miradi ya uwekezaji inayotekelezwa. Kipaumbele kitatolewa katika kupunguza vihatarishi na kuboresha mazingira ya uwekezaji, kuboresha upatikanaji wa taarifa kuhusu fursa zilizopo, kuharakisha maamuzi yanayohitajika na kuimarisha uratibu kati ya taasisi za Serikali na wawekezaji. Aidha, sekta binafsi itaeendelea kushirikishwa kupitia majadiliano, mashauriano na vikao kazi katika maandalizi ya mipango ya kisekta, utekelezaji, utatuzi wa changamoto na tathmini ya miradi ya maendeleo.

5.6 Mfumo wa Ufuatiliaji wa Uwekezaji

Katika mwaka wa fedha 2027/28, Serikali itaimarisha mfumo wa kufuatilia uwekezaji halisi wa sekta binafsi katika minyororo ya thamani zilizopewa kipaumbele. Mfumo huo utatumia viashiria vya sekta binafsi vilivyoainishwa katika FYDP IV, pamoja na viashiria mahsusi vya kupima maendeleo ya uwekezaji katika kila mnyororo wa thamani. Ufuatiliaji utahusisha hatua mbalimbali za mradi, kuanzia maandalizi na upatikanaji wa rasilimali hadi utekelezaji na kuanza kwa uzalishaji. Taarifa zitakazopatikana zitatumika kubaini vikwazo na kuelekeza hatua za Serikali zinazohitajika ili kuharakisha utekelezaji wa uwekezaji.

Taarifa za ufuatiliaji zitakusanywa na kuhakikiwa na taasisi zinazowajibika katika kila mnyororo wa thamani. Taarifa hizo zitatumika kufanya maamuzi na kushughulikia vikwazo vinavyoweza kuchelewesha uwekezaji. Utekelezaji unapohusisha taasisi zaidi ya moja, taasisi hizo zitaratibu hatua zao na kufuatilia utekelezaji wake ili miradi ya uwekezaji ifikie hatua zilizokusudiwa ndani ya muda uliopangwa. Matokeo ya ufuatiliaji yatazingatiwa katika maandalizi na utekelezaji wa mipango na bajeti za taasisi husika.

SURA YA SITA

UGHARAMIAJI WA MPANGO

6.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza mwelekeo wa ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2027/28 ambao ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 (Mpango wa IV). Aidha, kwa mwaka 2027/28, ugharamiaji wa Mpango unalenga kuongeza uwekezaji katika sekta za kimageuzi, kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi, kuongeza uwekezaji na kukuza uzalishaji wa ajira. Hatua hizi zitachangia kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani.

6.2 Mahitaji ya Rasilimali Fedha kwa Mwaka 2027/28

Mahitaji ya rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2027/28 yanakadiriwa kufikia kiasi cha shilingi trilioni 89.3 kama ilivyoainishwa katika Mpango wa IV. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 20.7 zinatarajiwa kutoka kwenye bajeti ya Serikali, sawa na asilimia 30.2 ya bajeti kuu ya Serikali. Shilingi trilioni 6.3 uwekezaji unaotarajiwa kutoka katika mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara, na shilingi trilioni 62.3 ni uwekezaji kutoka sekta binafsi. Kiasi hicho ni makadirio ya uwekezaji wa sekta binafsi kitakachotengenezwa katika ukuzaji wa mitaji.

6.2.1 Vyanzo vya Mapato ya Serikali kwa Mwaka 2027/28

Mapato yanayotarajiwa kugharamia utekelezaji wa Mpango 2027/28 yatatokana na vyanzo vitatu (3) vikuu kama ifuatavyo:

(i) Mapato ya ndani: kodi, mapato yasiyo ya kodi, gawio kutoka kwa mashirika ya umma na mapato ya halmashauri;

(ii) Rasilimali fedha za Nje: mikopo nafuu, misaada, na mikopo isiyo nafuu kwa miradi ya kibiashara; na

(iii) Mbinu bunifu ya ufadhili: ikijumuisha hati fungani za kijani, za miundombinu, na za halmashauri.

6.2.2 Uwekezaji wa Mashirika ya Umma

Mashirika ya Umma yanayojiendesha kibiashara yataendelea kuwa chanzo muhimu cha rasilimali za ugharamiaji wa maendeleo, kuboresha ufanisi na kuongeza mapato na faida. Lengo ni kufikisha mchango wa mashirika hayo katika mapato ya serikali hadi asilimia 10 ifikapo Juni 2028. Kadhalika, kupunguza utegemezi wa ruzuku na kuongeza matumizi yenye tija ya rasilimali. Mikakati ya kufikia malengo ya mwaka 2027/28 ni kama ifuatavyo:

(i) Kuimarisha utawala, usimamizi wa mapato na matumizi pamoja na kuhakikisha uwajibikaji wa mashirika ya umma;

(ii) Kuongeza matumizi ya masoko ya mitaji, hatifungani, ufadhili mchanganyiko, dhamana na ubia wa kimkakati katika kugharamia uwekezaji;

(iii) Kuimarisha ushirikiano na uunganishaji wa rasilimali miongoni mwa mashirika ya umma ili kuongeza uwezo wa kugharamia na kutekeleza miradi mikubwa; na

(iv) Kuongeza matumizi yenye tija ya rasilimali na mali zisizotumika kikamilifu kupitia ukodishaji, ubia au ubinafsishaji wenye faida.

6.2.3 Uwekezaji wa Sekta Binafsi

Sekta binafsi itaendelea kuwa chanzo muhimu cha ugharamiaji wa maendeleo kwa mwaka 2027/28. Mpango unalenga kuimarisha uwekezaji wa ndani na nje, kukuza masoko ya mitaji, kuimarisha ubia kati ya serikali na sekta binafsi, pamoja na kuboresha upatikanaji wa mikopo. Uwekezaji utakaofanywa na sekta binafsi kufikia malengo ya Mpango wa IV ya kuongeza uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje hadi kufikia asilimia 10 ya Pato la Taifa ifikapo 2030 na uwekezaji wa ndani wa sekta binafsi hadi asilimia 25–30 ya pato la taifa. Mikakati ya 2027/28 ya kufikia malengo yaliyoanishwa ni kama ifuatavyo:

(i) Kuendeleza ufunguaji na uunganishaji wa soko la mitaji na masoko ya kimataifa;

(ii) Kuimarisha maandalizi, uchakataji na ugharamiaji wa miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi;

(iii) Kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje katika sekta za kimkakati;

(iv) Kuimarisha mifumo ya dhamana na vyanzo bunifu vya ugharamiaji wa miradi; na

(v) Kuboresha upatikanaji na ubora wa mikopo kwa sekta binafsi kupitia maboresho ya sekta ndogo ya fedha, kupunguza mikopo chechefu na kuimarisha mitaji na ukwasi wa taasisi za fedha.

6.3 Vyanzo Bunifu na Mbadala

Serikali itaendelea kuimarisha matumizi ya vyanzo bunifu na mbadala vya fedha katika mwaka 2027/28 ili kuongeza rasilimali za kugharamia maendeleo, kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi na kuvutia mitaji ya muda mrefu. Vyanzo hivyo vitajumuisha hatifungani za kijani, hatifungani za Watanzania waishio ughaibuni, vyanzo mseto vya fedha, biashara ya kaboni, masoko ya mitaji, pamoja na uzalishaji wa mapato kutokana na mali zilizopo Pamoja na upatikanaji wa mapato kutokana na sehemu ya ongezeko la thamani ya ardhi (Asset Monetisation na Land Value Capture). Kwa ujumla, vyanzo bunifu na mbadala vinatarajiwa kuchangia kati ya shilingi trilioni 42–62, sawa na asilimia 9–13 ya rasilimali zinazohitajika kutekeleza Mpango wa IV. Mikakati ya 2027/28 ya kufikia malengo yaliyoanishwa ni kama ifuatavyo:

(i) Kuendeleza uandaaji na uuzaji wa hatifungani za kijani, hati fungani za Watanzania waishio ughaibuni na hatifungani za maendeleo na miundombinu;

(ii) Kupanua matumizi ya vyanzo mseto vya fedha, ikiwemo mikopo yenye masharti nafuu na fedha za mazingira, katika miradi na sekta za kimkakati;

(iii) Kuimarisha utekelezaji wa mfumo wa biashara ya kaboni na kuongeza uwezo wa Tanzania kunufaika na soko la kaboni;

(iv) Kuongeza mapato kwa kutekeleza Mkakati wa uzalishaji wa mapato kutokana na taarifa (*Data Monetisation)* kwa kutumia taarifa za Serikali zisizo za watu binafsi, kwa kuzingatia usalama wa taarifa; na

(v) Kuongeza matumizi yenye tija yarasilimali zisizotumika kikamilifu kupitia uzalishaji wa mapato kutokana na mali zilizopo na patikanaji wa mapato kutokana na sehemu ya ongezeko la thamani ya ardhi (*Asset Monetisation* na *Land Value Capture.*

SURA YA SABA

USIMAMIZI WA UTELEKEZAJI NA UFUATILIAJI WA MATOKEO YA MPANGO

7.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza mfumo wa uratibu wa kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2027/28. Mfumo huu unalenga kuhakikisha utekelezaji wa vipaumbele, programu za kielelezo, miradi shikizi na miradi ya kimkakati inatelekezwa kwa ufanisi ili kufikia matokeo yaliyokusudiwa, pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa taarifa za utekelezaji kwa wakati, ubainishaji wa changamoto na hatua stahiki zakuchukuliwa.

Utekelezaji wa mfumo wa ufuatiliaji na upimaji wa matokeo utazingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Uidhinishaji wa Miradi ya Maendeleo (National Development Plan and Approval Guideline - NDPAG) na Mwongozo wa Kitaifa wa Upimaji Matokeo na Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo. Aidha, mfumo wa e-Delivery utatumika kama nyenzo kuu ya kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji. Kadhalika, utatumika kufuatilia na kutathmini matokeo ya Mpango, programu na miradi ya maendeleo na kuainisha viashiria vya hatari. Vile vile, utabainisha changamoto za utekelezaji kwa wakati, kuthibitisha taarifa na matokeo, na kuimarisha uwajibikaji wa taasisi zinazotekeleza Mpango pamoja na kuwezesha matumizi ya taarifa katika kufanya maamuzi na kufanya marekebisho.

7.2 Ufuatiliaji, Tathmini na Matumizi ya Mfumo wa e-Delivery

Ufuatiliaji na tathmini ya matokeo ya utekelezaji wa Mpango utafanyika kwa kuzingatia taratibu na miongozo mbalimbali ikiwemo mpango wa ufuatiliaji na tathmini ya kila miradi pamoja na viashiria vya Mpango. Mfumo wa kidijitali wa ufuatiliaji wa matokeo utatumika kufungamanisha vipaumbele vya Mpango na taarifa za programu na miradi. Pia, utawezesha uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji zitakazooainishwa kwa kuzingatia malengo na viashiria vya Mpango IV. Aidha, mfumo huo utawezesha: kufuatilia utekelezaji wa Mpango kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa; kuhuisha na kupata taarifa za utekelezaji kwa wakati; kubaini miradi na programu zilizo nyuma ya ratiba; kubaini changamoto na hatua za maboresho; na kuzalisha taarifa na dashibodi kwa ajili ya maamuzi.

7.3 Utoaji na Matumizi ya Taarifa

Taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na viashiria vya Mpango zitaandaliwa na kuwasilishwa kila robo mwaka au kwa kuzingatia utaratibu wa utoaji wa taarifa wa mradi husika. Taarifa hizo zitawazesha kupima utekelezaji wa ADP, Mpango wa IV na Dira 2050, kubaini maeneo yenye changamoto na kuchukua hatua stahiki kwa lengo la kufikia malengo yaliyokusudiwa.

7.4 Mgawanyo wa Majukumu ya Ufuatiliaji na Uwasilishaji wa Taarifa

Taasisi zinazotekeleza Mpango zitawajibika kuandaa na kuwasilisha taarifa kwa kupitia mfumo wa e-Delivery. Tume ya Taifa ya Mipango itaratibu ufuatiliaji, uhakiki na uchambuzi wa taarifa, pamoja na kuwasilisha masuala yanayohitaji hatua au maamuzi katika ngazi husika. Aidha, kwa kushikiriana na wadau mbalimbali, Tume Tume ya Taifa ya Mipango itafanya ziara za ukaguzi itakapohitajika.

Kwa upande wa utekelezaji wa miradi na programu unaohusisha taasisi zaidi ya moja, wizara inayoratibu utekelezaji itawajibika kuwasilisha taarifa za matokeo ya pamoja, kwa kushirikiana na taasisi wezeshi. Jedwali 7.0 linaainisha shughuli, muda, mhusika na matokeo tarajiwa ya ufuatiliaji na tathmini.

Jedwali 7.0: Ratiba na Mgawanyo wa Majukumu ya Ufuatiliaji na Uwasilishaji wa Taarifa

Na.	Shughuli	Muda	Mhusika	Matokeo
1.	Uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mfumoo wa e-Delivery	Kila robo mwaka au kulingana na mpango kazi wa mradi husika	Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala na Mashirika ya Umma	Taarifa za utekelezaji
2.	Ufuatiliaji wa utekelezaji wa viashiria vya Mpango	Kila robo mwaka au kulingana na ratiba ya muda wa ufuatiliaji wa viashiria	Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala na Mashirika ya Umma	Taarifa za ufuatiliaji wa utekelezaji wa viashiria vya Mpango
3.	Vikao vya wadau kwa ajili ya kujadili taarifa za ufuatiliaji	Kila robo mwaka	Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala na Mashirika ya Umma	Hatua za kutatua changamoto zilizobainika katika taarifa za utekelezaji.
4.	Tathmini maalum	Inapohitajika	Tume ya Taifa ya Mipango/Taasisi husika	Taarifa ya tathmini
5.	Taarifa ya mwaka ya utekelezaji	Juni 2027	Tume ya Taifa ya Mipango	Taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mpango

SURA YA NANE

VIHATARISHI VYA MPANGO KWA MWAKA 2027/28 NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO

8.1 Utangulizi

Sura hii inaainisha vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28 pamoja na mikakati ya kukabiliana navyo. Utekelezaji wa Mpango unafanyika katika mazingira ya kiuchumi, kifedha, kijamii, kiteknolojia na kimazingira yanayobadilika. Hivyo, utambuzi wa mapema wa vihatarishi na kuweka mikakati na hatua stahiki za kukabiliana navyo ni muhimu ili kuhakikisha malengo ya Mpango yanafikiwa. Usimamizi wa vihatarishi unalenga kulinda utekelezaji wa vipaumbele na programu za kimkakati, Programu za Kielelezo na minyororo ya thamani ya kipaumbele, pamoja na kuhakikisha uwekezaji wa Serikali na sekta binafsi unaleta matokeo yaliyokusudiwa. Usimamizi huo utafungamanishwa na mifumo iliyopo ya utekelezaji (ufuatiliaji na tathmini, bajeti ya muda wa kati, mikataba ya utendaji na Mfumo wa E-Delivery) na utafuata mzunguko wa hatua tano za: kubaini vihatarishi; kutathmini uwezekano na athari; kuweka mikakati ya kudhibiti; kufuatilia na kutoa tahadhari ya mapema; kutoa taarifa na kuwasilisha maamuzi. Kanuni zinazoongoza hatua hizo ni uwajibikaji, uwazi, matumizi ya ushahidi, na ushirikiano wa kisekta.

8.2 Maeneo ya Vihatarishi na Mikakati ya Kukabiliana navyo

Vihatarishi vimegawanywa katika maeneo makuu matano: fedha, uchumi, taasisi, mazingira na mabadiliko ya tabianchi, na teknolojia. Mikakati ya kukabiliana navyo inajumuisha kuepuka vihatarishi, kupunguza uwezekano wa kutokea au ukubwa wa athari zake, kuhamisha sehemu ya athari kwa wahusika wengine na kukubali vihatarishi vinavyoweza kudhibitiwa kwa ufuatiliaji wa karibu. Jedwali Na. 8.1 linaonesha vihatarishi, athari zinazoweza kujitokeza, mikakati ya kukabiliana navyo pamoja na taasisi zinazowajibika na vipindi vya ufuatiliaji.

Jedwali 8.1: Vihatarishi na mikakati ya kukabiliana Navyo.

Eneo la Kihatarishi	Kihatarishi – Athari	Mikakati ya Kukabiliana navyo	Taasisi – Muda
Fedha	Kutopatikana kwa fedha kwa wakati — miradi kusimama; malipo ya wakandarasi kuchelewa.	Kuzingatia kalenda ya utoaji wa fedha kwa robo mwaka; kutoa kipaumbele kwa miradi inayoendelea; malipo kulipwa kulingana na matokeo.	MoF; MDAs; TAMISEMI – Kila robo mwaka
	Kuongezeka kwa gharama za hudumia deni — nafasi ya kifedha kupungua; mzigo wa deni kuongezeka.	Kutekeleza Mkakati wa usimamizi wa deni; Kukopa mikopo ya masharti nafuu; mikopo kuelekezwa kwenye	MoF; Benki Kuu – kila robo mwaka

Eneo la Kihatarishi	Kihatarishi – Athari	Mikakati ya Kukabiliana navyo	Taasisi – Muda
		miradi inayozalisha mapato.	
Uchumi	Mfumuko wa bei na gharama za maisha kupanda — bajeti kuvuka mipango.	Kutekeleza sera ya fedha inayolinda utulivu wa bei; Kuongeza akiba ya chakula na mafuta; na kuongeza uzalishaji wa ndani.	Benki Kuu; MoF; MIT – kila mwezi
	Thamani ya shilingi kushuka — gharama za uagizaji na deni la nje kuongezeka.	Kuimarisha akiba ya fedha za kigeni; kuongeza mauzo ya nje na utalii; na kuhimiza uzalishaji wa ndani.	Benki Kuu; MoF – kila mwezi
	Bei za bidhaa duniani kubadilika — mauzo ya nje na uwekezaji wa nje kupungua.	Kuongeza wigo wa masoko na bidhaa zinazouzwa nje ya nchi; na kuongeza thamani ya bidhaa za ndani.	MoF; Benki Kuu; MIT – kila robo mwaka
	Ukuaji mdogo wa sekta binafsi — mwitikio wa uwekezaji na ajira kupungua.	Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuimarisha huduma za upatikanaji wa umeme na usafirishaji; kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa biashara ndogo na za kati.	MoF; TISEZA; MIT; Halmashauri – kila robo mwaka
	Mivutano ya kisiasa na kiuchumi ya kikanda na kimataifa — minyororo ya ugavi kuvurugika.	Kutofautisha masoko na vyanzo vya ugavi; kuimarisha ushirikiano wa kikanda; kuimarisha akiba ya kimkakati ya bidhaa muhimu.	MoFA; MIT; Benki Kuu – endelevu
Taasisi	Udhaifu wa uratibu na mgawanyiko wa majukumu — kurudiwa kwa kazi; umiliki wa matokeo kutosemekana.	Kufafanua majukumu kwa miongozo na mikataba ya utendaji; kuboresha mikutano ya uratibu.	ORMU, NPC; Ofisi ya Waziri Mkuu - Uratibu – kila robo mwaka
	Kutopatikana kwa mwitikio wa uwekezaji binafsi — pengo la ufadhili; malengo ya uzalishaji kukosa.	Kuandaa miradi tayari kwa uwekezaji; kuimarsiha ushirikiano na sekta binafsi; na kuongeza majukwaa ya wawekezaji.	TIC; ORMU, NPC– kila robo mwaka
Mazingira na mabadiliko ya Tabianchi	Ukame, El- Nino, mafuriko na mabadiliko ya msimu — uzalishaji wa kilimo na nishati kupungua; miundombinu kuharibika.	Kuimarisha miundombinu inayohimili mabadiliko ya tabianchi; kuongeza eneo la umwagiliaji; kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora; kutekeleza tahadhari	Mazingira; Kilimo; TMA – msimu/mwaka

Eneo la Kihatarishi	Kihatarishi – Athari	Mikakati ya Kukabiliana navyo	Taasisi – Muda
		ya mapema; na kuimarisha upatikanaji wa bima ya mazao.	
	Maafa ya asili na dharura za afya — miundombinu kuharibika; fedha za dharura.	Kuboresha mifumo ya tahadhari ya mapema; Kuimarisha akiba ya dharura; Kutekeleza mipango miji inayohimili majanga; na kuimarisha uhamasishaji wa jamii.	Waziri Mkuu (Maafa); Afya – endelevu
Teknolojia	Vitisho vya usalama wa mtandao — data kupotea; huduma kuvurugika; imani kupungua.	Kutekeleza sera ya usalama wa mtandao; kuimarisha ukaguzi wa mifumo; kutoa mafunzo kwa watumishi; na kutelekeza mipango ya matukio.	MCIT; TCRA; MDAs – endelevu
	Upungufu wa ujuzi wa kidijitali — mifumo kutotumika kikamilifu; pengo la kidijitali kuongezeka.	Kutoa mafunzo ya kidijitali; kuimarisha vituo vya ubunifu; kuwekeza katika upatikanaji wa huduma rahisi kwa watumiaji; na utoaji wa elimu ya teknolojia shuleni na vyuoni.	Mawasiliano; COSTECH; Elimu – mwaka

8.2.1 Ufungamanishaji wa Vihatarishi na Mfumo wa e-Delivery

Vihatarishi na vikwazo muhimu vinavyohusiana na programu za kimkakati, Programu za Kielelezo na minyororo ya thamani ya kipaumbele vitaingizwa katika mfumo wa e-Delivery. Mfumo huo utatunza taarifa kuhusu kila kihatarishi, kiwango chake, taasisi inayowajibika, hatua za kukabiliana nacho na muda wa kukamilisha hatua hizo. Aidha, utawezesha kufuatilia hali ya utekelezaji kwa kutumia alama za rangi (kijani, njano na nyekundu), kuwasilisha changamoto zinazohitaji maamuzi katika ngazi za juu na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi katika ngazi za sekta na Baraza la Mawaziri.

8.3 Ufuatiliaji na Udhibiti wa Vihatarishi

Kila taasisi itaandaa na kuhuisha daftari la vihatarishi likionesha aina ya kihatarishi, uwezekano wa kutokea, ukubwa wa athari zake, viashiria vya tahadhari za mapema na hatua za kukidhibiti. Taarifa kutoka katika madaftari ya vihatarishi ya sekta, mikoa na halmashauri zitaunganishwa katika daftari la kitaifa. Mapitio ya vihatarishi yatafanyika kila robo mwaka na kila mwaka. Aidha, taarifa kuhusu hali ya vihatarishi na hatua zilizochukuliwa zitajumuishwa katika taarifa za utekelezaji wa Mpango za kila robo mwaka.

8.3.1 Viwango vya Uwezekano na Athari

Jedwali 8.2: Uainishaji wa viwango vya uwezekano na Athari

Kiwango	Uwezekano wa Kutokea	Ukubwa wa Athari
Juu	Inawezekana sana kutokea katika kipindi cha utekelezaji; mwenendo unaonyesha hali inajirudia.	Kuchelewesha au kutokamilika kwa programu nzima; upotevu mkubwa wa fedha; kushindwa kufikia malengo makuu.
Kati	Inawezekana kutokea; hali zinazosababisha kihatarishi zinaweza kujitokeza katika kipindi cha utekelezaji.	Kuchelewesha sehemu ya utekelezaji; kuongeza gharama; kupunguza ubora wa matokeo.
Chini	Uwezekano mdogo; hali hazijitokezi mara kwa mara.	Athari ndogo zinazoweza kudhibitiwa kwa urahisi ndani ya taasisi.

Kiwango cha jumla cha kihatarishi kitaamua mara ambazo ufuatiliaji utafanyika. Vihatarishi vya kiwango cha juu sana — vitahitaji hatua za haraka na uangalizi wa ngazi za juu za maamuzi, pamoja na ufuatiliaji wa kila mwezi. Vihatarishi vya kiwango cha juu — vitafuatiliwa kila mwezi au kila robo mwaka; vya kiwango cha kati kila robo mwaka; na vya kiwango cha chini — kila mwaka.

8.3.2 Mzunguko wa Ufuatiliaji, Utoaji Taarifa na Kuwasilisha Maamuzi

Uwasilishaji wa masuala yanayohitaji maamuzi utakuwa katika ngazi tatu: taasisi inayowajibika (hatua ya kwanza); kamati ya uratibu ya sekta na Tume ya Taifa ya Mipango (maamuzi ya kisekta); na Baraza la Mawaziri na Wizara ya Fedha kwa masuala yenye athari za kibajeti. Kuwasilishwa kwa ngazi ya juu hakuzui hatua za haraka za taasisi. Usimamizi madhubuti wa vihatarishi ni nguzo ya kulinda vipaumbele vya Mpango na kufanya maamuzi ya marekebisho kwa wakati.

Kalenda ya ufuatiliaji na utoaji wa taarifa itahusisha: (i) ufuatiliaji wa kila mwezi wa viashiria vya tahadhari za mapema unaofanywa na taasisi inayowajibika kwa kihatarishi husika; (ii) uhuishaji wa madaftari ya unaofanywa na wizara, idara na wakala wa Serikali, mikoa na halmashauri; (iii) mapitio ya kitaifa ya vihatarishi na uwasilishaji wa masuala yanayohitaji maamuzi kila robo mwaka au inapohitajika, chini ya uratibu wa NPC na MoF; (iv) mapitio ya mwaka ya vihatarishi yanayofanywa na NPC na MoF ili kutoa mapendekezo yatakayozingatiwa katika maandalizi ya bajeti ya mwaka unaofuata; na (v) ukaguzi wa kila mwaka wa ufanisi wa usimamizi wa vihatarishi unaofanywa na CAG na Mkaguzi Mkuu wa Ndani, pamoja na kuwasilisha taarifa za ukaguzi na mapendekezo ya maboresho.

KIAMBATISHO NA. I: AFUA ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2027/28

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
3.2 Mwenendo wa Uchumi Jumla	
3.2.1: Uthabiti na Utabirifu wa Mwenendo wa Uchumi Jumla	
Lengo 1: Kuwepo kwa Mazingira Thabiti ya Usimamizi wa Uchumi ili Kuinua Imani ya Wawekezaji na Utabirifu wa Mwenendo wa Uchumi	
1. Ukuaji wa Pato la Taifa wa asilimia 6.6 ifikapo mwaka 2027.	1.1 Kutumia vivutio zinavyozingatia ufanisiwa mauzo ya nje, ikiwa ni pamoja na marejesho ya ushuru katika bei ya umeme kwa makampuni ya viwanda yenye uthibitisho wa ongezeko la mauzo ya nje kwa mwaka.
	1.2 Kuboresha miundombinu ya masoko (biashara, malipo, maghala) ifikapo Juni 2028.
2. Mfumuko wa bei uliodumishwa ndani ya wigo uliopangwa wa kati ya asilimia 3 – 5 kwa mwaka.	2.1 Kuimarishwa kwa mfumo wa sera ya fedha, kwa kuimarisha utaratibu wa kuweka shabaha za mfumuko wa bei kila mwaka.
	2.2 Kuimarishwa kwa upatikanaji wa chakula na uthabiti wa bei, kwa kuongeza uzalishaji wa ndani, kuboresha mnyororo wa thamani wa kilimo, na kuanzisha utaratibu wa vocha za kidijitali za pembejeo kwa wakulima wadogo kila mwaka.
	2.3 Kuanzishwa mfumo wa kidijitali wa kitaifa wa ufuatiliaji wa bei za bidhaa muhimu kwa wakati na kongeza uwazi wa soko kila mwaka.
	2.4 Kudumisha utaratibu wa utunzaji wa akiba ya chakula na petroli toshelevu ya mahitaji kitaifa kwa angalau miezi sita, ili kupunguza athari za kuyumba kwa bei za nje, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	2.5 Kuimarishwa kwa uwianifu wa sera za fedha na bajeti ili kuhakikisha uwiano na utulivu wa kiuchumi kila mwaka.
3.2.2 Kuimarisha Ustahimilivu wa Kifedha	
Lengo 1: Kusimikwa kwa mfumo endelevu wa kifedha kwa kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani, kupunguza vihatarishi vya deni la Taifa sanjari na kuhakikisha uendelevu wa matumizi thabiti, uhakika wa upatikanaji wa fedha kwa uendelezaji wa miundombinu na upatikanaji wa huduma za jamii, na kudumisha nidhamu ya matumizi	
1. Makusanyo ya mapato ya ndani kuongezeka kutoka asilimia 14.9 hadi 20 ya Pato la Taifa.	1.1 Kuimarishwa ukusanyaji wa kodi kidijitali kupitia mifumo ya kiotomatiki, utoaji wa ankara ya kielektroniki na matumizi ya mifumo ya kikodi ya kisasa kwa zaidi ya asilimia 80 ya walipa kodi ifikapo Juni 2028.
2. Makusanyo ya kodi kuongezeka hadi 18 ya Pato la Taifa, ifikapo mwaka 2027/28.	2.1 Kuimarishwa taratibu kuwezesha urasimishaji wa shughuli za sekta isiyo rasmi, kwa kurahisisha michakato ya kukidhi masharti ya sheria za kodi na vivutio kufikia 2028.
	2.2 Kutekeleza maboresho ya mfumo wa kodi jumuishi unaozingatia uwezo na utaratibu wa misamaha ya kodi ili kuongeza usawa na ufanisi wa makusanyo, ifikapo Juni 2028
	2.3 Kuimarishwa na kuingiwa kwa makubaliano ya kimataifa na washirika wa biashara itakayowezesha mabadilishano ya taarifa za kodi, ili kuzuia vitendo haramu vya kifedha na ukwepaji wa kodi kwenye mifumo ya biashara za kidijitali, kila mwaka.
3. Makusanyo ya maduhuli/yasiyo ya kodi kuongezeka kufikia asilimia 5 ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2027/28.	3.1 Kufanya mapitio na marekebisho ya kina ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi, ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	i. Kusasishwa kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kwa kufanyia mapitio ya kina mifumo ya kisheria na taratibu na kuchagiza mabadiliko ya mifumo kuwa ya kidijitali na otomatiki ili kuongeza ufanisi ifikapo mwaka 2028.
	ii. Kuharakishwa upangaji wa matumizi ya ardhi, upimaji, na urasimishaji kwa kutumia teknolojia za kisasa, kama vile, picha za satelaiti na ndege zisizo na rubani, ili kupanua wigo wa vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi ifikapo Juni 2028.
4. Deni la Serikali kudhibitiwa kubaki ndani ya wigo wa kati ya asilimia 50 – 55 wa vigezo vya DSA ifikapo Juni 2028.	4.1 Kuimarishwa kwa mikakati ya usimamizi wa deni la serikali kwa kipindi chote, kwa kujielekeza kukopa katika vyanzo vya masharti nafuu na kupunguza mikopo aghali ya kibiashara muda wote kufikia 2028.
	4.2 Kufuatilia kwa karibu faida kwenye uwekezaji uliofanyika kwa fedha za mkopo, kuhakikisha faida inayopatikana na matokeo yake ni makubwa, kwamba matumizi ya mikopo yanakuwa mazuri, kila mwaka
5. Kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti inadhibitiwa chini ya asilimia 3 ya Pato la Taifa kila mwaka.	5.1 Kutekelezwa kwa mfumo wa bajeti ya matokeo kiutendaji na mapitio kila mwaka ya uhalali wa matumizi katika wizara zote za Serikali kufikia 2028.
	5.2 Kuimarisha mifumo ya matumizi ya fedha za umma muda wote ili kuongeza uwazi na uwajibikaji kufikia 2028.
	5.3 Kuimarisha mipango na usimamizi wa mifuko ya kitaifa ya dharura na maafa, ili kushughulikia kikamilifu matumizi ya mifuko hiyo yanayozidi kuongezeka kila mwaka.
6. Bajeti ya maendeleo kudhibitiwa ndani ya wigo wa kati ya asilimia 31 - 35 ya matumizi yote ya Serikali kila mwaka.	6.1 Kuimarishwa kwa ufanisi wa manunuzi na utoaji huduma za umma, kwa kuongeza matumizi ya mifumo ya kidijitali na kuweka ukomo bayana wa matumizi, kila mwaka

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	6.2 Kuongeza matumizi ya mifumo ya kidijitali ili kuboresha ufanisi katika utoaji wa huduma na matumizi ya fedha, kufikia Juni 2028.
3.2.3 Ustahimilivu na Usetushaji wa Sekta ya Nje	
Lengo 1: Kupunguza hatari za kiuchumi kwa kusetusha bidhaa za kuuza nje, kupunguza utegemezi uagizaji wa mahitaji kutoka nje na kuimarisha mizania ya malipo, na kuimarisha utabilifu wa biashara na ustahimilivu wa kiuchumi.	
1. Mchango wa mauzo ya bidhaa za viwandani nje kuongezeka kutoka asilimia 12 hadi 16,9 ya jumla ya mauzo yote ya bidhaa nje ifikapo Juni 2028.	1.1 Kutekeleza sera za viwanda zinazohamasisha kuongeza thamani katika kilimo, madini na uzalishaji viwandani, ifikapo Juni 2028.
	i. Kuanzishwa kwa mfumo rasmi wa motisha kwa wauzaji wa bidhaa za viwandani nje (kama vile kupunguza kodi na upatikanaji wa mikopo nafuu) ili kusaidia ongezeko la bidhaa za viwandani na zilizosindikwa zinazouzwa nje, ifikapo mwaka 2028.
	ii. Kuwezesha ongezeko la uzalishaji viwandani na usindikaji wa mazao ghafi ya kilimo, madini na maliasili zingine za uzalishaji viwandani ili kupunguza mauzo ghafi nje ya bidhaa ghafi, ifikapo Juni 2028.
	iii. Kuongeza uwekezaji katika miundombinu wezeshi kibiashara, ikiwa ni pamoja na kusasisha miundombinu na huduma za bandari, ujenzi wa vituo mahsusi vya usafirishaji na uchukuzi, na kuongeza ufanisi wa huduma za forodha, ifikapo Juni 2028.
2. Kiwango cha utegemezi uagizaji wa mahitaji kutoka nje kupungua kwa asilimia 15 kufikia Juni 2028.	2.1 Kuongeza uzalishaji wa malighafi na mahitaji mengine muhimu, sanjari na kupanua uwezo wa ndani wa uzalishaji viwandani wa bidhaa muhimu, kama vile, dawa za tiba ya binadamu, pembejeo na vifaa vya kilimo na nguo na mavazi ndani ya nchi, kupitia mkakati mahsusi wa ujenzi wa uchumi wa viwanda na ongezeko la uwekezaji katika ujenzi wa uwezo wa utafiti na maendeleo ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
3. Kuhakikisha nakisi ya urari wa malipo ya kawaida haizidi asilimia 3 ya Pato la Taifa, kufikia 2028.	3.1 Kuimarisha ujenzi wa akiba ya fedha za kigeni usiopungua uwezo wa uagizaji wa mahitaji kutoka nje wa aghalabu miezi minne na nusu kila mwaka.
	3.2 Kuhamasisha ongezeko la mauzo ya huduma nje, ikiwa ni pamoja na utalii na huduma za kifedha kwa usetushaji wa vyanzo vya mapato ya fedha za kigeni kila mwaka.
	3.3 Kuimarisha ushirikiano wa biashara kikanda kuweza kupunguza utegemezi wa nchi zilizoendelea kwa masoko ya mauzo, sanjari na kujenga uhimilivu wa misukosuko ya kiuchumi ya nje, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
3.3 Mabadiliko Muhimu katika Sekta Mageuzi	
3.3.1 Sekta ya Kilimo	
Kilimo-Mazao cha Kibiashara	
1. Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 7 bora, Kusini mwa Jangwa la Sahara zenye kilimo - mazao chenye uwezo wa ushindani, ifikapo Juni 2028.	1.1 Kuimarisha mamlaka za uthibiti na urekebu kuweza kuimarisha faida na ushindani katika uendeshaji wa kilimo- mazao kibiashara, kufikia Juni 2028.
	Kuwajengea uwezo wadhibiti, ili kusimamia viwango vya kimataifa na kupunguza kukataliwa kwa bidhaa nje, kufikia Juni 2028.
	Kuwianisha viwango vya kitaifa na vya kiitifaki za Jumuiya ya Afrika Mashariki Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Eneo la Biashara Huria la Bara la Afrika vya mazao, kufikia mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji kidijitali vyanzo vya mazao makuu ya biashara ya nje , kufikia mwaka 2028.
	1.2 Kufanya mapitio, kurekebisha na kutunga sheria mpya, ili kufuta urasimu na kurahisisha ufanyaji biashara kufikia Juni 2028
	Kufanya tathmini ya kina ya sheria za biashara za kilimo na uwekezaji, kufikia Juni 2028.
	Kuwianisha sheria za kitaifa na za Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika , Shirika la Biashara Duniani na mifumo ya kilimo bora kinachozingatia hali ya hewa kufikia mwaka 2028.
	1.3 Kuongeza fursa za upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu, riba nafuu na masharti nafuu kwa wakulima wa kibiashara na wadogo kutoka vyanzo vya ndani na nje kila mwaka.
	Kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo ili kupunguza hatari za uwekezaji wa muda mrefu (kila mwaka).
	Kuhamasisha ushirikiano na taasisi za fedha za ndani katika mifumo ya fedha mseto ili kuongeza mikopo kwa wafanyabiashara na wakulima wa kati na wadogo, kila mwaka.
	Kuanzisha Mfuko wa Kitaifa wa Dhamana ya Mikopo (kwa wakulima vijana na wanawake).
	1.4 Kupanua ufikiaji wa ruzuku za serikali na zana za kupunguza vihatarishi ili kuimarisha usalama wa kifedha na msaada kwa wakulima, kufikia Juni 2028.
	Kutekeleza programu za ruzuku zinazolenga pembejeo muhimu za kilimo, kufikia mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa kidijitali wa taarifa za soko, ili kutoa bei za wakati halisi mwelekeo wa mahitaji, na taarifa zingine za soko, kufikia mwaka 2028.
	Kuanzisha zana za kupunguza vihatarishi katika uwekaji wa mitambo ya kilimo , ikijumuisha motisha za kodi kwa ununuzi wa zana na vituo vya kukodisha zana za kilimo, kufikia 2028.
	Kuongeza zana za kupunguza vihatarishi vya kifedha katika sekta ya kilimo, ikijumuisha bidhaa ya bima ya kilimo mipango ya dhamana ya mikopo na kuimarisha mifumo ya ufadhili wa ushirika kufikia mwaka 2028.
	Kuhamasisha kilimo cha vitalu kwa kuandaa wakulima katika vikundi vilivyoboreshwa, ili kuongeza tija, kupunguza gharama za pembejeo, na kurahisisha upatikanaji wa masoko, kila mwaka.
	1.5 Kuanzisha mfumo wa kilimo cha mkataba kuwawezesha wakulima mmoja mmoja, kwa kuwapa masoko ya uhakika, upatikanaji wa pembejeo bora, msaada wa kitaalamu na bei thabiti, kwa kuwa na mapatano ya moja kwa moja na wanunuzi, kila mwaka.
	Kutengeneza mfumo sanifu wa kilimo cha mikataba, ili kuwalinda wote, mkulima na mnunuzi, kila mwaka
	1.6 Kuimarisha mnyororo wa thamani wa nguo, kwa kuzalisha pamba, kuichambua, kutengeneza nyuzi, kufuma vitambaa, kuvitia rangi, na kutengeneza bidhaa ya nguo iliyokamilika, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	i. Kuanzisha kituo cha kisasa cha uzalishaji wa nguo kinachotumia nishati bora, kwa kuboresha viwanda muhimu vya kuchambua pamba, kuendeleza kongani mbili au zaidi za viwanda vya nguo vilivyounganishwa, kufikia Juni 2028.
	ii. Tanzania kuwa kitovu kikuu cha usafirishaji wa nguo kwa kuongeza motisha maalum za uwekezaji, na kuzindua kampeni ya kimataifa ya "Made in Tanzania" kufikia Juni 2028.
	iii. Kuendeleza nguvukazi watu stadi katika sekta ya nguo kwa kuanzisha programu za mafunzo katika usanifu na utengenezaji wa nguo, na kuwawezesha vijana na wanawake 5,000 kufanya kazi viwandani kufikia mwaka 2028.
	1.7 Kufufua viwanda vya kilimo vilivyobinafsishwa na kushindwa kuzalisha , hususan viwanda vya nguo vya zamani (kama Urafiki, Mwatex, n.k.) ili kuongeza thamani, kufikia Juni 2028.
	Kutengeneza mkakati wa kitaifa wa kufufua viwanda vya nguo, kuweka kipaumbele katika kusasisha viwanda muhimu, kufikia Juni 2028.
	Kuhamasisha uwekezaji binafsi kwa ajili ya ufufuaji wa uchumi kupitia kifurushi maalum cha motisha na ushirikiano wa kimkakati kufikia Juni 2028.
	Kuhakikisha ushindani kwa kuelekeza matumizi ya pamba ya ndani na kuanzisha vituo vya teknolojia na mafunzo ya ujuzi kufikia Juni 2028.
2. Angalau asilimia 45 ya wakulima wapate pembejeo za kilimo bora za kilimo kufikia Juni 2028.	2.1 Kuimarisha mifumo ya upandaji wa mbegu bora zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi na viunganishi vya utafiti na ugani kufikia 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	2.2 Kuimarisha udhibiti wa ubora wa pembejeo na mifumo ya uthibiti, ili kuepuka bidhaa bandia kufikia 2028.
3. Ardhi ya kilimo inayoendelezwa kikamilifu kwa kutumia mbinu bora za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi kuongezeka hadi kufikia asilimia 40 kufikia Juni 2028	3.1 Kuasili mbinu za kilimo zinazohimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwa maeneo yote ya kilimo kufikia 2028.
	3.2 Kutekeleza kilimo cha teknolojia sahihi ya umwagiliaji kwa matone na majukwaa jumuishi kufikia 2028.
4. Uwiano wa maafisa ugani na wataalamu wa kilimo kuboreshwa kutoka 1:20,000 ya sasa hadi 1:10,000 ifikapo Juni 2028.	4.1 Kuimarisha upatikanaji endelevu wa huduma za ugani kwa mifumo ya teknolojia ya kidijitali kufikia Juni 2028.
	4.2 Kujenga mfumo thabiti wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi ili kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za ugani, kufikia Juni 2028.
Lengo 2: Sekta ndogo za mifugo na uvuvi imara na zenye tija kibiashara zinazoendesha ukuaji wa uchumi na maisha ya vijijini	
1.1.2. Mifugo na Uvuvi	
1. Angalau asilimia 50 ya mazao ya mifugo kufanyiwa ongezeko la thamani la kiwango cha pili kufikia mwaka 2028.	1.1 Kuimarisha uwezo wa kitaifa wa uzalishaji na jenetiki katika mifugo na ukulima wa ukuzaji viumbe maji kufikia Juni 2028.
	1.2 Kuendeleza kanda maalum za viwanda vya mifugo na uvuvi pamoja na miundombinu ya kusindika kufikia Juni 2028.
2. Uzalishaji wa ndani wa pembejeo za mifugo na uvuvi pamoja na vyakula vya wanyama kuongezeka kwa angalau asilimia 50 kufikia mwaka 2028.	2.1 Kuongeza uzalishaji wa pembejeo muhimu na aina ya mifugo iliyoboreshwa, kufikia Juni 2028.
3. Kufikia angalau asilimia 50 ya usambazaji wa soko la kikanda na kimataifa kwa samaki na mazao ya ufugaji	Kujenga na kusasisha bandari za uvuvi, maeneo ya kutua samaki, na vifaa vya kuhifadhia baridi kando ya pwani ya Bahari ya Hindi, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
wa viumbe maji kufikia mwaka 2028.	3.2 Kuanzisha mifumo ya viwanda vya samaki na ufugaji wa viumbe maji iliyoidhinishwa na tayari kwa mauzo ya nje, kufikia Juni 2028.
Lengo 3: Uzalishaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo ulioboreshwa unaohusisha kuunganisha kilimo cha msingi na usindikaji ili kuongeza thamani ya mazao, kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna, na kuinua kipato cha wakulima wadogo	
1.1.3 Mnyororo wa thamani wa chakula na usio wa chakula	
1. Kuanzisha Kanda za Ukuaji wa Kilimo (katika kanda mbili zitakazoanzishwa kufikia Juni 2028.	1.1 Kuanzisha maeneo yaliyounganishwa kwa ajili ya minyororo ya thamani wa chakula, vinywaji/bidhaa zisizo za chakula, na mifugo , kufikia Juni 2028
	1.2 Kuanzisha ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika usindikaji wa mazao ya kilimo na mnyororo wa thamani uliounganishwa, kufikia Juni 2028.
Lengo 4: Kuimarisha ugharamiaji bunifu katika kilimo, kukuza uendelevu wa kifedha na kuharakisha maendeleo ya kilimo kwa kuboresha upatikanaji wa mikopo nafuu, kuhimiza uwekezaji, na minyororo ya thamani inayostahimili mabadiliko	
1.1.4. Ugharamiaji Bunifu wa Kilimo	
1. Idadi ya wajasiriamali wa kilimo wanaopata huduma rasmi za kifedha kuongezeka kutoka asilimia 15 hadi asilimia 30 kufikia Juni 2028.	1.1 Kuunda vyombo na mifumo ya kifedha bunifu (masoko ya mitaji, benki za maendeleo, na fedha mchanganyiko kwa uwekezaji wa muda mrefu katika kilimo, kufikia Juni 2028.
	1.2 Kutekeleza mifumo ya kupunguza vihatarishi ili kuvutia uwekezaji binafsi katika maeneo yasiyofikiwa, kufikia Juni 2028.
2. Angalau asilimia 5 ya bajeti ya serikali kuelekezwa kwenye maendeleo ya kilimo, kila mwaka.	2.1 Kuweka utaratibu rasmi wa bajeti ya kimkakati ya kilimo na kuunganisha kilimo katika mipango ya maendeleo ya kiuchumi ya ndani kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Lengo 5: Kuhakikisha usambazaji endelevu wa mazao na huduma za misitu kwa kudumisha eneo la kutosha la misitu chini ya usimamizi bora, na kuboreshwa kwa afya ya mfumo wa ikolojia, kuimarisha maisha ya vijijini, na usambazaji wa uhakika wa malighafi kwa viwanda vya misitu	
1.1.5 Misitu ya Biashara	
1. Kupanua eneo la kibiashara kwa mashamba ya miti na vitalu vya jamii kufikia angalau hekta milioni 1.5 kufikia Juni 2028.	1.1 Kupanua na kuimarisha mashamba ya miti ya kibiashara na vitalu vya miti vya jamii, kufikia Juni 2028.
	1.2 Kuunganisha mbinu za usimamizi wa misitu zinazozingatia mabadiliko ya tabianchi kufikia Juni 2028.
	1.3 Kuanzisha ubia kati ya sekta ya umma na binafsi kwa ajili ya upanuzi wa misitu, kufikia Juni 2028.
Lengo 6: Kuhamasisha ukuzaji wa viwanda na biashara endelevu ya misitu ili kuongeza thamani ya mazao ya misitu, kusetusha bidhaa, kuongeza mapato ya nje, na kuzalisha bidhaa ndani mbadala wa zinazoagizwa toka nje	
2. Kuongeza mchango wa sekta ya misitu katika Pato la Taifa kufikia angalau asilimia 3- 4 na kuongeza mauzo ya nje ya mazao ya misitu kufikia dola za Marekani milioni 150-200 kufikia Juni 2028.	2.1 Kuendeleza viwanda vya misitu kupitia kuongeza thamani, kusetusha , na matumizi ya teknolojia ya kisasa katika usindikaji, kufikia Juni 2028.
	2.2 Kuhamasisha ugharamiaji wa mabadiliko ya tabia nchi na uwekezaji unaolinda mazingira ili kusaidia viwanda endelevu, kila mwaka.
	2.3 Kuimarisha sera wezeshi kwa viwanda vinavyotegemea misitu, ikijumuisha kuzingatia taratibu, uratibu, na ushirikishwaji, kufikia Juni 2028.
1.1.6 Ufugaji Nyuki	
Lengo 1: Kusasisha na kuendesha kibiashara sekta ya ufugaji nyuki kwa maisha endelevu, uzalishaji viwandani unaolinda mazingira, na ushindani wa mauzo ya nje kupitia uendelezaji wa ujuzi, matumizi ya teknolojia, na ujumuishaji wa soko	

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
1. Kuongeza uzalishaji wa asali na mazao ya nyuki nchini kwa asilimia 50 ya kiwango cha sasa kufikia Juni 2028.	1.1 Kuimarisha mifumo ya udhibiti, mazingira halisi, na viwango vya uzalishaji ili kutoa mazingira bora ya uzalishaji na uuzaji wa mazao ya nyuki kufikia mwaka 2028.
	1.2 Kusasisha mbinu za kuboresha ufugaji nyuki na kuwezesha mabadiliko kutoka mizinga ya asili kwenda kwenye vifaa vya kisasa vilivyosanifiwa kufikia Juni 2028.
	1.3 Kutekeleza mpango mkubwa wa kitaifa wa kupanda na kuhifadhi mimea rafiki kwa nyuki, ili kuingunisha na mabadiliko tabia nchi kitaifa, na juhudi za upandaji miti, kufikia 2028.
	1.4 Kuandaa na kusambaza mtaala wa kisasa wa ufugaji nyuki, kwa kukizingatia maeneo mbalimbali ya hali ya hewa na kuunganishwa na huduma za ugani za kilimo nchini kufikia 2028.
2. Kuongeza uwekezaji unaoongozwa na sekta binafsi katika mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki kwa asilimia 50 ya kiwango cha sasa na kuanzisha angalau biashara 5 kubwa za ufugaji nyuki zinazolenga masoko ya nje, kufikia Juni 2028.	2.1 Kutengeneza chapa bora ya kitaifa yenye mfumo wa kidijitali wa ufuatiliaji (na kusaidia wazalishaji kupata vyeti vya kimataifa kufikia Juni 2028.
	2.2 Kuwezesha ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na mipango ya wazalishaji wa nje katika ufugaji nyuki inayounganisha kampuni kubwa za kibiashara na wafugaji wadogo, ili kuhakikisha usambazaji thabiti wa malighafi bora, na kuhakikishia upatikanaji wa masoko ya uhakika na msaada wa kitaalamu kufikia Juni 2028.
	2.3 Kujenga na kuendeleza mradi wa mipango ya biashara iliyoidhinishwa, inayoweza kuwekezwa kwa ufugaji nyuki mkubwa, viwanda vya kusindika, na uzalishaji bidhaa, ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	2.4 Kuanzisha na kusimamia viwango vya kitaifa vya ubora kwa mazao yote ya nyuki, ili kuhakikisha usalama, kuongeza upatikanaji wa masoko ya kimataifa, na kujenga imani kwa walaji, kufikia Juni 2028.
3.3.2 Sekta ya Viwanda na Uzalishaji	
Lengo 1: Kuibadilisha Tanzania kuwa kituo kikuu cha utengenezaji bidhaa katika ukanda wa Afrika Mashariki kwa kufikia kiwango cha wastani cha ukuaji wa viwanda cha asilimia 9 kwa mwaka, na mchango endelevu wa sekta hiyo wa asilimia 15 katika Pato la Taifa	
Tanzania kuwa kati ya nchi 50 bora zenye urahisi wa kufanya biashara kufikia Juni 2028.	1.1 Kutengeneza sera ya taifa ya viwanda na mkakati wa viwanda 2050, inayohamasisha usetushaji na uongezaji thamani kwenye uzalishaji viwandani, kufikia Juni 2028.
	Kutengeneza kanuni ya kisheria na kitaasisi itakayowezesha utekelezaji wa dhati wa sera mpya ya viwanda kufikia Juni 2028.
	Kutekeleza sera mpya ya viwanda itakayojikita katika kipaumbele cha kuimarisha mnyororo wa thamani kama mwelekeo wa taifa katika kukuza maendeleo ya viwanda kufikia mwaka 2028.
	1.2 Kutengeneza sera lengwa ya bajeti na maboresho ya kanuni za kisheria ili kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja toka nje na uingizaji wa teknolojia na maendeleo ya viwanda vya ndani, kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha mfumo shindani wa kifedha unaotoa motisha maalum kwa uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni unaolenga uhawilishaji wa teknolojia na maendeleo ya viwanda vya ndani kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuanzisha mfumo wa kisheria uliorahisishwa, ikijumuisha kituo jumuishi cha uwekezaji (ili kurahisisha uwekezaji, kupunguza muda na gharama za kuanzisha, na uendeshaji biashara za viwanda, kufikia Juni 2028.
	1.3 Kuandaa mkakati wenye mfumo wa kukuza uwekezaji binafsi katika viwanda vya kuongeza thamani madini (viwanda vya uchakataji wa madini), uhamasishaji uwekezaji binafsi katika viwanda vinavyotumia madini, kufikia Juni 2028.
	i. Kuandaa mwongozo wa uwekezaji katika uzalishaji viwandani wa bidhaa za madini, ikijumuisha motisha za kisera, matumizi ya rasilimali za ndani, na fursa za utafiti na maendeleo ili kuonyesha ahadi ya thamani kwa wawekezaji, kufikia mwaka 2028.
	Kuzindua kampeni ya kimataifa ya uwekezaji iliyolengwa, kwa kuzingatia mfumo wa kitaifa wa usimamizi wa taarifa za viwanda kufikia mwaka 2027, kwa kutumia fursa za maonyesho ya biashara yaliyoboreshwa na ya kimataifa ili kuvutia wawekezaji mahiri katika maeneo yaliyobainishwa ya mnyororo wa thamani wa madini, kufikia Juni 2031. Kuanzisha dawati la kuwezesha uwekezaji katika uzalishaji wa bidhaa za madini, ifikapo Juni 2028.
	1.4 Kuweka kipaumbele cha kununua bidhaa zilizozalishwa za ndani kwa manunuzi ya serikali na kuhakikisha kuwa wazalishaji wa ndani wanapata mahitaji thabiti kwa bidhaa zao muda wote, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kutekeleza sera ya kuweka kima cha chini matumizi ya rasilimali za ndani (local content) katika ununuzi wa umma, kwa kutatenga angalau asilimia 30 ya matumizi ya bidhaa zinazostahiki kwa wazalishaji wananchi waliothibitishwa, kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha mpango wa kuwaendeleza wasambazaji kuwathibitisha na kuinua MSMEs kufikia viwango vya manunuzi serikalini, kufikia Juni 2028.
Mauzo nje kwa bidhaa ambazo zimezalishwa SEZ na EPZ kupanuka na kufikia asilimia 22 ya jumla yote ya mauzo nje ya sekta, ifikapo Juni 2028.	2.1 Kuanzisha maeneo ya ubunifu na teknolojia ili kuvutia uwekezaji wa utafiti na maendeleo, na utengenezaji wa bidhaa katika maeneo ya mauzo ya nje, hususan kwa viwanda vinavyotumia teknolojia ya hali ya juu, kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha mfumo maalum wa kanuni za kisheria kwa maeneo maalum ya ubunifu na teknolojia utakaotoa taratibu zilizorahisishwa na motisha zilizolengwa, kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha maeneo maalum ya ubunifu na teknolojia ikilenga sekta zenye fursa kubwa zaidi, kufikia Juni 2028.
	Kuboresha na kupanua Kanda Maalum za Kiuchumi (SEZ) na Kanda za Uzalishaji mauzo Nje (EPZ) zilizopo kwa kuweka miundombinu ya kisasa, kuweka kipaumbele katika kuendeleza kando ya reli ya kisasa (SGR), kufikia Juni 2028.
	2.2 Kuanzisha uzalishaji viwandani kwa kutumia teknolojia ya hali ya juu katika Kanda Maalum za Uchumi (SEZ) na Maeneo Maalumu ya Uwekekezaji (EPZ) kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kanda Maalum za Uchumi (SEZs) Maeneo Maalumu ya Uwekekezaji (EPZs) kuwekewa miundombinu ya msingi ya kidijitali (kama vile intaneti yenye kasi ya juu na mifumo ya IoT(na kusaidia kupitishwa kwa teknolojia ya Viwanda 4.0 kufikia Juni 2028.
	Kujenga mazingira mazuri ya kuanzishwa viwanda vya madawa ya binadamu vyenye ithibati, kufikia Juni 2028.
	kuanzisha motisha maalum kwa uzalishaji viwandani kwa kutumia mbinu za kisasa na kuanzisha vituo vya mafunzo ya ujuzi ndani ya kanda maalum za uchumi (SEZs) ili kuchapusha uwekezaji wa sekta binafsi, kufikia Juni 2028.
	2.3 Kuanzisha asilimia 50 ya Maeneo Maalumu ya Uwekekezaji/ Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZs) zenye vivutio maalum na masharti, kwa ajili ya uzalishaji wa viwanda vinavyotumia teknolojia ya juu na viwanda vya utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na madini, kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha teknolojia maalum ya hali ya juu (na kuimarisha mfumo wa vivutio vya kuongeza thamani madini katika Kanda Maalum za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZs), kufikia Juni 2028.
	Kuteua na kuboresha asilimia 50 ya Kanda zote Maalum za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZs) kama Kanda za Viwanda vya Hali ya Juu kufikia Juni 2031, na kuziwezesha kwa mahitaji muhimu ya miundombinu ya kidijitali na nguvukazi watu yenye ujuzi, ili kuendesha viwanda vinavyotumia teknolojia ya hali ya juu, kufikia Juni 2028.
	2.4 Kuhamasisha utengenezaji bidhaa zenye ufanisi wa nishati na rafiki wa mazingira, kulingana na viwango vya kimataifa na kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kutekeleza mfumo wa ukaguzi wa lazima wa nishati na mazingira kwa viwanda vyote vya uzalishaji na kuanza ukaguzi wa kufuata viwango kwa taasisi za ithibati, kufikia Juni 2028.
	Kuvutia Uwekezaji wa Moja kwa Moja wa Kigeni wa Kijani (Green FDI) kwa kutoa vivutio maalum kwa kampuni za kigeni zinazohamisha teknolojia ya hali ya juu ya viwanda safi na kuokoa nishati kwenda kwa viwanda vya ndani kila mwaka.
	Kuanzisha Mpango wa Motisha kwa uzalishaji unaojali mazingira unaotoa msamaha wa kodi kwa kampuni zinazopata vyeti vya kimataifa vya mazingira, kama vile ISO 14001, kufikia Juni 2028.
	2.5 Kuhakikisha wazalishaji wa ndani wanakidhi viwango vya ubora vya kimataifa ili kushindana katika masoko ya kimataifa, hasa kwa bidhaa za thamani ya juu, kila mwaka.
	Kuanzisha mtandao wa kitaifa wa vituo vya ukaguzi na uthibitisho vya kimataifa ifikapo mwaka 2028, ili kuwezesha wazalishaji wa ndani kuthibitisha bidhaa zenye thamani kubwa kufikia viwango vya kimataifa ndani ya nchi, kila mwaka.
	Kuanzisha na kuvutia hisa za uzalishaji wa bidhaa za thamani ya juu (elektroniki, dawa, mitambo na vipuri vya magari), kufikia Juni 2028.
Kuongezeka kielezo (index) cha mauzo nje ya bidhaa mseto kutoka 0.4 hadi 0.52, ifikapo Juni 2028.	3.1. Kuanzisha na kuongeza wigo wa uzalishaji wa ndani wa chuma, magari, makaa ya mawe na uzalishaji wa bidhaa za kielektroniki hadi kufikia angalau asilimia 40 na asilimia 1 katika mnyororo wa mauzo ya nje wa kikanda na kimataifa, mtawalia, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuendeleza maeneo maalumu ya kongani za viwanda kwa ajili ya chuma, magari na vifaa vya elektroniki, kuweka wazalishaji viwandani pamoja na vituo vya mafunzo ya ujuzi na vitovu vya mnyororo wa ugavi, kufikia mwaka 2029.
	Kuandaa vivutio vya kimkakati katika maeneo ya uzalishaji, ikijumuisha punguzo maalum la kodi, ruzuku ya viwango vya umeme, na vipaumbele kwenye kugharamia miradi itakayozingatia matumizi ya rasilimali za ndani na malengo ya mauzo ya nje, kufikia Juni 2028.
	3.2 Kutengeneza na kuuza nje bidhaa za viwandani za teknolojia ya juu katika masoko ya kimataifa (Ulaya, Asia, Amerika), kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha mtandao wa kitaifa wa vituo maalumu vya ubunifu vinavyolenga akili unde na uzalishaji wa viwango vya juu, ifikapo mwaka 2028, unaofikia viwango vya kimataifa ili kuwa injini ya ukuzaji wa bidhaa za teknolojia ya juu, kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha kituo au mpango maalum wa kuwezesha utafiti ifikapo mwaka 2029, pamoja na kutoa ruzuku kwa tafiti na maendeleo na unafuu wa biashara, na motisha maalum kwa wawekezaji, kufikia Juni 2028.
	Kuandaa Mpango wa Kimataifa wa uuzaji wa teknolojia ya juu nje, ifikapo mwaka 2030, ili kusajili bidhaa za teknolojia ya juu kwa viwango vya kimataifa na kuzindua kampeni maalum za kupenya kwenye masoko ya Ulaya, Asia na Amerika kufikia Juni 2028.
Lengo 2: Kuimarisha matumizi ya rasilimali za ndani na kukuza uchumi jumuishi unaolenga biashara ndogondogo ndogo na za kati (MSMEs)	

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
4.Kuongeza thamani katika uzalishaji kwa MSMEs kutoka asilimia 12 hadi 22, kufikia Juni 2028.	4. Kufanya mapitio na kuanzisha mifumo ya udhibiti kwa ajili ya kurasimisha MSMEs, kuongeza upatikanaji wa fedha, kujenga uwezo na upatikanaji wa masoko ya kikanda na kimataifa, maeneo ya biashara yaliyorasimishwa, na miundombinu wezeshi ya kutosha, kufikia Juni 2028.
	4.2 Kuandaa mpango wa kusaidia biashara ndogondogo na za kati (SMEs) za uzalishaji viwandani kupitia ruzuku/mikopo, kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha kituo maalum cha kuwezesha biashara ndogondogo na za kati (MSMEs) za uzalishaji, kutoa ruzuku na mikopo nafuu kwa ajili ya kuboresha teknolojia na kupanua biashara kufikia 2028.
	Kuanzisha mpango maalumu wa dhamana ya mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati, ili kuwezesha benki za kibiashara kutoa mikopo kwa ajili ya kuinua teknolojia na kupanua biashara, kufikia mwaka 2028.
	Kujumuisha huduma maalum za kusaidia biashara, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa fedha na msaada wa kitaalam ndani ya maeneo yote maalum ya viwanda vidogo na vya Kati (MSME parks) yanayofanya kazi, kufikia Juni 2028.
	4.3 Kuwezesha ushirikishwaji wa viwanda vidogovidogo vya ndani katika mnyororo wa ugavi wa viwanda kwa kusaidia viwango vya ubora, kujenga uwezo na upatikanaji wa masoko, kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha mpango wa kitaifa wa udhibiti wa ubora wa viwanda vidogovidogo (MSMEs) ili kusaidia kufikia viwango vya kimataifa vya uzalishaji, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuzindua mpango wa kitaifa wa kuunganisha minyororo ya ugavi, utakaosaidia kuoanisha biashara na makubaliano ya kandarasi kati ya biashara ndogondogo na za kati zilizothibitishwa na wazalishaji wakubwa, kufikia Juni 2028.
	Kuandaa mtaala wa mafunzo ya utayari wa kushiriki katika mnyororo wa usambazaji na kuupeleka kwa viwanda vidogo, kwa ajili ya taratibu za manunuzi, usafiri na usafirishaji, na kuongeza uzalishaji, kufikia Juni 2028.
3.3.3 Sekta ya Ujenzi	
Lengo 1: Kuanzishwa kwa sekta ya ujenzi endelevu, jumuishi, shindani kikanda, inayoongozwa na wakandarasi wa ndani, inayochochea ukuaji wa uchumi, kuendeleza viwanda, kuboresha viwango vya maisha, na kuhimiza maendeleo ya teknolojia na ubunifu	
Kuongezeka kwa thamani ya hisa za wakandarasi wa ndani wanaoshiriki katika miradi mikubwa ya ujenzi hadi asilimia 50, kufikia Juni 2028.	1.1 Kuandaa mwongozo wa ugharamiaji kwa wakandarasi utakaoimarisha upatikanaji wa fedha kwa kampuni za ndani na kuimarisha ushiriki wao katika miradi mikubwa, kufikia mwaka 2028.
	1.2 Kutekeleza mwongozo wa uwezeshaji wakandarasi wa ndani, utakaoelekeza malipo kufanyika ndani ya siku 30, kutoa kipaumbele kwa rasilimali za ndani katika manunuzi, na utekelezaji wa vifungu vya ubia vyenye viashiria (KPIs) vya uhawilishaji teknolojia kwa miradi yote ya umma, kufikia mwaka 2028.
	1.3 Kuboresha mfumo wa kupanga, kusimamia, kufuatilia na kutathmini ushiriki wa wananchi katika manunuzi ya umma, kufikia Juni 2028.
	1.4 Kutekeleza motisha ya kuhamasisha matumizi ya vifaa vya kisasa vya ujenzi na teknolojia, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	1.5 Kuzindua programu ya utayari wa kimataifa, ili kuzitunukia kampuni za ndani vyeti vya viwango vya kimataifa (kama ISO), kuongeza uaminifu na ushindani kwa miradi ya kikanda, kufikia Juni 2028.
2. Angalau asilimia 50 ya miradi mikubwa ya ujenzi kutekelezwa kupitia fedha zilizopatikana toka vyanzo mbadala, ikiwa ni pamoja na Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kufikia Juni 2028.	2.1 Kuimarisha na kutafsiri miongozo ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa kuwezesha kuandaliwa kwa miradi inayotekelezeka na inayoweza kupata ufadhili, kufikia mwaka 2027.
	2.2 Kutoa motisha za kifedha na zisizo za kifedha kwa wawekezaji binafsi, kila mwaka.
	2.3 Kuimarisha ujuzi wa watumishi wa umma katika kusimamia mikataba ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kila mwaka.
	2.4 Kuhamasisha matumizi ya zana za soko la mitaji (kama hisa na dhamana) ili kufadhili miradi mikubwa ya ujenzi, kila mwaka.
	2.5 Kuimarisha utekelezaji wa mifumo iliyopo ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa kuandaa orodha ya miradi inayoweza kupata ufadhili, kufikia mwaka 2028.
	2.6. Kuimarisha na kuendesha utendaji wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika Wizara, Idara, Wakala (MDAs) na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) ili kuvutia wawekezaji, kufikia mwaka 2028.
3. Angalau asilimia 50 ya kampuni za ujenzi za ndani zitatumia teknolojia za kisasa na mbinu endelevu katika miradi mikubwa ya ujenzi, kufikia Juni 2028.	3.1 Kuimarisha matumizi ya tafiti na teknolojia mpya katika sekta ya ujenzi, kila mwaka.
	Kuhamasisha ushirikiano kati ya makampuni ya ndani na ya kimataifa katika miradi mikubwa ya ujenzi, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kufadhili vituo vya ubunifu kwa ajili ya Utafiti na Maendeleo ya malighafi za ndani, kila mwaka.
	Kuimarisha uhawilishaji na usambazaji wa teknolojia za kisasa na utumiaji wa matokeo ya utafiti katika sekta ya ujenzi, kila mwaka.
	Kuanzisha mfumo endelevu wa ufadhili wa utafiti, ubunifu, na uboreshaji wa mifumo ya ujenzi, kufikia Juni 2028.
	Kuimarisha TanT, kufikia Juni 2028.
4. 80% ya kazi za kitaalamu na zenye ujuzi zinazopatikana katika sekta ya ujenzi kufanywa na wakandarasi wa ndani, ifikapo Juni 2028.	4.1 Kuimarisha matumizi ya tafiti na teknolojia mpya katika sekta ya ujenzi kila mwaka.
	Kuanzisha chuo cha kisasa cha mafunzo ya ujenzi ifikapo 2028 ili kuweka viwango na kutoa mafunzo katika nyenzo za kidijitali (utakaozingatia ujenzi rafiki wa mazingira, na usimamizi wa miradi ya kimataifa.
	Kutekeleza Mpango wa Taifa wa Mafunzo kwa Vitendo katika sekta ya ujenzi utakaowataka washiriki wa miradi mikubwa kushirikiana na taasisi za mafunzo ya ufundi, ili kuwezesha mafundi kupata ithibati ya ujuzi wa ujenzi wa kisasa, kila mwaka.
	Kuboresha programu za mafunzo kulingana na mahitaji ya sekta ya ujenzi, kila mwaka.
	Kuimarisha vyanzo vya upatikanaji wa fedha kusaidia mafunzo katika sekta ya ujenzi, kila mwaka.
	Kuimarisha programu maalum za mafunzo ya ufundi, kwa mafundi wananchi wa ujenzi, kila mwaka.
5. kujumuisha asilimia 30 ya miradi ya ujenzi katika	5.1 Kuhamasisha ujenzi wa kijani na stahimilivu, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
miundo yenye ufanisi wa matumizi ya nishati na mbinu za ujenzi rafiki kwa mazingira na ujenzi stahimilivu, kufikia Juni 2028.	Kuanzisha na kutekeleza Kanuni za Majengo ya Kijani (na Sera ya Manunuzi ya Umma ya Kijani kwa miradi yote mipya ya serikali, kufikia Juni 2028.
	Kuunda kanuni stahimilivu za miundombinu za kiufundi, viwango, na miongozo kufikia Juni 2028.
	Kuzindua kifurushi cha motisha ya teknolojia zinazotunza mazingira kinachotoa punguzo la kodi na ruzuku kwa miradi inayotumia nishati mbadala, ujenzi wa awali na ubunifu wa vifaa vya ndani, kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha na kuthibitisha wataalamu wa ujenzi katika usanifu, usimamizi na uthibitishaji wa majengo rafiki wa mazingira kupitia programu ya kitaifa ya kuongeza kasi ya ujuzi, kufikia Juni 2028.
	Kutekeleza programu za mafunzo ya kujenga uwezo wa wadau wa ujenzi kuhusu ujenzi wa kijani na kanuni za miundombinu stahimilivu, kila mwaka.
	Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya ujenzi unaotunza mazingira na ustahimilivu kila mwaka.
3.3.4 Sekta ya Madini na Uchimbaji Mawe	
Lengo 1: Kuendeleza sekta shindani na jumuishi ya madini inayotegemea viwanda na inayotumia kwa ufanisi rasilimali za madini huku ikidumisha na kuimarisha minyororo ya thamani ya ndani	
1. Asilimia 25 ya wataalamu wa sekta ya madini kupewa mafunzo ya umahiri, unaoendana na uongezaji thamani wa madini na uchumi wa viwanda, kufikia Juni 2028.	1.1 Kuhakikisha upatikanaji wa nguvu kazi yenye ujuzi ili kusaidia uongezaji thamani wa madini na uzalishaji viwandani kufikia mwaka 2028.
	1.2 Kupanua na kuboresha taasisi za mafunzo ya kiufundi (mfano, Moshi) ili kukuza nguvu kazi ya uchimbaji wa madini na uongezaji thamani, kufikia mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	1.3 Kuanzisha vyuo vya mafunzo ya madini na ufundi vilivyofungamanishwa, kwa lengo la kujenga mfumo endelevu wa kuzalisha wataalamu wenye ujuzi na utayari wa kufanya kazi katika sekta ya madini, kufikia Juni 2028.
	1.4 Kuboresha kanuni za maudhui ya ndani katika sekta ya madini kwa kuanzisha mfumo wa dhamana ya madini kufikia Juni 2028.
2. Kuongeza kiwango cha ufanisi wa usimamizi wa sekta ya madini kutoka kiwango cha sasa hadi angalau asilimia 65, kufikia Juni 2028.	2.1 Kuandaa na kutekeleza Mfumo Jumuishi wa Serikali-Mtandao (E-Government) katika sekta ya madini, kufikia Juni 2028.
	2.2 Kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa vyombo muhimu vya udhibiti (Tume ya Madini, Taasisi ya Jiolojia, nk) ili kuimarisha utawala, ukaguzi, uzingatiaji wa sheria, na usimamizi wa sera , kufikia mwaka 2028.
	2.3 Kuunganisha usimamizi wa sekta ya madini na viwango vya kimataifa, ikiwa ni pamoja na Mpango wa Uwazi wa Sekta ya Uchimbaji (EITI), kupitia utoaji wa taarifa za lazima za kila robo mwaka, kufikia 2028.
	2.4 Kuanzisha utaratibu wa pamoja wa uratibu kati ya Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs), na vyombo vya udhibiti wa madini, ili kurahisisha utoaji wa maamuzi, kufikia Juni 2028.
	2.5 Kuanzisha mfumo thabiti wa kitaifa wa uwekezaji katika sekta ya madini ili kurahisisha usaidizi wa wawekezaji, kupunguza ucheleweshaji kutokana na urasimu, na mfumo wa utatuzi wa malalamiko kufikia Juni 2028.
	2.6 Kuanzisha Kituo cha Kitaifa cha Ubora kwa ajili ya uchumi wa madini, uchimbaji wa kidijitali, ukadiriaji wa akiba, mbinu za kijiolojia na utii wa viwango vya mazingira, kijamii, na utawala bora kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	2.7 Kuweka Mikataba ya Maendeleo ya Jamii (CDAs) katika mfumo wa taasisisi na kusimamia kikamilifu uzingatiaji wa athari za kijamii na kimazingira kupitia mfumo thabiti wa kitaifa, kufikia Juni 2028.
3. Kuongeza ushiriki wa wanawake katika sekta ya madini kutoka asilimia 19 hadi asilimia 40, kufikia Juni 2028.	3.1 Kuimarisha mifumo ya kisheria na udhibiti ili kuhakikisha ushiriki sawa wa wanawake katika mnyororo mzima wa thamani wa madini, kufikia 2028.
	3.2 Kuanzisha programu na viwango vya kitaifa vya kuongeza uwezo wa kiufundi, usimamizi, na ujasiriamali kwa wanawake, kufikia Juni 2028.
	3.3 Kuanzisha mifumo maalum ya ugharamiaji na motisha, ikijumuisha upatikanaji wa mitaji, teknolojia, na vifaa, ili kuendeleza biashara za madini zinazoongozwa na wanawake, kufikia Juni 2028.
4. Kudumisha ushiriki wa vijana katika uchimbaji madini kwa angalau asilimia 10 ya jumla ya nguvu kazi katika sekta ya madini, kufikia Juni 2028.	4.1 Kuanzisha programu na motisha za kitaifa zinazohamasisha ubunifu wa kiteknolojia kwa vijana na masuala ya kidijitali katika sekta ya madini, kufikia Juni 2028.
	4.2 Kuandaa mfumo wa kitaifa wa kukuza umahiri kwa ajili ya kuboresha taaluma endelevu ya vijana wanaofanya kazi katika sekta ya madini, unaoendana na mabadiliko ya kidijitali ya sekta, na teknolojia mpya, kufikia Juni 2028.
	4.3 Kuanzisha mifumo ya udhibiti na ununuzi inayoweka masharti au kutoa motisha kwa zabuni ndogo (subcontracts) kwa biashara zinazomilikiwa na vijana katika nyanja mbalimbali za mnyororo wa thamani wa madini, kufikia Juni 2028.
Lengo 2: Kuongezeka kwa uanzishaji wa miradi mipya ya uchimbaji wa madini na kufunguliwa kwa miradi ya utafiti na uchimbaji wa madini iliyokwama, kuweka mazingira wezeshi na urahisishaji wa taratibu kwa wawekezaji wa ndani na wa nje (FDI) katika utafiti na maendeleo ya madini	

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
1. Kuongezeka kwa huduma za ramani za kijiolojia, kijiofizikia na kijiokemia zinaofanywa na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) na kufikia asilimia 100%, kufikia mwaka 2028.	1.1 Kufanya mapitio ya kina na uwiano wa mifumo ya kisheria na udhibiti wa madini, viwanda, fedha, na kodi ni hatua muhimu ya kuongeza kasi ya utafiti, kukuza maendeleo ya madini, na kusaidia viwanda vya madini, kufikia mwaka 2028.
	1.2 Kuimarisha uwezo wa kitaalamu na mifumo ya kusimamia uendeshaji wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania , ili kuinua utoaji wa huduma na ufanisi wa kitaasisi, kufikia Juni 2028.
	1.3 Kuipatia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) teknolojia za kisasa za uchoraji ramani za kijiolojia, kijiokifizikia na kijiokemia pamoja na maabara ya uchambuzi, ili kuwezesha upatikanaji kamili wa taarifa za kitaifa, kufikia mwaka 2028.
2. Kulibadilisha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kuwa kampuni ya umma ya kibiashara inayokidhi viwango vya kimataifa vya utawala bora na uendeshaji wa mashirika, ikiwa na angalau cheti cha ubora cha ISO 9001 na taarifa za fedha zilizokaguliwa kila mwaka, kufikia Juni 2028.	2.1 Kuifanya STAMICO kuwa kampuni ya kimkakati ya kitaifa, ya uchimbaji madini ambayo serikali ina umiliki mkubwa wa hisa ifikapo mwaka 2028, ili kuweka msingi wa mageuzi ya utawala bora wa kampuni.
	2.2. Kuiwezesha kifedha (mtaji) na kutoa mafunzo kwa watendaji na wafanyakazi, katika nyanja za ujuzi wa kiufundi, kifedha na kiutendaji, sambamba na kuboresha miundombinu na mifumo, kufikia Juni 2028.
	2.3 Kuiwezesha STAMICO kupata haki za uchimbaji wa madini na kuongeza shughuli za utafiti na uchimbaji kutoka migodi 3 hadi 7 na kuwa na ukuaji unaopimika na uzingatiaji wa viwango vya kimataifa, kufikia Juni 2028.
3. Kulibadilisha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kuwa kampuni ya umma ya kibiashara inayokidhi viwango vya kimataifa vya utawala bora na uendeshaji	3.1 Kuanzisha mfumo wa kimuundo wa kurahisisha uwekezaji kwa ajili ya kuvutia na kurasimisha ubia kati ya Serikali na wawekezaji binafsi katika miradi yenye tija ya uchimbaji wa madini, kufikia mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
wa mashirika, ikiwa na angalau cheti cha ubora cha ISO 9001 na taarifa za fedha zilizokaguliwa kila mwaka, kufikia Juni 2028.	3.2 Kuandaa mipango ya pamoja ya maendeleo ya miundombinu (barabara, umeme, maji, na vituo vya usafirishaji) kwa kushirikiana na wawekezaji binafsi ili kufungua fursa za madini na kuongeza tija ya sekta, kufikia Juni 2028.
	3.3 Kuanzisha vivutio vya kisheria, kiudhibiti na kifedha ili kuongeza mvuto wa ubia na uwekezaji wa muda mrefu katika sekta ya madini, kufikia 2028.
4. Kuidhinisha, kupata uwekezaji, na kuanza utekelezaji wa angalau miradi 5 ya kimkakati ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini, kufikia Juni 2028.	4.1 Kutoa kipaumbele na kuharakisha utoaji wa leseni na vibali vya udhibiti kwa miradi ya madini ya kimkakati na maeneo muhimu, ili kuvutia wawekezaji wa kimkakati, kufikia mwaka 2028.
	4.2 Kuanzisha ubia wa kimkakati kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa ajili ya miradi mikubwa, kama Liganga–Mchuchuma (chuma/chuma cha pua), viwanda vya uchenjejuaji nikeli, cobalt na shaba, pamoja na mitambo ya usindikaji wa madini adimu (Rare-Earth Minerals – REE), ili kuhakikisha upatikanaji wa fedha, uhawilishaji wa teknolojia, na utayari wa uendeshaji, kufikia Juni 2028.
	4.3 Kuendeleza miundombinu jumuishi na maeneo ya viwanda (nishati, usafiri, maji, na vifaa/logistics) ili kusaidia utekelezaji wa miradi ya madini na uchenjuaji wa madini, kufikia Juni 2028.
Lengo 3: Kuhamasisha uwekezaji wa ndani na wa kigeni (FDI) katika usindikaji, uchenjuaji, usafishaji, na utengenezaji wa madini ya viwandani na madini muhimu, kwa lengo la kuchochea maendeleo ya viwanda na ukuaji wa uchumi	
1. kuongezeka kwa mchango wa madini ya viwandani na madini muhimu (critical base metals) kupitia uongezaji thamani na uzalishaji wa viwandani hadi angalau asilimia	1.1 Kuanzishwa kwa viwanda vya kauri, mbolea, vioo, saruji, kemikali, dawa, na betri vinavyotumia madini ya viwandani na madini mkakati kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
3 kufikia Juni 2028.	1.2 Kuanzisha Kituo cha Teknolojia ya Madini Muhimu (Critical Minerals Technology Hub), kinachojulikana kama "Silicon Valley ya Dodoma," kwa ajili ya kuendeleza viwanda vya ndani vya betri za lithiamu-iron na teknolojia nyingine rafiki kwa mazingira (mradi wa kimkakati), kufikia Juni 2028.
	1.3 Kuwekeza katika uanzishaji wa mitambo ya kuyeyusha na kusafisha metali za msingi (kama vile shaba, zinki, bati, alumini, risasi, nikeli n.k.), kufikia Juni 2028.
Lengo 4: Kuongezeka kwa uzalishaji na mauzo nje ya dhahabu na vito, na hivyo kuinua nafasi ya Tanzania katika soko ya kimataifa la madini	
1. Kuongeza uzalishaji na uuzaji nje wa dhahabu na vito kwa angalau asilimia 30 ifikapo Juni 2031, ikichangiwa na ushirikishwaji wa migodi mikubwa na ya wachimbaji wadogo kurasimisha sekta, na kupatikana kwa fedha na teknolojia, kufikia Juni 2028.	1.1 Kuandaa na kutekeleza mfumo wa kitaifa wa urasimishaji wa wachimbaji wadogo na wa kati (ASM), utakaowawezesha kuwaunganisha katika minyororo rasmi ya ugavi, uzingatiaji wa sheria, na masoko ya kuuza nje, ifikapo mwaka 2028.
	1.2 Kuanzisha ubia wa kimkakati kati ya Serikali na sekta binafsi (PPPs) pamoja na ubia wa pamoja (joint ventures) ili kuvutia uwekezaji katika utafiti na uchimbaji mkubwa wa dhahabu na vito, ifikapo Juni 2028.
	1.3. Kuanzisha jukwaa la kitaifa la ugharamiaji na na teknolojia kwa wachimbaji wadogo (ASM) na wachimbaji wakubwa, likijumuisha mikopo yenye riba nafuu, ukodishaji wa vifaa, na msaada wa kitaalamu ili kuboresha ufanisi wa uzalishaji na ubora wa bidhaa, kufikia Juni 2028.
	1.4 Kuimarisha mifumo ya takwimu za kijiolojia na kijiospatia ili kuongoza utafutaji wenye tija na kuwezesha uchimbaji endelevu wa dhahabu na vito kufikia , Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
2. Kuongeza uzalishaji na mauzo ya nje ya dhahabu na vito kwa angalau asilimia 30 kupitia ushirikishwaji.	2.1 Kuongeza uwezo wa uchimbaji mkubwa wa dhahabu kwa kutoa leseni kimkakati kwa migodi mipya na kuboresha utendaji wa migodi iliyopo ili kufikia angalau migodi 7 inayofanya kazi kufikia Juni 2028.
	2.2 Kuimarisha hifadhi ya dhahabu ya taifa na usimamizi wa mikuo ya dhahabu kwa kuongeza akiba ya dhahabu ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kutoka tani 3.7 hadi tani 20, kufikia Juni 2028.
	2.3 Kuanzisha uongezaji thamani wa dhahabu nchini kupitia usafishaji uthibitisho wa ubora na uwekaji chapa ili kuongeza mapato ya kigeni na ushindani wa kimataifa, kufikia Juni 2028.
	2.4 Kuwezesha ubia wa kimkakati wa sekta ya umma na sekta binafsi ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje katika uchimbaji, uchakataji, na miundombinu ya madini ya kusafirisha nje, kufikia Juni 2028.
Lengo 5: Kuifanya Tanzania kuwa Kitovu cha Vito Afrika	
Kuwa na sekta ya vito yenye ushindani na inayodhibitiwa vizuri, ikiwa na angalau asilimia 40 ya biashara iliyorasimishwa, na miundombinu ya kuongeza thamani kuanzishwa, kufikia Juni 2028.	1.1 Kuandaa mfumo wezeshi wa kiudhibiti na kifedha kwa ajili ya utafiti, uchimbaji, uongezaji thamani, na biashara ya vito unaovutia wawekezaji wa ndani na wa kigeni, kufikia mwaka 2028.
	1.2 Kuimarisha programu za ukuzaji uwezo ili kujenga ujuzi, maarifa, na rasilimali kwa watu binafsi na taasisi katika sekta ndogo ya vito, kufikia Juni 2028.
	1.3 Kuanzisha miundombinu ya kimkakati ya uongezaji thamani wa vito, ikiwemo ukataji, ung'arishaji, utengenezaji wa mapambo ya vito, na vituo vya viwanda vya kukata na kusafisha vito, ikijumuisha kituo kikuu jijini Dodoma, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	1.4 Kuanzisha Eneo Maalum la Kiuchumi kwa ajili ya biashara na maonesho ya kimataifa ya vito jijini Dodoma kama mradi wa mfano kufikia , Juni 2028.
Vituo vikuu vya biashara ya vito vilivyothibitishwa nchini Tanzania vinavyolenga kuunganishwa rasmi na masoko ya kimataifa kuanzishwa, ifikapo Juni 2028.	2.1 Kujenga muunganiko na soko la kimataifa kupitia ubia na mashirika ya vito vya kimataifa, taasisi za biashara, na vituo vya elimu, kufikia Juni 2028.
	2.2 Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kitaifa wa utengenezaji wa chapa ya vito vya thamani, kwa lengo la kuvitambulisha vito vya Tanzania (ikiwemo tanzanite) katika masoko ya kimataifa, kufikia Juni 2028.
	2.3 Kuzitumia fursa za ushiriki katika maonesho ya kimataifa ya vito vya thamani na maonesho ya vito vya mapambo ili kuongeza utambulisho, kuvutia wanunuzi, na kuimarisha fursa za mauzo ya nje, kufikia Juni 2028.
3.3.5 Sekta ya Mafuta na Gesi	
Lengo 1 :Kuongeza utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi, ili kufungua kikamilifu fursa za rasilimali za nishati za taifa kwa ajili ya kuendeleza nishati endelevu na kukuza uchumi	
1. Kutekeleza mpango wa motisha mahsusi kwa ajili ya kuvutia uwekezaji katika utafiti wa mafuta na gesi, unaolenga kufikia angalau asilimia 50 ya mabonde ya mashapo ya Tanzania, kufikia Juni 2028.	1.1 Kufanya mapitio ya sera, sheria na kanuni zinazohusiana, ili kuimarisha mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji katika utafiti wa mafuta na gesi asilia, ifikapo June 2028.
	i. Kuimarisha mfumo wa kifedha na udhibiti wa utafutaji wa mafuta na gesi ifikapo 2028, kwa kutoa masharti yaliyo wazi, imara na vivutio maalum ili kuvutia mitaji hatarishi.
	Kuzindua mkakati maalum wa uhamasishaji wa utafiti wa mafuta na gesi asilia na kituo cha wazi cha taarifa kwa ajili ya kuonesha fursa za kijiolojia za Tanzania, kufikia mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuanzisha kituo kimoja cha huduma kwa wawekezaji wa mafuta na gesi asilia kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa leseni, vibali, na idhini za udhibiti, na kupunguza muda wa uidhinishaji maombi, kufikia mwaka 2028.
2. Kulifanya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuwa Kampuni ya Kibiashara inayokidhi viwango vya kimataifa, kufikia Juni 2028.	2.1 kubadilisha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kuwa kampuni ya umma ya viwango vya kimataifa, kufikia Juni 2028.
	Kuliwezesha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuongeza mara mbili wigo wake wa utafiti kwa kupewa vitalu vya ziada vilivyo na leseni, kufikia Juni 2028.
	Kuimarisha uwezo wa kibiashara wa Shirika la Tanzania (TPDC) kwa kupata mtaji, kuunda timu ya usimamizi wa shirika ya kiwango cha kimataifa, na kuboresha mifumo yake ya kiufundi, kufikia Juni 2028.
Lengo 2: Kuongeza uzalishaji na matumizi ya ndani ya gesi asilia nchini, ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa nishati kwa ajili ya viwanda vya ndani na ukuaji wa uchumi, kufikia Juni 2028	
1. Kuongezeka kwa Uzalishaji wa gesi asili nchi kavu kutoka MMSCFD 320 (milioni za futi za ujazo sanifu kwa siku) hadi MMSCFD 1000, kufikia Juni 2028.	1.1 Kuhamasisha ongezeko la uzalishaji wa gesi nchini, kufikia Juni 2031
	Kuongeza kasi ya majadiliano ya mkataba wa uwekezaji kwa mradi wa LNG wa Mtwara, kufikia mwaka 2028.
	Kuimarisha mnyororo wa thamani wa gesi asilia ya ndani kwa kuanzisha ushirikiano wa kimataifa wa uhamishaji wa ujuzi na kuboresha mtandao wa usambazaji wa gesi wa nchi kavu ili kupunguza upotevu wa usafirishaji kufikia Juni 2028.
	Kuongeza uzalishaji wa gesi nchi kavu kwa kuanzisha kisima kipya cha gesi, kufikia Juni 2028.
2. Matumizi ya gesi asilia nchini kuongezeka toka 290	2.1 Kuendeleza matumizi ya gesi asilia nchini, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
MMSCFD hadi 800 MMSCFD, ifikapo Juni 2028.	i. Anzisha vivutio vya matumizi ya gesi (kwa kutoa vivutio vya kifedha na visivyo vya kifedha kwa viwanda na kaya vinavyohamia kwenye matumizi ya gesi kufikia 2028.
	ii. Kuanzisha mpango wa kitaifa wa "Gesi kwa Viwanda" nchini, ambao utayataka maeneo makubwa ya viwanda kutumia gesi asilia, na hivyo kutengeneza uhitaji wa gesi hiyo, kufikia Juni 2028.
	iii. Kuanzisha Kituo cha Kitaifa cha Ubora wa Gesi ili kujenga uwezo wa kiufundi wa ndani, kusaidia Utafiti na Maendeleo katika matumizi ya gesi, na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi maalum kufikia Juni 2028.
Lengo 3: Tanzania kuwa kituo kinachoongoza cha uzalishaji na usafirishaji wa gesi barani Afrika, kwa kuongeza ushawishi katika masoko ya kikanda na kimataifa, na kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi wa Taifa	
1. Kuongeza usambazaji wa gesi katika Kituo cha Biashara ya Gesi cha Kikanda kutoka milioni 290 za futi za ujazo kwa siku, hadi milioni 3,500 za futi za ujazo kwa siku, kufikia Juni 2028.	1.1 Kuanza mchakato wa kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa wauzaji wakuu wa gesi barani Afrika.
	Kuhakikisha upatikanaji wa mikataba ya muda mrefu ya mauzo ya gesi na nchi muhimu ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kufikia Juni 2028.
	Kujenga kituo cha biashara ya gesi cha kikanda, chenye mabomba ya kuvuka mipaka na miundombinu ya kuhifadhia gesi, kwa ajili ya kusambaza gesi katika masoko ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, kufikia Juni 2028.
	Kujenga ushirikiano wa kimkakati katika sekta ya nishati na kuoanisha sera za biashara ya nishati za kuvuka mipaka na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika , ili kuwezesha biashara ya gesi katika ukanda huu, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
2. Uzalishaji wa gesi baharini utakaowezesha biashara ya mauzo ya LNG kufikia tani milioni 15 kwa mwaka kufikia Juni 2028.	2.1 Kukuza uzalishaji na mauzo nje ya gesi asilia ya kimiminika , kufikia Juni 2028.
	Kujenga mfumo thabiti wa udhibiti na kifedha utakaohakikisha mazingira rafiki kwa uwekezaji katika mradi wa LNG na uthabiti wa mikataba ya mauzo ya gesi kufikia mwaka 2028.
	Kuanzisha mradi wa kusindika gesi asilia ya kimiminika kwa ajili ya mauzo nje ya nchi, kufikia Juni 2028.
3.3.6. Sekta ya Utalii.	
Lengo 1: Kuimarisha shughuli, bidhaa, mbinu na uzoefu wa utalii ili kukuza uendelevu, ujumuishi na uimara, sambamba na kupanua fursa za ushiriki kwa jamii za wenyeji na kuhakikisha ukuaji wa muda mrefu wa sekta	
1. Kuboresha nafasi ya Tanzania katika Usafiri na fahirisi ya maendeleo ya utalii kutoka nafasi ya 81 hadi 60 kati ya nchi 119 duniani, kufikia Juni 2028.	1.1 Kusaidia maendeleo ya bidhaa na masoko mapya ya utalii, kufikia Juni 2028.
	Kuandaa na kuzindua bidhaa mpya za utalii zilizo tayari kuingia sokoni kwa kuzingatia tathmini ya kina ya vivutio vya utalii, kufikia mwaka 2028.
	Kuandaa mkakati wa kitaifa wa kusetusha utalii unaolenga kuvutia watalii wenye matumizi ya juu kutoka masoko mapya, kufikia mwaka 2028.
	Kuzindua kampeni za masoko ya kimataifa zilizolengwa kwa bidhaa mpya za utalii katika masoko mapya ya kimataifa, kufikia Juni 2028.
	1.2 Kuhamasisha uwepo na upatikanaji na fedha za gharama nafuu kwa ajili ya utalii, kila mwaka.
	Kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Utalii

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuanzisha mpango wa dhamana ya mikopo ya utalii ili kupunguza hatari kwa benki za biashara na kuwezesha upanuzi wa mikopo kwa sekta binafsi, kila mwaka.
	1.3 Kuimarisha uwezo wa maendeleo ya miundombinu ya utalii, kufikia Juni 2028.
	Kuwezesha Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi kuu za serikali kuwa na mifumo ya kisasa ya usimamizi wa miradi na fedha, ili kupanga, kununua, kufadhili, kutekeleza na kusimamia miradi mikubwa ya miundombinu ya utalii kwa ufanisi, kufikia Juni 2028.
	1.4 Kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali za utalii, kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha na kutekeleza mfumo wa kitaifa wa uthibitishaji wa utalii endelevu, unaowataka waendeshaji wote wa shughuli za utalii katika maeneo yaliyohifadhiwa kufuata viwango vya kimazingira na kitamaduni, kufikia Juni 2028.
	Kuweka sharti la utekelezaji wa mikataba ya mgao wa mapato kwa jamii katika miradi yote mipya ya utalii, ili kuhakikisha jamii za wenyeji zinapata sehemu ya moja kwa moja ya mapato ya utalii, kufikia Juni 2028.
	1.5 Kuimarisha uwezo wa uratibu wa shughuli za utalii, kufikia ,Juni 2028.
	i. Kuanzisha na kuendesha mfumo wa kitaasisi na sera kwa sekta ya utalii, kufikia mwaka 2028.
	Kuharakisha utekelezaji wa mifumo shirikishi ya kidijitali na majukwaa ya uratibu wa wadau, kufikia mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuimarisha uunganishaji na uhamasishaji wa pamoja wa maeneo yaliyohifadhiwa katika kanda za utalii za mashariki na kusini, kufikia mwaka 2028.
	Kuoanisha na kuunganisha hifadhi za taifa za kanda ya ziwa katika mizunguko ya utalii ya kikanda (Uganda na Rwanda), kufikia mwaka 2028.
	1.6 Kufanya uwindaji wa kitalii kuwa wa ushindani, kufikia Juni 2028.
	i. Kuimarisha utawala na uwezo wa kiutendaji wa sekta ndogo ya uwindaji wa kitalii, kufikia mwaka 2028.
	ii. Kuimarisha mifumo ya udhibiti na sera ili kuhakikisha uwindaji wa kitalii unakuwa endelevu na shindani, kufikia mwaka 2028.
	iii. Kukuza masoko mseto na kuboresha ongezeko la thamani katika mnyororo wa uwindaji wa kitalii, kufikia mwaka 2028.
	iv. Kuanzisha na kuimarisha maeneo ya usimamizi wa wanyamapori katika vijiji vinavyozunguka hifadhi, ili kuongeza jitihada za kupambana na ujangili na kushirikisha jamii katika uhifadhi, kufikia mwaka 2028.
	1.7 Kuanzisha taasisi ya Urithi wa Asili na Maeneo ya Kale chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kufikia mwaka 2028.
	Kufanya ukaguzi wa urithi wa asili na maeneo ya kale yote yaliyopo nchini, kufikia Juni 2028.
	Kuhamisha shughuli zote za urithi wa asili na maeneo ya kale kutoka taasisi zingine za Wizara ya Maliasili na Utalii kwenda kwenye taasisi ya Urithi wa Asili na Maeneo ya Kale Tanzania (TNHAS) kufikia mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	1.8 Kujenga imani zaidi kwa watalii na wageni wanaotembelea Tanzania, kufikia Juni 2028.
	i. Kuanzisha na kutekeleza ratiba ya uhakika ya kupitia kodi, ada na tozo zinazohusiana na utalii kila baada ya miaka mitatu , kufikia mwaka 2028.
	ii. Kuweka utaratibu wa lazima wa uanachama kwa wawekezaji wa utalii katika vyama vinavyotambulika vya sekta ya utalii, kufikia Juni 2028.
	1.9 Kutumia fursa za mikataba ya ushirikiano wa nchi na nchi, wa kikanda, na wa kimataifa kwa ajili ya kukuza na kuendeleza utalii wa ukanda wa pwani na baharini, kila mwaka.
	Kukuza na kuendeleza bidhaa za utalii rafiki wa mazingira katika fukwe katika maeneo ya pwani yenye kipaumbele, kufikia mwaka 2028.
	Kuanzisha Taasisi ya Hifadhi za Pwani na Maeneo ya Baharini Tanzania chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kufikia mwaka 2028.
2. Kuendeleza maeneo manne (4) maalum kiuchumi ya utalii na kuanza kazi, kufikia Juni 2028.	2.1 Kuongeza idadi ya Halmashauri za Serikali za Mitaa (LGAs) zinazoandaa ya na kutenga maeneo maalum kwa ajili utalii ya uwekezaji katika sekta utalii kutoka 13 hadi 26, kufikia mwaka 2028.
	Kuhalalisha na kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya halmashauri zote ili kuzuia mabadiliko ya matumizi ya ardhi yasiyopangwa ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya utalii, kufikia mwaka 2028.
	Kuagiza kutengwa, kutathmini, na kuhifadhi rasmi maeneo ya ardhi yanayofaa kwa uwekezaji wa utalii, kufikia mwaka 2028.
	2.2 Kujenga mifumo ya kifedha, kisheria na udhibiti ili kuvutia uwekezaji na kukuza biashara katika sekta ya utalii, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	i. Kufanya mapitio na mageuzi ya mifumo iliyopo ya kifedha, kisheria na udhibiti inayosimamia uwekezaji katika sekta ya utalii, kufikia mwaka 2028.
	ii. Kuanzisha na kusimamia kisheria marekebisho ya kodi, kanuni na taratibu, na mfumo wa udhibiti na urekebu unaosimamia uwekezaji katika sekta ya utalii kufikia mwaka 2028.
	2.3 Kuanzisha Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya Utalii kufikia Juni 2028.
	i. Kujenga na kuendesha vituo vya meli za kitalii katika bandari zilizopo (Dar es Salaam, Tanga, Mtwara) na maeneo mapya (Kilwa, Bagamoyo, Mafia), kufikia Juni 2028.
	ii. Kuanza na kuendesha huduma ya meli za kitalii katika Ziwa Victoria itakayounganisha Speke Bay, Mwanza, Musoma, Geita, Serengeti, Burigi–Chato, Kisumu na Entebbe, kufikia Juni 2028.
	Kujenga na kuendesha vituo vya mikutano vya kimataifa katika miji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Dodoma, kufikia Juni 2028.
	Kuendeleza Kisiwa cha Mafia kuwa kituo maalum cha kutia nanga meli za kitalii kufikia mwaka 2028.
	2.4. Kuandaa sera na mifumo shindani ya kuhimiza ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) katika maendeleo ya utalii, kwa kuzingatia miundombinu, ubora wa huduma, na utalii endelevu, kufikia Juni 2028.
	Kuimarisha na kuoanisha mifumo ya kisera, kisheria na ya udhibiti inayosimamia ubia kati ya sekta ya umma na sektabinafsi (PPP) katika sekta ya utalii, kufikia mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuanzisha mifumo ya utawala na usimamizi wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kuhakikisha maendeleo ya kimkakati ya miundombinu na ubora wa huduma, kufikia mwaka 2028.
	iii. Kuoanisha sera na mifumo ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na malengo ya utalii endelevu na jumuishi, kufikia Juni 2028.
Kuongezea kwa Ushiriki wa wananchi katika sekta ya talii hadi kufikia asilimia 10 kufikia Juni 2028.	3.1 Kurahisisha kanuni na taratibu za kiutawala ili kuwezesha wajasiriamali wa ndani kuingia kwenye soko la utalii, kufikia mwaka 2028.
	i. Kurahisisha taratibu za utoaji wa leseni na vibali kupitia uanzishaji wa jukwaa la kidijitali lenye huduma zote, kufikia mwaka 2028.
	ii. Kupitia, kurahisisha, na kuoanisha kanuni za utalii ili kuwaondolea urasimu wajasiriamali wa ndani, kufikia mwaka 2028.
	iii. Kuweka utaratibu rasmi wa kusaidia wajasiriamali wa utalii wa ndani, ikijumuisha ushauri wa kisheria, kifedha, na kiufundi, kufikia Juni 2028.
	3.2 Kuimarisha uwezo wa usimamizi wa biashara na ujasiriamali ili kuwawezesha wananchi, wakiwemo wanawake na watu wenye mahitaji maalum, kuanzisha na kuendeleza biashara zinazohusiana na utalii, kila mwaka.
	i. Kuanzisha mifumo jumuishi ya mafunzo na usaidizi wa ujasiriamali kwa biashara ndogondogo na za kati (SMEs) katika sekta ya utalii, kufikia Juni 2028.
	ii. Kuimarisha mifumo ya kisheria na udhibiti ili kuwezesha upatikanaji wa fedha na rasilimali kwa wajasiriamali wa ndani wa sekta ya utalii, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	3.3 Kuanzisha mfuko wa utalii ili kuwawezesha kampuni chipukizi na biashara ndogondogo na za kati kwa wajasiriamali wa ndani, kufikia Juni 2028.
	i. Kuanzisha na kuweka utaratibu wa kutoa msaada wa kifedha na kiufundi kwa wajasiriamali wadogo na wa kati (MSMEs) katika sekta ya utalii kupitia mfuko wa utalii (TBF), kufikia Juni 2028.
	3.4 Kuanzisha majukwaa ya wafanyabiashara wa ndani kushirikiana waendesha utalii wakubwa na masoko ya kikanda na kimataifa, kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha majukwaa ya kawaida na ya kidijitali, ili kurahisisha mitandao, ushirikiano, na upatikanaji wa soko kwa biashara za utalii za ndani, kufikia mwaka 2028.
	Kuanzisha rasmi mifumo ya kujenga uwezo na kusaidia upatikanaji wa masoko kwa biashara za utalii za ndani, kufikia Juni 2028.
	Kutayarisha orodha ya miradi iliyodhibitiwa, yenye masharti ya ushiriki wa watanzania katika hisa na umiliki wa biashara za utalii, kufikia mwaka 2028.
	Kusimamia kampuni za utalii zinazomilikiwa na wageni nchini kuoanisha usajili na uendeshaji wa sera zinazohimiza ushiriki wa wananchi, kufikia 2028.
4. Kuhifadhiwa na kuunganishwa kwa zaidi ya asilimia 12 ya maeneo ya vivutio vya utalii, kufikia Juni 2028.	4.1 Kuongeza ufikiaji wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa usafiri wa anga, kufikia Juni 2028.
	i. Kuboresha na kusimamia njia za kurukia ndege za viwanja vyote 39 vya ndege vilivyopo, ambavyo vinavyohudumia maeneo yaliyohifadhiwa, kufikia mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	ii. Kujenga viwanja vya ndege vipya na kuimarisha viwanja vya ndege vya kanda ambavyo viko karibu na maeneo muhimu yaliyohifadhiwa, kufikia Juni 2028.
	Kupitia na kurahisisha kodi, ada na tozo zinazohusiana na usafiri wa anga, ili kuimarisha muunganisho wa biashara ya utalii, kufikia mwaka 2028.
	4.2. Kuongeza huduma ya malazi yenye nyota moja hadi tano, kutoka 315 hadi 508, kufikia Juni 2028.
	Kuyatambua na kuyapa kipaumbele maeneo yenye upungufu wa malazi na kuanzisha mfumo wa uwezeshaji wa ardhi na miundombinu, kufikia mwaka 2028.
	ii. Kuanzisha na kuainisha viwango vya malazi, mifumo ya uainishaji, na miundo ya motisha, kufikia mwaka 2028.
	4.3 Kuhakikisha ufunguaji upya wa kudumu na ulinzi wa shoroba zote za wanyamapori nchini kote, kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha na kuainisha mfumo wa kisheria wa urejeshaji na ulinzi wa shoroba za wanyamapori, kufikia mwaka 2028.
	Kuimarisha sera, miundombinu, na mifumo ya ufuatiliaji ili kusaidia shoroba za wanyamapori, kufikia mwaka 2028.
	Kurasimisha mifumo ya ushirikishwaji wa jamii na utatuzi wa migogoro ili kusaidia ulinzi wa shoroba za wanyamapori, kufikia Juni 2028.
	4.4 Kuongeza vituo vya malazi ya gharama nafuu katika hifadhi za taifa kwa ajili ya watalii wa ndani kutoka 10 hadi 22, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	i. Kuandaa na kurasimisha mpango wa taifa wa upanuzi na uboreshaji wa vituo vya malazi ya gharama nafuu kwa watalii wa ndani, kufikia mwaka 2028.
	ii. Kuimarisha sera wezeshi na mbinu za motisha ili kuvutia uwekezaji na usaidizi wa uendeshaji wa malazi ya bei nafuu katika kila eneo lenye shughuli nyingi za utalii (protected area), kufikia Juni 2028.
	4.5 Kuanzisha mfumo wa kimtandao wa uhifadhi wa nafasi kwa watalii kufikia Juni 2028.
	i. Kuandaa na kutumia usanifu, viwango na mfumo jumuishi ya kidijitali, kwa ajili ya kurahisha matumizi ya mfumo wa kitaifa wa maombi ya uhifadhi wa nafasi za utalii, kufikia mwaka 2028.
	ii. Kuweka utaratibu rasmi wa kujenga uwezo na kutoa elimu kwa wafanyabiashara ya utalii, ili wapitishe na kutumia mfumo wa kuhifadhi nafasi mtandaoni kufikia mwaka 2028.
	4.6 Kuandaa fursa za kuvutia uwekezaji kwa wawekezaji wa kimataifa zinazolenga hoteli za kifahari, vivutio vya utalii na miundombinu ya utalii inayolenga masoko ya kimataifa, kufikia Juni 2028.
	i. Kupitia na kuimarisha sera za kutenga, kuandaa, na kugawa ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa kigeni katika miundombinu ya utalii wa daraja la juu, kufikia mwaka 2028.
	ii. Kuandaa na kuimarisha mfumo wa kurahisisha uwekezaji na vivutio ili kuvutia mitaji mikubwa ya kigeni, kufikia mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	iii. Kuendeleza na kuimarisha mifumo ya kukuza masoko na miundombinu, ili kuongeza imani ya wawekezaji wa kimataifa kufikia mwaka 2028.
	4.7 Kutoa motisha za kila mwaka kwa biashara za utalii ili kuchochea utekelezaji wa mbinu endelevu, ikiwa ni pamoja na upunguzaji wa taka, matumizi bora ya nishati, na uhifadhi wa mazingira, kufikia Juni 2028.
	Kuandaa na kutumia mfumo wa motisha za kifedha na utambuzi kwa ajili ya mbinu endelevu za utalii, kufikia mwaka 2028.
	Kuimarisha mifumo ya kujenga uwezo na mikakati ya masoko ya kimataifa ili kukuza maeneo mahiri ya utalii kufikia Juni 2028.
5. Angalau asilimia 40 ya biashara za utalii kuendeshwa kidijitali, kufikia Juni 2028.	5.1 Kuendeleza vituo vitano vya utalii wa kidijitali vilivyowezeshwa na teknolojia ya Intaneti ya Vitu, Akili Unde (na uchambuzi wa takwimu nyingi mchanganyiko (Big Data) ili kuboresha safari za wageni, kufikia mwaka 2028.
	i. Kuandaa na kutumia mifumo ya miundombinu ya utalii wa kisasa iliyounganisha teknolojia ya Intaneti ya Vitu (Akili Unde (AI), na uchambuzi wa Big Data, kufikia mwaka 2028.
	Kuimarisha mifumo ya kujenga uwezo na mikakati ya masoko ya kimataifa ili kukuza maeneo mahiri ya utalii kufikia Juni 2028.
	5.2 Kuzindua majukwaa ya mafunzo ya mtandaoni kwa wataalamu wa utalii ili kuimarisha ujuzi katika ukarimu, huduma kwa wateja, na uelewa wa kidijitali, kufikia Juni 2028.
	i. Kuandaa na kutumia usanifu, viwango, na mfumo wa maudhui kwa ajili ya majukwaa ya mafunzo ya utalii kwa njia ya mtandao, kufikia mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	ii. Kuanzisha mifumo ya mafunzo ya mtandaoni (online training platforms), ikijumuisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini (M&E), kufikia Juni 2028.
	5.3 Kuanzisha kituo cha taifa cha takwimu za utalii (National Tourism Data Hub) kwa ajili ya kukusanya, kuchambua, na kusambaza takwimu za wakati halisi (real-time) kuhusu mienendo ya watalii, mapendeleo yao, na mchango wa kiuchumi, kufikia Juni 2028.
	i. Kuandaa na kurasimisha usanifu, utawala, na mfumo wa uendeshaji wa kituo cha taifa cha takwimu za utalii, kufikia mwaka 2028.
	Kuanzisha mifumo ya kujengea uwezo na mifumo ya kusaidia mapokeo, ili kuhakikisha uendelevu katika kujifunza na ushiriki wa sekta nzima, kufikia mwaka 2028.
	iii. Kusanifisha na kurasimisha matumizi ya mfumo wa malipo uliounganishwa kwenye taasisi zote za Wizara ya Maliasili na Utalii, kufikia mwaka 2028.
	5.4 Kupevusha (kampuni changa za utalii zinazozingatia suluhisho bunifu za kidijitali, kama vile ziara za uhalisia , programu endelevu za usafiri na uzoefu wa kitamaduni, kufikia Juni 2028.
	i. Kuanzisha na kuimarisha vituo vya ubunifu na mifumo ya ugharamiaji kwa uanzishaji wa biashara changa za utalii kufikia mwaka 2028.
	ii. Kuweka utaratibu rasmi wa kujenga uwezo na kupata masoko ili kuunganisha wajasiriamali wachanga na masoko ya utalii ya ndani, kikanda, na kimataifa, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Kufikia kiwango cha matumizi ya mfumo jumuishi wa utalii wa kisasa nchini kwa asilimia 33, unaoendeshwa na majukwaa ya kidijitali, miundombinu na uboreshaji wa matumizi ya rasilimali kwa kutumia teknolojia za kidijitali kufikia Juni 2028.	6.1. Kuzindua uzoefu wa uhalisia pepe kwenye tovuti za kitamaduni na urithi, ili kuvutia watalii wanaopenda teknolojia za kisasa na kutoa uzoefu wa kipekee kwa watalii, kufikia Juni 2028.
	i. Kuandaa na kutumia teknolojia fungamani na viwango vya maudhui kwa uzoefu wa uonaji wa uhalisia (VR), kufikia mwaka 2028.
	ii. Kurasimisha ujengaji wa uwezo na mifumo ya masoko ya kimataifa, ili kupelekea uzoefu wa kipekee, kufikia Juni 2028.
	6.2 Kuanzisha mfumo thabiti wa ubunifu kwa ajili ya matumizi ya teknolojia bunifu katika sekta ya utalii kufikia Juni 2028.
	Kuendeleza miundombinu ya ubunifu pamoja na mifumo inayosaidia utawala, kufikia mwaka 2028.
	Kurasimisha programu za kujenga uwezo na mifumo ya sera inayosaidia matumizi ya teknolojia, kufikia Juni 2028.
	6.3 Kuimarisha nguvukazi watu kwa ujuzi unaohitajika kwa teknolojia za kisasa, kila mwaka.
	i. Kurasimisha programu za mafunzo endelevu na uboreshaji wa ujuzi katika mifumo ya kitaifa ya ujuzi wa utalii, kila mwaka.
	ii. Kuendeleza na kurasimisha ushirikiano na mifumo ya ithibati kupitia ushirikiano kati ya sekta, vyuo vya elimu na serikali kila mwaka.
	6.4 Kuutengeneza mazingira yanayotabirika na yanayofaa kwa utalii, ubunifu wa kiteknolojia na maendeleo ya rasilimali watu, kufikia Juni 2028.
	i. Kuimarisha mifumo ya sera, miundombinu, na ufadhili ili kusaidia ubunifu katika utalii, kufikia mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	ii. Kuweka utaratibu thabiti wa maendeleo ya rasilimali watu na njia za kubadilishana maarifa, kufikia Juni 2028.
7. Kuifanya Tanzania kuwa kituo kikuu cha utalii wa matukio utamaduni, na ikolojia kufikia Juni 2028.	7.1 Kuendeleza uzoefu wa kina wa utalii wa kitamaduni (mfano: Maeneo ya Urithi wa Dunia ya UNESCO, ziara za jamii za asili, sherehe za kitamaduni), unaovutia wasafiri wa kimataifa wanaopenda historia na utamaduni, kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha mifumo ya masoko ya kidijitali na mitandao ya kijamii, kufikia mwaka 2028.
	Kuweka mifumo ya kitaasisi ya ushiriki na ushirikiano wa kimkakati katika maonyesho ya kimataifa ya utalii, kufikia mwaka 2028.
	7.3 Kuandaa zana za ukusanyaji na uchakataji wa takwimu pamoja na kufuatialia utendaji wa sekta ya utalii, demografia ya watalii na masoko yanayoibukia ili kuoainisha huduma za utalii wa Tanzania na mahitaji ya kimataifa, kufikia Juni 2028.
	i. Kuanzisha na kurasimisha jukwaa la kituo shirikishi cha uangalizi wa takwimu za utalii, kufikia mwaka 2028.
	Kupitisha na kusanifisha uchambuzi wa kina wa takwimu na teknolojia zinazoibuka ndani ya kitovu cha takwimu, kufikia mwaka 2028.
	iii. Kurasimisha kukuza uwezo wa takwimu kwa wadau, utafiti wa masoko, na mifumo ya kupima ufanisi, kufikia mwaka 2028.
	7.4 Kuanzisha vituo vya mafunzo ya ufundi stadi kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kutoa programu maalum za mafunzo zinazoendana na viwango vya kimataifa vya utalii na mienendo inayoibuka, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuandaa mitaala na kurasimisha mifumo ya kukuza uwezo, kufikia mwaka 2028.
	Kuendeleza miundombinu ya kisasa na kuingiza viwango vya kiteknolojia katika vituo vya mafunzo, kufikia mwaka 2028.
	Kurasimisha uhusiano wa viwanda na mifumo ya ajira, kufikia Juni 2028.
	7.5 Kuhamasisha mikakati ya kukuza bidhaa za utalii za Tanzania, kuvutia watalii wa kimataifa wanaotumia kiasi kikubwa cha fedha, na kuingia katika masoko mapya ya kimataifa yanayokua kwa kasi katika sekta ya utalii duniani, kufikia Juni 2028.
	Kurasimisha mifumo ya kitaasisi ya ukuzaji, uendelezaji, na kusetusha bidhaa za utalii, kufikia mwaka 2028.
	ii. Kuimarisha miundombinu ya kiwango cha juu na upatikanaji wa masoko kupitia mifumo ya uwekezaji wa kimkakati, kufikia Juni 2028.
	Kuandaa na kurasimisha utambulisho wa chapa ya Tanzania duniani, kampeni za masoko, na mifumo ya ushirikiano wa kimkakati, kufikia Juni 2028.
	7.6 Kuendeleza ushirikiano na mashirika ya ndege ya kimataifa na waendeshaji wa safari za utalii ili kuanzisha njia mpya za usafiri, pamoja na kuitangaza Tanzania katika maonesho ya kimataifa ya utalii na majukwaa ya kidijitali, kila mwaka.
	Kuandaa na kurasimisha mifumo ya uunganishaji wa safari za anga na ufunguaji wa njia mpya za ndege, kufikia mwaka 2028.
	ii. Kuwa na ushirikiano rasmi na wa kimkakati na waendeshaji wa safari za utalii wa kimataifa, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	iii. Kuimarisha mifumo ya masoko ya kidijitali na ushiriki katika majukwaa ya kimataifa, kufikia Juni 2028.
	7.7 Kuendeleza miundombinu ya utalii, ikijumuisha malazi ya kisasa, vituo vya mikutano, mapumziko rafiki kwa mazingira, na mitandao ya usafiri (mfano: viwanja vya ndege, barabara na reli) ambayo inasaidia mnyororo wa thamani wa utalii, kila mwaka.
	Kutekeleza mifumo ya utalii wa hali ya juu na miundombinu ya mikutano (MICE), kufikia Juni 2028.
	Kurasimisha taratibu za uhifadhi wa mazingira na mifumo ya uendelezaji wa miundombinu ya usafirishaji wa kisasa kufikia Juni 2028.
	7.8 Kuanzisha Mamlaka ya Taifa ya Utalii na Ukarimu kufikia Juni 2028.
	i. Kutunga na kusimamia sheria ya muundo wa kitaasisi na utawala, kufikia mwaka 2028.
	ii. Kuanzisha, kurasimisha na kutumia sera, kanuni na mfumo wa viwango, kufikia Juni 2028.
8. Kuongezeka kwa idadi ya watalii wa kimataifa katika sehemu za kifahari kuongezeka kwa asilimia 8 kufikia Juni 2028.	8.1 Kurahisisha michakato ya viza na kuanzisha viza za baada ya kuwasili au viza ya kidijitali kwa masoko makuu, kufikia Juni 2028.
	i. Kuimarisha sera ya viza na mifumo ya kuwezesha michakato ya viza iliyorahisishwa, kufikia mwaka 2028.
	ii. kutayarisha na kurasimisha mifumo ya viza ya kidijititali (e-viza) salama na mifumo iliyounganishwa, kufikia mwaka 2028.
	8.2 kuanzisha mifumo ya malipo isiyohitaji pesa taslimu na majukwaa ya kidijitali, ili kuwapunguzia adha wasafiri, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	i. kuanzisha na kurasimisha mfumo wa malipo usio wa pesa taslimu, kufikia mwaka 2028.
	ii. kuanzisha na kusanifisha jukwaa la kitaifa la kitalii lililofungamanishwa kidijitali, kufikia mwaka 2028.
	iii. Kuimarisha mifumo ya usalama wa mtandao ili kulinda malipo na taarifa binafsi, kufikia Juni 2028.
	8.3 Kuanzisha programu za mafunzo kwa wataalamu wa utalii ili kuboresha ubora wa huduma za ukarimu uongozaji watalii na huduma kwa wateja wa kiwango cha juu, kufikia Juni 2028.
	i. Kuandaa mitaala inayolingana na viwango vya kimataifa, kufikia mwaka 2028.
	ii. Kuanzisha mifumo ya kisasa ya utoaji mafunzo na kujenga uwezo, kufikia 2028.
	iii. Kuanzisha miongozo ya ushirikiano kati ya sekta ya utalii na uendelezaji kitaaluma, kufikia mwaka 2028.
	8.4 Kujenga hoteli, sehemu za mapumziko na kutoa huduma za utalii zenye hadhi ya juu katika maeneo tengefu, kufikia Juni 2028.
	i. Kuandaa viwango vya miundombinu na vituo vya huduma za utalii, kufikia mwaka 2028.
	ii. Kuandaa miongozo ya kuboresha na kusimamia uzoefu wa wageni, kufikia mwaka 2028.
	8.5 Kukuza utalii endelevu ili kuvutia watalii wa kipato cha juu na wanaojali mazingira, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuandaa na kuanzisha viwango vya kijani (pamoja na mifumo ya ithibati, kufikia mwaka 2028.
	Kurasimisha mifumo ya kukuza miundombinu na uendeshaji endelevu, kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha miongozo ya ushirikishwaji wa jamii, kila mwaka
	iv. Kuanzisha miongozo ya kimataifa ya masoko na uhamasishaji wa utalii endelevu, kila mwaka.
3.3.7 Sekta ya Fedha	
Lengo 1: Kuimarisha utawala bora, ufanisi wa uendeshaji na uthabiti wa kifedha ili kuhakikisha ushindani na uimara wa sekta ya benki za biashara	
Kuongeza kiwango cha uwiano wa utoshelevu wa mtaji (CAR) kufikia zaidi ya asilimia 16.5, kufikia Juni 2028.	1.1 Kuimarisha udhibiti na usimamizi wa vihatarishi kwenye mahitaji ya mitaji, kufikia Juni 2028.
	1.2 Kuwezesha kuunganishwa na kununuliwa kwa benki dhaifu ili kuimarisha mitaji, kufikia Juni 2028.
	1.3 Kuanzisha na kuendesha uwekezaji wa muda mrefu wa sekta ya umma na sekta binafsi katika benki za biashara, kufikia Juni 2028.
Kuongeza uwiano wa amana kwa Pato la Taifa kufikia angalau asilimia 40, kufikia Juni 2028.	2.1 Kuimarisha mfumo wa fedha wa kidijitali unaoongozwa na matumizi ya takwimu, kufikia mwaka 2028.
	2.2 Kuanzisha mifumo ya kitaifa ya kuweka akiba inayotumia motisha zinazohusishwa na amana, kufikia mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	2.3 Kupanua kiwango cha ujumuishaji wa huduma za kifedha kupitia mawakala wa benki na upanuzi wa huduma za kidijitali nchi nzima, kufikia Juni 2028.
Kudhibiti mikopo chechefu kubaki chini ya asilimia 5, kufikia Juni 2028.	Kuanzisha mfumo wa kidijitali wa usimamizi wa vihatarishi vya mikopo unaotumia akili unde na uchambuzi wa takwimu kufikia Juni 2028.
	3.2 Kuweka sharti la matumizi ya mifumo madhubuti ya urejeshaji na ufuatiliaji makini wa mikopo, kufikia mwaka 2028.
	3.3 Kujumuisha sera za ukopeshaji zinazozingatia mazingira, jamii na utawala bora katika kanuni za kibenki, kufikia mwaka 2028.
4. Kupanua kiwango cha mikopo kwa sekta binafsi kufikia asilimia 25 ya Pato la Taifa, kufikia mwaka 2028.	4.1 Kuimarisha sera za ugawaji mitaji kulingana na vihatarishi kwa ajili ya kuhamasisha mikopo kwenye sekta zenye tija kubwa, kufikia mwaka 2028.
	4.2 Kuimarisha mifumo ya dhamana ya serikali kwenye mikopo ili kupunguza vihatarishi vya utoaji mikopo kwa biashara ndogondogo ndogo na za kati na sekta za kimkakati, kufikia Juni 2028.
	4.3 Kuanzisha jukwaa la kidijitali la kupima uwezo wa mkopaji kwa kutumia teknolojia ya fedha (fintech) na takwimu, kufikia Juni 2028.
5. Kuongezeka kwa kiasi cha watu wazima wanaopata na kutumia huduma rasmi za kifedha kufikia asilimia 90, ifikapo Juni 2028.	5.1 Kuanzisha programu za elimu ya fedha za kidijitali kufikia mwaka 2028.
	5.2 Kutoa motisha kwa benki za biashara kuanzisha akaunti na pochi za kidijitali zenye gharama nafuu kwa wananchi wa vijijini na makundi yaliyotengwa, kufikia Juni 2028.
	5.3 Kuunganisha majukwaa ya pesa za simu na benki ili kutoa huduma jumuishi, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Lengo 2: Kuimarisha mtaji wa Taasisi za Kifedha za Maendeleo (DFIs), na kuwezesha uwekezaji wa sekta binafsi, mifuko ya hifadhi ya jamii na makampuni ya bima ili kuwa na ukuaji na uendelevu, kufikia mwaka 2030	
Kuongeza mtaji wa DFIs kufikia angalau asilimia 1.25 ya Pato la Taifa, kufikia Juni 2028.	1.1 Kuanzisha mpango wa hatua kwa hatua wa serikali kuongeza mtaji wa uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni, kufikia mwaka 2028.
	1.2 Kusetusha vyanzo vya fedha kupitia hati fungani za ndani na ushirikiano na mifuko ya pensheni, na taasisi nyingine za uwekezaji.
	1.3 Kutumia mbinu za ugharamiaji mseto na kupata fedha, kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya na washirika wengine wa kimataifa, ifikapo Juni 2028.
2. Kufikia uwiano wa chini wa mtaji wa umma na binafsi wa 1:1.14 katika Uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni DFIs, kufikia Juni 2028.	2.1 Kuimarisha mifumo ya udhibiti ili kuruhusu ushiriki wa usawa wa ndani na nje ya nchi kwa wawekezaji binafsi wa ndani na nje, ikijumuisha ubinafsishaji kwa sehemu, kufikia Juni 2028.
	2.2 Kuwezesha ushiriki wa IFC, Benki ya Maendeleo ya Afrika , Benki ya Uwekezaji ya Ulaya , na taasisi kama hizo, ili kuchochea mitaji binafsi, kufikia Juni 2028.
	2.3 Kuongeza uwekezaji wa sekta ya kibinafsi, ikijumuisha makampuni, biashara za ndogondogo na za kati na wawekezaji wa taasisi, kufikia Juni 2028.
Lengo 3: Kuboresha mwongozo wa maendeleo ya Taasisi za Fedha za Maendeleo kwa kuimarisha usimamizi wa vihatarishi na kuboresha michakato ya tathmini ya mikopo na kuhakikisha ufanisi katika ufuatiliaji na urejeshaji wake	
1. Kudhibiti mikopo chechefu ya uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni kuwa chini ya asilimia 5, kufikia Juni 2028..	1.1 Kuimarisha udhibiti na mifumo ya usimamizi wa vihatarishi, kupitia nyenzo za teknolojia ya Akili unde, viwango vya usimamizi wa sekta binafsi, kusetusa mikopo, na zana zinazoendana na hisa, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	1.2 Kuongeza ugharamiaji wa miundombinu, uzalishaji viwandani, na kilimo, kila mwaka.
	1.3 Kupanua wigo wa ufadhili kwa biashara ndogondogo na za kati (SMEs) na kampuni chipukizi kwa kutumia mitaji ya hisa, uhitaji wa ubia and mikopo ya kidijitali, mara mbili kwa mwaka.
	1.4 Kuanzisha dirisha la ufadhili kwa teknolojia ya masuala ya fedha na makampuni yanayoendeshwa kiteknolojia, mara mbili kwa mwaka.
	1.5 Kutumia mfumo wa block chain kufadhili mnyororo wa thamani wa kilimo na ufadhili endelevu wa modeli za kijani, kila mwaka.
Lengo 4: Sekta ndogo ya bima iliyoimarishwa inayoongozwa na sekta binafsi ambayo huchochea ukuaji endelevu wa uchumi kwa kuongeza uwepo wa bima, kuimarisha uthabiti wa soko na kutoa na kusetusha bidhaa zinazoingizwa sokoni	
1. Kuongeza matumizi ya bima (jumla ya malipo kwa Pato la Taifa) hadi asilimia 2.6, kufikia Juni 2028.	1.1 Kuimarishwa kwa mifumo ya udhibiti, kukuza bima ndogo, na kuendesha programu za uhamasishaji nchi nzima kufikia Juni 2028.
	1.2 Kukuza ubunifu kupitia bima ya kidijitali, kilimo mahsusi na bidhaa za afya, na kuboresha ujuzi kufikia Juni 2028.
	1.3 Kuongeza ushiriki wa soko la bima ya kikanda na kimataifa kupitia viwango vya kimataifa vya uandishi, uhakikisho wa bima na madai, kufikia Juni 2028.
Lengo 5: Kuhamasisha usetushaji wa mitaji na kuongeza uzingatiaji wa kanuni, ikiambatana na viwango vya Nchi zenye Mapato ya Kati ya Juu (UMIC) ili kuchochea ukuaji wa uchumi na uhimilivu	

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
2. Kufikia asilimia 33 ya ufadhili wa mtaji mseto na ujumuishaji kamili wa huduma ndogo za kifedha vijijini, kufikia Juni 2028.	2.1 Kuimarisha mifumo ya usetushaji na kuanzisha biashara ndogondogo na za kati na mbinu za kifedha zinazofaa vijijini, ikijumuisha dhamana ya mikopo midogo midogo na miamala ya kidijitali ifikapo kufikia 2028.
	2.2 Kuwezesha uhimilivu na ujumuishwaji wa sekta ndogo ya fedha na ushirikishwaji wa sekta ya mikopo midogo midogo kupitia uwekaji rekodi za biashara zisizo rasmi kidijitali, kandarasi mahiri, na ufadhili unaozingatia mazingira, jamii na utawala ESG, ifikapo Juni 2028.
3. Asilimia 25 ya huduma za kifedha kupatikana kupitia mfumo wa kidijitali, kufikia Juni 2028.	3.1 Kutekeleza huduma za benki ndogo za kidijitali na huduma za simu/kidijitali katika maeneo ya vijijini ambayo hayana huduma ya kutosha, kufikia Juni 2028.
	3.2 Kuandaa majukwaa ya ukopeshaji yanayoendeshwa na akili unde pamoja na sera zinazosaidia teknolojia ya kifedha (fintech), ifikapo June 2028.
	3.3 Kuunganisha mifumo ya kidijitali ya mikopo midogo midogo na suluhu za fedha zisizodhibitiwa na mamlaka kuu (DeFi)
4. Kubadilika kuelekea mfumo unaoendeshwa kikamilifu na sekta ya mikopo midogo midogo kwa Biashara Ndogo na za Kati (SME), ukiwa na ujumuishi wa maeneo ya vijijini kwa asilimia 20–25, kufikia Juni 2028.	4.1 Kuimarisha mifumo ya udhibiti ili kuongeza ujumuishaji wa kifedha wa kwa biashara ndogo na za kati na vijijini, na kukuza uwekezaji wa vijijini, i kufikia, Juni 2028.
	4.2 Kuendesha programu za kitaifa za elimu ya kifedha kwa taasisi za fedha za kati MFIs na na biashara ndogo na za kati SMEs, ifikapo June 2028.
Lengo 6: Kuongeza mikopo na kuboresha udhibiti wa kanuni ili kuhakikisha unaendana na viwango vya UMIC ili kuchochea maendeleo endelevu na ustahimilivu wa kifedha	

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
1. Kupunguza kutengwa kwenye huduma za kifedha hadi chini ya asilimia 10, ifikapo Juni 2028.	1.1 Kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha kwa makundi yaliyokosa fursa, ikiwa ni pamoja na maeneo ya vijijini, kupitia ushirikiano kati ya mabenki, taasisi za mikopo midogo midogo (MFIs), na kampuni za teknolojia ya kifedha (fintechs) kufikia Juni 2028.
	Kuwezesha ujuzi wa masuala ya kifedha nchini kote ili kuongeza ufahamu wa manufaa ya akaunti, kufikia Juni 2028.
	1.3 Kusasisha huduma za sekta ya kifedha chini ya NFIF, ikijumuisha majukwaa kimtandao na kidijitali kupitia mabenki, kufikia Juni 2028.
2. Kuinua ukopaji rasmi, kufikia asilimia 31.2, kufikia Juni 2028.	2.1 Kufanya mageuzi ya mifumo ya mikopo, ili kuwezesha biashara ndogo na za kati, makampuni ya biashara ya vijijini, na sekta isiyo rasmi, kufikia Juni 2028.
	2.2 Kubadilisha utoaji wa mikopo kupitia mifumo ya kidijitali inayoendeshwa na akili unde na teknolojia ya kifedha (Fintech), kufikia Juni 2028.
3. Kuongeza umiliki wa akaunti za benki hadi asilimia 33 na ushiriki wa kuweka akiba hadi asilimia 35 kufikia Juni 2028.	Kupanua miundombinu ya huduma za kifedha kidijitali ikiunganishwa na ubunifu wa kampuni za teknolojia ya kifedha Fintech kutaifanya Tanzania kuibuka kinara wa kikanda wa Fintech, kufikia Juni 2028.
	3.2 Kutekeleza programu ya kitaifa ya ujuzi na utaalamu wa masuala ya fedha ili kuongeza imani na ushiriki wa watumiaji, ifikapo Juni 2028.
Lengo 7: Kuboresha mazingira ya biashara kwa ajili ya ukuaji wa mtaji wa biashara Tanzania na mfumowa uwekezaji binafsi kwa kuongeza upatikanaji wa fedha kwa kampuni chipukizi na Makampuni makubwa	
1. Kuongezeka kwa uwekezaji wa mtaji wa ubia (na uwekezaji binafsi wa hatua za awali kutoka dola za Marekani milioni 52 hadi zaidi ya dola za Marekani milioni	1.1 Kuanzisha Mtandao wa Kitaifa wa wawekezaji wa binafsi wa wa hatua za awali na kurekebisha kanuni za uwekezaji binafsi na uwekezaji wa mtaji kufikia mwaka 2028

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
242 kwa mwaka, kufikia Juni 2028.	1.2 Kuanzisha mfuko wa kitaifa kwa ajili ya kampuni chipukizi ili kuwezesha mitaji ya awali, ruzuku ya utafiti na maendeleo kutoka serikalini, na kuimarisha Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) kwa IPOs na M&A kufikia Juni 2028.
	1.3 Kwa kutumia ushirikiano wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika , kutavutia uwekezaji wa kikanda, kufikia Juni 2028.
Lengo 8: Kuongezeka kwa mitaji ya ubia na mikataba ya wawekezaji binafsi itakayowezesha ustawi wa mfumo wa kampuni chipukizi na ukuaji wa biashara unaoongozwa na ubunifu	
1. Kuongeza mikataba ya mitaji ya ubia na wawekezaji binafsi kutoka 10 hadi 30 kwa mwaka kufikia Juni 2028.	1.1 Kuanzishwa kwa Programu ya Kitaifa ya Usaidizi wa Hakimiliki (National IP Support Programme) ili kulinda bunifu za kampuni chipukizi kufikia mwaka 2028.
	1.2 Kuendeleza Hifadhi za Teknolojia (na Vituo vya Ubunifu ili kuchochea mabadiliko ya kidijitali na ujasiriamali, kufikia mwaka 2028.
Lengo 9: Kukuza ujasiriamali jumuishi na endelevu, utakaowezesha ushiriki katika ukuaji wa kiuchumi na kuleta athari chanya katika mazingira	
1. Kuboresha nafasi ya Tanzania katika Fahirisi ya Ubunifu Duniani kufikia nafasi ya 90, kufikia Juni 2028.	1.1 Kuanzisha kongani za kiteknolojia na vituo vya ubunifu na mfuko wa uwekezaji wa kibiashara uliokusudiwa wa kutumia akili unde teknolojia ya kibiologia na teknolojia za kimazingira, kufikia mwaka 2028.
	1.2 Kuanzisha masoko ya hisa ya upili ya kikanda, kurahisisha IPO tano (5) za kuanzisha biashara chipukizi na kuwezesha mifuko ya pensheni kuwekeza kwenye kampuni changa kufikia mwaka 2028.
	1.3 Kutekeleza mpango wa "kuhakikisha maendeleo ya baadaye" ili kuiwezesha Tanzania kupiga hatua kubwa za kimaendeleo, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
3.3.8. Sekta ya Michezo na Ubunifu	
Lengo 1: Kuimarishwa kwa ushindani wa ndani, kikanda na kimataifa wa tasnia ya michezo na ubunifu,kukuza ukuaji, na fursa za uwekezaji	
1. Ukuaji halisi wa sekta kutopungua asilimia 20 kwa mwaka, kufikia Juni 2028.	1.1 Kujenga na kuboresha miundombinu ya michezo (viwanja, vituo vya mafunzo na kumbi za michezo) kote nchini, kwa kuanzisha angalau vituo 5 vya ubora wa kimataifa, kufikia Juni 2028.
	i. Kuanzisha taasisi za kukuza vipaji za kikanda, na kudahili vijana 100,000 katika programu za michezo, kufikia Juni 2028.
	ii. Kuzindua programu za kila mwaka za ufadhili wa masomo ili kusaidia vijana wenye vipaji wasiopungua 100 kwenda shule za michezo na sekta za ubunifu ng'ambo, kufikia mwaka 2028.
	iii. Kuanzisha sera na vifurushi vya motisha kurahisisha upatikanaji wa ardhi ili kuvutia uwekezaji binafsi katika miundombinu ya michezo na sekta za ubunifu (sanaa/filamu), kufikia mwaka 2028.
	iv. Kujenga mfumo endelevu wa biashara ya michezo unaokuza utalii wa michezo katika ngazi zote, kufikia Juni 2028.
2. Kuvutia watalii zaidi 100,000 wa michezo kila mwaka kufikia Juni 2028.	2.1 Kuanzisha mfumo/utaratibu wa biashara ya michezo ili kukuza utalii wa michezo, kufikia Juni 2028.
	i. Kuanzisha mfumo/utaratibu wa biashara ya michezo ili kukuza utalii wa michezo, kufikia mwaka 2028.
3. Wasanii wa Tanzania kutambulika kimataifa katika angalau nyanja moja kuu ya ubunifu, kufikia Juni 2028.	3.1 Kujenga mfumo endelevu wa utengenezaji wa filamu, usambazaji na kurekodi muziki, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	i. Kuanzisha majukwaa ya kanda (zonal platforms) ili wasanii wa Tanzania waweze kuonyesha kazi zao kitaifa na kimataifa, kufikia mwaka 2028.
4. Angalau asilimia 10 ya maudhui iweze kupatikana duniani kote, kupitia majukwaa ya kidijitali, kufikia Juni 2028.	Kwa kutumia fursa ya ushirikiano na majukwaa ya kidijitali ya kimataifa, kupanua wigo wa wabunifu wa Tanzania, kufikia Juni 2028.
	Kuandaa mikakati ya kuongeza mauzo nje ya sanaa, muziki, filamu, na mitindo ya Tanzania, ikilenga masoko ya kimataifa, kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha vituo vya kulelea na vichapuzi vya ubunifu kwa wajasiriamali wabunifu, kwa kutoa ufadhili, ushauri na fursa za mitandao, kufikia Juni 2028.
5. Mashirika yote ya wabunifu na michezo ya Tanzania yawezeshe wasanii kupokea mirabaha kwa kazi zao kila mwaka, kufikia Juni 2028.	5.1 Kuimarisha mifumo ya Hakimiliki na Hatimiliki kufikia mwaka 2028.
	i. Anzisha mfumo bora wa usajili wa hakimiliki na IP ili kulinda wasanii wa ndani dhidi ya matumizi yasiyoidhinishwa na uharamia, kufikia mwaka 2028
	ii. Kuanzisha mfumo madhubuti wa kuwasaidia wabunifu na mashirika ya michezo Tanzania kuwa na uwezo wa kusajili na kulinda haki zao za miliki (IP), kufikia Juni 2028.
	iii. Kuanzisha huduma maalum za kisheria na kifedha kwa usimamizi wa Haki miliki (IP), ikijumuisha motisha za kifedha (kama kupunguza kodi) na zisizo za kifedha ili kulinda haki miliki IP na kibiashara, kufikia Juni 2028.
	iv. Kuhakikisha ulinzi wa hakimiliki kwa wabunifu wa kidijitali na watengeneza maudhui kwenye majukwa ya kieletroniki, kufikia Juni 2028.
	v. Kuhakikisha sheria za hakimiliki (IP) na kanuni za hakimiliki katika michezo zinatekelezwa kikamilifu, zikijumuisha haki za matangazo uuzaji wa bidhaa na maudhui ya kidijitali, kufikia Juni 2028.
3.3.9 Maendeleo ya Makazi na Biashara ya Ardhi na Majengo	

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Lengo 1: Kuboresha mazingira ya ushindani, uwazi na rafiki, kwa wawekezaji wa ndani na nje katika sekta ndogo ya majengo na ardhi (real Estate), ili kuchochea ukuaji wake na kuongeza mchango wake katika uchumi	
1. Kuongezeka kwa mchango wa sekta ya majengo katika pato la taifa kutoka asilimia 4 hadi 5 kufikia Juni 2028.	1.1 Kuimarisha mifumo ya udhibiti inayohusiana na maendeleo ya ardhi na miji, ili kuchochea maendeleo ya soko la majengo na ardhi, ifikapo mwaka 2028.
	1.2 Kuanzisha mfumo wa motisha kwa waendelezaji wa majengo na ardhi wanaowekeza katika miradi mikubwa, kufikia Juni 2028.
2. Kuendeleza jumla ya nyumba milioni 2 ili kukidhi ongezeko la idadi ya watu mijini, kufikia Juni 2028.	2.1 Kuanzisha na kuhamasisha ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kuongeza ugavi wa nyumba nafuu chini ya Mpango wa Nyumba Nafuu Tanzania (TAHP), kufikia Juni 2028.
	i. Kuanzisha mfumo wa motisha kwa nyumba zinazojengwa za utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, kufikia mwaka 2028.
	ii. Kuanzisha vituo mseto vya mijini vinavyounganisha makazi, biashara, na burudani, kufikia Juni 2028.
	2.2 Kuendeleza teknolojia za ujenzi endelevu na za gharama nafuu, ili kuharakisha ujenzi na kupunguza gharama, kufikia Juni 2028.
	i. Kuwezesha uhawilishaji wa wa teknolojia na uendelezaji wa ujuzi, kufikia Juni 2028.
	ii. Kutoa motisha kwa wazalishaji wa ndani wa vifaa vya ujenzi, kufikia Juni 2028.
3. Kuongeza Uwiano wa dhamana kwa Pato la Taifa kutoka asilimia 0.5 hadi 2, kufikia Juni 2028.	3.1 Kuanzisha na kuendesha dirisha/taasisi za fedha za nyumba kama TMRC/TIB zenye angalau Shilingi bilioni 100 za kitanzania, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	3.2 Kufanya marekebisho ya udhibiti ili kupunguza viwango vya riba ya mikopo ya nyumba kutoka wastani wa asilimia 15 hadi asilimia 12, kufikia Juni 2028.
	3.3 Kuanzisha na kuwezesha upatikanaji wa ardhi zenye huduma kwa waendelezaji binafsi na umma maeneo ya miji na pembezoni mwa miji, kufikia Juni 2028.
	3.4 Kuanzisha na kuhuisha benki za ardhi (land banks) kwa ajili ya kuendeleza miradi ya majengo na ardhi (real estate), kufikia mwaka 2028.
	3.5 Kuendeleza miundombinu na huduma za kijamii kwa ardhi iliyopimwa kwa ajili ya miradi, kufikia mwaka 2028.
4. Uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZs), Miji ya Kisasa Kongani za biashara za kimataifa na vitovu vya usafirishaji, kufikia jumla ya dola za Marekani bilioni 3, kufikia Juni 2028.	4.1 Kuanzisha miji ya kisasa mitatu (3) yenye mpango wa kujiendesha kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya usimamizi wa miji kwa ufanisi, kufikia Juni 2028.
	Kusanifu miji ya kisasa ifikapo mwaka 2028.
	Miundombinu ya kiteknolojia inayohitajika kwa ajili ya miji ya kisasa kukamilishwa, kufikia Juni 2028.
5. Kuongezeka kwa thamani ya jumla ya mali zinazosimamiwa na REIT na TAHF kufikia dola za Marekani bilioni 1.5, kufikia Juni 2028.	5.1 Kuongeza wigo wa Masoko ya mitaji kwa kuorodheshwa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja katika Majengo (REITs) na Mpango wa Nyumba Nafuu Tanzania (TAHP) kwenye soko la hisa la Dar es salaam kufikia Juni 2028.
	5.2 Kufadhiliwa kwa nyumba za gharama nafuu kupitia mipango mahsusi na mipango bora ya usimamizi kupitia REITs na TAHP, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	5.3 Kuanzishwa kwa maendeleo yanayozingatia Usafiri wa Umma kwa kujumuisha upangaji wa matumizi mchanganyiko ya ardhi na mifumo bora ya usafiri wa umma, kufikia Juni 2028.
	5.4 Kuandaa mpango wa usimamizi wa ToD, zana, na mbinu za ufadhili, kufikia mwaka 2028.
	5.5 Kuanzisha miundombinu ya kidijitali ili kuwezesha ulinzi kwa rehani za kielektroniki uhamishaji wa mali kidijitali, na mifumo ya mipango miji inayoongozwa na teknolojia ya akili unde, ifikapo Juni 2028.
6. Jumla ya asilima 50ya miamala ya majengo na ardhi kufanyika kidijitali, kufikia mwaka 2028.	6.1 Kuanzisha mfumo rafiki wa usajili wa mali kwa watu wasio raia, kupitia mageuzi ya sheria za udhibiti, kufikia Juni 2028.
	6.2 Kutekeleza mikakati ya usimamizi wa majengo na ardhi inayostahimili mabadiliko ya tabianchi, ikijumuisha kanuni za ujenzi na viwango, ili kuimarisha uendelevu katika ujenzi, kila mwaka.
	i. Kuanzisha viwango vya usanifu na vifaa vya ujenzi vinavyostahimili mabadiliko ya tabianchi , kufikia Juni 2028.
	Kupitishwa kwa kanuni za ujenzi unaostahimili mabadiliko ya tabianchi, kufikia Juni 2028.
Lengo 2: Uboreshaji wa nyumba na makazi ya watu unaolenga kuinua hali ya maisha na kuleta maendeleo shirikishi ya mijini	
1. Kuongezeka kwa idadi ya watu wanaoishi katika makazi yaliyopangwa kutoka asilimia 30 hadi 50, kufikia	1.1 Kutekeleza mageuzi ya msingi ya kisheria na mageuzi ya kisera za haki za ardhi, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Juni 2028.	i. Kutekeleza mageuzi ya kina ya kisheria, ili kuhakikisha haki za ardhi zilizo wazi, za uwazi, na zinazotekelezeka kwa raia wote, ikiwa ni pamoja na wanawake, vijana, na makundi ya wanyonge, kufikia mwaka 2028.
	ii. Kuoanisha mifumo ya kisheria, kimila, na kidini, ya umiliki wa ardhi, ili kuhakikisha ulinzi na utambuzi sawa wa haki za ardhi kufikia Juni 2028.
	iii. Kuimarisha utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa haki na ufanisi, kila mwaka.
	1.2. Kusasisha mifumo ya usimamizi wa ardhi na michakato yake, kufikia Juni 2028.
	Kuzindua Mfumo Jumuishi wa Taarifa za Ardhi wa Taifa, ambao unajumuisha taarifa za ramani, na mipango miji kufikia Juni 2028.
	Kurahisisha na kuhamishia madaraka ya utoaji hati za ardhi ngazi za chini ili kupunguza muda, gharama na urasimu, na hivyo kufanya urasimishaji wa ardhi kupatikana kwa urahisi, kufikia Juni 2028.
	Kutumia sekta binafsi katika upimaji, usimamizi wa takwimu na matumizi ya teknolojia katika kuchapusha utoaji wa huduma, kila mwaka.
3.3.11. Mabadiliko katika Sekta ya Biashara	
Lengo 1: Kuimarishwa kwa sekta ya biashara yenye ushindani wa kimataifa, iliyosetushwa, inayotumia teknolojia ya kidijitali, inayowezesha mauzo nje, kukuza ukuaji jumuishi kwa viwanda vidogo na vya kati na kuimarisha ushirikiano na masoko muhimu ya kikanda na kimataifa	
1. Kuongezeka kwa bidhaa zilizoongezwa thamani katika mauzo ya nje kwa asilimia 10, kufikia Juni 2028.	1.1 Kuanzisha vituo vya usindikaji wa mazao (agro-processing hubs) katika kanda maalum za mauzo ya nje, kupanua mifumo ya umwagiliaji, na kusambaza pembejeo bora kwa wakulima kufikia mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	1.2 Kuanzisha vivutio maalum vya kifedha na visivyo vya kifedha na kuboresha upatikanaji wa mikopo ya riba nafuu kwa biashara ndogondogo na za kati zinazoongeza thamani ya mazao kufikia Juni 2028.
	1.3 Kuendesha mafunzo ya kitaifa ya utunzaji wa mazao baada ya kuvuna, na usaidizi kwa vyama vya ushirika katika uwekaji chapa na vifungashio, kufikia Juni 2028.
	1.4 Kuzindua mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji wa kidijitali, majaribio ya blockchain kwa mauzo ya nje ya thamani ya juu, na kuongeza majukwaa ya ithibati ya blockchain/IoT kwa ufikiaji mpana wa soko, kufikia Juni 2028
2. Kupunguzwa kwa Kielezo cha Ujumuishaji wa Mauzo ya Nje kwa asilimia 10, kufikia Juni 2028.	2.1 Kuzindua jukwaa la usetushaji wa biashara linaloendeshwa na akili unde na kufanya utafiti wa masoko ya mazao yanayouzwa nje, ili kubainisha fursa mpya, kufikia mwaka 2028.
	2.2 Kurasimisha misheni za biashara nje ya nchi kufanyika ana kwa ana na kwa mtandao, ili kuwezesha majadiliano ya kibiashara kati ya nchi na nchi (bilateral trade), na kutoa motisha kwa bidhaa kupata ithibati na hivyo kurekebishwa kulingana na soko, kufikia Juni 2028.
3. Kuboreshwa kwa kielezo cha ugumu wa Mauzo ya Nje kufikia 0.04, ifikapo Juni 2028.	3.1 Kuunganisha akili unde na teknolojia ya roboti katika uzalishaji viwandani na kuanzisha kongani maalum za viwanda kwa ajili nya bioteknolojia, nanoteknolojia na sekta zingine za teknolojia ya juu, kufikia Juni 2028.
	3.2 Kuzindua vituo vya utafiti na maendeleo vya kimtandao, ili kuhamasisha mikataba ya uhawilishaji wa teknolojia na washirika wa kimataifa, na kuwezesha uhusiano na wauzaji bidhaa kwa viwanda vya hali ya juu, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	3.3 Kuongeza wigo wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi ili kujielekeza kwenye uzalishaji wa kisasa viwandani na teknolojia ya roboti, kufikia Juni 2028.
	4.1 Kutekeleza mfumo wa forodha unaotegemea teknolojia ya blockchain na kuanzisha malango ya biashara ya kidijitali inayovuka mipaka, ili kupunguza misuguano, kufikia mwaka 2028.
	4.2 Kuoanisha viwango vya kitaifa vya biashara na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda na kuandaa sera mahsusi za kurahisisha biashara mipakani, kufikia Juni 2028.
	4.3 Kuboresha mitandao ya usafiri na usafirishaji kwenda maeneo ya mipakani na kuanzisha kanda za masoko ya mipakani, ili kuchochea biashara ya ndani, kufikia Juni 2028.
5. Kuimarishwa kwa Kielezo cha Utendaji wa usafirishaji (LPI) kwa asilimia 10 ili kufikia nafasi ya 50 bora duniani kufikia Juni 2028.	5.1 Kusasisha miundombinu ya bandari na kuimarisha barabara pamoja na reli muhimu zinazounganisha bandari hizo na bohari za ndani kufikia mwaka 2028.
	5.2 Kutekeleza mifumo ya usimamizi wa bandari inayoendeshwa na akili unde na mifumo ya kidijitali, kujenga maghala ya kisasa na kutumia mifumo ya satelite kufuatilia shehena za mizigo, kufikia Juni 2028.
	5.3 Kuunganisha na kurahisisha michakato yote ya forodha katika maeneo makuu ya biashara ya kuingia na kutoka, kufikia Juni 2028.
	5.4 Kuanzisha vituo maalum vya mafunzo ya ugavi na usafirishaji, ili kujenga kikosi cha wafanyakazi wenye ujuzi katika mnyororo wa ugavi, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Kuongezeka kwa biashara ya kidijitali kuongezeka na kufikia asilimia 50 ya biashara yote, kufikia Juni 2028.	6.1 Kuanzisha na kuzindua majukwaa ya biashara ya kielektroniki yanayoendeshwa na akili unde kwa soko la Afrika na kuanzisha mfumo wa malipo ya kidijitali wa blockchain kufikia Juni 2028.
	6.2 Kutekeleza suluhu za usafirishaji za IoT (kwa uwasilishaji wa maili ya mwisho na uanzishwaji wa vituo vya kikanda vya biashara mtandao , ili kuboresha ufanisi, kufikia Juni 2028.
	6.3 Kuoanisha kanuni za kitaifa za biashara-mtandao kufikia Juni 2028.
3.3.12 Sekta Imara ya Biashara	
Lengo 1: Kuongezeka kwa uwekezaji wa sekta binafsi kunakoibua ubunifu, ushindani, na ushirikishwaji; kukidhi mahitaji ya ndani; na kuunganisha Tanzania katika minyororo ya thamani ya kimataifa ili kusaidia ukuaji wa uchumi endelevu	
1. Kuongezeka kwa uwekezaji binafsi hadi kufikia angalau asilimia 5 ya pato la taifa, kufikia mwaka 2028.	1.1 Kuweka mfumo thabiti wa utoaji wa motisha na usaidizi unaolengwa kwa wawekezaji wa kimkakati, uanzishaji wa teknolojia ya juu na biashara za kidijitali ili kukuza ubunifu, ujasiriamali na miundo ya biashara inayotegemea teknolojia, kufikia Juni 2028.
	Uhakiki wa kina wa kanuni za biashara ili kuboresha urahisi wa kufanya biashara kufikia mwaka 2028.
	ii. Kupitia mifumo ya udhibiti ya Mashirika ya Umma ili kuhakikisha uwazi na uwekezaji wenye faida, kufikia mwaka 2028.
	iii. Kuanzisha mwongozo mahsusi unaozingatia vigezo vya kutoa motisha iliyopangwa kwa uwekezaji wa kimkakati na makampuni chipukizi ya teknolojia ya juu, kufikia mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	iv. Kurahisisha michakato yote ya uwekezaji na kuimarisha uwezo wa mashirika ya kukuza uwekezaji kutatua migogoro, kufikia mwaka 2028.
	Kuwezesha ukuaji wa viwanda unaotegemea kongani na uwekezaji katika maeneo maalum ya kiuchumi, kufikia mwaka 2028.
	Kuongeza wigo wa huduma za kifedha na kuboresha miundombinu inayosaidia ukuaji wa biashara, kufikia Juni 2028.
2. Kuongezeka kwa ushiriki katika mnyororo wa thamani wa kidunia hadi angalau asilimia 25 ya pato la taifa, kufikia mwaka 2028.	2.1 Kutekeleza mabadiliko ya kimkakati ya kubadilisha uzalishaji wa ndani kuwa viwanda Shindani, vinavyolenga mauzo ya nje, kufikia Juni 2028.
	Kutekeleza programu ya kitaifa ya kuunganisha viwanda vidogo na vya kati vya ndani na kampuni kubwa za kimataifa ili kuongeza ushiriki kwenye mnyororo wa thamani, kufikia mwaka 2028.
	ii. Kutumia nafasi ya Kijiografia ya Kimkakati ili kuunganishwa kwa ufanisi zaidi na masoko ya kikanda na kimataifa, kila mwaka.
	iii. Kuandaa na kutekeleza mpango mkakati wa kuwezesha biashara kuinufaisha Tanzania kutokana na eneo lake la kijiografia kwa kuunganishwa vyema na masoko ya kikanda na kimataifa, kufikia mwaka 2028.
	iv. Kutoa kipaumbele kwa maendeleo ya sekta za kimkakati (k.m., usindikaji wa mazao ya kilimo, uzalishaji mdogo viwandani) kwa ajili ya mabadiliko ya kimuundo na mwelekeo wa kuuza nje, kufikia mwaka 2028.
3. Kudumisha kiwango cha chini cha mgao wa Gini na tofauti za kijiografia katika viwango vya sasa kufikia	3.1 Kuimarisha sera za kifedha za usambazaji upya ikijumuisha kodi shirikishi na programu za ulinzi wa jamii zinazolengwa, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
mwaka 2028.	3.2 Kuweka kipaumbele kwenye viwanda vinavyotumia nguvu kazi kubwa na usindikaji wa mazao ya kilimo katika maeneo ya vijijini na nusu-miji ili kutengeneza ajira kwa wingi, kila mwaka.
	3.3 Kuwekeza katika usafirishaji, nishati, na miundombinu ya kidijitali katika mikoa yote ili kupunguza tofauti kati ya miji na vijiji, kila mwaka.
	3.4 Kuhakikisha ubia na ushiriki wa lazima wa hisa za ndani katika miradi mikubwa ya uwekezaji wa kigeni uwekezaji wa moja kwa moja wa nje (FDI), kila mwaka.
3.3.13 Kuweka Mikakati ya Ushirikiano baina ya Nchi Mbili, Kikanda na Kimataifa katika Ulimwengu wa Mabadiliko	
Lengo 1: Kuimarishwa kwa uwezo wa nchi kukuza maslahi ya kiuchumi na kuinua ushawishi wa Tanzania duniani, kuchangia maendeleo endelevu na ushirikiano imara wa kimataifa	
1. Kutekeleza kikamilifu diplomasia ya uchumi, ili kuongeza ukuaji wa uwekezaji kwa asilimia 40, kufikia mwaka 2028.	1.1 Kubainisha na kuchapisha vipaumbele vya msingi vya kimkakati na maslahi ya Tanzania katika mawanda ya dunia, kufikia mwaka 2028.
	1.2 Kuimarisha uwezo wa kitaifa wa majadiliano na kuanzisha mfumo wa habari wa wakati halisi (real-time) kati ya misheni za kidiplomasia na taasisi za ndani kufikia mwaka 2028.
	1.3 Kuboresha mfumo wa ajira na miundo ya misheni za kidiplomasia, ili ilenge kwenye matokeo ya kiuchumi, kufikia Juni 2028.
	1.4 Kuimarisha Kituo cha Mahusiano ya Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim, kwa ajili ya kuwajengea uwezo kizazi kijacho cha wanadiplomasia ya kiuchumi, kufikia Juni 2028.
	1.5 Kuzindua na kutekeleza mkakati wa utambulisho wa kimataifa ili kuboresha taswira ya Tanzania kama kituo cha uwekezaji, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	1.6 Kupanua upatikanaji wa huduma za kibalozi katika miji ya kiuchumi muhimu na kuimarisha ushirikishwaji wa diaspora ili kuvutia uwekezaji na ujuzi, kufikia Juni 2028.
	1.7 Kuimarisha ulinzi wa haki miliki (na ushindani kwa kuzingatia viwango vya kimataifa, kufikia Juni 2028.
	1.8 Kuhakikisha ujumuishaji wa masuala ya jinsia na fursa za vijana katika maeneo yote ya ushirikiano wa kimataifa, kufikia Juni 2028.
3.3.14 Mienendo ya Kimataifa (Global Dynamics)	
Lengo 1: Kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kitovu imara cha nguvu za kiuchumi, kikanda na kimataifa, ifikapo Juni 2031, kupitia biashara ya kimkakati, uwekezaji na ushirikiano wa kidiplomasia, kuongeza ustahimilivu, ushindani na ustawi endelevu	
1. Tanzania kujumuishwa kikamilifu katika Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika, , Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika , kwa kufikia angalau asilimia 70 ya utekelezaji wa itifaki za biashara za kikanda kufikia mwaka 2028.	1.1 Kukamilisha mahitaji yote ya kuhaulisha sera ya biashara ya kikanda, kuhakikisha mtiririko huru wa bidhaa, huduma na mitaji wa itifaki za biashara za kikanda ifikapo Juni 2028.
	i. Kuhuisha sera za kitaifa za biashara na forodha kulingana na matakwa ya Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kufikia mwaka 2028.
	Kukamilisha mikataba yote iliyosalia ya biashara ya pande mbili na ya pande nyingi, inayohusiana na jumuiya za kikanda, kufikia Juni 2028.
	iii. Kuimarisha uwezo wa taasisi zinazohusika na uratibu masuala ya biashara kitaifa, kila mwaka.
	iv. Kuzindua mfumo jumuishi wa biashara ya kidijitali unaoendeshwa na akili unde , kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	v. Kutekeleza mfumo jumuishi wa forodha unaoendeshwa na teknolojia ya akili katika mipaka yote, kufikia Juni 2028.
	vi. Kuanzisha dirisha moja la mfumo unaotegemea teknolojia ya kidijitali ya block-chain, ili kurahisisha uwezeshaji wa michakato ya biashara, kufikia Juni 2028.
2. Kuimarisha diplomasia ya Tanzania kwa kuingia makubaliano ya ushirikiano wa kimataifa na wadau watatu 3 muhimu, kuongeza matumizi ya Kiswahili katika mashirika 4 ya kimataifa, na kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kazi katika angalau taasisi moja ya kimataifa iliyoendelea, ifikapo mwaka 2028.	2.1 Kuimarisha ushawishi wa kidiplomasia wa Tanzania katika kupata ushirikiano wa kimataifa na kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kazi, kufikia Juni 2028.
	i. Kuongeza mtandao wa balozi za Tanzania hadi kufikia nchi 60, kufikia Juni 2028.
	Kukuza diplomasia ya kitamaduni na ubadilishanaji wa elimu na nchi 25 na vyuo vikuu 35–40, kufikia Juni 2028.
	Kutekeleza huduma ya kutafsiri lugha ya kiswahili katika wakati halisi kupitia teknolojia ya akili unde katika mikutano na nyaraka nyaraka za Umoja wa Afrika, na Umoja wa Mataifa , kufikia Juni 2028.
	iv. Kuzindua jukwaa la diplomasia ya kidijitali linaloendeshwa na akili unde ili kuongeza ushirikiano wa kimataifa na uchambuzi, kufikia Juni 2028.
	v. Kuanzisha Baraza Maalumu la Biashara ya Kimataifa ili kuendeleza malengo ya diplomasia ya kiuchumi, kufikia Juni 2028.
3. Kuifanya Tanzania kuwa lango kuu la biashara barani Afrika, kwa kufikia TEU milioni 20 (za makontena kwa mwaka, kufikia Juni 2028.	3.1 Kuitangaza Tanzania ili kuwa lango kuu la biashara, kufikia Juni 2028.
	i. Kukamilisha usasishaji wa bandari za Dar es Salaam, Tanga, na Mtwara na kuzifanya kuwa za kisasa, na kuikamilisha ujenzi wa bandari ya Bagamoyo, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	ii. Kuzindua mfumo wa bandari bora unaoendeshwa na akili unde ili kuwezesha bandari kuwa na uwezo wa kufikia malengo ya TEU milioni 20, kufikia Juni 2028.
	iii. Kujenga reli na barabara maalum zinazounganisha bandari kuu na vituo vya mizigo vya bara kufikia Juni 2028.
	iv. Kuanzisha njia ya reli ya mwendokasi ya mizigo, ili kupunguza muda wa safari, kufikia Juni 2028.
	v. Kutekeleza mfumo unaoendeshwa na AI-wa uboreshaji wa usafirishaji na usambazaji katika bandari zote kuu na njia za usafiri kufikia Juni 2028.
	vi. Kujenga mtandao wa kitaifa wa mnyororo wa ugavi, kwa kutumia fursa yateknolojia ya IoT, blockchain, na akili unde, ili kuona mwanzo na mwisho wa shehena na kwa ufanisi, kufikia Juni 2028.
4. Kuanzishwa kwa mashirikiano ya uwekezaji kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa kwa lengo la kuvutia uwekezaji kutoka nje (FDI's) katika sekta muhimu, kufikia Juni 2028.	4.1 Kujadiliana na kuanzisha ushirikiano wa uwekezaji wa nchi na nchi, kikanda na wa kimataifa ili kuvutia Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka nje (FDIs) katika sekta muhimu za kimkakati, kufikia Juni 2028.
	i. Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kitaifa wa ushirikiano wa uwekezaji wa pande mbili, kikanda na kimataifa, kufikia mwaka 2028.
	ii. Kuanzisha vitengo vya kukuza ushirikiano wa uwekezaji (Investment Partnership Promotion Units - IPPUs) ndani ya TISEZA na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ili kuratibu na kufuatilia misheni za uwekezaji, kufikia mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kujadiliana na kufikia makubaliano mapya ya pande mbili, kikanda na kimataifa kwa ajili ya uwekezaji wa Moja kwa Moja (FDI) katika sekta za kimkakati, kufikia Juni 2028.
	Kuandaa na kuhifadhi orodha ya miradi ya kibiashara inayoweza kukopesheka na yenye matokeo makubwa, kwa ajili ya kuhamaisha uwekezaji kwenye miradi iliyolengwa, kufikia Juni 2028.
3.3.15 Urasimishaji wa Uchumi na Usimamizi Wake	
Lengo 1: Kuifanyia mabadiliko sekta isiyo rasmi kuwa injini ya ukuaji, kuchochea ushiriki wa sekta rasmi, na ukuaji wa uchumi	
1. Mchango wa sekta rasmi katika Pato la Taifa kuongezeka kutoka asilimia 55 hadi 63, kufikia Juni 2028.	1.1 Kuanzisha kitengo maalumu ndani ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) cha kukuza na kuendeleza Biashara Ndogo Ndogo na za Kati (MSMEs), kufikia Juni 2028.
	1.2 Kuzindua jukwaa la kidijitali, eneo moja la uandikishaji na jukwaa la uzingatiaji wa kodi, kufikia Juni 2028.
	1.3 Kuanzisha programu maalumu ya kusaidia kurasimisha biashara zisizo rasmi, kufikia Juni 2028.
	1.4 Kuandaa na kutekeleza motisha kwa sekta mahususi kwa lengo la kuwezesha urasimishaji, kufikia Juni 2028.
	1.5 Kuingiza biashara zisizo rasmi zilizosajiliwa kwenye minyororo ya ugavi ya sekta rasmi ya serikali na binafsi kupitia programu ya maendeleo ya wasambazaji, kufikia Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
2. Kupunguza ajira katika sekta isiyo rasmi kutoka asilimia 29 hadi 22, kufikia Juni 2028.	2.1 Kuandaliwa kwa programu ya kitaifa kwa ajili ya kuongeza ujuzi na mafunzo ya ufundi, programu hii ni mahususi kwa ajili ya kusaidia wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi kupata ujuzi wa kuwawezesha kupata ajira katika sekta rasmi zenye ujuzi wa juu, kufikia mwaka 2028.
	2.2 Kutekeleza mpango wa motisha za ajira rasmi kwa biashara zinazoajiri na kuwabakiza wafanyakazi wanaohama kutoka sekta isiyo rasmi, kwa kutoa ruzuku za muda wa mishahara au mikopo ya kodi, kufikia 2028.
	2.3 Kuimarisha ukaguzi wa kazi na mifumo ya utekelezaji, ili kuhakikisha viwango vya haki vya kazi, ulinzi wa wafanyakazi, na michango ya usalama wa kijamii, na kufanya ajira rasmi kuwa ya kuvutia zaidi, kila mwaka.
	2.4 Kuwezesha kuanzishwa kwa ushirika na vyama vya biashara ili kuwezesha wajasiriamali wadogo wa sekta isiyo rasmi kuunganisha rasilimali, kupata masoko makubwa, na kurasimishwa kwa pamoja, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
3.4. Kujenga Uwezo wa Binadamu na Maendeleo ya Jamii	
3.4.1. Jamii iliyoelimika, yenye ujuzi na inayojifunza	
Lengo 1: Kuwa na jamii iliyoelimika, yenye ujuzi na inayojifunza kwa kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu bora, jumuishi na mafunzo endelevu ya ujuzi.	
1. Kuongeza uwiano wa wasichana na wavulana wanaopata malezi na makuzi bora utotoni kwa asilimia 20 na udahili elimu bora ya awali kutoka asilimia 88.8	1.1 Kuongeza upatikanaji na ubora wa miundombinu ya vituo vya malezi na maendeleo ya mtoto na elimu ya awali ili kuwajengea msingi bora na kuwaandaa tayari kwa elimu ya msingi

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
hadi 96.7 ifikapo Juni 2028.	Malezi na elimu ya awali kwa watoto kuwa ya lazima na mfumo wa uandikishaji kuimarishwa kupitia utambuzi katika ngazi ya jamii kitaifa.
	Kuhakikisha angalau asilimia 20 ya watoto wenye umri wa miaka 3–4 wanapata huduma za malezi na makuzi katika vituo bora vya maendeleo ya awali ya mtoto.
	1.2 Kuhakikisha upatikanaji wa walimu wenye sifa na ujuzi, miundombinu rafiki na rasilimali za kujifunzia kwa watoto zinazozingatia umri pamoja na huduma za WASH, ifikapo 2028.
	Kuhakikisha upatikanaji wa walezi na walimu wenye sifa na ujuzi na usawa katika ugawaji wa rasilimali za kufundishia na kujifunzia zinazozingatia umri stahiki katika shule zote za awali, ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa programu maalumu za mafunzo kwa walezi na walimu wote wa vituo vya malezi, makuzi na madarasa ya awali, ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha ujuzi wa walimu kupitia mafunzo endelevu kazini ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji, ifikapo Juni 2028.
	1.3. Kujumuisha huduma za maendeleo ya mtoto katika sekta za elimu, afya na lishe ili kuhakikisha maendeleo jumuishi ya awali kwa mtoto, ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha uratibu wa kisekta kuanzia ngazi ya taifa hadi jamii ili kuwa na utekelezaji shirikishi wa programu za malezi, elimu, afya na lishe.
	Kuboresha na kusimamia utekelezaji wa viwango vya ubora wa huduma za maendeleo ya awali ya mtoto kwa kutumia miongozo inayokidhi matarajio ya jamii, taifa na kimataifa, ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
2. Kuongeza uwiano wa wanafunzi wanaopata elimu bora kwa usawa katika shule za msingi kutoka asilimia 98.2 hadi 100 ifikapo Juni 2028.	2.1 Kupunguza uwiano kati ya wanafunzi na mwalimu na kuimarisha ubora wa walimu katika shule za msingi.
	Kuboresha upatikanaji wa walimu, hususan wa masomo ya STEM na lugha ya Kiingereza, pamoja na kuhakikisha ufanisi wa matumizi ya walimu waliopo .
	Kuimarisha ubora wa walimu kupitia utekelezaji wa programu endelevu za maendeleo ya taaluma (CPD) zinazozingatia mbinu bunifu za ufundishaji na teknolojia za kisasa.
	2.2 Kuinua ubora wa ufundishaji na mazingira ya kujifunzia katika shule za msingi, ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha na kuwezesha vituo vya mafunzo kwa lengo la kuendeleza kada ya ualimu.
	Kuimarisha upatikanaji wa elimu bora na usawa kwa shule za msingi kupunguza utoro, kukatisha masomo, kuinua uhitimu, ufanisi wa matokeo ya kujifunza, na kiwango cha wanafunzi wanaovuka kuingia ngazi ya elimu ya sekondari.
	Kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali za kufundishia na kujifunzia ili kufikia uwiano wa kitaifa wa mwalimu kwa wanafunzi wa 1:40, ifikapo Juni 2028.
	2.3 Kuimarisha ujumuishi na ushiriki wa jamii katika maendeleo ya elimu ya msingi, ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha mifumo ya utambuzi na tathmini ya mahitaji maalum ya wanafunzi.
	Kuimarisha uwezo wa walimu wa shule za msingi za elimu maalum na jumuishi.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuimarisha ushiriki wa jamii katika kupanga na kutekeleza shughuli za maendeleo ya shule.
	Kuimarisha stadi msingi za kusoma, kuandika na kuhesabu pamoja na matokeo ya ujifunzaji, ifikapo Juni 2028.
	2.4. Kuanzisha mfumo maalum wa walimu wa shule za msingi, ifikapo Juni 2028.
3. Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaopata elimu bora kwa usawa katika shule za sekondari kutoka asilimia 75.3 kufikia asilimia 100 sanjari na kuongeza upatikanaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kutoka asilimia 4 hadi 30 ifikapo Juni 2028.	3.1 Kuajiri na kudumisha walimu wenye sifa na ujuzi maalum, hususan wa masomo ya STEM na lugha kila mwaka
	Kuimarisha mfumo wa idhibati na utoaji wa leseni, kwa kuuhusisha na ujuzi wa ufundishaji wa masomo mahsusi, umahiri na ufanisi k, kufikia mwaka 2031, ifikapo Juni 2028.
	3.3 Kusasisha mazingira kufundishia ujifunzaji katika shule za sekondari, kila mwaka.
	Kuboresha mazingira ya kujifunzia katika shule za sekondari ili kuendana na mahitaji ya kisasa, ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha na kuwezesha vituo vya mafunzo ya walimu kwa kuvipatia vifaa na teknolojia inayohitajika kwa maendeleo ya kitaaluma, kila mwaka.
	3.4 Kupanua na kuimarisha elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (TVET), ifikapo Juni 2028.
	Kuboresha na kuongeza miundombinu ya mafunzo ya amali katika shule za sekondari, kila mmwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuimarisha ushirikiano wa shule na shughuli za viwanda ili kuimarisha upatikanaji wa mafunzo kwa vitendo, uanagenzi na programu za kukuza ujuzi, kila mwaka.
	Kuweka maabara na maeneo maalumu ya kulea ubunifu (maker spaces) yenye vifaa vya kisasa kwa ajili ya shughuli za STEM na TVET.
	3.5 Kuimarisha Elimu Bora na Jumuishi ya Sekondari, ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha mifumo wa kubaini na kutathmini mahitaji maalum ya kila mwanafunzi wa sekondari kila mwaka.
	Kuboresha umahiri wa walimu wa sekondari wa elimu maalumu na elimu jumuishi, kila mwaka.
4. Kuongeza kiwango cha wanafunzi wa wanaoendelea na elimu ya sekondari ya juu hadi angalau kufikia asilimia 30 ifikapo Juni 2028.	4.1 Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na Elimu ya Juu pamoja na kuboresha miundombinu, ifikapo Juni 2028.
	Kujenga na kuboresha vyuo vikuu, vyuo vya ufundi na vituo huria vya kujifunzia katika mikoa yote, ifikapo Juni 2028.
	Kuongeza upatikanaji wa elimu ya juu kupitia programu za kujifunzia kwa masafa, mtandaoni na mifumo huria ya elimu, kila mwaka.
	4.2 Kuwianisha mitaala ya elimu ya juu na mahitaji ya sekta ya viwanda, ifikapo Juni 2028.
	Kutekeleza utaratibu shirikishi wa mapitio ya mitaala kujibu mahitaji ya sekta ya viwanda na mabadiliko ya teknolojia kwa kukushauriana ya wadau\, ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za elimu ya juu na sekta ya viwanda kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa mafunzo kwa vitendo na ajira kwa wahitimu, kila mwaka.
	Kukuza vituo vya ubunifu na viatamizi vinavyoungwa mkono na wadau wa sekta ya viwanda, kila mwaka.
	4.3 Kutumia diplomasia ya uchumi kuimarisha fursa na ubora wa elimu ya juu, ifikapo Juni 2028.
	Kukuza ushirikiano wa kimataifa katika elimu kupitia programu za udhamini, ubadilishanaji wa wanafunzi na utafiti wa pamoja, kila mwaka.
Kufikia angalau asilimia 50 ya nguvu kazi yenye ujuzi wa kidijitali ifikapo Juni 2028.	5.1 Kuweka mfumo endelevu wa ujifunzaji wa kidijitali na elimu kwa masafa, ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha mifumo ya ujifunzaji mitandaoni ili kupanua fursa ya elimu kwa watu wazima na mafunzo ya ujuzi, kila mwaka.
	Kukuza ubunifu katika utengenezaji wa maudhui ya kidijitali, programu za simu na mifumo ya ujifunzaji, kila mwaka.
	5.2 Kuimarisha mazingira ya utafiti na uvumbuzi wa teknolojia, ifikapo Juni 2028.
	Kuweka mifumo ya udhibiti inayowezesha matumizi salama ya teknolojia mpya kwa kuzingatia maadili na faragha, ifikapo m waka 2028.
	Kuongeza uwekezaji katika utafiti wa teknolojia zinazoibukia kama akili mneemba (AI), bioteknolojia na sayansi ya mazingira, kila mwaka.
	5.3 Kukuza fursa za ujifunzaji endelevu na ubunifu, ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kupanua vituo vya ujifunzaji kwa watu wazima vinavyozingatia stadi za msingi, ujuzi wa kidijitali na mbinu sdadi za maisha, kila mwaka.
	Kujenga mfumo thabiti wa ubunifu nchini kwa ushirikiano kati ya taasisi za elimu ya juu, viwanda, na serikali, ifikapo Juni 2028.
3.4.2 Nguvukazi watu Yenye Uwezo na Ari	
Lengo 1: Kuwa na nguvu kazi yenye uwezo na ari ya kazi, ili kuongeza tija na ubunifu	
1. kuongezeka kwa nguvukazi watu yenye ujuzi, ufundi na utaalamu unaohusiana na ubunifu wa viwandani kufikia angalau asilimia 35 ya jumla ifikapo Juni 2028.	1.1 Kuwianisha maendeleo ya ujuzi nchini na viwango vya kimataifa
	Kupitia na kuhuisha mitaala ya TVET kuendana na viwango vya kimataifa na mabadiliko ya mahitaji ya soko la ajira, ifikapo Juni 2028
	Kuwianisha na viwango vya kimataifa vya ujuzi katika sera za elimu, mafunzo na ajira, kila mwaka.
	1.2 Kuongeza usawa katika upatikanaji wa huduma za TVET, ifikapo Juni 2028.
	Kupanua vituo vya TVET hususan katika maeneo ya vijijini na maeneo yenye upungufu wa huduma.
	Kuendeleza na kutekeleza mitaala, miundombinu, na mbinu za kufundishia zinazozingatia jinsia na ushirikishwaji ifikapo Juni 2028.
	1.3 Kuimarisha mfumo wa ujifunzaji na utambuzi endelevu wa ujuzi, ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa na kutekeleza mfumo wa utambuzi wa ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi, ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuimarisha mfumo wa ujifunzaji kwa watu wazima kupitia programu za kila mwaka zinazokuza njia wazi za kazi na utambuzi wa ujuzi.
2. Kiwango cha nguvukazi watu yenye ujuzi wa kidijitali kufikia angalau asilimia 50 ifikapo Juni 2028.	2.1 Kuboresha miundombinu ya TVET na kuwa ya kisasa pamoja na muundo wa ufadhili, ifikapo Juni 2028.
	Kukuza ushirikiano wa uwekezaji wa ubia wa maendeleo ya TVET kati ya sekta za umma na binafsi (PPP), kila mwaka.
	Kuvipatia vituo vya mafunzo zana za kisasa, maabara, na mazingira ya kujifunzia ya kidijitali, kila mwaka.
	2.2 Kukuza ujuzi wa msingi kwa maendeleo ya uchumi wa kidijitali, ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha na kuimarisha vituo vya kijamii vya ubunifu wa kidijitali vijijini na mijini kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo, ifikapo Juni 2028.
	Kujumuisha umahiri wa kidijitali katika programu zote za mafunzo na elimu endelevu, ifikapo Juni 2028.
3. Kuongeza kiwango cha nguvukazi watu yenye ujuzi, hususan katika teknolojia, uhandisi na uchambuzi wa taarifa ifikapo Juni 2028.	3.1 Kuimarisha programu za mafunzo kwa vitendo na mafunzo kazini, kila mwaka.
	Kuimarisha programu za mafunzo kwa vitendo kwa kushirikiana na waajiri katika sekta za ubunifu na viwanda, kila mwaka.
	Kuhalalisha mfumo wa utambuzi wa uzoefu, mafunzo kwa vitendo na programu za uanagenzi katika utoaji wa vyeti na sifa za kitaifa, ifikapo Juni 2028.
3.4.3 Kusimamia na Kuitumia Fursa ya Kidemografia	

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Lengo la 2: Kuhakikisha Tanzania inanufaika na fursa ya kidemografia kupitia maendeleo ya rasilimali watu, ajira zenye staha, ujasiriamali, maendeleo ya biashara, na uwezeshaji kiuchumi ili kuwa na ukuaji wa uchumi jumuishi na kuboresha maisha.	
1. Kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana wa umri wa kati ya miaka 15–34 kutoka asilimia 21.5 hadi 19.3 ifikapo Juni 2028.	1.1 Kuwianisha elimu na ujuzi unaotolewa na mahitaji ya soko la ajira, ifikapo Juni 2028.
	Kushirikisha sekta binafsi katika kubaini ujuzi unaohitajika katika sekta za uzalishaji na utoaji wa huduma kwa mitaala ya mafunzo, kila mwaka.
	Kujumuisha ujuzi, teknolojia zinazoibukia na stadi za maisha katika mitaala ya elimu, ifikapo Juni 2028.
	Kukuza ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi ili kuingiza teknolojia mpya na ujuzi mahsusi wa kisekta katika programu za kukuza ujuzi, kila mwaka.
	1.2 Kuimarisha usawa wa jinsia katika elimu na ajira, ifikapo ifikapo Juni 2028.
	Kujenga na kuzipatia vifaa shule za wasichana hususan zilizo katika maeneo ya pembezoni sanjari na kuhamasisha ushiriki wa wasichana katika masomo ya STEM na ufundi, kila mwaka.
	Kuwezesha huduma za malezi ya watoto na kuhamasisha mazingira rafiki katika familia na maeneo ya kazi, ikiwa ni pamoja na kuongeza utekelezaji wa sera za usawa kwa wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi na shughuli kubwa za uchumi, kila mwaka.
	1.3 Kukuza ujasiriamali na ubunifu kwa Vijana, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuanzisha na kuimarisha vituo vya ubunifu na viatamizi kwa vijana, kila mwaka.
	Kutoa huduma jumuishi za maendeleo ya biashara ikiwemo fedha na masoko, kila mwaka.
	1.4 Kukuza fursa za uchumi wa kidijitali na ajira za mtandaoni, ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha mifumo ya kuunganisha vijana na ajira za kidijitali, kila mwaka.
	Kuwajengea vijana ujuzi wa kujitangaza na kusimamia kazi za kujiajiri, kila mwaka.
	1.5 Kuimarisha kasi ya urasimishaji wa sekta isiyo rasmi, kila mwaka.
	Kuweka mfumo wa vivutio unaozingatia ufanisi wa utendaji na taratibu zitakazochochea kasi ya urasimishaji wa biashara na kupunguza mzigo kwa wafanyabiashara kufikia 2028.
	1.6 Kuwajumuisha Diaspora katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo, kila mwaka.
	Kuweka vivutio kwa wataalamu wa Kitanzania walioko nje kurejea au kuchangia katika sekta za afya, elimu na teknolojia, ifikapo Juni 2028.
	Kukuza ushirikiano wa kitaaluma na utafiti kati ya diaspora na taasisi za utafiti za ndani, kila mwaka.
2. Kiwango cha utegemezi kutoka asilimia 87.4 hadi 79.4 ifikapo Juni 2028.	2.1 Kuongeza upatikanaji wa huduma rafiki za afya ya uzazi kwa vijana ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuongeza upatikanaji wa huduma rafiki za afya ya uzazi, mafunzo ya stadi za maisha na elimu kwa vijana, ifikapo Juni 2028.
	Kujumuisha elimu ya afya ya uzazi katika mitaala ya elimu, kila mwaka.
3. Angalau asilimia 20 ya wazee wa zaidi ya miaka 60 kufikiwa kikamilifu na mpango wa hifadhi ya jamii ifikapo Juni 2028.	Kuimarisha mifumo ya hifadhi ya jamii na uchumi jumuishi, ifikapo Juni 2028.
	Kuongeza mafao ya uzeeni na programu zisizohitaji michango, hususan kwa wazee wenye kipato cha chini katika sekta isiyo rasmi kila mwaka.
	Kuwezesha ujasiriamali kwa wazee kupitia mikopo na mafunzo, kila mwaka
	3.2 Kuimarisha mifumo ya malezi ya wazee ya kijamii, ifikapo Juni 2028.
	Kupeleka maafisa ustawi wa jamii katika ngazi ya wilaya na kata kwa ajili ya kuwasaidia wazee na walezi, kila mwaka.
	Kutambua na kuongeza mbinu za jadi/kijamii zilizo bora za kuhudumia wazee sanjari na kutoa mafunzo ya utunzaji wa wazee kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii, kila mwaka.
	3.3 Kuimarisha huduma za dharura kwa wazee, ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha mifumo ya kutoa tahadhari mapema kwa kuzingatia mahitaji na mawasiliano ya wazee na kuhusisha viongozi wa jamii na maafisa ustawi kusambaza taarifa wakati wa dharura, kila mwaka.
3.4.4 Soko la Ajira na Mazingira ya Kazi	
Lengo la 3: Kusasisha mfumo wa soko la ajira la Tanzania ili kuongeza nafasi za ajira zenye staha na kujenga nguvukazi watu iliyo tayari na ari kwa mustakabali wa baadae.	
Angalau ajira milioni 8 zenye staha kupatikana kupitia uwekezaji na ubunifu ifikapo Juni 2028.	1.1. Kuimarisha mazingira ya biashara ilikuruhusu ukuaji wa biashara ndogo, za kati (SMEs) na ubunifu (startups), ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuanzisha vituo vya kitaifa vya ubunifu vinavyotoa malezi ya biashara, ufadhili na miundombinu ya kazi, ifikapo Juni 2028.
	Kukuza uwekezaji katika utafiti na maendeleo (R&D), ubadilishanaji wa teknolojia na ushirikiano wa kimataifa kwa ajili ya upatikanaji wa masoko, kila mwaka.
	iii. Kuvutia uwekezaji mkubwa unaozalisha ajira, ifikapo Juni 2028.
	iv. Kutekeleza kampeni mahsusi za kuvutia uwekezaji kutoka makampuni makubwa ya ndani na kimataifa.
	Kuendeleza maeneo maalum ya kiuchumi na viwanda yaliyo vibali na miundombinu iliyo tayari kuwezesha shughuli za viwanda kuanza uzalishaji moja kwa moja na kutoa ajira kutokana na biashara mpya zitakazoanzishwa, ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha ukuaji na urasimishaji wa biashara, ifikapo Juni 2028
	Kutoa huduma za kifedha na kiufundi kwa SMEs zenye uwezo wa kukua, kila mwaka.
	Kutekeleza vivutio kuwezesha urasimishaji wa biashara, ifikapo Juni 2028
2. Ajira katika sekta za umma na shughuli za viwanda zenye thamani kuongezeka kwa angalau asilimia 10 ifikapo Juni 2028.	2.1 Kuanzisha na kufungamanisha utoaji wa mafunzo ya ujuzi na mahitaji ya viwanda vya kisekta, ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha programu za ushirikiano kati ya sekta za umma na binafsi zinazolenga kukuza upatikanaji wa mafunzo kwa vitendo ya teknolojia mpya, nishati safi na viwanda vya thamani, ifikapo Juni 2028.
	Kushirikiana na sekta binafsi kuanzisha vituo vya mafunzo vyenye teknolojia za kisasa, ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	2.2 Kukuza uwekezaji katika shughuli za viwanda, ifikapo Juni 2028.
	Kutoa vivutio maalum vya kifedha na visivyo vya kifedha ili kuvutia na kudumisha uendelevu wa uwekezaji katika sekta zenye thamani ya juu kama vile: teknolojia, viwanda vya dawa, na viwanda thamani ya juu, kila mwaka.
	Kukuza ushirikiano kati ya makampuni ya kimataifa, startups za ndani na SMEs ili kuwaunganisha katika minyororo ya thamani ya kimataifa na kutengeneza ajira zinazohitaji ujuzi wa juu, ifikapo Juni 2028.
3.4.5 Jamii jumuishi na iliyolindwa	
Lengo la 1: Kuongeza wigo wa jamii jumuishi iliyolindwa kwa kuongeza shughuli za hifadhi ya jamii ili kupunguza vihatarishi na kuhakikisha usawa wa fursa kwa makundi yote.	
1. Kuhakikisha angalau asilimia 40 ya watu walio katika mazingira hatarishi wanafikiwa na kulindwa ifikapo Juni 2028.	1.1 Kutekeleza sheria zinazolinda usawa na kupinga ubaguzi, ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha uwezo wa taasisi za udhibiti, urekebu, wakaguzi wa kazi, na mahakama kusimamia sheria zinazokataza ubaguzi kijinsia, umri, ulemavu au kabila, kila mwaka.
	Kujumuisha mbinu sahihi kimataifa katika mfumo wa kitaifa, ifikapo Juni 2028.
	1.2 Kuhakikisha upatikanaji sawa wa ardhi kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi, ifikapo Juni 2028.
	Kutekeleza sera za mageuzi ya usimamizi wa ardhi kuwezesha umiliki sawa kwa wanawake na watu wenye ulemavu, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kukuza programu za umilikishaji ardhi na kuimarisha vituo vya pamoja vya utoaji huduma kwenye maeneo yasiyofikika na yasiyo na huduma ili kuwainua wananchi kiuchumi, ifikapo Juni 2028.
	1.3 Kujumuisha sekta isiyo rasmi katika mifumo ya hifadhi ya jamii, ifikapo Juni 2028.
	Kutekeleza mifumo ya usajili wa kidijitali iliyorahisishwa kwa uandikishaji wa wafanyakazi katika sekta isiyo rasmi kila mwaka.
	Kuhuisha mifumo ya kitaifa ya hifadhi ya jamii ili kufikia wafanyakazi wote wa sekta isiyo rasmi, ifikapo Juni 2028.
	1.4. Kuboresha na kuimarisha programu za hifadhi ya jamii, ifikapo Juni 2028.
	Kupitia na kuboresha Programu za TASAF na PSSN ili ziweze kutumia daftari la kidijitali kuhifadhi kumbukumbu za walengwa, kuboresha ufuatiliaji, na kupunguza utegemezi wa wafadhili ifikapo Juni 2028.
	Kujumuisha vipengele vya ujuzi na kipato katika programu za hifadhi ya jamii ili kuwawezesha walengwa kujitoa katika umaskini, kila mwaka.
	Kujenga uwezo wa mamlaka za serikali za mitaa katika kusimamia utoaji wa hifadhi ya jamii kwa ufanisi, ifikapo mwaka 2028.
	Kushirikisha sekta binafsi katika uwekezaji wa hifadhi ya jamii, ifikapo Juni 2028.
	1.5. Kujumuisha mafunzo ya afya ya akili katika elimu na huduma za jamii, ifikapo Juni 2028.
	Kujumuisha elimu ya afya ya akili katika mitaala yote ya elimu, ifikapo mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuongeza moduli za afya ya akili katika mafunzo ya walimu na programu za maendeleo ya kitaaluma, kila mwaka.
	Kuimarisha mazingira ya shule na jamii yanayokuza ustawi,kupunguza unyanyapaa na kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya ya akili.
3.4.6. Kuboresha huduma ya afya kwa wote	
Lengo la 1: Kuboresha afya ya wananchi, ili kuongeza tija, na kupunguza tofauti katika upatikanaji wa huduma za afya.	
Vifo vya watoto wachanga kupungua kutoka 43 hadi 27 kwa vizazi hai 1,000 ifikapo Juni 2028.	1.1. Kuimarisha Huduma za Afya ya mama na mtoto mchanga, ifikapo Juni 2028.
	Kuajiri, kutoa mafunzo na kupeleka wakunga wenye ujuzi katika vituo vyote vya afya ili kufikia asilimia 90 ya upatikanaji ifikapo Juni 2028.
	Kuweka vifaa muhimu vya uchunguzi na dawa katika vituo vya ANC na PNC, ifikapo Juni 2028.
	Kuondoa gharama za moja kwa moja za huduma za ANC na PNC kwa wanawake wanaoishi katika maeneo yasiyofikika kirahisi, ya kipoto cha chini na wanaoishi katika mazingira hatarishi, ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha kliniki zinazotembea za huduma za ANC/PNC kufikia jamii za wafugaji zinazoishi katika maeneo yasiyofikika, kila mwaka.
	1.2. Kutekeleza Programu za Lishe kitaifa kwa akina mama na watoto, kila mwaka.
	Kuongeza upatikanaji wa vyakula vilivyoongezewa virutubisho kwa watoto wenye umri wa miezi 6–24, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuhakikisha utoaji wa kirutubisho cha vitamini A na dawa za minyoo kwa watoto chini ya miaka 5, ifikapo Juni 2028.
	Kusambaza virutubisho kwa watoto wadogo, kila mwaka.
	Kuimarisha kliniki zinazotembea za ANC/PNC ili kufikia jamii za mbali na wafugaji wanaohama, kila mwaka.
	1.3. Kuimarisha mfumo wa mafunzo ya taratibu za utoaji lishe kwa watoto wadogo na wachanga, Juni 2028.
	Kuwaandaa na kuwajengea uwezo wahudumu wa afya ngazi ya jamii ili waweze kutoa mafunzo ya taratibu za unyonyeshaji katika ngazi ya jamii, kila mwaka.
	Kutekeleza utoaji elimu ya unyonyeshaji kwa wanaume ili kuongeza ushiriki wao.
	1.4. Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya ya mama na mtoto ngazi ya jamii, ifikapo Juni 2028.
	Kutoa mafunzo kwa angalau asilimia 50 ya wahudumu wa afya katika huduma za mama na mtoto ngazi ya jamii, yakilenga elimu ya afya ya akili na saikolojia, ifikapo Juni 2028.
	Kujumuisha uchunguzi wa afya ya akili katika huduma za ujauzito na baada ya kujifungua ifikapo Juni 2028
2. Kuongeza wigo wa Bima ya Afya kutoka asilimia 15 hadi 35 ifikapo Juni 2028.	2.1 Kuongeza wigo wa upatikanaji wa bima ya afya kwa wote, ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kutekeleza sera za bima ya afya kwa wote zinazohakikisha upatikanaji sawa, kwa kuzingatia makundi katika sekta isiyo rasmi, wananchi wa vijijini, wanawake, vijana na makundi maalum, kila mwaka.
	Kuimarisha uwezo wa mamlaka za serikali za mitaa kuongoza uandikishaji wa wananchi katika afua ya bima kwa wote, kila mwaka.
	2.2 Kuimarisha Bima ya Afya ya Jamii, ifikapo Juni 2028.
	Kubuni vifurushi vya malipo vyenye gharama nafuu na vinavyobadilishika ili kuendana na mapato ya misimu na hali halisi ya uchumi wa eneo husika, ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha huduma tembezi za uandikishaji wa Bima ya Afya ya Jamii katika maeneo yasiyofikika kirahisi, kila mwaka.
	2.3 Kutumia majukwaa ya mtandaoni kuhamasisha kujiunga na bima ya afya na utoaji wa huduma, ifikapo Juni 2028.
	Kutumia mifumo ya kidijitali kwa ajili ya kurahisisha usajili wa bima ya afya na malipo ya michango ya wateja, ifikapo Juni 2028.
	Kujifunza kutoka mafanikio ya nyenzo za kidijitali za nje kuandaa nyenzo za ndani katika lugha rafiki kwa watu wenye mahitaji maalumu ili kuongeza ujumuishi wa makundi hayo, ifikapo Juni 2028.
3. Kupunguza idadi ya vifo vya akina mama wajawazito kwa kila vizazi hai 100,000 kutoka 104 hadi 85, ifikapo Juni 2028.	3.1 Kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya ya mama na mtoto kwa wote ifikapo Juni 2028.
	Kupanua upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi ziliyo rafiki kwa vijana na mashuleni, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za upimaji na usimamizi wa wajawazito wote kabla na baada ya kujifungua, ili kubaini na kudhibiti mapema matatizo ya uzazi, ifikapo Juni 2028.
4. Kupunguza kiwango cha jumla cha uzazi kutoka 4.8 (mwaka 2022) hadi 4.1, ifikapo Juni 2028.	4.1 Kujumuisha elimu ya afya ya uzazi katika ngazi zote za shule, ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha utoaji wa mafunzo ya afya ya uzazi yananayoendana na umri, yaliyojumuishwa katika programu za shule nchini katika ngazi zote, kila mwaka.
	Kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali na vyombo vya habari ili kukuza elimu ya afya ya uzazi, kila mwaka.
	4.2 Kutekeleza Sera zenye motisha ili kuwabakiza wasichana shuleni na kuwalinda dhidi ya vihatarishi vya ujana wakati wa balehe, ifikapo Juni 2028.
	Kuboresha miundombinu ya shule, ikiwemo vyoo kwa ajili ya usafi kwa wasichana, ili kujenga mazingira wezeshi ya kujifunzia, kila mwaka.
	Kuhusisha wazazi na walezi kupitia warsha ili kushughulikia vikwazo vya kiutamaduni na kiuchumi vinavyokabili elimu ya wasichana.
	4.3 Kuongeza programu za afya za jamii zinazohamasisha ushiriki wa wanaume, ifikapo Juni 2028.
	Kukuza elimu ya pamoja kwa wanandoa kuhusu uzazi wa mpango, kila mwaka.
	Kuhamasisha waajiri kusaidia programu za afya ya uzazi kwa wafanyakazi, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Kuongezeka kwa Umri wa kuishi kutoka miaka 68.3 hadi 70.4 ifikapo Juni 2028.	5.1 Kukuza programu za kinga na ugunduzi wa mapema wa magonjwa yasiyoambukiza, ifikapo Juni 2028.
	Kujumuisha uchunguzi wa vipengele hatarishi vya magonjwa yasiyoambukiza, ikiwemo shinikizo la damu, Kisukari kwenye damu, na na fahirisi za uzito wa mwili katika utoaji wa huduma za msingi za afya za kila siku, Juni 2028.
	Kuimarisha mifumo ya rufaa ili kudhibiti kwa wakati na kufuatilia watu waliogunduliwa kuwa na magonjwa yasiyoambukiza, kila mwaka.
	5.2 Kutekeleza afua za lishe na chakula bora, kila mwaka.
	Kuimarisha huduma za ushauri wa lishe kwa jamii, kwa kuwalenga wajawazito, watoto wachanga, na watu wenye magonjwa yanayotokana na unene uliopitiliza, kila mwaka.
	Kutumia majukwaa ya mawasiliano hususan simu za mkononi kutoa ushauri na kuikumbusha jamii umuhimu wa lishe, kila mwaka.
	5.3 Kuimarisha mfumo wa kitaifa wa afua mbalimbali wa magonjwa yasiyoambukiza, ifikapo Juni 2028
	Kujumuisha uratibu wa mfumo wa kitaifa wa sekta mbalimbali wa magonjwa yasiyoambukiza, katika mifumo rasmi ya kitaasisi kwa ajili ya kukinga, kudhibiti, na kutibu magonjwa yasiyoambukiza, ifikapo Juni 2028
	Kuimarisha mifumo ya mawasiliano ya sekta mbalimbali katika matumizi ya mara kwa mara ya takwimu za magonjwa yasiyoambukiza, kila mwaka.
Kupunguza ueneaji wa magonjwa Makuu ya Kuambukiza ikiwemo UKIMWI, Malaria, na Kifua Kikuu kwa angalau asilimia 30 kutoka viwango vya sasa, ifikapo Juni 2028.	6.1 Kupanua huduma za kinga na upimaji wa UKIMWI na VVU, kila mwaka.
	Kuongeza upatikanaji wa kinga kabla ya kuambukizwa (PrEP) na kuongeza huduma za tohara ya hiari kwa wanaume (VMMC), kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuhakikisha huduma za upimaji wa VVU zinapatikana kwa asilimia 100 katika vituo vyote vya afya na programu za kuifikia jamii, ifikapo Juni 2028.
	6.2 Kutekeleza programu za udhibiti wa vimelea vya malaria nchi nzima, kila mwaka.
	Kutekeleza programu za kudhibiti vimelea vya malaria nchi nzima, ikiwemo vyandarua vyenye viuatilifu, unyunyiziaji wa dawa ndani ya nyumba, na udhibiti wa vyanzo vya mazalia ya mbu, ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha usafi wa mazingira kwenye jamii ili kuondoa mazalia ya mbu, kila mwaka.
	6.3 Kuimarisha afua za kudhibiti kifua kikuu (TB), ifikapo Juni 2028.
	Kutekeleza hatua za udhibiti wa maambukizi ya kifua kikuu (TB), ikiwemo kupima watu wengi na kuboresha hewa bora katika maeneo ya umma, ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha vitengo tembezi vya upimaji wa kifua kikuu vyenye vifaa vya X-ray na mashine za GeneXpert, katika maeneo ya vijijini na yasiyofikika kirahisi, kila mwaka.
	6.4 Kuanzisha kampeni za uelimishaji jamii kuhusu kuzingatia kinga ya magonjwa, upimaji, na uzingatiaji wa matibabu, ifikapo Juni 2028.
	Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa afya wa jamii (CHWs), wafanyakazi wa huduma za jamii na wanaojitolea, ili kutoa elimu ya afya kuhusu kinga ya magonjwa, upimaji, na uzingatiaji wa matibabu, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kujenga uwezo wa waandishi wa habari wa ndani na wataalamu wa vyombo vya habari kuhusu utangazaji wa habari za afya ulio sahihi, wa kimaadili, na usio na unyanyapaa, kila mwaka.
	Kusaidia ujumuishwaji wa jumbe zenye kuelimisha kuhusu magonjwa kupitia majukwaa ya huduma za kifedha kwa njia ya simu za mkononi (mobile money), mifumo ya usafiri na maeneo mengine yanayofanana na hayo, kila mwaka.
7. Asilimia 58.0 ya jumla ya idadi ya watu wanaopata huduma za afya wanafikiwa na kupatiwa huduma kwa ubora na gharama nafuu ifikapo Juni 2028.	7.1 Kurahisisha sheia, kanuni na taratibu za uwekezaaji katika sekta ya huduma za afya ili kurahisisha ushiriki wa sekta binafsi, ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha vituo vya huduma za pamoja kwa ajili ya vibali vyote vya udhibiti wa uwekezaji kwa sekta binafsi ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha uwezo wa vyombo vya udhibiti (mfano, TMDA) ili viweze kutoa uangalizi wa haraka na wa uwazi, kila mwaka.
	7.2 Kuunganisha tiba mbadala sambamba na kisasa, ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha mfumo wa kitaifa kwa waganga wa jadi na wataalamu wa mitishamba, kwa kukuza mifumo ya rufaa mtambuka pamoja na wataalamu wa tiba-biolojia, kila mwaka.
	7.3 Kuimarisha maadili ya kitaaluma kwa wafanyakazi wa afya, kila mwaka.
	Kuimarisha ushirikiano kati ya vyombo vya udhibiti wa huduma za afya na vyombo vya sheria ili kushughulikia utovu mkubwa wa nidhamu wa kitaaluma, kila mwaka.
	Kujumuisha miongozo ya maadili ya kimataifa katika kanuni za kitaifa za maadili kwa wafanyakazi wote wa afya, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
8. Kujumuishwa kwa usimamizi wa afya na takwimu za kidijitali ili kutoa huduma za afya kwa ufanisi, ifikapo Juni 2028.	8.1 Kuhakikisha muunganiko wa utendaji kazi wa mifumo ya taarifa za afya, ifikapo Juni 2028.
	Kufungamanisha mifumo ya afya katika ngazi zote (msingi, sekondari, na kitaalamu) ya sekta ya umma na sekta binafsi, ifikapo Juni 2028.
	Kuhakikisha utendajikazi wa kimfumo kati ya mifumo ya kliniki na majukwaa ya vifaa na ugavi, ili kuwa na uratibu mzuri kati ya utoaji wa huduma na upatikanaji wa vifaa, ifikapo Juni 2028.
9. Kupunguza uagizaji wa bidhaa muhimu za afya kwa asilimia 20, ifikapo Juni 2028.	9.1 Kuweka vivutio kwa ajili ya uwekezaji kwa uzalishaji wa ndani wa bidhaa za afya, ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha vivutio vya kodi, sera za fedha, na udhibiti kwa ajili ya viwanda vya ndani vinavyozalisha teknolojia za afya za msingi na za hali ya juu, ifikapo Juni 2028.
	Kutoa mikopo yenye riba nafuu au dhamana za mikopo kwa kampuni zinazojishughulisha na uzalishaji wa ndani wa teknolojia za afya, kila mwaka.
	9.2 Kuimarisha minyororo ya ugavi wa dawa zinazozalishwa nchini, ifikapo Juni 2028.
	Kuhakikisha malighafi kwa ajili ya sekta ya dawa zinapatika kwa gharama nafuu kupitia ushirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi, kila mwaka.
	Kurahisisha uidhinishaji wa vibali vya kikanuni na forodhakwa malighafdi ya kutengeneza madawa, ili kupunguza ucheleweshaji, ifikapo Juni 2028.
10. Tanzania kuwa kati ya vituo vikuu viwili (2) vya utalii wa matibabu katika ukanda wa Afrika mashariki na kati,	10.1 Kutumia diplomasia ya afya na kuhamasisha utalii wa afya, ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
ifikapo Juni 2028.	i. Kuanzisha mahusiano rasmi ya kidiplomasia ya afya na itifaki zilizokubaliwa na nchi jirani na nchi washirika wapya, kila mwaka.
	ii. Kuandaa program za pamoja za mafunzo na majukwaa ya ubadilishanaji wa taaluma katri wa wataalam wa afya, ndani na nje ya mipaka ya nchik, kila mwaka.
3.4.7 Usalama wa Chakula na Lishe	
Lengo la 1: Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe, kwa lengo la Kupunguza Njaa na Kuongeza Ubora wa Afya ya Umma.	
1. Idadi ya Watu Wanaopata Chakula Chenye Lishe ya uhakika kwa Mwaka Mzima kuongezeka hadi asilimia 60, ifikapo Juni 2028.	1.1 Kutekeleza Programu ya Kitaifa ya Uimarishaji wa Chakula.
	i. Kurasimisha uongezaji wa virutubisho (vikiwa na chuma, folic acid), katika vyakula vikuu mafuta ya kula, na vyakula vya ziada vya watoto wachanga, ifikapo mwaka 2028.
	ii. Kuagiza kisheria uwekaji wa madini ya iodine kwenye Chumvi ya (Universal Salt Iodisation) na kuhakikisha uzingatiaji wa asilimia 100 kwa wazalishaji wote, ifikapo Juni 2028.
	iii. Kutoa vivutio vya kikodi kwa uzalishaji wa ndani wa vyakula vilivyoimarishwa vya kutosha na chumvi yenye iodine, kupitia ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi, ifikapo Juni 2028.
	1.2 Kuimarisha afua mchanganyiko za Taifa ya Chakula kwa ajili ya Lishe, ifikapo Juni 2028.
	i. Kukuza uzalishaji na utumiaji wa mazao yenye wingi wa madini chuma, provitamini A, na mazao mengine yenye virutubisho vingi kupitia huduma za ugani na usaidizi wa kimasoko, ifikapo mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	ii. Kujumuisha elimu ya lishe inayozingatia jinsia katika shule za sekondari, programu za vijana, na kampeni za kuelimisha umma kila mwaka.
	1.3 Kujumuisha Huduma za Lishe katika Huduma za Afya ya Msingi na huduma ya Mama na mtoto, ifikapo Juni 2028.
	i. Kupachika uchunguzi wa upungufu wa damu (anemia), upimaji wa alama za chuma (iron biomarker testing), na ushauri nasaha wa lishe katika taratibu za kitaifa za huduma kabla ya kujifungua (ANC), ifikapo Juni 2028.
	ii. Kupanua Mpango wa Hospitali Rafiki kwa Mtoto (BFHI) kwa vituo vyote vya afya vya umma na maeneo ya kunyonyesha mahali pa kazi, kila mwaka.
	iii. Kujumuisha huduma za lishe katika huduma za msingi za afya ili kupunguza idadi ya watu wenye utapiamlo, kila mwaka.
	1.4 Kuwezesha Mifumo ya Kitaifa ya Ufuatiliaji na uwezeshaji wa Lishe, ifikapo Juni 2028.
	i. Kuanzisha na kuimarisha mifumo ya kitaifa ya ufuatiliaji wa upungufu wa virutubisho muhimu (Vitamini A, iodini, chuma) kwa wanawake na watoto, ifikapo Juni 2028.
	ii. Kujenga uwezo wa wahudumu wa afya wa jamii kwa ajili ya utambuzi wa mapema wa utapiamlo kwa kutumia nyenzo kama vile MUAC na alama za uzito-kwa-urefu kila mwaka.
	Iii Kuunganisha malengo ya kupunguza Utapiamlo Mkubwa wa Ghafla (GAM) katika Mpango wa Pili wa Taifa wa Lishe wa Sekta Mtambuka (NMNAP II), ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	1.5 Kuhakikisha Viwango vya Kitaifa vya Usalama na Ubora wa Chakula vinazingatiwa, ifikapo Juni 2028.
	i. Kupanua Mfumo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Magonjwa Yatokanayo na Chakula kwa kutumia uchanganuzi wa kijiografia, kila mwaka.
	ii. Kutoa vivutio kwa ajili ya mifumo ya uidhinishaji inayohusika na uzingatiaji wa sheria kwa wasindikaji wa chakula, biashara ndogo na za kati (SMEs), na biashara za kilimo ili kuhakikisha utiifu wa 100% wa viwango vya kitaifa, ifikapo Juni 2028.
3.4.8 Upatikanaji na Uunganishwaji wa Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira kwa Wote	
Lengo 1: Kuwezesha uunganishwaji wa maji safi katika ngazi ya taifa ili kuongeza upatikanaji wa maji safi kwa kaya na jamii.	
1. Kuunganishwa kwa maji safi na salama yenye gharama nafuu na endelevu kwa asilimia 60 ifikapo Juni 2028.	1.1 Kuwezesha usimamizi jumuishi wa rasilimali za maji na sera zinazohimili mabadiliko ya tabianchi, ifikapo Juni 2028.
	i. Kufanya marekebisho ya Sera ya Taifa ya Maji (2002) ili kujumuisha masuala ya ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, upatikanaji wa maji, na kanuni za ESG (Mazingira, Jamii na Utawala), ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuimarisha usimamizi wa maeneo ya vyanzo vya maji katika mabonde yote ya mito na kujenga uwezo wa serikali za mitaa katika usimamizi wa maji unaohimili mabadiliko ya tabianchi, kila mwaka.
	iii. Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika usimamizi endelevu wa rasilimali za maji, kila mwaka.
	1.2 Kupanua na kusasisha miundombinu ya usambazaji wa Maji kuwa ya kisasa, Kila Mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	i. Kujenga visima vipya na miradi ya maji ya bomba katika vijiji 200, kila mwaka.
	ii. Kuboresha miundombinu ya kusukuma na kusambaza maji katika mikoa na majiji yote kila mwaka.
	iii. Kuendelea na ujenzi wa mtandao wa Maji wa Ziwa Victoria/Ziwa Tanganyika na kuanzisha mfumo mzuri wa usimamizi, ifikapo Juni 2028.
	iv. Kukarabati mitandao iliyopo ya kusambaza maji na kupunguza upotevu wa maji yasiyoingiza mapato kupitia ufungaji wa mita na utambuzi wa uvujaji kila mwaka ili kuongeza mtandao wa mabomba yaliyoounganishwa kutoka asilimia 30% hadi 55%=, ifikapo Juni 2028.
	1.3 Kuboresha Ubora wa Maji Kitaifa, ifikapo Juni 2028.
	i. Kuimarisha mifumo ya kijamii ya ufuatiliaji wa ubora wa maji kufikia asilimia 50 ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs), kila mwaka.
	ii. Kufanya Kampeni za uelewa kitaifa kuhusu utupaji salama wa taka na kupunguza utupaji wa kemikali hatarishi kila mwaka.
Matumizi ya mifumo ya kidijitali katika utoaji wa huduma za maji na usafi kufikia asilimia 70 mijini na asilimia 40 vijijini ifikapo Juni 2028.	2.1 Kusanifu mifumo ya kisasa ya usimamizi wa matumizi ya maji.
	i. Kutekeleza mradi wa majaribio wa mita janja za maji (smart meters) na visima vya ubora wa maji (water quality sensors) katika miji ya Dar es Salaam, Arusha, na Mwanza, ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuendesha kampeni za za kuelimisha umma kuhusu utupaji salama wa taka na kupunguza kemikali hatarishi, kila mwaka, ifikapo Juni 2028.
	2.2 Kuhamasisha matumizi ya mifumo ya maji inayotumia nishati ya jua, ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kufunga pampu za maji zinazoendeshwa kwa nishati ya jua kwenye visima vya maji vilivyo maeneo ya vijijini, kila mwaka.
	Kutoa mafunzo kila mwaka kwa mafundi na vyama vya watumiaji maji kuhusu uendeshaji na matengenezo ya pampu za maji zinazotumia nishati ya jua ili kufikia asilimia 30 ya maeneo ya vijijini, ifikapo Juni 2028.
Upatikanaji wa huduma bora na za kutosha za usafi na usafi wa mazingira na kutokomeza kujisaidia vichakani kufikia asilimia 80 ifikapo Juni 2028.	3.1 Kuboresha huduma za usafi mijini na pembezoni mwa miji, ifikapo Juni 2028.
	Kupanua na kuboresha miundombinu ya maji taka katika miji mikubwa, kila mwaka.
	Kuimarisha usimamizi, udhibiti na ufuatiliaji wa huduma za maji taka, kila mwaka.
	Kugatua mfumo wa kutibu majitaka kwa kuhamasisha viwanda kutibu majitaka kabla ya kuyaachia kwenye mazingira na kuhimiza matumizi ya mitambo midogo ya kisasa ya kutibu majitaka, ifikapo Juni 2028.
	3.2 Kutokomeza kujisaidia vichakani na kuhamasisha usafi kwa wote, ifikapo Juni 2028.
	Kupanua upatikanaji wa miundombinu ya usafi ya gharama nafuu kwa kuzingatia mahitaji ya wanawake, wasichana na makundi maalumu, kila mwaka.
	Kuhamasisha matumizi salama ya bidhaa za majitaka, kila mwaka.
3.4.9 Jamii Iliyoshikamana, Inayowajibika na Inayoshiriki	
Lengo la 1: Jamii iliyoshikamana na yenye uwajibikaji, inayochangia umoja wa Kitaifa na mshikamano wa kijamii	

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Kufikia angalau asilimia 35 ya wanawake katika nafasi za uongozi kwenye biashara, serikali na elimu ifikapo Juni 2028.	1.1 Kuandaa programu za uhamasishaji wa wanawake kwenye nafasi za uongozi ili kufikia asilimia 40 ya uwakilishi katika serikali kuu na za mitaa, ifikapo Juni 2028.
	Kufanya kampeni za uhamasishaji nchini, kila mwaka.
	Kutoa mafunzo kwa wanawake kuhusu kushiriki kwenye siasa, kila mwaka.
	1.2 Kuweka miongozo ya jinsia katika uteuzi wa bodi ili kufikia asilimia 35 ya wanawake katika bodi na tume, ifikapo Juni 2028.
	Kufanya marekebisho ya sheria za uteuzi wa umma ili kujumuisha hitaji la uwiano wa asilimia 35 ya usawa wa kijinsia, ifikapo Juni 2028.
	Kuhamasisha sekta Binafsi kufuata malengo ya uwiano wa kijinsia kila mwaka.
	1.3 Kuhakikisha asilimia 35 ya nafasi za uongozi wa juu katika kampuni za umma zinashikiliwa na wanawake, ifikapo Juni 2028.
	Kushirikiana na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji – CMSA na Dhamana na Soko la Hisa kutekeleza sera ya jinsia, kila mwaka.
	Kuwashirikisha vyama vya kisekta kuwa mabalozi wa usawa wa kijinsia, kila mwaka.
2. Kuweka misingi ya Tunu za Taifa (heshima, mshikamano, utambulisho wa kitaifa) kwa asilimia 60 ya wananchi ifikapo Juni 2028.	2.1 Kuanzisha majukwaa ya mijadala ya Kijamii inayohamasisha umoja, uzalendo na maadili, ifikapo Juni 2028.
	Kuwashirikisha wasanii na washairi kuhamasisha jumbe za umoja kupitia sanaa, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuhamasisha vyombo vya habari kutoa habari chanya zenye kuimarisha mshikamano, kila mwaka.
	2.2 Kuimarisha mafunzo ya uzalendo na uwajibikaji wa kiraia shuleni, kila mwaka.
	Kushirikiana na vyombo vya Habari kutoa Taarifa kuhusu jitihada za shule na mafanikio ya wanafunzi katika kukuza maadili na uzalendo kila mwaka.
	Kujumuisha hadithi na simulizi za asili Katika nyenzo za kujifunzia na kufundishia kila mwaka.
3.4.10 Maendeleo Jumuishi Vijijini	
Lengo Na. 2: Kuimarisha maendeleo Jumuishi vijijini ili kupunguza tofauti na maeneo ya mijini na kuboresha maisha ya vijijini	
1. Asilimia 30 ya vijiji kuwa na mipango ya matumizi ya ardhi na asilimia 40 ya ardhi kusajiliwa ifikapo 2028.	1.1 Kuhuisha mifumo ya kisera na kisheria kuhusu usimamizi wa ardhi.
	i. Kuhuisha Sheria ya Ardhi, Sheria ya Matumizi ya Ardhi na sheria nyingine za Ardhi, ifikapo Juni 2028
	ii. Kuekeleza miradi ya majaribio katika mikoa iliyochaguliwa ili kupima ufanisi wa sera zinazopendekezwa kabla ya ya kuziingiza nchi nzima, ifikapo Juni 2028
	1.2 Kuimarisha urasimishaji na mipango ya matumizi ya ardhi vijijini, ifikapo Juni 2028.
	i. Kuhamasisha jamii kupitia kampeni za uelimishaji kila mwaka kuhusu mipango ya matumizi ya ardhi na urasimishaji.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	ii. Kuanzisha na kutoa mafunzo kwa kamati za ardhi za vijiji kila mwaka ili kuhakikisha uendelevu na usimamizi wa taarifa za ardhi.
2. Kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao kwa asilimia 30 ifikapo Juni 2028.	2.1 Kuimarisha usimamizi wa rasilimali maji na miundombinu ya kilimo, kila mwaka.
	i. Kuwekeza na kuimarisha skimu ndogo za umwagiliaji, visima vya maji na uvunaji maji, ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuhimiza matumizi ya teknolojia zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi kama umwagiliaji wa matone na pampu zinazoendeshwa kupitia nishati ya jua, kila mwaka.
	iii. Kuwekeza katika miundombinu muhimu ikiwemo barabara za mashambani na miundombinu ya kuhifadhi mazao kila mwaka ili kupunguza upotevu wa mavuno.
	2.2 Kutoa ruzuku ya pembejeo muhimu kwa wakulima wadogo, kila mwaka.
	i. Kutoa ruzuku za mbegu bora, mbolea na viuatilifu muhimu, kikla mwaka.
	ii. Kutoa ruzuku kwenye chakula cha mifugo ili kuimarisha ukuaji fungamanishi wa kilimo, kila mwaka.
3. Asilimia 60 ya wajasiriamali na wakulima wa vijijini wafikiwe na huduma za kifedha ifikapo Juni 2028.	3.1 Kupanua wigo wa huduma maalumu za kifedha kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya vijijin,i kila mwaka.
	i. Kuanzisha na kutoa bidhaa maalumu za mikopo midogo kwa ajili ya wakulima, vijana, wanawake na kilimo biashara, kila mwaka.
	ii. Kusambaza na kutumia maafisa ugani kutoa elimu ya fedha kwa wakulima, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
3.4.11 Mabadiliko ya Vyama vya Ushirika	
Lengo la 3: Kuimarisha vyama vya ushirika ili kuchochea maendeleo Vijijini na kuwapa nguvu wanachama wa vyama vya ushirika.	
1. Kuanzisha mfumo wa uongozi unaozingatia uwajibikaji, ubunifu na ukuaji endelevu wa vyama vya ushirika ifikapo Juni 2028.	1.1 Kuanzisha sera na mfumo wa kisheria wa vyama vya ushirika ili kuimarisha mfumo wa uongozi wenye uwazi na uwajibikaji, ifikapo Juni 2028.
	i. Kuwajengea uwezo Wizara inayohusika na vyama vya ushirika na Serikali za Mitaa kuhusu usimamizi na usuluhishi wa migogoro, kila mwaka.
	ii. Kuimarisha utoaji wa motisha za kisheria na kisera zinazowezesha vyama vya ushirika kuweka akiba, kupata mikopo na kuwekeza, kila mwaka.
	1.2 Kuwezesha vyama vya ushirika kupata huduma za kifedha.
	Kutoa mikopo ya muda mrefu yenye riba nafuu kwa ajili ya uwekezaji, ununuzi wa vifaa, huduma za kuhifadhi mazao na uchakataji, kila mwaka.
	ii. Kukuza mikopo ya mtaji wa uendeshaji inayoendana na misimu ya kilimo, kila mwaka.
3.4.12 Kupanua Tabaka la Kati.	
Lengo la 4: Kuimarisha tabaka la kati ili kuwezesha ukuaji jumuishi, ukuaji wa soko la ndani na ushiriki katika sekta rasmi kila mwaka	
1. Kuongeza kwa tabaka la kati kutoka asilimia 12 hadi asilimia 18 ifikapo Juni 2028.	1.1 Kuanzisha National Digital Livelihoods Programme, ifikapo Juni 2028.
	i. Kutoa mafunzo ya ujuzi wa masoko ya kidijitali, biashara ya kidijitali na ujuzi nwa kujiajirin (freelancing skills), kila mwaka.
	ii. Kuweka mfumo rasmi wa utolewaji wa tuzo ya taifa ya ubunifu wa kidijitali, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	iii. Kuwezesha uanzishwaji wa biashara mpya za mtandaoni, kila mwaka.
	1.2 Kuanzisha mipango ya ukusanyaji wa mali za Serikali (Government-Backed Asset Accumulation Programmes), ifikapo Juni 2028.
	i. Kutoa hati mpya 100,000 za umiliki wa ardhi kila mwaka.
	ii. Wezesha ukoidishaji wa mali 20,000 zenye uwezio wa kuzalisha, na mpango huo juwe umeanza, ifikapo Juni 2028.
	1.3 Kuanzisha jukwaa la "Chanzo cha Maisha Diaspora Platform", ifikapo Juni 2028.
	i. Kuwezesha uwekezaji wa Dola za Marekani milioni 50 kutoka kwa Diaspora, ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuwarejesha wataalamu 500 kutoka Diaspora katika Taasisi za ndani, ifikapo Juni 2028.
	iii. Kuanzisha Jukwaa la kidijitali la Diaspora, ifikapo Juni 2028.
	1.4 Kuanzisha Integrated Economic Growth Centres kwenye miji midogo, ifikapo Juni 2028.
	i. Kukamilisha Growth Centres katika Majiji maalumu ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuwezesha urasimishaji wa biashara zisizo rasmi 10,000 na kuzalisha fursa za ajira mpya 5,000 kwenye majiji, kila mwaka.
	1.5 Kuzindua Programu za Uchumi wa Buluu na Kijani, ifikapo Juni 2031
	i. Kutoa mafunzo ya ujuzi kwa watu 5,000 kwa mwaka kuhusu uchumi wa buluu na Kijani, kila mwaka.
	ii. Kutoa ruzuku kwa biashara mpya za uchumi wa kijani/buluu, kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	iii. Kuzindua Programu husika, ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
3.5. Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi	
3.5.1. Uhifadhi wa Mazingira	
Lengo 1: Kuimarisha uwezo wa usimamizi wa mazingira na kuweka misingi ya uendelevu katika sekta zote ili kuhakikisha usalama na ustawi wa Ikolojia kwa Kizazi cha sasa na Kijacho	
Kuhifadhi bioanuai kwa kulinda na kusimamia angalau asilimia 60 ya mifumo ya ikolojia ya bahari, maji baridi na ardhi ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha kikosi kazi cha taasisi mbalimbali ili kufuatilia na kutekeleza sheria katika ikolojia ya maeneo ya mipakani ifikapo mwezi Juni 2028.
	Kuimarisha mifumo ya kisheria ya kupambana na ujangili, biashara haramu ya wanyamapori na uvamizi wa maeneo tengefu - ifikapo mwezi Juni 2028
	Kuandaa na kutekeleza angalau miradi 20 ya kipato mbadala kwa jamii zinazozunguka maeneo muhimu ya ikolojia kufikia 2028.
	Kurasimisha makubaliano ya usimamizi shirikishi na jamii 50 zilizo jirani na maeneo tengefu, ikiweka bayana majukumu na tija kwa pande zote ifikapo Juni 2028.
	Kurejesha angalau hekta milioni mbili (2) za maeneo yaliyoharibika zaidi (misitu, ardhioevu na matumbawe) kwa kuchukua hatua muhimu ikiwemo kudhibiti kuenea kwa viumbe na mimea vamizi ifikapo Juni 2028.
	Kufanya ufuatiliaji wa asilimia 60 ya mifumo ya ikolojia iliyo katika hifadhi kwa kutumia satelaiti ya Taifa na Ndege-nyuki (Drone) na kutoa taarifa kwa umma kila mwaka kuhusu maendeleo ya viashiria vilivyowekwa ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuongeza ufadhili na kuimarisha ugharamiaji wa uhifadhi wa bioanuai kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha ikiwemo kutoka katika mifuko/programu za kufadhili mazingira na ubia kati ya Sekta ya umma na sekta binafsi ifikapo Juni 2028.
Kuifanya Tanzania kuwa kati ya nchi 20 bora barani Afrika katika fahirisi za uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi ifikapo Juni 2028.	Kuimarisha Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira- NEMC na kuanzisha mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji wa ubora wa maji ifikapo Juni 2028.
	Kuwezesha upatikanaji wa fedha za Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi kupitia hati fungani za kijani, biashara ya kaboni na ubia kati ya Sekta ya umma na sekta binafsi kila mwaka.
	Kuchukua hatua mbalimbali kupunguza uchafuzi wa hewa ikiwemo kuchochea usafiri na usafirishaji unaohifadhi mazingira kwa kubadili angalau asilimia tano (5) ya mabasi kuanza kutumia nishati ya umeme katika miji mikubwa ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha uhimilivu wa mazingira dhidi ya mabadiliko ya hali ya hewa kwa kutekeleza Programu ya "Tanzania ya Kijani" kupitia kilimo janja rafiki kwa mazingira ifikapo 2028.
	Kufungamanisha masomo ya mazingira katika mitaala na kufanya kampeni za uelimishaji kitaifa kuhusu mazingira ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha ubora wa hewa kwa kudhibiti uchafuzi kutoka viwandani na vyombo vya usafirishaji. Pia, Kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu ifikapo Juni 2028.
	Kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za kilimo zinazozingatia uhifadhi wa mazingira ifikapo 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kutekeleza programu za upandaji miti kupitia "Tanzania ya Kijani" ifikapo 2028.
	Angalau asilimia 5 ya mabasi ya abiria mijini na asilimia 3-5 ya bajaji, guta na pikipiki ziwe zinatumia nishati ya umeme, hususan katika miji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Dodoma, ifikapo 2028.
Kupunguza kasi ya ukataji misitu kutoka asilimia 1.0 mwaka 2025 hadi asilimia 0.85 ifikapo Juni 2028.	Kuimarisha mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji wa misitu kwa kutumia satelaiti ili kudhibiti uvunaji haramu wa magogo ifikapo 2028.
	Kusimamia utekelezaji wa marufuku ya kitaifa ya uvunaji haramu wa magogo yenye thamani kubwa kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo za kidijitali ifikapo 2028.
	Kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kufikia lengo la asilimia 50 ya kaya zote nchini na taasisi ifikapo 2028.
	Kuongeza wigo wa mpango wa pamoja wa usimamizi wa misitu na utekelezaji wa modeli inayotoa fursa kubwa kwa jamii kushiriki katika shughuli za uhifadhi ifikapo 2028.
	Kuanzisha na kuendesha miradi mitano (5) ya kijamii ya biashara ya kaboni (REDD+) ili kuwawezesha wananchi kupata kipato mbadala kwa jamii zinazotegemea Misitu ifikapo 2028.
	Kuanzisha vituo vya urejerezaji wa mazingira ya misitu katika katika kanda ili kufikia lengo la upandaji wa miti milioni 100 na kurejesha hekta milioni 1 za ardhi iliyoharibiwa ifikapo 2028.
Kupima na kupanga matumizi ya angalau asilimia 40 ya ardhi yote nchini ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha na kuutumia mfumo wa kidijitali wa kitaifa wa upangaji wa matumizi ya ardhi na usajili ifikapo 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kutekeleza mipango jumuishi ya matumizi bora ya ardhi na kupanua umilikishaji rasmi wa ardhi kufikia asilimia 40 ya eneo la kitaifa la ardhi ifikapo 2028.
	Kufanya tathmini ya kina ya mifumo ikolojia muhimu, ikijumuisha ardhioevu zote za kitaifa ifikapo 2028.
Kuhifadhi na kusimamia kwa uendelevu asilimia 50 ya ardhioevu ya kitaifa ifikapo Juni 2028.	Kuimarisha uwezo wa kitaasisi kwa kutoa mafunzo kwa maafisa wa usimamizi wa ardhioevu angalau 200 na kuanzisha Kikosi Kazi cha Kitaifa cha Ardhioevu ifikapo 2028.
	Kuweka mipaka kwa kuzingatia sheria husika ili kulinda angalau 20% ya ardhi oevu zote zisizolindwa ili kuzilinda kutokana na uvamizi na uharibifu ifikapo 2028.
	Kuandaa na kutekeleza angalau programu tano (5) za majaribio za usimamizi wa vyanzo vya maji na ardhioevu kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa ifikapo 2028.
	Kutoa mafunzo na kushirikisha angalau vikundi 50 vya jamii katika usimamizi wa ardhioevu na kusaidia maendeleo ya maisha endelevu, katika ardhioevu ifikapo 2028.
	Kuanzisha na kuimarisha mifumo na zana za ufuatiliaji wa kidijitali (ndege nyuki, GIS, Akili Unde) ili kuhakikisha uhifadhi thabiti wa ardhioevu ifikapo 2028.
	Kuanzisha na kuimarisha mpango/programu za ushirikiano za kikanda ili kuhakikisha usimamizi shirikishi wa mifumo ikolojia ya ardhioevu inayovuka mipaka ifikapo 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Kuhakikisha uhifadhi na ulinzi wa asilimia 60 ya maeneo makuu ya vyanzo vya maji (Kagera, Mara, Ruaha Mkuu, Momba, Lufurio, Ruvu, Wami na Ruvuma) kufikia Juni 2028.	Kuandaa na kutekeleza mipango ya urejerezaji wa ardhi iliyoharibiwa kupitia upandaji miti kwa wingi na kuruhusu uoto wa asili katika mabonde lengwa ifikapo 2028.
	Kuhamasisha na kuwezesha matumizi endelevu ya miundombinu ya Skimu za Umwagiliaji ili kuongeza asilimia 20 ya tija katika maeneo ya kilimo ndani ya mabonde yaliyoainishwa ifikapo 2028.
	Kuongeza uwezo wa Bodi za Mabonde zilizopo kwa kutoa mafunzo kwa angalau maafisa 150 na kusimamia kwa karibu uzingatiaji wa taratibu za uendeshaji wa mabonde ifikapo 2028.
Kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa taka ngumu mijini na huduma za usafi hadi asilimia 60 kufikia Juni 2028.	Kuwekeza katika miundombinu ya kisasa ya ukusanyaji taka (malori, mapipa, vituo vya kukusanyia taka) na kuongeza huduma kwa maeneo ya mijini yasiyohudumiwa ifikapo Juni 2028.
	Anzisha mitambo ya kusafisha na kutibu maji katika angalau 30% ya miji kufikia 2028.
	Imarisha mifumo ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi ili kuwezesha uwekezaji katika mitambo ya kuchakata taka kuwa nishati na bidhaa zingine kama mbolea ifikapo 2028.
	Kupunguza taka ngumu katika maeneo ya mijini kwa angalau 30% kwa kushirikisha watoa huduma binafsi na Mashirika ya Kijamii katika utoaji wa huduma ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha na kutekeleze mpango wa ushirikiano wa kikanda ili kushughulikia uchafuzi wa plastiki katika Bahari ya Hindi, maziwa makuu na mito ifikapo 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Kufikia asilimia 40 ya ardhi iliyopangwa ifikapo Juni 2028.	Kuwianisha sera zote za ardhi za taifa na kuingiza masuala ya kukabiliana na uhimilivu wa tabianchi katika mfumo wa kisheria wa upangaji matumizi ya ardhi ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha na kuendesha vitengo vya upangaji matumizi ya ardhi vilivyogatuliwa katika angalau asilimia 50 ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) ili kuongoza utekelezaji katika ngazi ya chini ifikapo Juni 2028.
	Kuongeza matumizi ya teknolojia za upangaji ardhi kwa njia ya kijiografia na kidijitali kufikia angalau asilimia 60 ya vijiji kufikia 2028.
	Kufanya majaribio/utafiti na kuongeza zana za akili-unde katika uchambuzi wa kina wa taarifa na takwimu kuhusu matumizi ya ardhi katika angalau mikoa 2 ili kuwezesha mchakato wa ufanyaji maamuzi ifikapo 2028.
	Kuanzisha na kuhuwisha mifumo ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ili kushirikisha sekta binafsi katika upimaji ardhi, mipango na mipango ya maendeleo ifikapo 2028.
Kuhakikisha usimamizi na uhifadhi wa angalau asilimia 40 ya rasilimali nyeti za mimea, wanyama na misitu kufikia Juni 2028.	Kuanzisha na kuimarisha Kituo cha Taifa cha Rasilimali za Kijenetiki kufikia 2030, chenye jukumu la kujenga mfumo endelevu na imara wa usimamizi wa rasilimali za kijenetiki za mimea, wanyama na misitu.
	Kuingiza uhifadhi wa rasilimali za kijenetiki katika mifumo ya kitaifa ya usalama wa chakula, lishe na ulinzi wa bioanuai ifikapo 2028.
	Kuhifadhi kwa utaratibu anuwai mimea, wanyama na misitu kupitia mbinu za uhifadhi nje ya makazi asilia (ex-situ) na ndani ya makazi asilia (in-situ) kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuanzisha na kuendeleza kanzidata ya kitaifa ya kidijitali ya rasilimali za kijenetiki ili kuhakikisha upatikanaji taarifa/takwimu kwa watafiti na watunga sera ifikapo Juni 2028
	Kuanzisha mfumo wa uwazi na ufanisi wa upatikanaji na ugawaji wa faida zitokanazo na rasilimali za kijenetiki, unaoendana na itifaki ya Nagoya ili kukuza upatikanaji wa haki na ugawaji wa faida kwa uwazi ifikapo Juni 2028.
	Kushiriki kikamilifu katika tafiti na ushirikiano na taasisi za ndani na kimataifa ili kuimarisha uhifadhi na matumizi ya rasilimali za kijenetiki kila mwaka.
Kujumuisha kanuni na vigezo vinavyozingatia mazingira na masuala ya kijamii (Environemantal, Social Governance – ESG) katika muundo wa uchumi wa Tanzania na kuhakikisha vigezo hivyo vya ESG vinatekelezwa na 50% ya makampuni yaliyoorodheshwa katika Soko la Hisa na 30% ya taasisi za fedha zilizo na leseni ifikapo Juni 2028.	Anzisha na weka jukumu la kuripoti utekelezaji wa hatua kwa hatua wa vigezo vya ESG kwa kampuni zote zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa, kwa kuanzia na 20% ya makampuni makubwa zaidi ifikapo Juni 2028.
	Imarisha miongozo kwa taasisi zote za fedha zilizoidhinishwa kuhusu kujumuisha hatari za hali ya hewa na hatari nyingine za ESG katika usimamizi na tathmini ya mikopo na michakato ya kufanya maamuzi ya uwekezaji ifikapo Juni 2028.
	Kuendeleza na kuanzisha vivutio vya kodi kwa kampuni zinazofikia utendaji wa juu wa utekelezaji vigezo vya ESG ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha hitaji la mitaji ya upendeleo ili kutoa motisha kwa benki kutoa mikopo ya kijani kwa miradi endelevu ya mazingira (mathalani, kupunguza kiasi cha mtaji ambacho benki inapaswa kushikilia dhidi ya mikopo ya "kijani") ifikapo 2028.
	Kuanzisha fahirisi ya uendelevu (Sustainability Index) kwa makampuni ya ndani yaliyoorodheshwa katika Soko la Hisa ili kupima uzingatiaji katika uhifadhi wa mazingira ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuanzisha bidhaa/huduma za kifedha mahususi kwa ajili ya kuhamasisha utekelezaji wa vigezo vya ESG, kama vile hatifungani za kijani, mikopo nafuu ya kufadhili miradi ya mazingira ifikapo 2028.
	Kuzindua mpango wa kitaifa wa kujenga uwezo katika masuala ya ESG kwa ushirikiano na taasisi za elimu/kitaaluma na jumuiya za wazalishaji ili kutoa mafunzo kwa angalau wasimamizi 1,000 wa mashirika, wajumbe wa bodi na wachambuzi wa masuala ya fedha kila mwaka.
	Kuandaa na kusambaza mwongozo na mfumo wa utoaji taarifa za utekelezaji/uzingatiaji wa ESG kwa kila sekta ili kusaidia makampuni mkubwa na madogo (SMEs), kuelewa na kutekeleza mahitaji mapya ya kuripoti kwa ufanisi ifikapo 2028.
3.5.2. Mipango na Usimamizi wa Miji iliyoboresha na endelevu.	
Lengo la 1: Kukuza upangaji mzuri wa miji ulio endelevu kwa kuongeza miundombinu ya kisasa, kuboresha ufanisi wa matumizi ya ardhi na kuimarisha usafiri wa mijini unaoruhusu ukuaji wa uchumi wa taifa ifikapo 2050.	
Angalau asilimia 50 ya wakazi wapya wa mijini waishi katika makazi yaliyopangw a rasmi, huku mfumo wa kitaifa wa ardhi wa kidijitali ukiwa unafanya kazi kufikia Juni 2028.	Kuandaa na kuendesha mfumo wa kitaifa wa upangaji miji na taarifa za ardhi ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha utekelezaji wa sheria za upangaji miji na matumizi ya ardhi ili kudhibiti ukuaji holela wa makazi yasiyo rasmi ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha uwezo wa mamlaka za mitaa katika masuala ya utawala wa mijini, usuluhishi/upatanishi, na mipango shirikishi ifikapo Juni 2028.
Ufanisi katika mfumo wa usafirishaji mijini kuboreshwa kwa angalau asilimia 15 ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha mifumo mahiri ya usafiri wa umma inayotumia nishati ya umeme (kama BRT, mabasi ya kielektroniki) yenye miundombinu ya kielektroniki katika utozaji wa nauli katika angalau miji miwili mikuu ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kutekeleza sera za usafiri usio wa magari (non-motorised transport - NMT), ikijumuisha ujenzi wa njia maalum za kuendesha baiskeli na kutembea kwa miguu, katika miji mikuu 2–3 ifikapo Juni 2028.
Angalau asilimia 20 ya miradi mipya ya miundombinu ya miji kujumuisha usanifu unaozingatia uzalishaji mdogo wa hewa ukaa na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabia nchi na miji mahiri miwili ya majaribio ifikapo Juni 2028.	Kujumuisha ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi na Usimamizi wa Vihatarishi vitokanavyo na Majanga (Disaster Risk Management (DRM)) katika maandalizi ya angalau asilimia 70 ya mipango miji ifikapo Juni 2028.
	Kuanza matumizi ya nishati mbadala, ikijumuisha nishati ya jua na upepo iliyounganishwa na gridi ya taifa, ili kutoa huduma za mijini, kufikia MW 225 ifikapo Juni 2028.
	Kuzindua miji miwili ya majaribio yenye miundombinu ya kidijitali, ufanisi katika utoaji wa huduma za umma na makazi yanayostahimili tabianchi ifikapo Juni 2028.
	Kutoa motisha katika miradi ya makazi na maboresho mahsusi ya sera ya ardhi ili kuchochea soko la nyumba za gharama nafuu ifikapo Juni 2028.
	Kuongeza wigo wa programu za makazi nafuu na kuandaa kongani/SEZs moja hadi mbili kupitia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPPs) ifikapo Juni 2028.
	Kuhamasisha vyanzo bunifu wa fedha kwa ajili ya maendeleo ya miji ikiwemo kutoa hatifungani za kijani za Manispaa ifikapo Juni 2028.
3.5.3. Mageuzi na usimamizi endelevu wa ardhi	
Lengo la 2: Kuimarisha usimamizi endelevu na wenye tija wa ardhi kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa umiliki wa ardhi, kuboresha upangaji wa matumizi ya ardhi na kukuza ukuaji endelevu wa uchumi.	

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Kurasimisha ardhi kwa kuimarisha usajiliwa na utoaji haki miliki wa ardhi kutoka asilimia 30 (2023) hadi angalau asilimia 50 ifikapo Juni 2028.	Kuimarisha mifumo ya kisheria na kanuni zinazoongoza ugawaji endelevu wa ardhi na kuzingatia usawa wa kijinsia katika hati miliki za ardhi ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa mwongozo wa kitaifa wa kuzuia, kusuluhisha na kutatua migogoro ya ardhi ifikapo Juni 2028.
	Kujumuisha ulinzi wa mazingira, ustahimilivu wa hali ya hewa, na programu za urejelezaji katika maamuzi yote ya usimamizi wa ardhi ifikapo Juni 2028.
Kuongezeka kwa miamala ya ardhi inayosimamiwa na kurekodiwa kupitia mifumo ya kidijitali kutoka 10% (2023) hadi angalau 40% kufikia Juni 2028.	Kuimarisha usimamizi wa ardhi kwa kimtandao/kielekroniki kwa kuunganisha GIS na Akili Unde ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha Vituo vya Huduma ya Pamoja za Ardhi ikihusisha matumizi ya teknolojia ya kidijitali katika maeneo yote ya kipaumbele ili kuwarahisishia wananchi kufikia huduma za ardhi kwa gharama nafuu ifikapo Juni 2028.
	Kutoa mafunzo kwa angalau asilimia 50 ya maafisa ardhi katika ngazi ya Serikali za Mitaa kuhusu matumizi ya mifumo ya kidijitali, GIS, usuluhishi wa migogoro na usimamizi wa ardhi unaozingatia tabianchi ifikapo Juni 2031
3. Eneo la ardhi lililotengwa kwa matumizi ya viwanda kuongezeka kutoka asilimia 5 (2023) hadi angalau asilimia 7 ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha benki ya kitaifa ya ardhi kwa ajili ya kusimamia na kutenga ardhi kwa matumizi ya kongani za viwanda, SEZs na shoroba kubwa za usafirishaji ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa na kutekeleza mipango maalum ya matumizi ya ardhi kwa ajili ya ukuaji wa viwanda katika Kanda za Vipaumbele 3 – 5 zinazounganishwa kimkakati na miundombinu ya usafiri na usafirishaji ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kubuni na kutekeleza mifumo ya vivutio vya kodi ili kuvutia uwekezaji katika matumizi ya ardhi kwenye shughuli za viwanda na usafirishaji kwa angalau Maeneo Maalumu ya Uwekezaji matatu ifikapo Juni 2028.
3.5.4. Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi	
Lengo la 1: Kuimarisha uhimilivu wa tabianchi unaohifadhi urithi wa asili wa Tanzania kwa ustawi wa kizazi cha sasa na kijacho.	
Uhimilivu wa tabianchi kuingizwa katika mifumo yote ya kitaifa ifikapo Juni 2028.	Kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Mabadiliko ya Tabianchi katika sekta zote muhimu na Mamlaka za serikali za mitaa, na kuuunganisha katika mipango na bajeti za kila mwaka ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa mkakati wa kitaifa wa utafutaji wa fedha za mazingira na kuimarisha Mfuko ya Kitaifa wa Mazingira (National Climate Fund - NCF) na mageuzi ya utawala ifikapo Juni 2028.
	Kutumia fursa za uwekezaji wa binafsi kwa kutoa hati fungani za kijani na kuanzisha bidhaa za mbalimbali za kifedha ili kuhamasisha angalau dola za Marekani milioni 200 kufikia Juni 2028.
	Kujumuisha elimu ya masuala ya tabianchi katika ngazi zote za mitaala ya kitaifa na kuandaa Viwango vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (TVET) - ifikapo Juni 2028.
Kupunguza uzalishaji wa gesi joto (GHG) kwa asilimia 30–35 na kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika umeme wa taifa kufikia asilimia 75 ifikapo Juni 2028.	Kuongeza nishati safi ya kupikia kwa angalau asilimia 50 ya kaya na kutekeleza programu za matumizi ubora wa nishati ili kupunguza matumizi ya nishati kwa asilimia 10 katika sekta muhimu ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuongeza nishati mbadala kwa kuongeza uwezo wa kuzalisha MW 500-700 za uwezo mpya na kusambaza umeme kwa 30% ya kaya zisizo kwenye gridi ya taifa kupitia mifumo ya jua ifikapo Juni 2028.
	Kuanziasha hudumaza usafiri waumma ulio rafiki kwa mazingirakwa kuanzisha mabasi 200 ya umeme na miundombinu/vituo vya kuongezea umeme katika miji mikubwa ifikapo Juni 2028.
	Anzisha soko la kaboni lenye mfumo wa kupanga bei na wa kuwezesha mauziano ya viwango vya uchafuzi (Emissions Trading System (ETS)) ifikapo Juni 2028.
Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa kukabiliana na hasara na uharibifu (Loss and Damage) ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa hasara na uharibifu kwa ajili ya kuratibu maandalizi, urejeshwaji na fedha za kukabiliana na athari za tabianchi zisizoweza kuepukika ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha na kupanua mifumo ya uhamishaji wa vihatarishi na bima (bima huru, ya mazao) ili kutoa huduma ya kitaifa kwa jamii zilizo hatarini ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha na kuongeza wigo wa mifumo ya uokozi and fidia katika ngazi ya jamii kwa mikoa angalau mitano inayokabiliwa zaidi na changamote za hali ya hewa kufikia Juni 2028.
	Kuhamasisha na kuanzisha mfuko maalum wa hasara na uharibifu kwa kutumia vyanzo bunifu kama vile bima za tabianchi, angalau kufikia dola za Marekani milioni 100 kwa mwaka ifikapo Juni 2028.
Lengo la 2: Kuchochea teknolojia na ubunifu katika kilimo, mifugo, uvuvi na misitu ili kujenga minyororo ya thamani yenye ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha ukuaji endelevu wa uchumi ifikapo 2050	

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Asilimia 30 ya wazalishaji katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kutumia teknolojia rafiki kwa mabadiliko ya tabianchi ifikapo Juni 2028.	Kutumia mifumo ya kisasa ya umwagiliaji inayoendeshwa kwa njia ya mtandao na mfumo wa ufuatiliaji wa udongo ili kuboresha matumizi ya maji katika kilimo ifikapo Juni 2028.
	Kuongeza majukwaa ya ushauri kwa wakulima, wavuvi na wafugaji ili kutoa taarifa za hali ya hewa na soko kwa wakati halisi ifikapo Juni 2028.
	Kutumia mifumo ya kisasa ya kidijitali ya ufuatiliaji wa mifugo ili kuimarisha usimamizi na masoko ya mifugo ifikapo Juni 2028.
Asilimia 20 ya viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo kutumia nishati jadidifu na kutekeleza mbinu stahimilivu za mabadiliko ya tabianchi ifikapo Juni 2028.	Kuwekeza katika majokofu na vyombo vingine vya uhifadhi vinayotumia umeme wa jua ili kuimarisha utunzaji na kulinda thamani ya bidhaa za uvuvi, ufugaji na mbogamboga ifikapo 2028.
	Kuwezesha kongani za viwanda vya kilimo zinazoendeshwa kwa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi zenye mifumo ya kidijitali kwa ajili ya ufanisi wa matumizi ya rasilimali ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha mifumo ya udhibiti wa ubora inayoendeshwa na Akili Unde katika usindikaji wa chakula na uvuvi ili kuimarisha thamani na usalama wa bidhaa ifikapo Juni 2028.
Kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno kwa asilimia 15, na asilimia 40 ya biashara ya mazao ya kilimo kupitia matumizi ya teknolojia mbalimbali ikiwemo ya kidijitali ifikapo Juni 2028.	Kukuza na kuimarisha biashara kwa njia ya mtandao na huduma za fedha kiganjani/kwa njia ya simu za mkononi hususan miongoni mwa biashara ndogo na za kati pamoja vyama vya ushirika ili kuwaongezea ushindani na wigo wa soko ifikapo 2028.
	Kuwekeza katika majokofu na maghala yanayostahimili hali ya hewa katika maeneo yenye uhaba wa chakula ili kupata akiba ya chakula ifikapo Juni 2028

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuanzisha majukwaa jumuishi ya takwimu yanayounganisha uzalishaji, usafirishaji na mahitaji ya watumiaji ili kuboresha ufanisi wa minyororo ya ugavi ifikapo Juni 2028.
Mfumo wa Utoaji Tahadhari Mapema na Uwezo wa Taasisi	
Lengo la 1: Kuanzisha mfumo jumuishi wa sekta mbalimbali wa utoaji wa tahadhari ya mapema utakaoimarisha uhimilivu wa taifa kupitia taarifa za wakati, za kuaminika na zinazoweza kuchukuliwa hatua katika sekta za mazingira, uchumi, afya na kijamii ifikapo 2050.	
Kuongeza uwekezaji na ugharamiaji wa Mfumo wa Utoaji wa Tahadhari ya Mapema (EWS) kwa angalau asilimia 0.2 ya Pato la Taifa kwa mwaka, ifikapo Juni 2028..	Kuanzisha mifumo ya Ubia baina ya sekta ya umma na binafsi kwa ajili ya kufadhili miundombinu ya tahadhari ya mapema ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha programu ya kuwezesha ubunifu wa mifumo ya tahadhari ya mapema mahususi kwa ajiri ya sekta binafsi na jamii ifikapo 2028.
	Kutenga angalau asilimia 30 ya bajeti ya uboreshaji wa teknolojia ya maafa/majanga katika akili-unde (AI), takwimu na teknolojia nyingine za kisasa ifikapo Juni 2028.
Kutumia teknolojia ya kidijitali kutoa taarifa za tahadhari ya mapema katika kanda zote zenye hatari kubwa ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha mifumo ya tahadhari za moja kwa moja (automated) katika maeneo 2–3 yenye hatari kubwa yanayokumbwa mara kwa mara na changamoto za tabianchi kufikia Juni 2028.
	Kujumuisha mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa taarifa na takwimu kama satelaiti, droni, IoT katika mfumo wa Taifa wa Tahadhari ya Mapema ili kuweza kutambua kwa wakati vihatarishi mbalimbali ifikapo Juni 2028.
	Kuhakikisha mfumo wa usambazaji taarifa unawafikiwa watu wote, kwa wakati unaofaa, kwa lugha mbalimbali na katika maeneo yote yenye hatari kubwa ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Kuongeza idadi ya watu wanaofikiwa na Mfumo wa Utoaji wa Tahadhari ya Mapema (EWS) kutoka asilimia 2 (2023) hadi angalau asilimia 30 ifikapo Juni 2031, kwa kuongeza mifumo jumuishi ya kijamii kwa angalau miji 10.	Kuanzisha kampeni za kitaifa za uhamasishaji katika sekta mbalimbali kuhusu Mfumo wa Utoaji wa Tahadhari ya Mapema na kuanzisha mazoezi ya majaribio kila mwaka katika sekta mbalimbali ifikapo Juni 2028
	Kubuni kwa pamoja itifaki za tahadhari mahususi kwa sekta na wadau na kuziwasilisha katika miundo inayoweza kufikiwa kirahisi (mfano kwa kutumia Kiswahili) ifikapo Juni 2028.
	Kuongeza mifumo ya utoaji tahadhari mapema iliyounganishwa na jamii ili kuhakikisha utendakazi katika ofanya kazi, iliyounganishwa na jamii kufikia Juni 2028.
3.5.6. Kuimarisha Ushiriki katika Biashara ya Kaboni	
Lengo la 1: Kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kinara wa kikanda katika biashara ya kaboni, kuchochea mapato endelevu, ajira zinazotokanazo na uchumi wa kijani na uhimilivu wa tabianchi.	
Kuanzisha sera ya taifa ya biashara ya kaboni na mfumo wa urekebu ifikapo Juni 2028.	Kufanya mapitio na kuhuisha miongozo na kanuni za biashara ya kaboni za kitaifa ili kuendana na mwenendo na viwango vya masoko ya kimataifa ifikapo 2028.
	Kuanzisha mfumo wa ndani wa kupanga bei kaboni kwa sekta za kipaumbele ifikapo 2028.
	Kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa Kituo cha Taifa cha Kaboni ili kiweze kuratibu na kusimamia mfumo wa biashara ya kaboni kwa ufasaha ifikapo 2028.
Kuanza kufanya kazi kikamilifu kwa mfumo wa kitaifa wa kidijitali wa Upimaji, Utoaji Taarifa na Uthibitishaji (MRV)	Kuandaa na kuendesha mfumo imara wa kitaifa wa kidijitali wa upimaji, utoaji taarifa na uthibitishaji na jukwaa la usajili wa biashara ya kaboni ifikapo 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
na usajili wa biashara ya kaboni ifikapo Juni 2028.	Kuwekeza katika teknolojia za kisasa, zenye uwazi na zinazotoa taarifa kwa wakati mfano setilaiti ili kuboresha ujumuishaji wa mfumo imara wa kitaifa wa kidijitali wa upimaji, utoaji taarifa na uthibitishaji ifikapo 2038.
	Kuanzisha vivutio na mifumo ya kifedha (mfano: punguzo la kodi, hati fungani za kijani) ili kuvutia wawekezaji wa ndani na jamii kushiriki katika miradi ya biashara ya kaboni ifikapo 2028.
	Kuwezesha uundaji wa vyama vya ushirika na mashirika ya kijamii ili kushiriki kwa pamoja katika miradi ya biashara ya kaboni na na kusimamia manufaa yake ifikapo 2028.
Angalau miradi ya biashara ya kaboni ya kiwango cha juu 15- 20 iwe imethibitishwa na kuanza kufanya kazi ifikapo Juni 2028.	Kufanya tathmini ya kitaifa ya awali ili kutambua miradi iliyopo na kutenga maeneo ya misitu yenye sifa ya kutumika katika biashara ya kaboni ifikapo 2028.
	Kuiwezesha na kuithibitisha miradi ya biashara ya kaboni katika sekta za kipaumblele (katika misitu, bahari, nishati jadidifu, usimamizi wa taka na kilimo endellevu) ili kufikia lengo la kuwa na miradi 15-20 inayofanya kazi ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha ustawi wa biashara za kaboni zilizosajiriwa ndani ya nchi na kikanda ili kujenga msingi wa kulifikia soko la kimataifa ifikapo Juni 2028.
Angalau asilimia 15 ya miradi ya kaboni iwe imeshirikisha/jumuisha jamii ifikapo Juni 2028.	Kutekeleza programu za kujenga uwezo na ushiriki katika biashara ya kaboni katika ngazi ya jamii, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, wawekezeji katika biashara ya kaboni ifikapo 2028.
	Kuanzisha na kufanya majaribio ya vituo vya biashara ya kaboni katika ngazi ya serikali za mitaa katika Halmashauri 2-5 ili kuwezesha miradi inayoongozwa na jamii ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kutoa motisha (ikiwemo za kikodi, hatifungani za kijani mapumziko ya kodi, dhamana ya kijani, fedha zinazozunguka) ili kuvutia wawekezaji wa ndani na jumuiya kushiriki katika miradi ya biashara ya kaboni ifikapo 2028.
	Kusaidia uanzishwaji wa vyama vya ushirika vya kijamii kushiriki katika miradi ya biashara ya kaboni ifikapo Juni 2028.
3.5.7. Kuimarisha Manufaa ya Uchumi wa Buluu	
Lengo la 1: Kutumia rasilimali za bahari na maji baridi kwa njia endelevu ili kuchochea ukuaji jumuishi wa uchumi, kuzalisha ajira, kulinda mazingira na kuboresha maisha, pamoja na kuchochea ubunifu na kuimarisha usimamizi.	
Kuongezeka kwa mchango wa uvuvi na ufugaji samaki katika Pato la Taifa kufikia asilimia 3.5 ifikapo 2028.	Kuanzisha maeneo makubwa ya ufugaji samaki yenye vituo vya kuzalisha vifaranga, viwanda vya chakula cha samaki pamoja na miundombinu ya uchakataji ili kuongeza uzalishaji na uongezaji thamani ya samaki ifikapo Juni 2028.
	Kuwekeza katika mtandao wa usafirishaji na uhifadhi wa bidhaa zinazoharibika na kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa kidijitali ili kupunguza upotevu baada ya mavuno na kulinda ubora wa kukidhi viwango katika masoko ya kimataifa ifikapo Juni 2028.
	Kutoa mikopo nafuu na ruzuku kwa wavuvi na wafanyabiashara wadogo na wa kati ili kuwawezesha kutumia vifaa vya kisasa, mbinu endelevu na kuwekeza katika uongezaji thamani ifikapo Juni 2028.
	Kusimamia na kutekeleza viwango vya uvunaji vinavyozingatia tafiti za kisayansi na kulinda maeneo muhimu ya kuzaliana samaki ili kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu wa sekta kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuwekeza katika viwanda vikubwa vya uzalishaji wa chakula cha samaki ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha maeneo makubwa ya ufugaji samaki yenye vituo vya kuzalisha vifaranga, viwanda vya chakula cha samaki pamoja na miundombinu ya uchakataji ili kuongeza uzalishaji na uongezaji thamani ya Samaki ifikapo Juni 2028.
	Kuongeza miundombinu ya usafirishaji na kuhifadhia bidhaa za uvuvi zinazoharibika ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
3.6. Vichocheo vya Kusukuma Maendeleo	
3.6.1 Nishati Itakayowezesha Ukuaji wa Uchumi wa Viwanda	
Lengo 1: Sekta ya nishati inaongozwa kisasa, kwa uwazi na ufanisi, sanjari na kuwa na wataalamu wenye ujuzi kuweza kutoa huduma za kuaminika, bunifu na endelevu	
Nguvukazi watu yenye wataalamu wa nishati angalau 10,000 kitaifa walio na ithibati kufikia Juni 2028.	Kuandaa Mpango Jumuishi wa Kitaifa wa Maendeleo ya Ujuzi katika Sekta ya Nishati ifikapo Juni 2028.
	Kutekeleza Mkakati wa Mpango Jumuishi wa Kitaifa wa Maendeleo ya Ujuzi katika Sekta ya Nishati ifikapo Juni 2028.
Kuhakikisha kuwepo kwa uwazi, ufanisi na uwajibikaji katika uendeshaji wa sekta ya nishati nchini kufikia Juni	Kuimarisha mifumo ya udhibiti na urekebu katika usimamizi madhubuti na ufanisi wa sekta ya nishati ifikapo 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
2028.	Kuandaa kanuni wazi na zenye nguvu ya kisheria katika usimamizi wa Mashirika na makampuni ya umma katika uendeshaji wa sekta ya nishati sanjari kuwea masharti kwa kutoa taarifa za fedha na utekelezaji ifikapo 2028.
Lengo 2: Tanzania iwe imefanyia marekebisho sekta yake ya nishati kuwa ya ushindani, uwazi na uendelevu wa kifedha, ikiwa ni pamoja na kubadilishwa kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuwa kampuni ya kibiashara na shughuli zake kutenganishwa katika vitengo vitatu vya uzalishaji, usafirishaji na usambaji wa umeme zinavyofanya kazi kwa kujitegemea na kuendeshwa kwa taratibu zinazo zingatia utendaji utakaowezesha ushindani na ushiriki wazi wa sekta binafsi na utoaji wa huduma za uhakika.	
Shirika la Umeme Tanzania kuwa imebadilishwa kuwa kampuni tatu za kibiashara zinazojitegemea za Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji wa umeme ifikapo Juni 2028.	3.1 Kufanyika kwa maboresho ya muundo wa taasisi na kifedha kupitia mkaguzi huru, kuboresha mpango kazi na kuhuisha kanuni za uendeshaji kuendana na matakwa ya sheria Ifikapo Juni 2028.
	3.2 Kutenganisha miundo ya uhasibu na usimamizi katika shughuli za uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ifikapo Juni 2028.
	3.3 Kutunga sheria na nyenzo za udhibiti ili kuifungua sekta kuruhusu ushiriki wa sekta binafsi katika taasisi za Uzalishaji na Usambazaji, na kuligawa Shirika la Umeme Tanzania ili kuanzisha mashirika ya umma yanayojitegemea katika Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji ifikapo Juni 2028.
	3.4 Kuanzishwa kwa mfumo wa bei za umeme zinazoakisi gharama halisi (cost-reflective tariffs) na uwazi ili kupunguza ruzuku na kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi.
	3.5 Kuanzishwa kwa mikataba ya udhibiti na usimamizi wa utendaji (performance-based regulation and management contracts) ili kuboresha ufanisi, kupunguza hasara, na kuimarisha utoaji wa huduma.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
4. Kuanzisha mfumo huru, unaogharamiwa kikamilifu na kufanya kazi kwa mamlaka kamili katika kuratibu usambazaji na kuruhusu wasambazaji wengine na kukuza ufanisi wa soko la ratibu umeme ifikapo Juni 2028.	4.1 Kuandaliwa kwa mwongozo wa udhibiti na urekebu, na uendeshaji wa soko huru la umeme kwa kushirikiana na EWURA na wadau wa sekta wa nishati wa sekta binafsi na umma ifikapo 2028.
	4.2 Kuitambua na kuiwezesha EWURA, kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Mipango, kuwa inaandaa na kuratibu utekelezaji Mpango wa Taifa wa nishati ya umeme ifikapo mwaka 2028.
	4.3 Kukusanya fedha, misaada ya kitaalam na ujenzi wa uwezo wa kitaasisi unaohitajika kuanzisha msimamizi wa soko huru la nishati ya umeme pamoja na utayari wa uendeshaji wake kila mwaka.
	4.4 Kuwezesha muundo wa Soko Huru la Umeme wenye mamlaka kamili ya upangaji, usawa na, kanuni wazi za upatikanaji, na uratibu wa soko la ushindani kati ya wazalishaji wa umma na binafsi ifikapo Juni 2028.
Lengo la 3: Tanzania kuwa na miundombinu ya nishati thabiti, unganishi na iliyo tayari kwa uwekezaji ambayo inawezesha upatikanaji wa uhakika wa nishati ya umeme kwa matumizi ya ndani, biashara ya umeme na nchi jirani, na iliyojengwa kwa ubia endelevu kati ya sekta za umma na binafsi pamoja na inakua na sekta ya nishati yenye utumia mitaji itokanayo na mipango ya hifadhi za mazingira.	
5. Angalau njia moja ya msongo wa kV 400 ijengwe sanjari na kuimarishwa kwa mtandao mkuu wa usafirishaji wa umeme ili kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini na uendeshaji wa biashara ya umeme kikanda ifikapo Juni 2028.	5.1 Kujengwa kwa kiunganishi kimoja (1) mpakani cha msongo wa 400kV inayounganisha Tanzania na nchi za Zambia, Uganda na Kenya ili kuimarisha ubadilishanaji thabiti wa umeme kikanda ifikapo Juni 2028.
	5.2 Kutumia mifumo ya SCADA na teknolojia za kisasa katika gridi na angalau asilimia 90 ya vituo vya udhibiti kikanda ifikapo 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	5.3 kusasisha gridi ya taifa ya usafirishaji wa umeme katika vishoroba zilizopewa vya kipaumbele kwa kiwango cha 400kV kuhakikisha utayari wa kupokea na kusafirisha umeme wenye uwezo mkubwa kwa matumizi ya kwa biashara kikanda ifikapo Juni 2028.
	5.4 Kuwianisha kanuni na taratibu za uendeshaji wa gridi umeme nchini na zile za umeme wa pamoja kwa nchi za ukanda wa Kusini na Mashariki Mashariki (SAPP na EAPP) mtawalia, angalau kwa asilimia 70 kufikia Juni, 2028.
6 Angalau kiasi cha Dola za Marekani bilioni 7 ziwe zimekusanywa kutoka vyanzo vya mikopo ya masharti nafuu na hatifungani za mazingira kwa ajili ya kufadhili uzalishaji na usafirishaji wa nishati safi ya umeme nchini ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha na kutumika Mfumo wa ufadhili wa nishati safi ya kupikia - kufikia Juni, 2028.
	Kuanzishwa kwa mwongozo wa mfumo wa ufadhili wa nishati safi ya kupikia ifikapo Juni, 2028.
	Kuanzisha ushirikiano na Benki za Maendeleo za Kimataifa na mifuko yaufadhili ya mabadiliko ya tabianchi ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa mfumo wa kitaifa wa upangaji wa miradi ya kipaumbele inayozingatia mabadiliko ya tabia nchi ifikapo Juni 2028.
Lengo 4: Kuongeza a uwezo wa uzalishaji umeme nchini Tanzania kufikia MW 8,000 ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadae, kuimarisha ujenzi wa sekta ya viwanda na kuhakikisha upatikanaji wa nishati kwa wote ifikapo 2031	
7. Wastani wa matumizi ya nishati ya umeme kwa mtu kuongezeka kufikia 600 kWh ifikapo Juni 2028.	7.1. Kuharakisha utekelezaji wa miradi mikubwa ya uzalishaji wa nishati safi ya umeme (wa maji, jua, upepo, jotoardhi, gesi na nyuklia) ifikapo Juni 2028.
	7.2 Kuandaa mpango kabambe jumuishi wa upanuzi wa uzalishaji wa umeme ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	7.3. Kutumia ruzuku kwa uunganishaji wa umeme katika kaya na teknolojia za nje ya gridi ifikapo Juni 2031.
8. Uwezo wa uzalishaji wa nishati safi nchini kuongezeka kufikia MW 8,000 ifikapo Juni 2028.	8.1 Kuzindua kwa awamu mitambo mikubwa ya uzalishaji wa umeme wa maji, jua, upepo na jotoardhi kwa awamu ifikapo Juni 2028.
	8.2 Kuandaliwa na kuanza ujenzi wa mtambowa uzalishaji wa umeme wa nyuklia wa uwezo wa MW 1,000 kwa majaribio e ifikapo Juni 2028.
	8.3. Kuandaa na kutekeleza mifumo ya vivutio na minada ya ushindani kwa wazalishaji binafsi wa umeme (IPPs) ifikapo Juni 2028.
Lengo 5: Kuongeza kiwango cha nishati jadidifu katika mseto wa nishati ya umeme angalau kufikia asilimia 50, kuweza kupunguza uzalishaji wa hewaukaa na kuimarisha ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi.	
9. Uwezo wa kuzalisha MW 1,700 umeme wa jotoardhi, MW 500 za umeme wa upepo, na MW 715 za umeme jua ifikapo Juni 2028.	9.1 Kuharakisha utoaji wa leseni za nishati jadidifu (RE) na taratibu za vibali vya mazingira kwa kurahisisha hatua za udhibiti, kuweka muda maalumu wa utekelezaji na kuimarisha uratibu wa kitaasisi ifikapo Juni 2028.
	Kufanyika kwa mapitio na kufungamanisha mifumo ya udhibiti ya nishati jadidifu ifikapo Juni 2028.
10. Angalau asilimia arobaini ya uzalishaji wa umeme itokane na vyanzo vya nishati jadidifu ifikapo Juni 2028.	10.1 Kuanzisha Kituo jumuishi cha pamoja cha Kutoa vibali vya Nishati Jadidifu ifikapo Juni 2028.
	Kuboresha miundombinu ya gridi (mifumo ya usimamizi na udhibiti wa gridi, teknolojia za kuongeza uthabiti wa mfumo wa umeme,mifumo ya uhifadhi wa betri, na miunganiko) ili kusaidia ujumuishaji wa asilimia 80 ya nishati jadidifu ifikapo Juni 2028.
Gridi ya Taifa iwe imefanyiwa matengenezo kuongezea uwezo wa kuweza kuchukua asilimia 80 ya nishati ya	Kuanzisha kanda za uzalishaji wa nishati jadidifu na vituo vya ubunifu ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
umeme mbadala inayotazamiwa kuzalishwa karibuni, ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha mnada wa ushindani wa nishati jadidifu na mifumo ya ufadhili ya hati fungani za kijani/ nishati safi ifikapo Juni 2028.
	11.3 Kuwezesha usambazaji wa MW 300 kutoka katika gridi ndogo za jamii za ifikapo Juni 2028.
	Kuweka rasmi wa kupanga ustahimilivu na uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na utyari wa hifadhi ya nishati ya jua ifikapo Juni 2028.
Lengo 6: Mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini Tanzania kuboreshwa ili kupunguza kiwango cha upotevu wa umeme kwa sababu za kiufundi na kibiashara kuwa angalau chini ya asilimia 5 pamoja na kuhakikisha uthabiti wa gridi	
Kupunguza upotevu wa umeme katika mfumo wa Taifa kutoka asilimia 14.2 hadi asilimia 12.4 ifikapo Juni 2028.	Kubadilishwa kwa angalau asilimia 70 ya transfoma zilizochakaa na kuboreshwa kwa kilomita 1,000 za njia kongwe za usambazaji wa umeme mijini kupunguza mzigo na hasara za kiufundi ifikapo Juni 2028.
	12.2 Kubadilisha transfoma zilizochakaa na kuboresha njia za umeme mijini ifikapo Juni 2028.
Kujenga vituo vidogo 100 vya kupooza umeme vijijini na mifumo ya gridi ya teknolojia za kisasa katika mikoa mikubwa ifikapo Juni 2028.	13.1 Kuwekeza katika gridi za umeme vijijini na miundombinu ya usambazaji bora ifikapo Juni 2028.
	13.2 Kuanzisha usimamizi na ratiba ya ukarabati wa gridi ya taifa kwa kutumia teknolojia ya kidijitali kufikia Juni 2028.
	13.3 Kutumia mita za teknolojia za kisasa kwa asilimia 100 kwa wateja wa kibiashara na wa kati ifikapo 2028.
	13.4 Kutumia nyaya za umeme za chini ya ardhi katika maeneo yenye msongamano mkubwa mijini ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	13.5 Kuongeza wigo wa ushiriki wa sekta binafsi katika usafirishaji na usambazaji wa umeme kupitia Makampuni Huru kwenye kanda za viwanda ifikapo Juni 2031.
Lengo Na. 7: Kaya nchini kupata umeme wa uhakika na gharama nafuu kwa asilimia 100	
Kuongeza wastani wa uunganishwaji wa umeme kwa kaya nchini kutoka asilimia 49 hadi asilimia 55.2 kitaifa na uunganishaji wa umeme vijijini kutoka asilimia 36 hadi asilimia 42.8 ifikapo Juni 2028.	Kutekeleza kampeni ya kitaifa ya uunganishaji wa umeme kwa kaya mpya milioni 4 ifikapo Juni 2028.
	Kufanya mapitio,kurahisisha taratibu na kupunguza gharama za uunganishaji wa umeme za uunganishaji kwa asilimia 50 kwa kaya za kipato cha chini ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha utaratibu wa kutoa vivutio vinavyozingatia ufanisi wa utendaji kwa wawekezaji binafsi wanaotoa huduma katika maeneo ya vijijini ifikapo Juni 2028.
Uhakika wa upatikanaji wa umeme kwa ngazi ya kaya uimarike kufikia angalau 80% ifikapo Juni 2028.	Kujenga vituo vidogo 100 vya kupooza umeme kwa maeneo ya vijijini pamoja na kuboresha transfoma za maeneo ya vijijini ifikapo Juni 2028.
	Kutumia gridi za na mifumo ya ufuatiliaji ya kisasa kwa angalau asilimia 80 katika ya maeneo ya vijijini ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha mikataba ya matengenezo kwa kigezo cha ufanisi wa utendaji kwa watoaji wa huduma za umeme katika maeneo ya vijijini ifikapo Juni 2028.
Lengo 8: Kuimarisha uhakika na uthabiti wa upatikanaji wa umeme nchini kwa kuwa na vyanzo mchanganyiko, vikijumuisha matumizi ya kimkakati ya mashapo yamakaa ya mawe na nishati jadidifu sanjari na matumizi ya teknolojia zenye uchafuzi mdogo wa hewa	

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Angalau mitambo yenye uwezo wa kuzalisha MW 1,000 za umeme wa makaa ya mawe yenye kuzingatia vigezo vya kimazingira ifikapo Juni 2028.	Kutambuliwa na kutengwa kwa maeneo yenye makaa ya mawe na kuharakisha utoaji wa leseni kwa ajili ya mitambo ya uzalishaji wa umeme wa makaa ya mawe wa MW 3,000 ifikapo Juni 2028.
	Kuhamasisha ubia kati ya sekta za umma na binafsi na kuweka mfumo wa dhamana kwa uwekezaji katika matumizi ya teknolojia safi za makaa ya mawe, ikijumuisha mifumo ya kupunguza salfa katika gesi na teknolojia za kunasa hewa ukaa ifikapo Juni 2028.
	Kuanzishwa kwa mwongozo wa Mfumo Endelevu wa Uzalishaji Umeme unaotokana na Makaa ya Mawe utakaosimamia uibuaji wa miradi na ufuatiliaji wa mazingira ifikapo Juni 2028.
Kuwa na utaratibu wa kudumu wa ziada ya umeme wa kiwango cha asilimia 20 ifikapo Juni 2028.	Kuongeza uunganishaji wa umeme wa gridi kufikia MW 1,500 kupitia gesi, umeme wa maji na mifumo ya nishati jadidifu kufikia Juni 2028.
	Kuanzishwa kwa Sera ya Kimkakati ya Nishati ya Akiba yenye sharti la kuwa na akiba isiyopungua ziada asilimia 20 ya umeme ifikapo 2028.
	Kutekelezwa kwa mfumo wa maoteo wa wakati halisi wa mahitaji na upatikanaji wa nishati ili kuimarisha usimamizi wa akiba ifikapo Juni 2028.
3.6.2. Usafirishaji na biashara ya uchukuzi fungamanishi kufikia masoko ya kimataifa	
Lengo 1: Ufanisi na ufungamanishi wa miundombinu ya usafirishaji na biashara ya uchukuzi kuimarishwa kwa kuboresha usafirishaji wa watu, bidhaa na rasilimali mijini na mikoani ili kuchochea ukuaji endelevu, , maendeleo ya uchumi viwanda, na kuboresha upatikanaji wa masoko ya kimataifa	
Miundombinu ya Barabara	

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Kuwa na mfumo jumuishi, endelevu na barabara zenye teknolojia ya kisasa nchini ifikapo Juni 2028.	Kuanza usanifu wa barabara zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi na kwa zana za kidijitali (akili unde na mifumo ya taarifa za kijiografia) kwa ajili ya kupanga ukarabati wa barabara, taa za barabarani zinazoendeshwa kwa nishati ya jua, na mifumo ya kisasa ya kuongoza vyombo vya usafiri barabarani ifikapo Juni 2028.
	Kutumia mifumo ya teknolojia mahiri ya barabara, ikiwemo mitambo ya kufuatilia mwenendo wa usalama wa barabarani wa wakati, utozaji wa malipo ya matumizi ya njia za kidijitali, mizani ya kidijitali, na udhibiti wa uzito ifikapo Juni 2028.
	Kutengeneza ramani kidijitali za barabara za vijijini ambazo hazijaanishwa na kuzingiza katika ramani ya dunia na zana huria ili kusaidia upangaji, matengenezo na kukabiliana na matukio ya dharura ifikapo Juni 2028.
	Kuwekeza katika miundombinu ya mijini ili kupunguza msongamano wa magari katika miji mikuu ikiwemo Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Mbeya na Mwanza na kurahisisha usafiri na uchukuzi mijini ifikapo Juni, 2028.
Kuongeza kiwango cha barabara za lami kutoka asilimia 8.6 hadi 10.58 ifikapo Juni 2028.	Kujenga, kukarabati na kufanyia matengenezo barabara za mikoa na vijijini zinazoiunganisha kanda za kilimo, madini na viwanda na masoko kufikia Juni 2028.
	Kupanua mtandao wa barabara za kisasa na mifumo ya Usafiri wa Mabasi yaendayo Haraka (BRT) katika miji mikuu ifikapo Juni 2028.
	Kuendeleza barabara zinazoiunganisha Tanzania na nchi jirani za Jumuiya ya Afrika Mashariki Na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ili kukuza biashara ya kikanda ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kujenga barabara mpya za mwendokasi zinazounganisha miji mikubwa na vituo vya kiuchumi, zikiwa viwango vya juu vya usanifu ifikapo Juni 2031.
	Kusanifu na kujenga madaraja ya kisasa kuwezesha kuvuka mito mikubwa, kuimarisha uthabiti wa barabara na kuwa utambulisho wa kikanda ifikapo Juni 2031
	Kupanga na kujenga kwa majaribio ya barabara za magari ya umeme zikiwana vituo vya kuchajishia magari ya mizigo na abiria katika njia zenye misongamano mikubwa ifikapo Juni 2031
Kufikia asilimia 35 ya kiwango cha matengenezo ya barabara ifikapo Juni 2028.	Kuimarisha mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji wa miundombinu na rasilimali za barabara, ikijumuisha mifumo ya utunzaji wa taarifa kwa teknolojia za GIS na za taarifa utekelezaji mwaka za miundombinu kuweza kujua maendeleo na athari zake ifikapo Juni 2028.
	Kuongeza bajeti ya matengenezo ya barabara na kubuni vyanzo vipya vya kugharamia ifikapo Juni 2028.
	Kutenga ardhi kwa ajili ya njia na kujenga mabomba chini ya ardhi kwa upitishaji wa maji, umeme, intaneti na maji- taka mijini kuweza kupunguza uchimbaji na uharibifu wa miundombinu mara kwa mara ifikapo Juni 2028.
Usafiri wa Anga	
Farihisi ya Muunganiko wa Usafiri wa Anga kuongezeka kutoka asilimia 0.35 mwaka 2025 hadi asilimia 0.85 ifikapo Juni 2028.	Kuongeza uwezo wa majengo ya abiria, maegesho ya ndege, njia za kuruka na kutua ndege, na miundombinu ya usafirishaji wa katika viwanja vikuu vya kimataifa ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kukarabati na kupanua uwezo wa viwanja vidogo vya ndege katika mikoa ya Mbeya, Dodoma, Tabora, Kigoma, Mtwara, Musoma, na Shinyanga ifikapo Juni 2028. Kuanzisha majengo mahsusi kwa usafirishaji wa mizigi katika viwanja vya ndege vya Mbeya, Dodoma, Tabora, Kigoma, Mtwara, Musoma na Shinyanga.
	Kuweka mifumo ya rada za ufuatiliaji wa mwenendo wa ndege na kusambaza satelaiti katika anga la Tanzania ifikapo Juni 2028.
	Kuwianisha taratibu za utoaji wa leseni, usalama wa anga na wa nchi jirani kuwezesha usafiri wa kikanda kufanyika bila vikwazo na kuwa na anga huru ifikapo 2028.
	Kujenga kituo cha kitaifa cha mafunzo ya usafiri wa anga kwa ushirikiano na wadau wa kimataifa ili kuzalisha marubani, wahandisi, waongozaji ndege, wahudumu na huduma za droni.
	Kutumia mifumo ya Kieletroniki ya kuhakiki taarifa kwa kutumia alama za vidole katika milango ya kusafiria, viza na uthibitisho wa kiafya ili kuboresha usalama, kasi na ufanisi wa huduma za abiria ifikapo 2028.
	Kutumia mifumo ya Kieletroniki ya kuhakiki taarifa kwa kutumia alama za vidole katika milango ya kusafiriia, viza na uthibitisho wa kiafya ili kuboresha usalama, kasi na ufanisi wa huduma za abiria 203 ifikapo Juni 2028.
	Kununua ndege za Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na kuboresha mindombinu wezeshi ya utoaji wa huduma ya usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo.
Usafiri wa reli	

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Kuongeza eneo lenye mtandao wa reli kutoka kilomita 4.97 kwa eneo mraba la kilomita 1,000 kufikia kilomita 7.98 ifikapo Juni 2028.	Kukamilisha ujenzi wa reli za mizigo na abiria kwa kiwango cha reli ya kimataifa kuunganisha Dar es Salaam–Dodoma–Mwanza, Isaka–Kigali (Rwanda), Tabora–Kigoma, Uvinza Musongati (Burundi) – Uvira (DRC), Tabora–Mpanda–Karema na Mtwara–Mbambabay–Mchuchuma–Liganga (shoroba ya kusini) ifikapo Juni 2028.
	Kukarabati reli ya upana wa mita ikiwemo maunganisho, hasa ya Dar–Tanga–Arusha ifikapo Juni 2028.
	Kujenga njia mahsusi za reli kutoka njia kuu kufikia maeneo ya migodi (mf. Liganga, Mchuchuma) na maeneo ya viwanda (mf. Bagamoyo, Kisarawe, Mlandizi) ifikapo Juni 2028.
	Kuwianisha huduma za reli na meli katika maziwa makuu (Victoria, Tanganyika, Nyasa) kati ya bandari na njia za reli ifikapo Juni 2028.
	Kujenga au kuboresha maghala na vituo vya mizigo katika vituo vikubwa vya reli, kama Tabora, Mwanza na Kigoma ifikapo Juni 2028.
	Kuboresha miundombinu chakavu (reli, nguzo, mawe) kutoka Dar es Salaam hadi New Kapiri Mposhi ifikapo Juni 2028.
	Kufanyia maboresho sheria na taratibu za uwekezaji Shirika la Reli ya Tanzania na Zambia kuruhusu ushiriki wa waendeshaji binafsi, wakodishaji na wabia wa usafirishaji na biashara ya uchukuzi ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha au kupanua bandari kavu katika shoroba wa usafirishaji na uchukuzi katika miji ya Mbeya, Tunduma na Mpika (Zambia) ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Msongamano wa abiria katika miji mikubwa kupungua kwa asilimia 40 ifikapo Juni 2028.	Kukamilisha, kwa awamu, ujenzi wa reli za abiria za umeme mijini zinazounganisha vitongoji vikuu na maeneo ya kibiashara.
	Kujenga miundombinu unganishi ya usafiri mijini, ikiunganisha ainambalimbali za usafiri vituo vya reli, mabasi ya mwendokasi, mabasi ya mikoani na vituo vya mizigo ifikapo Juni 2028.
	Kuanza utekelezaji wa mfumo wa kidijitali wa tiketi na mnyororo wa usafiri unaounganisha reli, BRT, mabasi ya jiji na huduma za usafirishaji wa mizigo ifikapo Juni 2028.
	Kuwekeza kwenye mabehewa ya umeme na miundombinu ya bora ya nishati kukuza uendeshaji wa reli za zilizo rafiki kwa mazingira na zenye utoaji mdogo wa hewa chafu ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha mfumo fungamanishi wa reli ya abiria Jijini Dar es Salaam kama mradi wa kielelezo ili kupunguza msongamano kwa angalau asilimia 40 na kuboresha muunganiko wa usafiri kupitia vituo vya usafiri wa aina mbalimbali ifikapo Juni 2028.
	Kujenga mifumo ya kisasa ya reli ya abiria katika Mikoa ya Arusha, Mwanza na Dodoma, ikijumuishwa na mitandao ya usafiri wa ndani na miundo mbinu inayolenga usafiri wa umma ifikapo Juni 2028.
	Imarisha mafunzo ya kitaifa ya reli na usafirishaji, yakiwemo mafunzo ya ufundi stadi na uthibitishaji wa lazima kwa wahandisi wa reli, waendeshaji wa mabehewa na mitambo ya reli, wahudumu wa treni, na mameneja wa usimamizi wa usafirishaji ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kushirikiana na waendelezaji wa reli za mijini wa kimataifa kutoka kampuni za kimataifa za (CRRC, Alstom, Siemens Mobility) kwa uhaulishaji wa teknolojia na utekelezaji kufikia Juni 2028.
Usafiri wa Maji	
Kuongeza ujazi wa miundombinu ya usafiri wa maji kutoka km 3.2 kwa kila kilomita za mraba 1,000 kufikia ujazi wa kilomita 4.36 kwa kila kilomita za mraba 1,000 ifikapo Juni 2028.	Kujenga Bandari ya Kina Kirefu ya Bagamoyo kama lango la kimataifa la kimkakati ifikapo Juni 2028.
	Kukarabati na kuboresha bandari za mwambao wa bahari ya hindi na maziwa makubwa (Mwanza, Bukoba, Musoma, Kigoma, Kasanga, Itungi, Liuli, Mbamba Bay) ikiwa na vifaa vya kisasa vya mizigo, abiria na vifaa vya kuhifadhi baridi kufikia Juni 2028.
	Kujenga maeneo maalum ya kiuchumi (SEZs) na viwanda vinavyotumia bandari katika Mwanza, Kigoma, Mtwara, Mbeya, Kilwa na Bagamoyo. Kuchochea ubiasharishaji unaoongozwa na mauzo ya nje ifikapo 2028.
	Kutumia mifumo ya kidijitali katika shughuli zote za bandari—tiketi, mizigo, forodha na ufuatiliaji wa meli ifikapo Juni 2028.
	Kuhuisha na kuratibu kanuni za uongozaji ili kuhakikisha uwiano wa utoaji wa leseni za vyombo vya usafirishaji, utozaji wa tozo na taratibu za ukaguzi kwa mujibu wa viwango vya EAC, SADC na COMESA ifikapo Juni 2028.
	Kuendeleza vituo vya usafirishaji vyenye mifumo mchanganyiko vya bandari kavu zilizounganishwa na bandari kuu na maziwa, ili kuboresha muda wa mzunguko wa mizigo na kuimarisha minyororo ya thamani ya kikanda.ifikapo Juni 2028

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kusimika mifumo ya ufuatiliaji wa hali ya hewa kwa wakati halisi, rada na mifumo ya usalama inayotegemea satelaiti katika maziwa na maeneo ya ukanda wa pwani ifikapo 2028.
	Kujenga vituo bora vya mafunzo ya usafiri wa majini na usafirishaji vyenye uthibitisho wa lazima kwa marubani wa meli, wahandisi, mafundi mitambo na wafanyakazi wa gati ifikapo Juni 2028.
	Kujenga na kukarabati meli katika Maziwa Makuu na Bahari kwa ajili ya kurahisisha usafiri na usafirishaji kwa njia ya maji.
Mabomba ya Mafuta	
Kuongeza mtandao wa mabomba kutoka km 1,500 hadi angalau km 2,200 ifikapo Juni 2028.	Kukamilisha ujenzi na kuanza uendeshaji wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Uganda hadi Bandari ya Tanga, ili kuiweka Tanzania kama njia kuu ya usafirishaji wa mafuta ghafi Afrika Mashariki na kuchochea shughuli za kiuchumi katika ukanda wa mradi ifikapo Juni 2028.
	Kuboresha na kuongeza mtandao wa bomba la gesi asilia uliopo kutoka Mtwara na Songo Songo hadi vituo muhimu vya mijini (k.m. Dodoma, Mwanza, Arusha, Mbeya) na maeneo ya viwanda na Maeneo ya Maalum ya uwekezaji (SEZ) ili kuwezesha upatikanaji wa gesi kwa gharama nafuu kwa ajili ya uzalishaji wa umeme, viwanda na usafiri ifikapo Juni 2028.
	Kujenga mabomba ya bidhaa mbalimbali kutoka bandari za pwani (Dar es Salaam, Tanga, Mtwara) hadi kwenye bohari za nchi kavu (Dodoma, Mwanza, Kigoma) ili kupunguza utegemezi wa meli za barabarani, kuboresha usalama na kupunguza gharama za usafiri ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kujenga mifumo ya kuweka gesi katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha na Morogoro kwa ajili ya gesi ya kupikia majumbani, taasisi za umma na mabasi ya mijini na viwanda vidogo ifikapo Juni 2028.
	Kusimika mabomba ya gesi katika SEZ na IDZ zilizopangwa (k.m. Bagamoyo, Mtwara, Kibaha) ili kuboresha urahisi wa kufanya biashara na kuvutia wawekezaji wa viwanda ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha maabara ya kisasa kwa ajili ya kupima vifaa vya bomba, vali na mita za kupimia maji jijini Dar es Salaam au Dodoma ili kuhakikisha udhibiti wa ubora, viwango vya usalama na kusaidia wazalishaji wa ndani ifikapo Juni 2028.
Sayansi, Teknolojia na Ubunifu	
Tanzania kuwa kinara wa kikanda katika sayansi, teknolojia na ubunifu ifikapo 2028.	Kutoa ufadhili endelevu kwa Utafiti na Maendeleo, ubunifu na biashara ya teknolojia kila mwaka.
	Kuanzisha mwongozo endelevu wa kitaifa wa ugharamiaji wa muda mrefu wa utafiti na maendeleo, ubunifu na biashara ya teknolojia ifikapo Juni 2028.
	Kulinda na kuendeleza ubunifu wa ndani kupitia mfumo imara wa haki miliki (IP) ifikapo Juni 2028.
	Kujumuisha masuala ya Sayansi, Teknolojia, Hisabati na Uhandisi na umahiri wa kidijitali katika ngazi zote za elimu na kuboresha elimu ya ufundi stadi (TVET) ujifunzaji wa muda mrefu, ili kujenga nguvu kazi iliyo tayari kwa ubunifu ifikapo Juni 2028.
	Kuwezesha nguvu kazi ujuzi wa juu wa Kidijitali kwaa ajili ya kusaidia ubunifu katika sekta zote kila mwaka

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuboresha upatikanaji wa takwimu za utafiti na ushirikiano wa kitaasisi kila mwaka
	Kusaidia Utafiti na Maendeleo katika nishati jadidifu, bioteknolojia, kilimo na uendelezaji taka kila mwaka.
	Kukuza mifumo ya ikolojia ya ubunifu kwa vijana katika ngazi zote ilikuongeza wigo wa ushirikishwaji na kujenga uwezo wa ubunifu kuanzia ngazi ya chini kwenda juu kila mwaka.
Angalau asilimia 10 ya Pato la Taifa kuchangiwa na sayansi, teknolojia na ubunifu ifikapo 2028.	Tumia mitandao ya maarifa ya kimataifa kwa ajili ya ugharamiaji, uhawilishaji wa teknolojia, na ushirikiano wa utafiti wa kimataifa kila mwaka.
	Kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma ya intaneti ya kasi ya juu yenye gharama nafuu ili kusaidia ubunifu wa kidijitali na uchumi wa kidijitali kufikia ifikapo 2028.
	Kusimamia upitishaji na upanuzi wa AI, blockchain, IoT na bioteknolojia katika sekta za kipaumbele (kilimo, afya, nishati, viwanda) ifikapo Juni 2028.
	Kuongeza wigo wa maeneo ya utafiti katika tafiti kama vile tafiti za kilimo kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi, nishati mbadala, bioteknolojia na teknolojia za afya ifikapo Juni 2028.
	Kuendeleza vituo maalumu vya utafiti, ubunifu na ujasiriamali vinavyolenga sekta za kiuchumi zenye athari kubwa kufikia Juni 2028.
	Kukuza iteknolojia za ndani ya nchi ili kuimarisha ushindani wa Tanzania na nafasi yake ya kuuza nje katika masoko ya kiteknolojia ya kikanda na kimataifa kufikia ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kutumia teknolojia zinazoibuka (AI, otomatiki, roboti, IoT) kuendesha ubiasharishaji, tija na uzalishaji na ongezeko la thamani kila mwaka.
	Kujenga miji ya kisasa na maeneo ya ubunifu (smart cities) wa kiteknolojia kwa ajili ya kufanya majaribio, kupanua wigo na kubiasharisha biashara ya teknolojia kwa kizazi kijacho ifikapo Juni 2028.
	Tumia takwimu, Akili unde na ujifunzaji wa mashine kuongeza tija na kuanzisha fursa mpya za kiuchumi katika sekta za kimkakati kila mwaka
	Kusaidia ubunifu wa teknolojia ya kijani na uendelevu ili kuifanya Tanzania kuwa kinara kikanda katika nishati safi, usimamizi wa taka na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi kwa mwaka. Kuanzisha teknolojia ya mnyororo wa thamani wa ugavi inayowezesha kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa ndani katika sekta kama vile kilimo, viwanda na nishati kila mwaka.
3.6.4. Mfumo wa utafiti na maendeleo	
Lengo la 1: Kuanzishwa kwa Mfumo endelevu wa utafiti na maendeleo unaoendeshwa kidijitali, unaoendesha ushindani wa kimataifa na kuleta maboresho yanayoweza kupimika katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika sekta muhimu ifikapo 2050	
Vijana milioni 1 kuwa na ujuzi wa Akili Unde na ujuzi wa juu wa kidijitali ifikapo 2028.	Kuandaa na Mkakati Wa kiTaifa Wa Ujuzi Wa Akili Unde (AI) ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha mpango maalum wa kukuza ujuzi wa baadaye (Tanzania Future Skills Accelerator (TFSA) ifikapo Juni 2028.
	Kujumuisha masomo ya coding, roboti na umahiri wa kidijitali katika mfumo wa elimu ya msingi ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuziwezesha shule na vituo vya ufundi na ufundi stadi – TVET kupata maabara za Akili Unde.
	Kuingia ubia na makampuni ya kimataifa ya Akili Unde kwa ajili ya kutoa mafunzo yenye ithibati na vyeti.
Kuongeza uwekezaji katika utafiti na maendeleo (R&D) kutoka asilimia 0.56 hadi angalau asilimia 0.8 ya Pato la Taifa ifikapo 2028.	Kuandaa na Mkakati wa Kitaifa wa Ujuzi Wa utafiti na maendeleo chini ya COSTECH ifikapo Juni 2028.
	Kutunga Sheria ya ugharamiaji wa utafiti na ubunifu (Research and Innovation Finance Act) ili kuhakikisha kuwa na bajeti endelevu za Utafiti na Maendeleo ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha Mfuko wa Uhawilishaji Teknolojia kwa Makampuni yanayoibukia (startups) na vyuo vikuu ifikapo Juni 2028
	Kuweka vivutio vya kodi (tax incentives) kwa shughuli za Utafiti na Maendeleo ili kuongeza uwekezaji wa sekta binafsi ifikapo Juni 2028.
	Kuwezesha angalau asilimia 50 ya SMEs kutumia teknolojia za viwanda 4.0 ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha kanda nne za teknolojia (tech parks) katika miji ya Dodoma, Mwanza, Arusha na Mbeya ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha maabara za kitaifa za Akili Unde (AI) na Kituo cha Super computing ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa Mwongozo wa kitaifa wa Akili Unde na miundombinu ya supercomputing
	Kuandaa Mkakati wa kitaifa wenye dhamana ya serikali wa ugharamiaji wa tafiti kwa sekta za kipaumbele ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Kuongeza idadi ya vituo vya ubunifu kutoka 5 vya sasa kufikia angalau 10 ifikapo Juni 2028.	Kuimarisha Sera ya Taifa ya Ubunifu (National Innovation Policy) ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha Kituo cha Ubunifu wa Akili Unde na Mnemba jijini Uchambuzi Mpana wa Takwimu Dar es Salaam ifikapo Juni 2029
	Kujenga angalau vituo vitatu vya sayansi na teknolojia katika kanda ifikapo Juni 2028.
	Kuweka mfumo rasmi wa maabara za maarifa asilia (Indigenous Knowledge Labs) ifikapo Juni 2028.
	Kujumuisha program za kukuza na kulea ubunifu katika vyuo vikuu vyote nchini ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha vituo atamizi vya utafiti na maendeleo katika vituo vyote vya ubunifu zote ili kusaidia startups za utafiti.
Asilimia 100 ya tafiti muhimu zinazohusiana na malengo ya kimkakati zinatumika ifikapo Juni 2028.	Kuandaa na kuzindua hazina ya kitaifa ya utafiti ya uwazi na inayofikika kufikia Juni 2028.
	Kuanzisha jukwaa la pamoja la sera na utafiti kati ya wizara ifikapo Juni 2031.
Kuanzisha Mwongozo wa Kitaifa wa Agenda ya Utafiti na kuhakikisha mipango ya taasisi zote inalingana ifikapo Juni 2028.	Kufufua Mwongozo wa kitaifa wa Uratibu wa tafiti pamoja na kanzidata ya kitaifa ya watafiti ifikapo Juni 2028.
	Kuhakikisha wizara zote zinaoanisha mipango yao ya utafiti ya agenda ya utafiti ya kitaifa ifikapo Juni 2028.
	Kutumia mifumo ya Akili unde ya ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa agenda ya utafiti ya kitaifa ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha Baraza la Taifa la Utafiti ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuunganisha taasisi zote za utafiti kwenye jukwaa la kidijitali la agenda ya utafiti ya kitaifa ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa mkakati wa ugharamiaji wa agenda ya utafiti ya kitaifa ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa utabiri wa hali ya hewa unaotumia Akili Unde ifikapo Juni 2028.
	Kuibadilisha TARI kuwa Taasisi Mahiri ya Utafiti wa Kilimo ifikapo Juni 2028.
	Oanisha teknolojia za kidijitali na zinazoibuka katika Sera ya Taifa ya Kilimo kufikia Juni 2028.
Ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika utafiti kuongezeka kwa asilimia 50 ifikapo 2028.	Kuandaa mwongozo wa ushirikiano wa kimataifa wa utafiti (International Research Cooperation Framework) ifikapo Juni 2028.
	Kutengeneza mfumo wa ushirikiano kati ya sekta binafsi na sekta ya umma katika utafiti wa kimataifa ifikapo Juni 2028.
Kuanzisha kwa hazina ya wazi ya kitaifa ya takwimu (National Open Data Repository - NODAR) na Mwongozo wa Maadili ya takwimu ifikapo 2028.	Kuanzisha Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa takwimu Data (National Data Governance Board).
	Kuanzisha kwa hazina ya wazi ya kitaifa ya takwimu (National Open Data Repository - NODAR) ifikapo Juni 2028
	Kutekeleza mwongozo wa maadili ya Akili Unde na usalama wa taarifa (AI Ethics and Data Protection Framework) ifikapo Juni 2028.
3.6.5. Kuwekeza katika Mfumo Ikolojia Unaotegemea Takwimu	

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Lengo 3: Kuanzishwa kwa mfumo imara wa ikolojia unaotegemea takwimu, wenye mifumo bora na jumuishi ya takwimu, ili kuimarisha utoaji wa maamuzi sahihi, ubunifu wa kidijitali na maendeleo jumuishi ya kijamii na kiuchumi ifikapo 2050.	
Asilimia 100 ya miongozo ya takwimu za ufuatiliaji na tathmini ya Dira 2050 na Mpango Elekezi 2050 ziwe zimewianishwa ifikapo Juni 2028.	Kuandaa na kupitisha mpango kazi wa Kitaifa wa Maendeleo ya Takwimu inayooanisha matokeo ya takwimu na malengo ya Dira 2050, ikijumuisha muda wa utekelezaji na mwongozo wa ufuatiliaji, ifikapo Juni 2028.
	Kufanya mapitio ya sheria ya Takwimu ili kuingiza mahitaji mapya ya takwimu pamoja na maboresho ya muundo wa usimamizi wa takwimu ifikapo Juni 2028.
	Kushirikiana na Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali (MDAs) na sekta binafsi zinafungamanisha Dira 2050, kuonanisha viashiria vinavyoendana na Dira 2050 katika mifumo yao ya utoaji taarifa kwa kuzijengea uwezo na kuzipa msaada wa kitaalamu ifikapo 228.
	Kuhakikisha ulinganifu na muunganiko wa mifumo yote mikuu ya takwimu ndani ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu ili kuwezesha upatikanaji wa takwimu kwa wakati halisi, uchambuzi na katika kufanya maamuzi ya kisera ifikapo Juni 2028.
	Kujumuisha makundi muhimu ya takwimu kama vile picha za setelaiti, takwimu za simu za mkononi, taarifa za mitandao ya kijamii, taarifa za tovuti, taarifa za sensa na big data katika mifumo ya takwimu ya taifa ifikapo Juni 2028.
	Kuboresha na kuimarisha mifumo ya wazi ya takwimu na dashibodi za umma zinazoonyesha angalau sekta kuu mbili za maendeleo ili kuongeza uwazi na matumizi ya takwimu katika maamuzi ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuweka mfumo wa kuchapisha takwimu za wakati halisi za viashiria muhimu vya kiuchumi na kijamii kwa kila robo mwaka ili kuwa na majibu ya kisera na kwa wakati ifikapo 2028.
Bajeti ya Maendeleo ya Ofisi za Takwimu Kitaifa ziwe zimeongezeka kufikia angalau asilimia 0.4 ya Pato la Taifa (GDP) ifikapo 2028.	Kuanzisha mifumo mitatu ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa ajili ya kuwekeza kwenye teknolojia za kisasa za ukusanyaji wa takwimu na mifumo ya uchambuzi wa takwimu (ugharamiaji bunifu + teknolojia) ifikapo 2028.
	Kuweka katika muundo wa kidijitali na kuunganisha mifumo ya usimamizi ya takwimu katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha ulinganifu na utoaji taarifa kwa wakati ifikapo 2028.
	Kuongeza wigo wa aina za takwimu za kiofisi na kuanzisha aina mpya za takwimu za kipaumbele kwa kutumia zana za kidijitali na mbinu bora zilizoboreshwa ifikapo Juni 2028.
	Kuhakikisha takribani asilimia 70 ya watakwimu na wanasayansi wa takwimu wanakamilisha mafunzo yaliyoidhinishwa katika matumizi ya takwimu kubwa akili unde na , AI na teknolojia zinazoibukia ifikapo 2028.
Mfumo wa Taifa wa Takwimu ubadilishwe kuwa wa kidijitali kwa angalau asilimia 80 ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha miundombinu jumuishi ya kitaifa ya takwimu (uhifadhi wa takwimu kwenye cloud, dashibodi za wakati halisi) ifikapo Juni 2028.
	Kuhamisha kwa asilimia 100 ya ukusanyaji mkubwa wa takwimu kwenda kwenye majukwaa ya kidijitali (CAPI, programu za simu) ambayo ni hatua hatua muhimu ya mabadiliko ya kidijitali ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha programu za utafiti wa Akili unde na sayansi ya takwimu katika vyuo vikuu nchini ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuandaa na kuzindua Mtaala wa Kitaifa wa Mafunzo ya Takwimu unaolenga sayansi ya takwimu, big data, Akili unde na utumiaji wa mifumo inayojiendesha na kujisimamia ifikapo Juni 2028.
	Kuweka utaratibu wa matumizi ya Akili unde na maamuzi yanayotokana na uchambuzi wa takwimu Serikalini, ikiwa ni pamoja na kuanzisha vitengo maalumu vya uchambuzi wa takwimu ifikapo Juni 2028.
Muda wa kuchakata data kupunguzwa kwa asilimia 50 ifikapo Juni 2028.	Kuongeza wigo wa ukusanyaji takwimu kwa simu na teknolojia za utambuzi wa mbali kufikia aslimia 100 kwa maeneo lengwa ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha vitengo vya Akili unde na uhandisi wa takwimu katika Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara mbalimbali ifikapo Juni 2028.
	Kuweka majukwaa ya uoanishaji na na uchakataji wa takwimu inayoendeshwa na Akili unde ifikapo 2028.
	Kuanzisha dashibodi za takwimu za wakati halisi katika wizara za kisekta ifikapo Juni 2028.
	Kutekeleza machine learning algorithim katika vitengo muhimu vya takwimu serikalini ili kuharakisha uhakiki, uchambuzi wa takwimu, na maoteo mbalimbali ya takwimu ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha kituo cha Taifa cha Utafiti wa Akili unde kwa ajili ya Takwimu na matumizi ya blockchain katika usalama wa takwimu ifikapo Juni 2028.
Kuanzishwa kwa mfumo wa kiintelijensia wa kidijitali wa taarifa za idadi ya watu na makazi kwa wakati halisi ifikapo Juni 2028.	Kuanzishwa kwa mfumo jumuishi wa kitaifa wa usajili wa matukio muhimu ya kiraia unaounganisha taaarifa za vizazi, vifo, ndoa, uhamiaji na kitambulisho cha taifa katika wizara na Taasisi zote, kuwezesha uwepo wa kumbukumbu za, sahihi kidemografia ifikapo 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kutungwa na kutekelezwa kwa weka mifumo ya kisheria na usimamizi wa takwimu kwa ajili ya mifumo ya kidijitali ya idadi ya watu ili kuhakikisha faragha ya takwimu, usalama, ulinganifu wa mifumo na uwajibikaji wa taasisi ifikapo Juni 2028.
	Kufanya Sensa za Watu na Makazi kwa kutumia njia za kidijitali kwa kutumia tablet, GPS na dashibodi za wakati halisi ifikapo 2028.
	Kuweka mfumo wa ufuatiliaji wa wakati halisi wa maendeleo ya sensa, ubora wa takwimu na uendeshaji wa kazi katika mikoa yote, kwa kutumia dashibodi za moja kwa moja zinazoweza kufikiwa na timu za uratibu za ngazi ya kitaifa na kikanda ifikapo 2028.
	Kuanzishwa kwa Rejesta Jumuishi ya Watu na Makazi kwa kuunganisha CRVS, NIDA na mifumo ya kiutawala kwa ajili ya kuendelea kuhuisha takwimu za kidemographia ifikapo 2028.
	Kuanzishwa kwa jukwaa la kitaifa la ujumuishaji wa takwimu za watu kwa wakati halisi likiunganisha CRVS, sensa za kidijitali, mifumo ya kijiografia (GIS) na kanzidata ya takwimu za kiutawala, kusaidia kupata taarifa za kidemografia za wakati halisi ifikapo Juni 2028.
	Kuanza kwa utekelezaji wa mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji wa taarifa za kidemografia kwa wakati halisi unaojengwa kupitia majukwaa yanayojiendesha yenyewe na ulinganifu wa mifumo kutoka sekta muhimu kama afya, elimu na uhamiaji ifikapo Juni 2028.
	Kutumia zana za kijiografia na Akili unde kufuatilia mienendo ya idadi ya watu kwa kutumia picha za satelaiti, takwimu na chunguzi kwa jili ya kuwa na taarifa za wakati husika ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuanzishwa kwa dashibodi salama na jumuishi ya taarifa za idadi ya watu inayopatikana kwa watumiaji waliothibitishwa wa taarifa za kidemografia kwa wakati halisi kwa ajili ya upangaji, ufuatiliaji na kukabiliana na dharura ifikapo 2028.
3.6.6. Mageuzi ya Kidijitali	
Lengo 1: Jamii jumuishi iliyounganishwa na yenye ujuzi wa kidijgtali, inayowezeshwa na miundombinu salama itakayosaidia ubunifu, utoaji huduma na mageuzi ya kijamii na kiuchumi katika mikoa yote nchini.	
Kufikia angalau asilimia 80 ya uunganishwaji wa kidijitali nchini ifikapo Juni 2028.	Kuandaa na kuendesha vituo vya maarifa ya kidijitali katika kila mkoa ili kuongeza uwezo wa kidijitali, ujuzi na ubunifu kwa vijana, wanawake na makundi maalumu.
	Kutekeleza mkakati wa uratibu wa uwekaji wa miundombinu ya TEHAMA kwa Serikali na Sekta Binafsi ili kuongeza ufanisi katika miundombinu ya fiber optic na kuharakisha uunganishwaji wa broadband nchi nzima.
	Kuanzisha jukwaa salama na jumuishi la kubadilishana takwimu na taarifa kati ya sekta ya umma na binafsi.
	Kutoa msaada wa kifedha na kitaalamu kwa biashara ndogo ndogo, na za kati (MSMEs) ili kuziwezesha kutumia teknolojia za kidijitali, majukwaa ya kidijitali na biashara mtandaoni (e-commerce) kwa lengo la kuongeza tija na kukuza ujumuishaji wa kiuchumi.
	Kusimamia na kuamuru uanzishaji na utekelezaji wa huduma za kidijitali zinazoweza kufikiwa na kutumika na watu wenye ulemavu ili kuhakikisha usawa wa upatikanaji wa huduma hizi kwa makundi yote ya kijamii ifikapo 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya kidijitali vya bei nafuu, vilivyotengenezwa ndani au kuingizwa kutoka nje kwa makundi yote ya jamii.
Lengo 2: Kuimarisha miundombinu ya kitaifa ya usalama wa mtandao na mifumo ya usimamizi, huku tukitumia kimkakati teknolojia zinazoibuka, ili kulinda mageuzi ya kidijitali ya Tanzania na kuiweka nchi katika nafasi ya ushindani wa kimataifa	
Kuasili matumizi ya teknolojia zinazoibukia kwa asilimia 100 ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha vituo maalumu vya utafiti na maendeleo na mafunzo ya akili unde katika AI, robotics, IoT, blockchain na teknolojia zingine zinazoibukia ili kujenga uwezo wa kitaalamu wa nchi ifikapo 2028.
	Kuendeleza uwezo wa ndani katika teknolojia za setelaiti, uchunguzi wa anga na matumizi ya takwimu kwa kushirikiana na taasisi za anga za kimataifa ili kuunga mkono vipaumbele vya maendeleo ya taifa ifikapo Juni 2028.
	Kukuza matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira, vituo vya takwimu vinavyotumia nishati kidogo na mifumo ya kompyuta inayotumia matumizi kidogo ya nishati katika sekta za umma na binafsi ifikapo Juni 2028.
Mashambulizi ya kimtandao kupunguzwa kwa asilimia 80 ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha na kuendesha Kituo cha Kitaifa cha Uendeshaji wa Usalama (SOC) kilicho na vifaa kamili kwa ajili ya kufuatilia, kugundua, na kukabiliana na vitisho na mashambulizi ya mtandao kwa wakati halisi ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha Timu ya Kitaifa ya Kukabiliana na Matukio ya Usalama wa kimtandao (CSIRT) na Baraza la Usimamizi wa Usalama wa Mtandao ili kuratibu jitihada za usalama wa mtandao kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na kusimamia vihatarishi vya usalama wa kimtandao ifikapo Juni 2028.
	Kuendesha mazoezi ya kitaifa ya usalama wa mtandao mara kwa mara ili kupima uwezo wa kukabiliana na matukio, kuongeza utayari, na kuimarisha ustahimilivu wa miundombinu muhimu ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuhakikisha takwimu zote za serikali na sekta muhimu zinahifadhiwa ndani ya mamlaka ya nchi, chini ya mifumo salama cloud, ili kuimarisha wa takwimu, faragha na usalama wa taarifa ifikapo Juni 2028.
Lengo 3: Mfumo thabiti, jumuishi na wenye rasilimali za kutosha wa ubunifu na teknolojia zinazoibukia unaochochea ujasiriamali, utafiti na maendeleo (R&D) na utatuzi wa kiteknolojia	
Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 10 bora Afrika katika fahirisi ya ubunifu ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha mfumo maalum wa ufadhili ili kutoa ruzuku, mtaji wa mwanzo, na msaada wa uwekezaji kwa ubunifu wa kidijitali wenye matokeo makubwa na na miradi ya utafiti kote Tanzania ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha jukwaa la kukuza uuzaji, upatikanaji wa masoko, na uwekezaji katika suluhisho za kidijitali zilizotengenezwa ndani ya nchi kwaaajili ya ukuaji wa uchumi na ujasiriamali ifikapo Juni 2028.
	Kurasimisha ushirikiano kati ya vyuo vya elimu, vituo vya utafiti, na sekta binafsi ili kuharakisha utafiti na maendeleo yanayotekelezeka (R&D), kukuza ujuzi, na uhawilishaji wa teknolojia ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha mtandao ulioratibiwa wa vituo atamizi (incubators) na vichocheo vya ukuaji (accelerators) ili kulea kampuni changa (startups), kuongeza wigo wa biashara za kidijitali zenye uwezekano mkubwa wa kukua, na na kurahisisha upatikanaji wa masoko ndani na nje ya nchi ifikapo Juni 2028.
Lengo 4: Kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa usimamizi wa mageuzi ya kidijitali nchini katika sekta zote.	
Angalau asilimia 80 ya mifumo ya kidijitali ya sekta kuwa imefungamanishwa ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha taasisi kwa ajili ya kujenga uwezo wa uongozi, uwezo wa kitaalamu na usimamizi wa mageuzi ya kidijitali katika sekta zote, ili kuhakikisha utekelezaji wenye ufanisi na usimamizi madhubuti ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa viwango vya ubora, usalama, usiri na ubora kwa mifumo yote ya kidijitali ya umma na binafsi, ili kuwezesha utoaji wa huduma jumuishi ifikapo Juni 2028.
	Kujumuisha na kuboresha mifumo ya udhibiti ili kuwezesha modeli za biashara ya kidijitali, ulinzi wa taarifa, usalama mtandao na ubunifu ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha jukwaa jumuishi la kidijitali la serikali kwa ajili ya kuunganisha mifumo yote ya kisekta, kuwezesha utoaji huduma bila vikwazo na kufuatilia maendeleo ya mabadiliko ya kidijitali ifikapo Juni 2031
3.6.7. Miundombinu na Huduma za TEHAMA	
Lengo 1. Miundombinu dhabiti na jumuishi ya TEHAMA inayohakikisha muunganiko wa kidijitali nchini, kuimarisha ujuzi wa kidijitali kwa makundi yote ya watu na kuwezesha matumizi yenye maadili ya teknolojia zinazoibukia ili kuchochea maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.	
Matumizi ya intanenti yenye kasi kuongezeka kufikia angalau asilimia 80 ifikapo Juni 2028.	Kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano na wasimamizi ili kuhakikisha upatikanaji wa mtandao wa 5G katika miji yote, ili kuwezesha upatikanaji wa huduma ya intaneti ya kasi na ya kuaminika kwa ajili ya biashara, elimu na huduma za serikali
	Kusambaza huduma ya itanenti (Wi-Fi) ya bure au ya gharama nafuu katika maeneo ya kimkakati yaliyochaguliwa katika taasisi za umma, maeneo ya wazi na vituo vya umma ili kuongeza upatikanaji wa huduma za intaneti kwa wananchi, wakiwemo walio katika maeneo ya pembezoni kila mwaka.
	Kutekeleza mifumo ya udhibiti inayochochea uwekezaji wa sekta binafsi katika maeneo yasiyyo pata huduma za kutosha ili kuhakikisha upatikanaji wa usawa wa huduma za kidijitali katika maeneo ya vijijini na maeneo ya pemebzoni kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuandaa miradi maalumu ya miundombinu kwa kutumia fiber, wireless na teknolojia za setelaiti ili kuunganisha jamii za vijijini na maeneo ambayo ni hayafikiki kwa urahisi.
	Kushirikiana na waendeshaji wa setelaiti kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za kidijitali nchini, hususani katika maeneo yenye changamoto ya miundombinu ya ardhini ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kidijitali.
Uelewa wa matumizi ya kidijitali kuongezeka kutoka asilimia 30 hadi angalau asilimia 60 ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha Taasisi ya Kitaifa ya Mafunzo ya Kidijitali (DTI) ifikapo Juni 2028
	Kutoa mafunzo kwa walimu 30,000 juu ya teknolojia zinazoibukia ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa mifumo ya elimu ya kisasa inayoendeshwa na Akili Unde ikijumuisha majukwaa ya elimu mtandao yanayotumia Akili Unde ifikapo Juni 2028.
	Kujumuisha Akili Unde na usalama mitandaoni katika mitaala ya elimu ifikapo Juni 2028.
	Kujumuisha ujuzia wa kidijitali katika mtaala wa elimu wa Taifa katika ngazi zote, kuhakikisha angalau asilimia 60 ya wanafunzi wanapata ujuzi wa msingi wa kidijitali ifikapo Juni 2028.
	Kutekeleza programu za kitaifa za mafunzo ya ujuzi wa kidijitali katika jamii zinazolenga makundi yasiyopata huduma za kutosha ili kuwafikia angalau watu milioni 20 ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa uthibitishaji wa ujuzi wa kidijitali na kuhakikisha angalau asilimia 50 ya nguvu kazi inapata cheti/uthibitisho wa kiwango cha awali ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Mifumo ya Usalama Mtandao na Ulinzi wa Takwimu kutekelezwa kwa asilimia 100 kila mwaka.	Kuimarisha mfumo wa kisheria wa Taifa wa Usalama Mtandao na Ulinzi wa Taarifa ifikapo Juni 2028.
	Kuhakikisha uimara wa mifumo ya usalama mtandao kwa kufanya tathmini za mara kwa mara za usalama mtandao, majaribio na ukaguzi kila mwaka.
	Kuanzisha Kituo cha Kitaifa cha Uendeshaji wa Usalama Mtandao ifikapo Juni 2028.
	Kutoa mafunzo ya usalama mtandao kwa wataalamu wote wa TEHAMA katika sekta muhimu kila mwaka.
Kupanda kwa kiwango cha kuasili akili unde (AI Adoption Index) kutoka kiwango cha chini hadi cha kati ifikapo Juni 2028.	Kuendeleza sera kamili pamoja na mfumo wa kisheria na kanuni za udhibiti wa Akili Unde ifikapo Juni 2028
	Kufanya mapitio ya kila mwaka juu ya utekelezaji wa mfumo wa udhibiti wa Akili Unde ifikapo Juni 2028.
3.6.8. Huduma za Mawasiliano na Usafirishaji Kiposta	
Lengo 1. Kuboresha upatikanaji wa huduma za mawasiliano zenye kuaminika, nafuu na za kasi ya juu, mijini na vijijini, ili kuwezesha ushiriki jumuishi wa kidijitali, ukuaji wa uchumi na maisha bora kwa wote ifikapo 2050	
Upatikanaji wa huduma za posta kwa wote, muunganisho wa kidijitali na huduma salama za biashara mtandaoni (e-commerce) umefikiwa ifikapo Juni 2028.	Kukuza na kuwezesha matumizi ya intaneti inayotumia setelaiti katika maeneo ambayo miundombinu ya ardhini haiwezekani ifikapo Juni 2028.
	Kuboresha upatikanaji wa huduma za posta za kisasa na huduma za kusafirisha vifurushi (courier) zinazojumuishwa na mifumo ya fedha kidijitali katika maeneo ya pembezoni ili kuhakikisha upatikanaji nchi nzima ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa na kutekeleza mfumo jumuishi (harmonized framework) wa huduma za posta na usafirishaji vifurushi ndani nan je ya nchi ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuboresha mfumo wa kitaifa wa anwani za makazi, unaounganishwa na majukwaa ya Mifumo ya Taarifa za Kijiografia (GIS), ili kusaidia utoaji bora na wenye ufanisi wa huduma za usafirishaji na huduma za usambazaji wa barua na mizigo midogo nchini kote ifikapo Juni 2028.
	Tanzania kuongoza na kuwa kitovu cha Biashara Mtandao (e-Commerce) Afrika Mashariki na ukanda wa Kusini mwa Afrika kwa kutumia huduma za usafirishaji, majukwaa ya kidijitali, na urahisishaji wa huduma za usafirishaji ifikapo Juni 2028.
Fahirisi ya ushindani wa huduma za kidijitali kuongezeka hadi asilimia angalau 50 ifikapo Juni 2028.	Kufanya tathmini za mara kwa mara za utoaji wa huduma za kidijitali na miundombinu, na kutumia ubunifu na mbinu bora ili kuhakikisha ubora na ushindani ifikapo Juni 2028.
	Kuhuisha na kutekeleza mifumo ya kisheria kwa ajili ya kulinda watumiaji wa huduma za kidijitali ili kuhakikisha usalama, uwazi na uwajibikaji katika biashara mtandaoni (e-commerce) na usafirishaji wa vifurushi ifikapo 2028.
Kuimarishwa kwa usalama wa mtandao na kuongezeka kwa imani kwa raia, kutekelezwa kwa mifumo ya kitaifa ya usalama wa mtandao kwa asilimia 100 ifikapo Juni 2028.	Kutoa elimu kwa wananchi, waafanya biashara na taasisi za umma kuhusu matumizi salama ya teknolojia za kidijitali, cyber hygiene na vihatarishi vipya vya kimtandao ili kujenga uaminifu katika huduma za kidijitali
	Kuwezesha shughuli za kitafiti zinazolenga katika uibuaji wa teknolojia mpya, zana na uvumbuzi wa kukabiliana na vihatarishi vya kidijitali, ili kuimarisha ustahimilivu katika mitandao ya mawasiliano.
	Kuhamasisha ushirikiano kati ya taasisi za kiserikali, kampuni za teknolojia, na wataalamu wa usalama mtandao ili kuendeleza ubunifu, kushirikishana mbinu bora, na kuimarisha uwezo wa taifa wa kujilinda kimtandao.
3.6.9 Mazingira ya Biashara na Uwekezaji	

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Lengo 1. Kuimarisha uhamasishaji wa uwekezaji kupitia uanzishwaji wa mazingira ya ushindani, uwazi, ufanisi na mfumo wa taasisi, wenye hadhi ya nchi ya nchi ya uchumi wa kipato cha kati cha juu kufikia mwaka 2050.	
Kutoa huduma za serikali kwa njia ya kidijitali kwa angalau asilimia 50 kufikia Juni 2028.	Kuandaa mwongozo wa sera ya Serikali Mtandao ifikapo Juni 2027
	Kutekeleza Mfumo wa Kitaifa wa utambulisho cha Kidijitali (Digital ID) ifikapo Juni 2028.
	Kuunda mfumo wa ufuatiliaji wa kodi unaoutumia akili mnembe (AI) ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha miundombinu ya kidijitali na uwezo wa taasisi za serikali ili kufanikisha upatikanaji wa huduma mtandao kwa asilimia 60 ifikapo Juni 2028.
Kufungamanisha huduma wezeshi za biashara zitakazowezesha takribani asilimia 50 ya miamala ya biashara kufanyika kidijitali na kuwezesha upatikanaji wa huduma kidijitali kwa wajasiriamali wadogo na kampuni zinazoibukia kufikia Juni 2028.	Kuendeleza miongozo ya udhibiti wa biashara ya kidijitali ifikapo Juni 2028.
	Kuboresha upatikanaji na uwezo wa kidijitali kwa wajasiriamali wadogo na wa kati na biashara chipukizi kupitia zana, mafunzo na majukwaa maalumu ili kuwawezesha kushiriki katika biashara za mtandaoni (online trade) ifikapo Juni 2028.
	Kuhamasisha matumizi ya mifumo salama ya malipo na miamala ya kidijitali katika mifumo ya biashara ili kuhakikisha angalau asilimia 60 ya biashara za wajasiriamali wadogo na wakati zinafanyika kidijitali ifikapo Juni 2028.
Kuongeza mchango wa uwekezaji kutoka nje katika Pato la Taifa kufikia takribani asilimia 10 kila mwaka ifikapo Juni 2028.	Kukamilisha maboresho ya sera ya uwekezaji ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha vituo vya uwekezaji katika mikoa yote nchini ifikapo 2028.
	Kuimarisha udhamini wa uwekezaji (Investment Ombudsman) ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuimarisha jukwaa la kidijitali la usajili wa uwekezaji ifikapo Juni 2029
	Kuhamasisha utoaji wa vivutio za uwekezaji katika teknolojia ya hali ya juu ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa miongozo ya uwekezaji kwa sekta za teknolojia ya hali ya juu ifikapo Juni 2028.
Kuwezesha uwekezaji wa angalau asilimia 5 ya teknolojia mpya za hali ya juu ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha angalau kanda maalumu tatu za akili unde na kanda za ubunifu wa kidijitali ifikapo Juni 2028.
Kuwezesha angalau asilimia 15 ya nguvu kazi kuwa na ujuzi wa kisasa na wa kitaalamu ifikapo Juni 2028.	Kuandaa programu ya kitaifa ya kujenga ujuzi katika uwekezaji ifikapo Juni 2028.
	Kuongeza wigo wa ushirikiano katika mafunzo ya ufundi ifikapo Juni 2028.
Kuongeza miradi ya maendeleo ya miundombinu kupitia Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kufikia takribani asilimia 20 ifikapo Juni 2028.	Kuwezesha angalau miradi mitano ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwam mwaka ili kuimarisha maendeleo ya miundombinu ifikapo Juni 2028.
Kuwezesha uwekezaji katika teknolojia wenye thamani ya takribani Dola za Marekani Bilioni 2 kufikia Juni 2028.	Kupanua motisha kwa viwanda vya kisasa kila mwaka ili kufanikisha jumla ya uwekezaji wa teknolojia wa Dola za Marekani bilioni 2 (USD 2B) ifikapo Juni 2028.
Lengo 2: Kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili kuiweka Tanzania katika nafasi ya tatu bora miongoni mwa nchi zenye uchumi rafiki wa biashara barani Afrika, kwa lengo la kuongeza kasi ya uwekezaji na kuharakisha urasimishaji wa biashara katika sekta zote ifikapo mwaka 2050.	
Tanzania kushika nafasi ya tatu kati ya vituo vinavyovutia zaidi kwa biashara na uwekezaji barani Afrika kufikia Juni 2028.	Kutenganisha malengo ya ukusanyaji mapato na majukumu ya udhibiti ili kuhakikisha tozo zinagharamia utoaji huduma ifikapo Juni 2028.
	Kuratibu na kusanifu upya vyombo vya udhibiti ili kuharakisha ukuaji wa biashara na uwekezaji ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuzingatia na kuunganisha kanuni zinazofanana na kuondoa urudufu ili kupunguza gharama za miamala ifikapo Juni 2028.
	Kufanya tathmini ya athari za udhibiti (Regulatory Impact Assessments – RIAs) kwa kanuni zote na sheria ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA by-laws) zinazoweza kuathiri biashara kufikia Juni 2028.
	Kuongeza imani kwa wawekezaji kupitia sera za kukabiliana na vihatarishi dhamana za mapato, na utatuzi wa migogoro kwa haraka ifikapo Juni 2028.
Kurasimisha biashara kwa asilimia 80 na kuweka mfumo wa kidijitali wa taratibu za biashara ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha wakala maalum wa kukuza uwekezaji na kampuni changa bunifu kufikia 2028.
	Kuwezesha ushiriki wa kampuni zinazoibukia na wafanyabiashara wadogo wadogo wasio rasmi katika ubia kati ya sekta ya umma na binafsi ifikapo Juni 2028.
	Kukuza fursa za soko la Tanzania ndani ya soko huru la AfCFTA na Jumuiya ya Afrika Mashariki ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
3.7. Misingi ya Uendelevu wa Taifa	
3.7.1. Kuimarisha Utawala Bora, Demokrasia, Usalama na Utulivu	
Lengo la 1: Kuimarisha uwazi, uwajibikaji, maadili, na tunu za kidemokrasia, pamoja na amani na utulivu ili kuwezesha ushiriki wenye ufanisi na usawa wa wanajamii wote katika maendeleo ya taifa	
Kuimarika kwa vitendo vya utoaji maoni na uwajibikaji hadi kufikia - 0.45 ifikapo Juni 2028.	Kufanya mapitio ya kina ya mifumo iliyopo ya kikatiba na kisheria ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa mageuzi ya kisheria na kiutawala baada ya utekelezaji wake ifikapo Juni 2028.
	1.1. Kufanya Mageuzi ya Kitaasisi ili Kuhakikisha Utawala Bora wa Rasilimali za Taifa na Usimamizi Endelevu wa Mipango ya Kijamii na Kiuchumi ya Muda Mrefu ifikapo Juni 2028.
	i. Kufanya mageuzi katika mifumo ya sasa ya kitaasisi ili kuhakikisha kuwa mihimili yote ya dola inawajibika kwa usimamizi wa pamoja na huru katika matumizi ya rasilimali za taifa na katika maamuzi yanayogusa maslahi ya taifa ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuandaa na kutekeleza mfumo wa ushirikishwaji wa kijamii na kitaasisi katika usimamizi wa rasilimali za taifa ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha au kuanzisha chombo huru kitakachohakikisha kuwa manufaa yatokanayo na kupungua kwa gharama na kuongezeka kwa tija vinavyotokana na matumizi ya rasilimali za taifa yanagawanywa kwa usawa kwa umma ili kupunguza pengo la kijamii ifikapo Juni 2028.
	Kufanya mapitio na maboresho ya muundo wa taasisi muhimu za umma, hususan mashirika ya umma na taasisi za udhibiti, ili kuondoa urudufu wa majukumu, vitendo vya kutafuta faida binafsi, na ukosaji wa ufanisi ifikapo Juni 2028.
	1.2 Kuandaa Mikakati ya Kuoanisha Sheria za Kimila na Sheria za Kiserikali katika Masuala ya Usawa wa Kijinsia na Haki za Binadamu ifikapo Juni 2028.
	Kufanya ukaguzi wa kitaifa wa sheria za kimila ili kubaini maeneo yenye migongano, mwingiliano, au kinzani na sheria za kiserikali ifikapo mwaka 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuandaa na kutekeleza mikakati ya jinsia na haki za binadamu ifikapo Juni 2028.
	1.3 Kukuza ushiriki jumuishi katika uchaguzi kwa kujumuisha masuala ya jinsia, vijana na watu wenye ulemavu katika sera na taratibu za uchaguzi ifikapo Juni 2028.
	Kuoainisha na kuratibu sera za kitaasisi ifikapo Juni 2028.
	Kuendeleza miundombinu, zana na majukwaa yatakayowezesha ushiriki wa watu wenye mahitaji maalum katika michakato ya uchaguzi ifikapo Juni 2028.
	1.4 Kuandaa na kutekeleza programu ya kitaifa ya muda mrefu ya utoaji wa huduma za msaada wa kisheria, hususan kwa wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na jamii zenye kipato cha chini, kwa kushirikiana na asasi za kiraia na sekta binafsi ifikapo Juni 2028.
	i. Kufanya mapitio na kuandaa programu ya kitaifa ya muda mrefu ya utoaji wa huduma za msaada wa kisheria yenye uwazi na ushirikishwaji mpana ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuandaa na kutekeleza mfumo wa elimu ya uraia, utetezi pamoja na ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji ifikapo Juni 2028.
2. Fahirisi ya Mtazamo wa Rushwa (CPI) imeimarika kutoka 41/100 (2024) hadi 55/100 ifikapo Juni 2028.	2.1 Kuweka mfumo wa kidijitali katika huduma za mahakama na utawala ili kuimarisha uwazi ifikapo Juni 2028.
	2.2 Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mifumo ya mikataba ya wazi na ununuzi wa kielektroniki ifikapo Juni 2028.
	2.3 Kuimarisha majukwaa ya maoni ya wananchi na mifumo ya kushughulikia malalamiko kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
3. Farihisi ya utulivu wa kisiasa, amani na usalama kimeimarika kufikia +0.10 ifikapo Juni 2028.	Kuboresha mifumo ya ulinzi na usalama kwa kutumia teknolojia za kisasa ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha mfumo wa polisi jamii na kuandaa programu ya pamoja ya ushirikishwaji, ushiriki na uhusishwaji wa wananchi ifikapo Juni 2028.
	Kufanya mapitio ya mitaala ya mafunzo ya polisi ili kuleta mabadiliko ya mtazamo kuelekea utoaji bora wa huduma kwa wananchi ifikapo Juni 2028.
	Kufanya mapitio ya Jeshi la Magereza la Tanzania na vyombo vingine vinavyohusika kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume ya Rais ya Haki Jinai ifikapo Juni 2028.
Lengo 2: Kuimarisha utumishi wa umma unaoendana na mahitaji ya wananchi, unaowajibika na unaozingatia maadili kwa ajili ya utawala bora na utoaji huduma wenye ufanisi	
1.1 Kufanya maboresho na kurahisisha muundo wa Wizara na Wakala za Serikali kwa kuzipanga katika idadi ndogo zenye majukumu mapana ili kuongeza ufanisi na wepesi wa utekelezaji ifikapo Juni 2028.	
1. Ufanisi wa Serikali kiboreshwe kufikia -0.30 ifikapo Juni 2028.	1.1 Kufanya mapitio ya kina ya majukumu na muundo wa taasisi za Wizara, Idara na Wakala pamoja na mifumo yake ifikapo Juni 2028.
	Kufanya tathmini ya mahitaji ya watumishi ili kuboresha upangaji wa rasilimali watu kwa kuzingatia muundo mpya wa wizara na taasisi pamoja na mahitaji ya mabadiliko ya kidijitali katika utoaji wa huduma ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha jukwaa litakalowawezesha mawaziri na viongozi wakuu wa serikali kujibu madai na malalamiko ya wananchi ifikapo Juni 2028.
	Kutekeleza maboresho ya muundo wa wizara, idara na wakala kwa awamu ifikapo Juni 2028.
	1.2 Kuanzisha Mfumo Jumuishi wa Kidijitali wa Uchumi ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kubuni na kuendeleza usanifu wa jukwaa kuu la mfumo Jumuishi wa Kidijitali wa Uchumi ifikapo Juni 2028.
	Kuweka katika mfumo wa kidijitali na kuunganisha kanzidata na majukwaa muhimu ya taarifa za kiuchumi katika taasisi zote za serikali ifikapo Juni 2028.
	Kubuni na kuendeleza miundombinu na mifumo ya ulinzi wa taarifa na usalama wa mtandao ifikapo Juni 2028.
	1.3 Kuimarisha uwezo wa kitaaluma, kiufundi na kiuongozi katika sekta ya umma ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa na kutekeleza programu jumuishi ya mafunzo na mwongozo wa kujenga uwezo ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa na kutekeleza mfumo jumuishi wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji ifikapo Juni 2028.
	1.4 Kuimarisha uundaji wa modeli za kiuchumi na maoteo ya mapato ya Serikali ifikapo Juni 2028.
	Kufanya mapitio ya modeli iliyopo kwa kuzingatia mahitaji ya maendeleo ya baadaye na mbinu bora za kimataifa ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa na kutekeleza programu ya mapitio na uboreshaji wa mara kwa mara wa modeli kadri takwimu mpya, mbinu na mahitaji mapya yanavyojitokeza ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa programu ya kitaifa ya maadili na utamaduni wa kazi katika utumishi wa umma, ikijumuisha mafunzo ya mara kwa mara ya maadili na ushauri wa uongozi katika taasisi zote za serikali ifikapo Juni 2038.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
2. Kufikia angalau asilimia 80 ya taasisi za umma zenye kuonesha utamaduni wa kazi wenye utendaji wa juu, maadili na uwajibikaji nchini ifikapo Juni 2028.	2.1 Kuweka utaratibu wa tathmini ya utendaji wa watumishi kwa mfumo wa nyuzi 360 pamoja na mifumo ya maoni ya papo kwa papo katika taasisi zote za umma ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa sera na miongozo ya tathmini ya utendaji ya nyuzi 360 pamoja na mfumo wa maoni ya wakati halisi ifikapo Juni 2028.
	Kufanya mapitio, kuanzisha na kuunganisha majukwaa ya kidijitali ya kusimamia tathmini ya utendaji na maoni ya wakati halisi ifikapo Juni 2028.
3. Kiwango cha kuridhika na huduma za umma kuongezeka kutoka asilimia 45 (2024) hadi asilimia 70 ifikapo Juni 2028.	3.1 Kuanzisha mikataba ya utendaji kazi kwa viongozi wakuu wa umma ifikapo Juni 2028.
	3.2 Kuanzisha programu endelevu za maendeleo ya kitaaluma na mafunzo ya maadili kila mwaka.
	3.3 Kuongeza ugatuzi wa kifedha ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi ifikapo Juni 2028.
Lengo la 3: Kuimarisha uadilifu na kuaminika kwa taasisi zinazosimamia mahusiano ya wananchi	
Utawala wa Sheria uboreshwe kufikia -0.20 ifikapo Juni 2028.	1.1 Kukuza ushirikiano na wadau wa kikanda na kimataifa kwa ajili ya kubadilishana maarifa kuhusu kuimarisha mifumo ya kisheria ifikapo Juni 2028.
	Kukuza ushirikiano na wadau wa kikanda na kimataifa kwa ajili ya kubadilishana maarifa kuhusu kuimarisha mifumo ya kisheria ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa na kutekeleza programu na majukwaa ya kubadilishana maarifa ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Imani ya wananchi kwa taasisi za umma kiongezeka kutoka asilimia 52 (2024) hadi asilimia 75 ifikapo Juni 2028.	2.1 Kuimarisha taasisi za usimamizi na ukaguzi (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, na Kamati za Bunge) ifikapo Juni 2028.
	2.2 Kutekeleza mifumo ya uwazi katika ajira na upandishaji vyeo kila mwaka.
	Kukuza majadiliano ya kitaifa kuhusu mageuzi ya utawala ifikapo Juni 2028.
3.7.2. Kujenga Utawala Imara na Wenye Ufanisi katika Serikali za Mitaa	
Lengo la 1: Kufikia Utawala Imara na Wenye Ufanisi katika Serikali za Mitaa	
Mamlaka za Serikali za Mitaa kufikia uhuru wa kiutendaji kwa asilimia 100 ifikapo Juni 2028.	Kuimarisha Sera ya Kitaifa ya Ugatuzi wa Madaraka na Mfumo wa Kisheria ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha majukwaa ya kidijitali ya utoaji huduma katika ngazi za mitaa pamoja na mifumo ya kupokea maoni ya wananchi ifikapo Juni 2028.
	Kubuni na kuendeleza majukwaa ya kidijitali ya utoaji huduma na mifumo ya maoni ya wananchi ifikapo Juni 2028.
	Kusambaza na kuanza kutekeleza majukwaa na mifumo ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa na kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha mfumo wa uhamishaji wa rasilimali za fedha kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ifikapo Juni 2028.
	1.7. Kuboresha na kupanua vyanzo vya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ifikapo Juni 2028.
	1.8. Kuimarisha usimamizi wa fedha, uwajibikaji na uwazi ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	1.9. Kukuza Maendeleo ya Uchumi wa Serikali za Mitaa kama chanzo muhimu cha mapato ifikapo Juni 2028.
Miundo ya kiutawala ya Serikali za Mitaa na mifumo ya usimamizi wa Serikali Kuu kuboreshwa kwa asilimia 100 ifikapo Juni 2028.	2.1 Kufanya mapitio ya muundo wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuwezesha utekelezaji bora wa sera, msaada wa kitaalamu na ufuatiliaji wa utendaji, kwa lengo la kuimarisha utawala wa ugatuzi na uhuru wa Serikali za Mitaa ifikapo Juni 2028.
	2.2 Kuoanisha na kuratibu mifumo ya kisheria na kitaasisi inayohusiana na ugatuzi wa madaraka ifikapo Juni 2028.
	2.3 Kubuni, kuendeleza na kutumia zana na majukwaa ya kidijitali kwa ajili ya uratibu, uwazi, uwajibikaji na ufanisi wa utekelezaji ifikapo Juni 2028.
	2.4 Kuboresha majukumu na kazi za viongozi wa ngazi za mikoa na serikali za mitaa ili kuongeza ushirikiano na kukamilishana katika utoaji wa huduma bora na zenye uwajibikaji ifikapo Juni 2028.
	2.5 Kurekebisha miundo ya kiutawala kwa kuzingatia uwiano wa idadi ya watumishi na majukumu yao ifikapo Juni 2028.
3. Ushiriki wa wananchi na uwajibikaji wa mitaa husika katika asilimia 80 ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) umefikiwa ifikapo Juni 2028.	3.1 Kuweka msingi wa kisheria wa mipango shirikishi na bajeti shirikishi katika ngazi ya kata na vijiji kupitia marekebisho ya sera na utekelezaji wake ifikapo Juni 2028.
	Kufanya mapitio ya kina ya miundo iliyopo, mifumo ya kisheria na taratibu za utekelezaji ifikapo Juni 2028.
	Kubuni, kuendeleza na kuanza kutekeleza mifumo na taratibu jumuishi za ushiriki wa wananchi na utekelezaji wake ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	3.2 Kusambaza matumizi ya zana za tathmini ya jamii na ukaguzi wa kijamii angalau asilimia 60 ya Serikali za Mitaa ifikapo 2028 na kufikia utekelezaji wa kitaifa ifikapo Juni 2028.
	Kubuni na kuendeleza zana za tathmini ya jamii ifikapo Juni 2028.
	Kusambaza kwa awamu matumizi ya zana za tathimini ya jamii katika Serikali za Mitaa zote ifikapo Juni 2028.
	3.3. Kuanzisha majukwaa ya kidijitali ya maoni ya wananchi (kupitia ujumbe mfupi wa simu, tovuti na programu za simu) kwa ajili ya ufuatiliaji wa utoaji wa huduma katika Serikali za Mitaa zote ifikapo Juni 2028.
	Kusambaza na kuanza kupitia majukwaa ya kidijitali ya maoni ya wananchi katika Serikali za Mitaa zote ifikapo Juni 2028.
	Kusambaza na kuanza kuyatumia katika Serikali za Mitaa zote ifikapo Juni 2028.
	Kutoa mafunzo na kuziwezesha taasisi za utawala wa mitaa, madiwani, kamati za maendeleo za kata, serikali za vijiji na asasi za kiraia ili kuimarisha ushiriki wa wananchi na mifumo ya maoni ifikapo Juni 2028.
	3.4 Kuimarisha uwezo wa madiwani pamoja na kamati za maendeleo za kata na vijiji kama majukwaa ya ushirikiano katika utoaji wa huduma na ubunifu wa maendeleo ya ngazi ya jamii ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa na kuanzisha programu na majukwaa ya usimamizi wa mabadiliko na ubunifu katika ngazi ya jamii ifikapo Juni 2028.
	Kutekeleza kikamilifu programu na majukwaa ya ubunifu katika halmashauri zote, kata na vijiji ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Lengo la 2: Kuboresha mifumo ya kifedha na kiutawala iliyogatuliwa	
Sehemu ya mapato ya ndani ya Serikali za Mitaa iongezeke kutoka asilimia 12 (2024) hadi asilimia 25 ifikapo Juni 2028.	Kutoa mamlaka mapana zaidi kwa Serikali za Mitaa kuanzisha na kusimamia kodi za ndani ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha mfumo wa uhamishaji wa rasilimali kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa unaozingatia utendaji ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha uratibu kati ya Tume ya Taifa ya Mipango, Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Serikali za Mitaa kila mwaka.
Lengo la 3: Kuimarisha uwajibikaji na uwazi katika Serikali za Mitaa	
1. Kiwango cha kuridhika kwa wananchi na utendaji wa Serikali za Mitaa kiongezeke kutoka asilimia 40 (2024) hadi asilimia 65 ifikapo Juni 2028.	1.1 Kusambaza na kutekeleza majukwaa ya bajeti shirikishi na mipango shirikishi ifikapo Juni 2028.
	1.2 Kuweka mifumo ya kidijitali katika taarifa za fedha na mifumo ya utoaji huduma ya Serikali za Mitaa ifikapo Juni 2028.
	1.3 Kuanzisha kamati huru za ukaguzi wa hesabu katika Serikali za Mitaa ifikapo Juni 2028.
Lengo la 4: Kuimarisha uthabiti wa kitaasisi na kifedha wa Serikali za Mitaa	
Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinazokidhi viwango vya utoaji huduma kuongezeka kutoka asilimia 45 (2024) hadi asilimia 75 ifikapo Juni 2028.	Kujenga uwezo wa watumishi wa Serikali za Mitaa katika usimamizi wa miradi na mipango kila mwaka.
	1.2 Kukuza ushirikiano kati ya Serikali za Mitaa, sekta binafsi na asasi za kiraia ifikapo Juni 2028.
3.7.3 Kuimarisha usimamizi wa mifumo ya kidijitali na takwimu	
Lengo la 1: Kuanzisha mfumo salama wa utawala wa kidijitali ifikapo mwaka 2050.	

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
1. Asilimia 50 ya huduma za serikali kuwa zimewekwa katika mfumo wa kidijitali ifikapo Juni 2028.	1.1 Kuimarisha sera, mifumo ya kisheria na kitaasisi ili kuhakikisha utawala bora wa kidijitali serikalini ifikapo Juni 2028.
	i. Kufanya mapitio na kuoanishwa kwa sera na sheria zinazohusiana na utawala wa kidijitali ifikapo Juni 2028.
	ii. Kufanya mapitio na kuandaa viwango pamoja na miongozo ya kuoanisha mifumo ya kidijitali na usimamizi wa takwimu ifikapo Juni 2028.
	iii. Kuimarisha miundo ya taasisi, mamlaka na ujuzi wa taasisi iliyopo inayosimamia utawala wa kidijitali ifikapo Juni 2028.
	1.2 Kuboresha, kuendeleza na kulinda miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ifikapo Juni 2028.
	1.3 Kuboresha miundombinu ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma za serikali ifikapo Juni 2028.
	1.4 Kuendeleza na kutekeleza zana na majukwaa yanayooanishwa katika mifumo ya kidijitali ifikapo Juni 2028.
	1.5 Kutumia mifumo salama ya vitambulisho vya kidijitali ifikapo Juni 2028.
	1.6 Kuanzisha majukwaa yanayoweza kutumika kwa urahisi kupitia simu za mkononi ili kuwezesha wananchi wengi kupata huduma mbalimbali ifikapo Juni 2028.
	1.7 Kuboresha usanifu na michakato ya huduma za TEHAMA ifikapo Juni 2028.
	1.8 Kurahisisha na kuboresha huduma za serikali ili kupunguza urasimu ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	1.9 Kuanzisha na kuendesha majukwaa ya kupokea maoni ya wananchi ifikapo Juni 2028.
2. Angalau asilimia 90 ya wananchi kuwa na kitambulisho cha kidijitali na uwezo wa kupata huduma za kielektroniki ifikapo Juni 2028.	2.1 Kuendeleza nyezo na majukwaa salama ya huduma za kielektroniki ifikapo Juni 2028
	i. Kuendeleza majukwaa rafiki kwa mtumiaji yanayounganishwa na mifumo ya vitambulisho vya kidijitali ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuanzisha mfumo wa kisheria na miundombinu salama ya kuhifadhi taarifa kwa ajili ya kulinda faragha, usalama wa mtandao na ulinzi wa takwimu ifikapo Juni 2028.
	iii. Kuanzisha matumizi ya Jamii Namba kwa ajili ya utoaji wa huduma jumuishi, bora na wenye ufanisi ifikapo Juni 2028.
	2.2. Kuandaa na kutekeleza programu za elimu ya matumizi ya teknolojia za kidijitali na uhamasishaji ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa na kutekeleza programu za ushirikiano zitakazounganisha taasisi za umma, asasi za kiraia, sekta binafsi na wananchi kwa ufanisi ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa miongozo ya uhamasishaji kupitia vyombo mbalimbali vya habari pamoja na mafunzo kuhusu matumizi ya vitambulisho vya kidijitali na huduma za kielektroniki ifikapo Juni 2028.
3. Mifumo mahiri ya takwimu kuboreshwa, kusambazwa na kuunganishwa kikamilifu katika sekta mbalimbali ifikapo Juni 2028.	3.1. Kuandaa sera ya takwimu huria ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa na kutekeleza sera ya takwimu huria katika sekta mbalimbali ifikapo Juni 2028

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuimarisha na kuunganisha mifumo ya takwimu ili kuongeza upatikanaji na uhakika wa huduma pamoja na kubadilishana taarifa ifikapo Juni 2028.
4. Kuimarisha kiwango cha "uimara" katika farihisi ya Ustahimilivu wa Usalama wa Mtandao wa Taifa ifikapo Juni 2028.	4.1. Kuimarisha sera na mifumo ya kisheria ya usalama wa mtandao ifikapo Juni 2028.
	i. Kufanya mapitio na kuhuisha sera na sheria zinazohusiana na uhalifu wa mtandao, ulinzi wa takwimu na faragha ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuandaa miongozo ya uzingatiaji wa usalama wa mtandao, utekelezaji wake pamoja na mfumo wa uthibitishaji ifikapo Juni 2028.
	4.2 Kuimarisha miundombinu na uwezo wa kiufundi kwa ajili ya kugundua, kuzuia na kukabiliana na vitisho vya mtandao ifikapo Juni 2028.
	i. Kuboresha Kikosi cha Kitaifa cha Kukabiliana na Dharura za Kompyuta pamoja na vikosi maalum vya sekta mbalimbali ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuanzisha majukwaa ya kubadilishana taarifa za vitisho vya mtandao kati ya sekta ya umma na binafsi ifikapo Juni 2028.
	iii. Kuimarisha Kituo cha Kitaifa cha Uendeshaji wa Usalama wa Mtandao ifikapo Juni 2028.
	4.3 Kuboresha uratibu wa taasisi na utawala wa usalama wa mtandao ifikapo Juni 2028.
	i. Kufanya mapitio na kuimarisha sera, sheria na mifumo ya kitaasisi ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuimarisha au kuanzisha chombo kinachosimamia uratibu na utawala wa usalama wa mtandao ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuanzisha na kuendesha vitengo maalum vya usalama wa mtandao katika taasisi zote za umma ifikapo Juni 2028.
	Kufanya ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA mara kwa mara kila mwaka.
	4.4 Kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na kikanda katika masuala ya usalama wa mtandao ifikapo Juni 2028.
	Kuoanisha sera na sheria za kitaifa na mikataba ya kikanda na kimataifa ya usalama wa mtandao ifikapo Juni 2028.
	Kufanya mapitio na kutekeleza itifaki za ushirikiano wa kimataifa katika kukabiliana na matukio ya usalama wa mtandao ifikapo Juni 2028.
	Kushiriki katika tafiti na ubunifu wa pamoja na washirika wa kikanda na kimataifa kila mwaka.
	4.5 Kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi, asasi za kijamii na wananchi ifikapo Juni 2028.
	Kuwezesha uwekezaji wa sekta ya umma na binafsi katika kuendeleza utafutaji wa suluhisho wa usalama wa mtandao kila mwaka.
	ii. Kuendeleza majukwaa ya kidijitali ya wadau mbalimbali kwa ajili ya kubadilishana taarifa mara kwa mara ifikapo Juni 2028.
	iii. Kuanzisha na kutekeleza programu za elimu ya usalama wa mtandao kwa wananchi, taasisi na makundi maalum ifikapo Juni 2028.
Lengo la 2: Kufikia upatikanaji wa huduma za kidijitali kwa wote	
Matumizi ya intaneti kuongezeka kutoka asilimia 79.3 (2024) hadi asilimia 98 ifikapo Juni 2028.	Kupanua miundombinu ya mtandao wa intaneti ya kasi katika maeneo ya vijijini ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	1.2 Kutoa ruzuku kwa vifaa vya kidijitali ili viweze kupatikana kwa gharama nafuu ifikapo Juni 2028.
	1.3 Kuanzisha kampeni za kitaifa za elimu ya matumizi ya teknolojia za kidijitali ifikapo Juni 2028.
Lengo la 3: Kuboresha mifumo ya kitaasisi na TEHAMA	
1. Mifumo inayoweza kuunganishwa katika Wizara, Idara, Wakala na Serikali za Mitaa kuongezeka kutoka asilimia 20 (2024) hadi asilimia 80 ifikapo Juni 2028.	1.1 Kuandaa mfumo wa kitaifa wa kuoanisha mifumo ya kidijitali ifikapo Juni 2028.
	1.2 Kuunganisha majukwaa ya TEHAMA yaliyogawanyika katika taasisi mbalimbali ifikapo Juni 2028.
	1.3 Kuimarisha mifumo ya usalama wa takwimu na ulinzi wa faragha ifikapo Juni 2028.
Lengo la 4: Kuboresha huduma za umma kupitia mifumo ya kidijitali	
1. Huduma muhimu zinazotolewa mtandaoni kuongezeka kutoka asilimia 35 (2024) hadi asilimia 85 ifikapo Juni 2028.	1.1. Kuweka katika mfumo wa kidijitali huduma zenye mahitaji makubwa (kodi, leseni, afya, elimu) ifikapo Juni 2028.
	1.2. Kuanzisha majukwaa ya ushiriki wa wananchi katika masuala ya utawala (ifikapo Juni 2028.
	1.3. Kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa ufuatiliaji wa utoaji wa huduma ifikapo Juni 2028.
Lengo la 5: Kujenga upya mifumo ya kitaifa ya takwimu ili iwe imara na himilivu	
Idadi ya sera zinazotumia uchambuzi wa takwimu za wakati halisi kuongezeka kutoka asilimia 15 (2024) hadi asilimia 70 ifikapo Juni 2028.	Kuanzisha Kituo cha Kitaifa cha Takwimu chenye uwezo wa uchambuzi wa takwimu kubwa ifikapo Juni 2028.
	1.2 Kukuza mipango ya takwimu huria kila mwaka.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	1.3. Kuwajengea uwezo watumishi katika uchambuzi wa takwimu na utungaji wa sera kisayansi kila mwaka.
3.7.4. Kukuza Mabadiliko ya Mtazamo ili Kuwezesha Utekelezaji wa Mageuzi	
Lengo la 1: Kuimarisha utekelezaji, uratibu na ufuatiliaji wenye ufanisi wa mageuzi makuu ya kimuundo yaliyobainishwa katika Mpango Elekezi 2050 ili kuharakisha mabadiliko endelevu ya maendeleo.	
1. Angalau asilimia 70 ya mifumo ya utawala wa taasisi iwe imefanyiwa mageuzi na kuanza kutekelezwa ifikapo Juni 2028.	1.1 Kuimarisha Kitengo cha Mageuzi kilicho chini ya Ofisi ya Rais ili kuratibu na kufuatilia mageuzi yanayohusisha sekta mbalimbali ifikapo Juni 2028.
	Kufanya mapitio ya mfumo wa sasa wa kitengo hicho ili uendane na mahitaji ya maendeleo ya baadaye ifikapo Juni 2028.
	Kukibadilisha kitengo hicho kiwe taasisi inayolenga matokeo, inayounganisha utaalamu wa sekta mbalimbali na inayotumia mifumo ya kidijitali ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa dashibodi ya kidijitali itakayowezesha ufuatiliaji wa wakati halisi wa matokeo ya mageuzi katika sekta mbalimbali ili kuimarisha maamuzi yanayotegemea takwimu na uwajibikaji katika sekta ya umma ifikapo Juni 2028.
	1.2 Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa utekelezaji wa mageuzi pamoja na mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na uwajibikaji unaozingatia matokeo ili kutekeleza kikamilifu dhana ya 4Rs ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa na kutekeleza mkakati wa usimamizi wa mabadiliko pamoja na mawasiliano ili kupata uungwaji mkono wa wadau katika ngazi zote za jamii ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuandaa na kuunganisha viashiria vya kimkakati vya utendaji kwa nguzo zote kuu za mageuzi na makundi mbalimbali ya kijamii ifikapo Juni 2028.
	Kuweka utaratibu wa mapitio ya mara kwa mara ya utendaji ili kuhakikisha uwajibikaji na usimamizi unaobadilika kulingana na mahitaji katika utekelezaji wa 4Rs ifikapo Juni 2028.
	Kuwezesha matumizi ya nyezo za ustawi wa jamii ili kuimarisha mabadiliko ya mtazamo kwa wananchi ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha chombo au kikosi kazi cha kitaifa cha usimamizi wa mageuzi kitakachosimamia utekelezaji wa mageuzi yanayohusiana na 4Rs ifikapo Juni 2028.
	Kujenga uwezo wa Wizara, Idara na Wakala kupitia mafunzo maalum na msaada wa kitaalamu ili kuoanisha mikakati ya taasisi na vipaumbele vya Mpango Elekezi 2050 ifikapo Juni 2028.
2. Mfumo wa kidijitali wa ufuatiliaji na tathmini ya mageuzi kuanzishwa na kujaribiwa katika angalau asilimia 30 ya Wizara, Idara na Wakala ifikapo Juni 2028.	2.1. Kubuni na kusambaza dashibodi ya kitaifa ya kidijitali ya ufuatiliaji na tathmini inayozingatia matokeo ili kufuatilia hatua za mageuzi ifikapo Juni 2028.
	2.2. tathmini ya mahitaji pamoja na mashauriano ya watumiaji katika Wizara, Idara na Wakala ifikapo Juni 2028.
	2.3. na kujaribu mfano wa dashibodi katika taasisi chache zilizochaguliwa kwa majaribio ifikapo Juni 2028
	2.4. Kusambaza dashibodi ya kidijitali katika angalau asilimia 30 ya Wizara, Idara na Wakala ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Lengo la 2: Kuendesha mabadiliko ya kitaifa ya mtazamo kwa kuingiza katika mifumo ya kijamii maadili ya ujasiriamali, uwazi, ubunifu, usawa na ushiriki wa wananchi	
1. Kuimarisha na kuweka katika mifumo rasmi maadili ya uongozi yanayounga mkono mageuzi na utoaji wa huduma bora katika sekta zote ifikapo Juni 2028.	1.1 Kuendesha mikutano, programu na warsha za viongozi wa ngazi za juu kila mwaka ili kuimarisha maadili ya uongozi.
	Kuandaa na kutekeleza mfumo wa kitaifa wa maadili ya uongozi ulioundwa kwa ushirikiano na viongozi wa sekta ya umma, sekta binafsi na asasi za kiraia ifikapo Juni 2028.
	Kukuza utamaduni wa kuhimiza mabadiliko ya mtazamo katika majukwaa yote ya uongozi ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa na kutekeleza programu maalum za mafunzo kuhusu uongozi wa mageuzi na uongozi wenye maadili katika sekta zote kila mwaka.
	Kuanzisha programu za ushauri wa kiutendaji kwa viongozi wa ngazi za juu kuhusu kufanya maamuzi yanayobadilika kulingana na mazingira ifikapo Juni 2028.
	Kuimarisha vitengo vya utafiti na ubunifu ili kuratibu na kuharakisha mipango ya mageuzi ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa na kutekeleza programu za kujenga uwezo katika utafiti, ubunifu na usimamizi wa mabadiliko katika Wizara, Idara, Wakala na Serikali za Mitaa ifikapo Juni 2028.
	Kukuza programu za kubadilishana maarifa na taasisi za utafiti na ubunifu za ndani na za kimataifa ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	1.3 Kuwapa mafunzo viongozi wa dini, kimila na jamii ili wawe mabalozi wa mabadiliko ya mtazamo kwa kutumia ujumbe unaoendana na tamaduni za jamii ifikapo Juni 2028.
	i. Kuandaa programu ya mafunzo inayounganisha dhana ya utawala wa sheria na maadili ili kukuza uongozi wenye uwajibikaji kila mwaka.
	ii. Kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ili kupima athari za programu hiyo katika sekta mbalimbali ifikapo Juni 2028.
	1.4 Kuanzisha na kuendesha vituo, vilabu na programu za uongozi katika ngazi ya kitaifa na kikanda kwa ajili ya kukuza uongozi katika sekta zote ifikapo Juni 2028.
	i. Kuimarisha au kuanzisha Taasisi ya Kitaifa ya Uongozi kwa ajili ya maendeleo ya viongozi wa sekta ya umma na binafsi ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuandaa mitaala maalum ya uongozi kwa sekta mbalimbali ifikapo Juni 2028.
	iii. Kushirikiana na vyuo vikuu kuanzisha programu za uongozi zinazotambuliwa kitaaluma ifikapo Juni 2028.
	1.5 Kuimarisha mifumo ya urithishaji wa uongozi ili kuhakikisha mwendelezo wa utoaji wa huduma ifikapo Juni 2028.
	i. Kufanya uchambuzi wa vipaji katika sekta mbalimbali ili kubaini viongozi wa baadaye ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuanzisha mifumo ya uongozi wa mzunguko ili kujenga uzoefu wa sekta mbalimbali ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	iii. Kuweka mifumo ya urithishaji wa uongozi inayozingatia maadili na utendaji ifikapo Juni 2028.
	1.6. Kuanzisha programu rasmi za ushauri na malezi ya uongozi ifikapo Juni 2028.
	Kuandaa miongozo, nyenzo na majukwaa ya ushauri wa uongozi katika sekta zote ifikapo Juni 2028.
	Kuunganisha viongozi wakuu na wataalamu wa ngazi ya kati kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa uongozi kila mwaka.
	Kuanzisha tuzo na utambuzi wa kitaifa kwa wakufunzi na washauri bora wa uongozi ifikapo Juni 2028.
	1.7. Kuanzisha programu za kubadilishana uzoefu wa uongozi ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha majukwaa ya viongozi wa ngazi za juu kubadilishana uzoefu kuhusu utawala na usimamizi ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuandaa mfumo wa kubadilishana maarifa, ushauri na mafunzo kati ya sekta mbalimbali ifikapo Juni 2028.
	iii. Kuanzisha programu za pamoja za malezi ya viongozi wenye mtazamo wa mageuzi katika sekta zote ifikapo Juni 2028.
	1.8. Kuanzisha programu za kukuza vipaji vya vijana na maendeleo ya uongozi kwa kuzingatia mahitaji ya maendeleo ya baadaye ifikapo Juni 2028.
	i. Kuanzisha programu za ushauri wa viongozi wakuu kwa viongozi chipukizi katika sekta zote ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	ii. Kuanzisha programu za mafunzo kwa vitendo na ushirika (kwa vijana wenye vipaji katika taasisi za ngazi za juu ifikapo Juni 2028.
	iii. Kuanzisha majukwaa ya mazungumzo kati ya vizazi mbalimbali kuhusu maadili na utawala ifikapo Juni 2028.
	1.9 Kuimarisha mifumo ya maadili na uadilifu katika sekta zote ifikapo Juni 2028.
	i. Kufanya mapitio na kuimarisha mifumo ya lazima ya utoaji wa tamko la mali kwa viongozi wa ngazi za juu ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuendesha majukwaa ya mara kwa mara ya maadili kati ya viongozi na wananchi ili kujenga uaminifu kila mwaka.
	iii. Kutambua hadharani viongozi wanaoonyesha uadilifu katika uongozi na utoaji wa huduma ifikapo Juni 2028.
	1.10 Kuanzisha mifumo ya mawasiliano inayokuza mabadiliko ya tabia, mitazamo na maadili ya uongozi katika sekta zote ifikapo Juni 2028.
	i. Kuanzisha kampeni za kitaifa zinazohamasisha uongozi unaoweka huduma kwa wananchi mbele ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuhamasisha viongozi katika sekta zote kuwa mfano wa kuigwa katika maadili ya uongozi kila mwaka.
	iii. Kuanzisha majukwaa ya umma yanayoonesha mafanikio ya mabadiliko ya mitazamo na tabia katika uongozi ifikapo Juni 2028.
	1.11. Kukuza mwelekeo mpya wa kitamaduni ili kuimarisha mabadiliko ya mitazamo na tabia ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kuoanisha kanuni za maadili ya viongozi na tunu za jamii pamoja na mahitaji ya maendeleo ya baadaye ifikapo Juni 2028.
	Kuweka utoaji huduma unaomlenga mwananchi kama kigezo muhimu katika uteuzi na upandishaji vyeo ifikapo Juni 2028.
	Kuweka mifumo ya maoni ya wananchi ili viongozi waweze kusikiliza na kuchukua hatua kwa kuzingatia maoni ya wananchi ifikapo Juni 2028.
2. Mabadiliko ya mtazamo katika utawala na sekta ya kufikiwa ifikapo Juni 2028.	2.1. Kufanya mapitio na kufuta sheria zilizopitwa na wakati pamoja na kanuni za utumishi wa umma ili kuondoa utamaduni wa udhibiti uliopitiliza na kuimarisha majukumu yanayomweka mwananchi kipaumbele katika utoaji wa huduma ifikapo Juni 2028.
	Kufanya ukaguzi wa udhibiti na sera katika mifumo ya utumishi wa umma ifikapo Juni 2028.
	Kufanya mapitio, kuanzisha na kuendesha mifumo hiyo kwa kuzingatia mahitaji ya maendeleo ya baadaye ifikapo Juni 2028.
	iii Kuandaa miongozo na vitabu vya taratibu ili kuwezesha utekelezaji wa mifumo iliyofanyiwa mageuzi ifikapo Juni 2028.
3. Kujenga Upya Imani na Ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi kupitia majukwaa ya majadiliano ya mara kwa mara na kuimarisha mipango ya sera za pamoja ifikapo Juni 2028.	3.1. Kuimarisha majukwaa ya mazungumzo kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika ngazi ya kitaifa na kisekta ifikapo Juni 2028.
	i. Kufanya mapitio ya kiutendaji ya majukwaa yaliyopo ya mazungumzo kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuanzisha au kuboresha mifumo ya majadiliano kati ya sekta binafsi na serikali kwa kila sekta husika ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	iii. Kuweka mifumo ya ufuatiliaji na mrejesho ili kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya pamoja na ahadi za sera zinazotokana na majukwaa ya majadiliano ifikapo Juni 2028.
	3.2. Kuanzisha Kituo cha Mafunzo ya Utawala wa Masoko kwa watumishi wa umma ifikapo Juni 2028.
	i. Kubuni na kuandaa mfumo wa mafunzo na mitaala ya utawala wa masoko kwa kushirikiana na taasisi za kitaaluma, wawakilishi wa sekta binafsi na wataalam wa kimataifa ifikapo Juni 2028.
	ii. Kufanya majaribio ya programu za mafunzo katika taasisi zilizopo za utawala wa umma ifikapo Juni 2028.
	iii. Kuanzisha au kuboresha taasisi zilizopo za mafunzo ili ziwe vituo vya mafunzo ya utawala wa masoko na rasilimali za kitaifa kwa ajili ya kujenga uwezo endelevu ifikapo Juni 2028.
4. Kukuza Mwananchi Mwenye Uwezo, Ushiriki na Uwajibikaji ifikapo Juni 2028.	4.1. Kuingiza katika mitaala ya elimu ya taifa mada za ujasiriamali, ujuzi wa kidijitali, usawa wa kijinsia na uwajibikaji wa kiraia kuanzia elimu ya msingi hadi elimu ya juu ifikapo Juni 2028.
	Kufanya mapitio ya mitaala iliyopo ili kuingiza kikamilifu masuala ya ujasiriamali, ubunifu, ujuzi wa kidijitali, usawa wa kijinsia na uwajibikaji wa kiraia katika masomo yote na katika ngazi zote za elimu (kuanzia msingi hadi elimu ya juu) ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha moduli maalum za mafunzo katika vyuo vya ualimu ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
	Kufundisha angalau asilimia 30 ya walimu na wakufunzi nchini kuhusu namna ya kufundisha mada za elimu ya uraia kwa kutumia mbinu shirikishi, jumuishi na zinazotegemea miradi ifikapo Juni 2028.
	4.2 Kuanzisha majukwaa ya ngazi ya jamii kwa ajili ya bajeti shirikishi na kupokea maoni ya wananchi kuhusu utawala kila mwaka.
	Kuanzisha vikao vya mipango shirikishi angalau asilimia 70 ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ifikapo Juni 2028.
	Kubuni, kuendeleza na kusambaza jukwaa la kidijitali linaloweza kutumika kwa simu za mkononi ambapo wananchi wanaweza kuona bajeti za serikali za mitaa na mipango ya miradi, pamoja na kutoa maoni kuhusu huduma za umma na miradi ya maendeleo ifikapo Juni 2028.
	4.3 Kukuza programu za ubunifu zinazoongozwa na jamii, zenye kulenga vijana ifikapo Juni 2028.
	i. Kuanzisha angalau kituo kimoja cha ubunifu wa vijana katika kila kanda, ambapo vijana wanaweza kubuni na kuendeleza suluhisho za changamoto za maeneo yao ifikapo Juni 2028.
	ii Kuanzisha na kuendesha Programu ya Changamoto za Ubunifu wa Jamii kwa Vijana ifikapo Juni 2028.
	Kuanzisha rasmi Tuzo za Kitaifa za Uraia zitakazotolewa kila mwaka ili kukuza fahari ya uraia na uwajibikaji ifikapo Juni 2028.
	i. Kuandaa programu ya tuzo pamoja na vigezo na muundo wa utoaji wa Tuzo za Kitaifa za Uraia ifikapo Juni 2028.
	ii. Kuanza kutekeleza rasmi programu ya utoaji wa tuzo hizo ifikapo Juni 2028.

Shabaha	Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2027/28
Lengo 3: Kuimarisha maadili ya uadilifu, uzalishaji na uwajibikaji	
1.Farihisi ya maadili ya kitaifa kuongezeka kutoka asilimia 50 (2024) hadi asilimia 75 ifikapo Juni 2028.	1.1. Kuendesha kampeni za elimu ya uraia ifikapo Juni 2028.
	Kukuza majukwaa ya mazungumzo kati ya serikali, sekta binafsi na asasi za kiraia kila mwaka.
	1.3 Kutoa motisha na kutambua hadharani watu wanaoonyesha uadilifu na mifano bora ya maadili ifikapo Juni 2028.
Lengo la 4: Kuboresha mifumo ya elimu na uongozi	
1. Mitaala inayolenga ubunifu na maendeleo ya viwanda kuongezeka kutoka asilimia 30 (2024) hadi asilimia 70 ifikapo Juni 2028.	1.1 Kurekebisha mitaala ili kuzingatia sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati, maadili na ubunifu ifikapo Juni 2028.
	1.2 Kuanzisha akademia za uongozi na programu za malezi ya viongozi ifikapo Juni 2028.
	1.3 Kushirikiana na sekta binafsi katika programu za mafunzo kwa vitendo na ufundi stadi ifikapo Juni 2028.

KIAMBATISHO NA. II: MAELEZO YA KINA KUHUSU PROGRAMU ZA KIELELEZO, MIRADI SHIKIZI, NA MAENEO YA MINYORORO YA THAMANI

(i)	**Mji wa Ikolojia ya Bahari Bagamoyo na Usafirishaji Fungamanishi**

Lengo ni kujenga kituo cha kisasa cha shughuli za bahari na viwanda vitakavyojumuisha bandari, huduma za usafirishaji na ugavi, uzalishaji wa viwandani na huduma za mijini. Utekelezaji wa programu hii utaenda sambamba na uimarishaji wa miundombinu, ubunifu katika uchumi wa buluu na ushindani wa biashara.

Miradi shikizi	
(i)	Reli ya kisasa ya SGR inayounganisha Ruvu na Bagamoyo, pamoja na kipande cha 3 - 8 cha reli ya kati vinavyounganisha Tabora, Mwanza, Kigoma na Msongati pamoja na vipande vya reli kuelekea Kabanga na Buzwagi;
(ii)	Barabara ya inayounganisha Pangani hadi Bagamoyo, Barabara inayounganisha Kigamboni - Chanika – Kibaha - Bunju (km 715);
(iii)	Uendelezaji, uboreshaji na upanuzi wa viwanja vya ndege;
(iv)	Uendelezaji wa Bandari ya Mbegani;
(v)	Ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano ya kisasa, ikiwemo Mkongo wa Taifa Mawasiliano;
(vi)	Viwanda vya dawa hususan kwa kuanzisha viwanda vya uzalishaji wa dawa;
(vii)	Kitovu Cha biashara ya ugavi na usafirishaji njia mbalimbali na biashara ya mtandao;
(viii)	Mradi wa kuendeleza biashara na mfumo fungamanishi wa usafirishaji na uchukuzi nchini;
(ix)	Kukuza ujuzi kupitia taasisi ya mafunzo ya ufundi stadi kwa umahiri maalumu; na

Miradi shikizi	
(x)	Upanuzi Bandari ya Dar es Salaam.

Maeneo ya Minyororo ya Thamani	
(i)	Utalii na Huduma za Ukarimu: miundombinu ya utalii wa pwani, ikiwemo hoteli, vituo vya mapumziko na huduma za burudani, pamoja na kukuza utalii wa matukio na utalii wa meli za kitalii;
(ii)	Viwanda na Uzalishaji: uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya mauzo ya nje, ikiwemo viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vinavyotengeneza nguo, chakula, vifaa wa kielektroniki, mashine, magari, pamoja na uchakataji wa chuma, kemikali na mbolea;
(iii)	Usafirishaji na Ugavi wa Bahari: kushughulikia mizigo, uhifadhi na usafirishaji wa bidhaa, huduma za ugavi, pamoja na huduma za bandari;
(iv)	Biashara na huduma za kifedha: kituo cha biashara ya mtandao;
(v)	Huduma za kifedha na ugavi: biashara ya bidhaa zisizotozwa ushuru na usafirishaji wa bidhaa kwa masoko ya nje; biashara ndogo na za kati pamoja na watoa huduma; Maendeleo ya majengo na huduma za msingi; mafunzo ya ujuzi na uundaji ajira; Utafiti, ubunifu na teknolojia: vituo wa utafiti na ubunifu, pamoja na matumizi ya teknolojia katika uzalishaji wa viwandani na biashara changa;
(vi)	Mawasiliano na mifumo ya kidijitali: miundombinu ya kidijitali itakayorahisisha biashara na uwekezaji, usimamizi wa ugavi na usafirishaji kwa wakati, urahisishaji wa biashara kwa njia za kisasa, na utangazaji wa utalii kwa nia za kidijitali.

(ii) Kitovu Changamani cha Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga

Lengo ni kujenga kituo changamani cha chuma na makaa ya mawe kwa ajili ya uzalishaji na kuongeza thamani ya madini (chuma na makaa ya mawe) hivyo kupunguza utegemezi wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje.

Miradi Shikizi	
(i)	Reli ya Kisasa ya SGR kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay pamoja na maeneo ya Mchuchuma na Liganga (km 1,000);
(ii)	Mradi wa Maganga Matitu kwa ajili ya madini ya chuma yanayopatikana wilayani Ludewa;

Miradi Shikizi	
(iii)	Mradi wa Kiwira kwa ajili ya kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe, wenye uwezo wa zaidi ya megawati 200;
(iv)	Barabara ya Mawengi - Manda (km 110), Mkiu – Mavanga - Madaba(km 112), Nkomang'ombe - Liganga(km70), Nkomangombe - Mchuchuma (7 km) na Igawa - Tunduma pamoja na barabara ya mchepuko ya Uyole (km 266);
(v)	Uendelezaji, uboreshaji na upanuzi wa miundombinu ya usafirishaji hususan viwanja wa ndege na bandari;
(vi)	Miundombinu ya mawasiliano, ikiwemo Mkongo Taifa Mawasiliano; na
(vii)	Maendeleo ya ujuzi kupitia taasisi za elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa ajili ya ujuzi maalumu.

Maeneo ya Minyororo ya Thamani	
(i)	Madini na uchimbaji: uchimbaji wa chuma na makaa ya mawe na uzalishaji chuma;
(ii)	Nishati: uzalishaji, usambazaji na usafirishaji wa nishati;
(iii)	Ujenzi na usafirishaji: reli, barabara, huduma za ugavi na uhifadhi wa bidhaa, pamoja na majengo;
(iv)	Viwanda: viwanda vya chuma na bidhaa za chuma; viwanda vinavyotegemea chuma kama malighafi, ikiwemo mashine, vipuri vya magari, Vifaa vya ujenzi na zana za kilimo; pamoja na viwanda vya kemikali na bidhaa zitokanazo na uzalishaji huo, ikiwemo saruji, gesi za viwandani na mbolea;
(v)	Ujuzi, huduma na ubunifu: kuimarisha rasilimali watu, ikiwemo kutoa mafunzo ya ufundi na utaalamu kwa sekta za madini na nishati: kufanya tafiti; na kuchochea maendeleo pamoja na ubunifu wa teknolojia ya chuma na mazingira; na
(vi)	Ushirikiano wa kibiashara: huduma na shughuli saidizi katika mnyororo wa ugavi, ikiwemo usafirishaji, upishi na utengenezaji wa bidhaa za metali.

(iii)	**Programu ya Kitaifa ya Umwagiliaji na Mageuzi ya Viwanda vya Uchakataji wa Mazao ya Kilimo**

Lengo ni kuboresha na kuongeza miundombinu ya umwagiliaji na uchakataji wa mazao ya kilimo ili kuongeza tija, kuimarisha minyororo ya thamani ya viwanda vya kilimo na kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza ushindani kwa mazao katika mauzo ya nje.

Miradi shikizi	
(i)	Kilimo: miradi ya umwagiliaji katika Mabonde ya Rufiji, Songwe na Mara inayolenga kuongeza uzalishaii kwa ajili ya mauzo ya nje;
(ii)	Barabara za Rufiji - Kilwa, Kilwa – Morogoro; Igawa - Tunduma pamoja na barabara ya mchepuo wa uyole (km 266.9); na Handeni – Kiberashi - Singida (km 434.33) pamoja na barabara za kuunganisha maeneo ya uzalishaji vijijini.
(iii)	Ugavi na usafirishaji: kuendeleza, kuboresha na kupanua viwanja vya ndege, bandari na bandari kavu, vitovu vya ugavi wa mazao ya kilimo pamoja na miundombinu ya kuhifadhi na kusafirisha mazao katika hali ya ubaridi;
(iv)	Mradi wa Bugwema kwa ajili ya umwagiliaji Jumuishi wa Kisasa na Kilimo cha Biashara:
(v)	Shamba Kubwa la Lumpungu la Umwagiliaji kwa ajili ya Kilimo cha Biashara;
(vi)	Mradi wa Bonde la umwagiliaji la Kamsamba;
(vii)	Mradi wa Kuendeleza Umwagiliaji Membe; na
(viii)	Kitovu cha biashara, ugavi na usafirishaji wa njia mbalimbali pamoja na biashara mtandao.

Maeneo ya Minyororo ya Thamani	
(i)	Kilimo: miradi ya umwagiliaji katika Mabonde ya Rufiji, Songwe na Mara inayolenga kuongeza uzalishaii kwa ajili ya mauzo ya nje;

Maeneo ya Minyororo ya Thamani	
(ii)	Barabara: Rufiji—Kilwa, Kilwa—Morogoro, Igawa—Tunduma pamoja na barabara ya mchepuo wa uyole (km 266.9), Handeni—Kiberashi—Singida (km 434.33), parnoja na barabara za kuunganisha maeneo ya uzalishaji vijijini.
(iii)	Ugavi na usafirishaji: kuendeleza, kuboresha na kupanua viwanja vya ndege, bandari na bandari kavu, vitovu vya ugavi wa mazao ya kilimo pamoja na miundombinu ya kuhifadhi na kusafirisha mazao katika hali ya ubaridi;
(iv)	Mradi wa Bugwema wa umwagiliaji Jumuishi wa Kisasa na Kilimo cha Biashara:
(v)	Shamba Kubwa la Lumpungu la Umwagiliaji kwa Kilimo cha Biashara;
(vi)	Mradi wa Bonde la umwagiliaji la Kamsamba;
(vii)	Mradi wa Kuendeleza Umwagiliaji Membe; na
(viii)	Kitovu cha biashara, ugavi na usafirishaji wa njia mbalimbali pamoja na biashara mtandao.

(iv)	**Kitovu cha Teknolojia na Uchakataji wa Madini Adimu Dodoma**

Kituo hichi kinalenga kuifanya Dodoma kuwa kitovu cha kitaifa cha ubunifu na teknolojia kwa kuunganisha uongezaji thamani wa madini, miundombinu ya uchumi wa kidijitali na mifumo utafiti wa viwanda.

Miradi Shikizi	
(i)	Barabara barabara ya Nyakahura - Kabanga (km 141), barabara ya Dodoma -Iringa – Mbeya; Barabara ya mwendokasi ya Kibaha - Morogoro - Dodoma (km 465), na barabara ya Kidatu Lupilo - Lumecha/Songea (km 512);
(ii)	Ugavi na usafirishaji: uendelezaji, uboreshaji na upanuzi wa bandari, viwanja vya ndege na vituo vya ugavi;
(iii)	Kitovu cha kitaifa Cha utafiti na ubunifu katika akili unde na kompyuta;
(iv)	Miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano;
(v)	Mradi wa magadi soda Engaruka;

Miradi Shikizi	
(vi)	Utafiti na maendeleo: tafiti za teknolojia na uchumi kwa ajili ya kuboresha viwanda vya madini; na
(vii)	Kukuza ujuzi: taasisi mahiri za elimu na mafunzo ufundi stadi.

Maeneo ya Minyororo ya Thamani	
(i)	Madini: kobalti, lithiamu, heliumu, grafaiti na nikeli; viwanda na uzalishaji: kuzalisha bidhaa za viwandani kama betri, aloi na bidhaa nyingine zinazotokana na madini muhimu;
(ii)	Nishati na miundombinu: uzalishaji nishati jadidifu inayotokana na jua, maji, upepo na jotoardhi, usambazaji wa umeme na mifumo ya gridi, pamoja na usimamizi wa maji safi na usafi wa mazingira;
(iii)	Utafiti, maendeleo na ubunifu: Vituo vya utafiti, maendeleo ya ujuzi, teknolojia za uchakataji wa kemikali, matumizi ya mifumo ya kisasa viwandani na biashara changa; na
(iv)	Biashara, ugavi na huduma za kifedha: uchakataji bidhaa kwa ajili ya mauzo ya nje na urahisishaji wa biashara, mifumo ya ugavi na usafirishaji pamoja na huduma za kifedha na uwekezaji ikiwemo hatifungani za kijani, mitaji bunifu na fedha zinazotokana na biashara ya kaboni kwa ajili ya kuwezesha biashara changa na biashara ndogo na za kati.

(v)	**Kiwanda cha Kuchakata Gesi asilia ya Kimiminika Lindi**

Lengo ni kuanzisha kituo cha kimataifa cha usafirishaji wa gesi asilia iliyoyeyushwa kwa ajili ya mauzo ya nje kitakachoharakisha mageuzi ya sekta ya nishati, kuongeza mapato na maendeleo ya mnyororo wa thamani viwandani.

Miradi shikizi	
(i)	Uendelezaji wa barabara kuu ya Mtwara - Dar es Salaam
(ii)	Bomba la kusafirisha gesi; na
(iii)	Taasisi mahiri za kuendeleza ujuzi na viwanda vya kuchakata gesi.

Maeneo ya Minyororo ya Thamani	
(i)	Nishati: utafutaji wa gesi asilia; usafishaji wa gesi (usafirishaji kwa njia ya mabomba, matenki ya kuhifadhia, vituo vya kupokea na kusafirisha gesi); vitengo vya kurejesha gesi kutoka hali ya kimiminika; usambazaji na mauzo ya nje;
(ii)	Mradi wa Kinyerezi Ill wa kuzalisha umeme wa megawati 1,000 kwa kutumia gesi asilia;
(iii)	Viwanda na Uzalishaji: bidhaa za kemikali zitokanazo na mafuta na gesi asilia, uzalishaji wa mbolea, gesi asilia iliyoshindiliwa, na usambazaji wa gesi kwa matumizi ya viwandani;
(iv)	Huduma za baharini, ugavi na ujenzi: miundombinu ya baharini, huduma za ugavi, huduma za ujenzi na uhandisi, pamoja na uboreshaji wa bandari;
(v)	Maendeleo yatokanayo na ujuzi, teknolojia na huduma kifedha: mafunzo ya rasilimali watu katika uhandisi wa mafuta na gesi, shughuli za baharini, uchomeleaji na udhibiti wa mifumo ya uzalishaji; uhawilishaji wa teknolojia na ubunifu; huduma za kifedha; na biashara za wananchi.

(vi)	**Kitovu cha Kisasa cha Viwanda na Uchumi wa Buluu katika Ukanda wa Ziwa Makuu**

Lengo ni kuwezesha eneo la kanda ya ziwa kuwa kitovu cha kikanda katika viwanda usafiri na usafirishaji na uchumi wa buluu ili kuunganisha masoko ya Eneo Huru la Biashara Afrika, kupanua fursa za kujipatia kipato katika sekta za uvuvi, madini na uchakataji wa mazao ya kilimo, na kuhimiza maendeleo ya viwanda na matumizi ya teknolojia ya kidijtali.

Miradi shikizi	
(i)	Kuboresha shirika la ndege la Taifa;
(ii)	Meli ya Mizigo inayotumia reli Iliyopachikwa;
(iii)	Barabara za kikanda zinazounganisha Bukoba, Kyaka, Simiyu, Shinyanga na Mara;
(iv)	Barabara za kikanda zinazounganisha Tanzania na Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo;

Miradi shikizi	
(v)	Uendelezaji, uboreshaji na upanuzi viwanja ndege na bandari;
(vi)	Kiwanda cha kutengeneza vifaa tiba na dawa; na
(vii)	Vituo vya ufundi stadi na ubunifu kwa ajili ya uhandisi wa bahari, matumizi ya mifumo ya kisasa ya viwanda, usafirishaji na ugavi pamoja na ujasiriamali.

Maeneo ya Minyororo ya Thamani	
(i)	Uchakataji na usafirishaji wa samaki kwa ajili ya mauzo nje ya nchi;
(ii)	Uchenjuaji wa dhahabu na Vito uliofungamanishwa na Kitovu cha Madini Muhimu Dodoma na Ubunifu wa Teknolojia kupitia Soko la Madini ya Thamani;
(iii)	Mnyororo wa thamani wa kuchakata pamba kuwa nguo na ngozi kuwa bidhaa za ngozi;
(iv)	Uchakataji wa kahawa na chai ili kuongeza thamani;
(v)	Mazao ya umwagiliaji yatakayofungamanisha na masoko ya mazao kikanda ya Kenya, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; na
(vi)	Kuimarisha uendeshaji wa Shirika la Ndege la Tanzania.

(vii)	**Programu Shirikishi ya Uendelezaji wa Miji Nchini**

Lengo ni kujenga miji imara, jumuishi na endelevu kwa kutumia miundombinu na huduma za kisasa, upanuzi wa makazi nafuu, kuzalisha ajira za kijani na kidijitali, na kuimarisha usimamizi wa miji unaozingatia mabadiliko ya tabianchi.

Miradi shikizi	
i.	Usimamizi endelevu ardhi ya Mijini;
ii.	Miundombinu ya msingi;

Miradi shikizi	
iii.	Makazi nafuu na miundombinu ya huduma za kijamii;
iv.	Usambazaji nishati safi, miundombinu ya msingi inayohimili mabadiliko ya tabianchi;
v.	Vituo wa kisasa wa huduma za afya;
vi.	Vituo wa mapumziko na burudani;
vii.	Mifumo fungamani ya usafiri na usafirishaji na kitovu cha biashara mtandao; na
viii.	Miji ya kisasa inayosimamiwa kwa kutumia majukwaa ya kidijitali yanayowezeshwa na akili unde.

Maeneo ya Minyororo ya Thamani
Mnyororo wa thamani wa makazi na ujenzi utaunganishwa na huduma za usafiri na usafirishaji hivyo kuchochea ukuaji wa sekta ya huduma na kuzalisha ajira; na uwekezaji katika nishati utachochea maendeleo ya miundombinu kisasa na kukuza uchumi wa kidijitali.